# Njia ya Haki

## Habari Njema kwa Waislamu

Habari na mafundisho ya manabii wa Mungu ndani ya Tora, Zaburi na Habari Njema (Injil)

**Kitabu 2**

**par P.D. Bramsen**

**Everyday Publications Inc.**
310 Killaly Street W.
Port Colborne, ON
Canada L3K 6A6

# Njia ya Haki

## Kitabu cha Pili

Copyright © 1998
P.D. Bramsen
The Way of Righteousness (Le Chemin de la Justice)

Traduit en Swahili par permission
par G.I. Harlow

Copyright © 2006
Everyday Publications Inc. / The Way of Righteousness
ISBN 0-88873-146-9
*Cette série est aussi disponible dans d'autres langues.*

Pour permission de traduire Le Chemin de la Justice dans
d'autres langues veuillez contracter:
TWOR@iname.com / www.twor.com

*Imprimé au Canada*

# Njia ya Haki

*Habari na mafundisho ya manabii wa Mungu*
*ndani ya Tora, Zaburi na Habari Njema (Injil)*

## Utangulizi

***"Hata logo ikilala mia za miaka ndani ya maji halitageuka mamba kamwe"*** (mezali ya Wawolof wa Senegal) . . . ***vivyo hivyo kushikamana na dini hakuwezi kugeuza mtu kuwa haki.*** Desturi za dini na matendo mema yanasaidia watu kufikili wao ni *watu wa haki* na kuwafanyiza kuonekana kama wenye *haki mbele ya watu,* lakini hayawafanyizi *haki* ***mbele ya Mungu****.*

***Njia ya Haki*** ni tafsiri kwa Swahili-Congo ya **"Yoonu Njub"** — programmes 100 za radio kwa kiwolof kwa Waislamu wa Senegal ya Afrique de l'Ouest. Kuanza na Tora ya Musa programmes hizi zinapeleka wasikiaji kwa safari ya Maandiko ya manabii kuona kusudi lisilobadiliki kamwe la Mungu kwa watu wa dunia na kusikia jibu la furaha kubwa la Mungu kwa neno ambalo nabii Yobu aliuliza miaka elfu ine mbele, ***"Mtu anaweza kuwa na haki mbele ya Mungu namna gani?"*** (Yobu 9:2)

Sasa programmes hizi zimechapwa kwa Swahili ndani ya vitabu vitatu kusaidia Waislamu na watu wengine vilevile kufahamu habari hizi za *manabii ya Mungu* vizuri zaidi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kitabu 1 — | Masomo | 1-28 | *Njia ya Haki ndani ya TORA* |
| Kitabu 2 — | Masomo | 29-45 | *Njia ya Haki ndani ya TORA* |
| | Masomo | 46-59 | *Njia ya Haki ndani ya ZABURI na MANABII* |
| Kitabu 3 — | Masomo | 60-88 | *Njia ya Haki ndani ya HABARI NJEMA* |
| | Masomo | 89-100 | *Njia ya Haki – MUHTASARI* |

Waislamu wanaamini ya kwamba Mungu amefunua mapenzi yake kwa njia ya vitabu vitakatifu vine (Tora, Zaburi, Habari Njema, Qur'an). Lakini Waislamu wachache tu wamekuwa na njia kusoma Habari Njema ya Mungu ndani ya Tora, Zaburi, na Maandiko ya Habari Njema. **Masomo haya 100 yanawapatia njia kufanya hivi.**

Watu wengi wanashangaa wakati wanaposikia ya kwamba Qur'an kinaagiza Waislamu kuamini Tora (Taurat), Zaburi na Habari Njema (Injil), sehemu za Maandiko Matakatifu kwa Kiebrania na Kiyunani yanayoita *Biblia.* (Biblia ni kilatin kwa *Kitabu).*

Waislamu wengi wanasema ya kwamba maandiko ndani ya vitabu vya Tora, Zaburi na Habari Njema yamegeuzwa na haifai kuyaamini. Lakini masemo haya si kweli. Kuna karatasi elfu za maandiko ya vitabu hivi vinavyochungwa kwa pahali mbalimbali pa dunia. Karatasi hizi ziliandikwa mia za miaka mbele ya Qur'an. Kuna mafundisho mengine juu ya neno hili ndani ya Somo 90. Lakini hatuhitaji kusimamia Neno la Mungu kwani linasimama imara, Neno takatifu la Mwenyezi Mungu. Neno ambalo inatupasa kufanya si kulisimamia lakini ***kuisoma***.

> *"Maana Neno la Mungu ni hai, lenye nguvu na ukali kupita ukali wa upanga unaokata ngambo mbili, likitoboa hata kutenga nafsi na roho, na viungo na mafuta ndani ya mifupa; nalo ni jepesi kufahamu mawazo na makusudi ya moyo. Hakuna kiumbe kinachofichwa mbele yake, lakini vitu vyote ni utupu na kufunuliwa mbele ya macho yake yeye aliye na maneno yetu."*
>
> (Wabrania 4:12,13)

Ndiyo, uwezo wa kuchoma roho ya **Kweli ya Mungu** na utamu wa milele wa **njia ya haki ya Mungu** zinastahili kwa watu kuwa tayari kupata mateso na hata mauti kwa sbababu yake. Nabii Solomono aliandika, *"**Katika njia ya haki** ni uzima; na katika mapito yake hakuna mauti"* (Mezali 12:28) Allahu Akbar! Mungu ni mkubwa, na kwa wote wanaonyenyekea njia yake ya haki anatoa ahadi kuwapa bila bei neno ambalo dini na matendo mema hayawezi kutupatia: wokovu toka azabu na uwezo wa zambi, kuhesbiwa haki na kujua ya kwamba zambi zetu zimesamehewa, zamiri safi, salama kubwa moyoni, furaha rohoni ambayo hakuna neno linaweza kuharibu, tabia mpya, upatano wa karibu na Mungu, na kao pamoja naye katika Paradiso kwa milele!

Tunaweka kwa Mungu watu wote wanaosoma masomo haya mia moja, kwa Mungu yule mwenye huruma na rehema, **mwenye haki**—anayetaka kutolea ahadi hii ya kuleta uzima na kugeuza maisha kwa mtu ye yote anayekubali kuipokea.

> ***"Mutanitafuta, na kuniona wakati mutakaponitafuta kwa moyo wenu wote."*** (Yeremia 29:13)

# Fahirisi

## *Kitabu 1*

Habari na Mafundisho ya Manabii wa Mungu
kupatana na Tora


| | | |
|---|---|---|
| | | *ukurasa* |
| | *Utangulizi* | 3 |
| *Somo* | | |
| 1 | Mungu amesema (Mwanzo) | 11 |
| 2 | Mungu ni namna gani? (Mwanzo 1) | 17 |
| 3 | Shetani na Malaika (Mwanzo 1:1; Isaya 14; Ezekieli 28 | 22 |
| 4 | Namna Mungu alivyoumba dunia (Mwanzo 1:1-26) | 27 |
| 5 | Kwa sababu gani Mungu aliumba mtu (Mwanzo 1:26,27; 2:7) | 32 |
| 6 | Adamu na Hawa (Mwanzo 2) | 37 |
| 7 | Namna gani zambi ilivyoingia duniani (Mwanzo 3:1-6) | 43 |
| 8 | Tunda la zambi ya Adamu (Mwanzo 3:7-19) | 48 |
| 9 | Ahadi ya ajabu (Mwanzo 3:15,21-24) | 53 |
| 10 | Njia ya sadaka (Mwanzo 4:1-5) | 59 |
| 11 | Kutotubu kwa Kaina (Mwanzo 4:1-16) | 65 |
| 12 | Nabii Enoka (Mwanzo 4, 5) | 70 |
| 13 | Nabii Noa : Saburi na gazabu (Mwanzo 6) | 76 |
| 14 | Noa na garika kubwa (Mwanzo 7) | 81 |
| 15 | Noa na uaminifu wa Mungu (Mwanzo 8, 9) | 86 |
| 16 | Babeli! (Mwanzo 10, 11) | 91 |
| 17 | Ukumbusho #1 (Mwanzo 1-11) | 97 |
| 18 | Abrahamu: Kwa sababu gani Mungu alimwita (Mwanzo 11,12) | 102 |
| 19 | Imani ya Abrahamu: (Mwanzo 13-15) | 108 |
| 20 | Abrahamu na Isimaeli (Mwanzo 16,17) | 113 |
| 21 | Abrahamu: Uharibifu wa Sodomo na kuzaliwa kwa Isaka (Mwanzo 18-21) | 119 |

| *Somo* | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| 22 | Sadaka ya Abrahamu (Mwanzo 22) | 125 |
| 23 | Esau na Yakobo (Mwanzo 25) | 131 |
| 24 | Yakobo anageuka Israeli (Mwanzo 28-32) | 137 |
| 25 | Aibu ya Yosefu (Mwanzo 37-39) | 143 |
| 26 | Kutukuzwa kwa Yosefu (Mwanzo 40-42) | 149 |
| 27 | Baki la habari za Yosefu (Mwanzo 42-50) | 155 |
| 28 | Ukumbusho wa kitabu cha kwanza cha Tora (Mwanzo 1-50; Kutoka 1) | 161 |

## *Kitabu 2*

**Masomo 29 – 59**

| | | |
|---|---|---|
| | *Utangulizi* | 3 |
| 29 | Musa (Kutoka 1,2) | 11 |
| 30 | Musa anakutana na Mungu (Kutoka 3,4) | 17 |
| 31 | Ulizo la Farao: Bwana ni nani? (Kutoka 4-7) | 23 |
| 32 | Hukumu kumi (Kutoka 7-10) | 29 |
| 33 | Mwana-Kondoo ya Pasaka (Kutoka 11,12) | 35 |
| 34 | Njia katikati ya Bahari (Kutoka 13-15) | 41 |
| 35 | Chakula jangwani (Kutoka 16,17) | 47 |
| 36 | Mlima Sinai (Kutoka 19, 20) | 53 |
| 37 | Amri Kumi (Kutoka 20) | 59 |
| 38 | Kusudi la Amri Kumi (Kutoka 20) | 65 |
| 39 | Amri zinazovunjwa (Kutoka 32) | 71 |
| 40 | Hema ya Kusanyiko (Kutoka 24-40, Walawi 16) | 77 |
| 41 | Kutokuamini kwa Waisraeli (Hesabu 13,14) | 83 |
| 42 | Nyoka ya shaba (Hesabu 20,21) | 89 |
| 43 | Maneno ya mwisho ya Musa (Torati) | 95 |
| 44 | Yosua na inchi ya Kanana (Yosua) | 101 |
| 45 | Waamuzi na Ruta (Waamuzi na Ruta) | 107 |
| 46 | Samweli, Saulo na Daudi (1 Samueli 1-16; Zaburi 8,23) | 113 |
| 47 | Daudi na Goliata (1 Samweli 17; Zaburi 27) | 121 |
| 48 | Mfalme Daudi na ahadi ya Mungu (1 Samweli 18 - 2 Samweli 7) | 127 |
| 49 | Mfalme Daudi na Bati-Seba (2 Samweli 11,12; Zaburi 51,32) | 133 |
| 50 | Nabii Daudi na Masiya (Zaburi 1, 2) | 139 |

| *Somo* | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| 51 | Mafundisho mengine toka Zaburi (Zaburi 22) | 145 |
| 52 | Nabii Solomono (1 Wafalme 2-10; Zaburi 72) | 151 |
| 53 | Nabii Elia (1 Wafalme 6-18) | 157 |
| 54 | Nabii Yona (Yona) | 163 |
| 55 | Nabii Isaya (Isaya) | 169 |
| 56 | Nabii Yeremia (Yeremia) | 175 |
| 57 | Nabii Danieli (Danieli 1,6) | 181 |
| 58 | Nabii Zekaria (Zekaria) | 187 |
| 59 | Jumlisho la unabii wa manabii (Malaki) | 193 |

## *Kitabu 3*

### Masomo 60 –100

| | | |
|---|---|---|
| | *Utangulizi* | 3 |
| 60 | Nabii Yoane (Luka 1) | 11 |
| 61 | Tangazo (Luka 1; Matayo 1) | 17 |
| 62 | Masiya anazaliwa (Luka 2; Matayo 2) | 23 |
| 63 | Mwana mtakatifu (Luka 2; Matayo 3,4) | 29 |
| 64 | Mwana-Kondoo wa Mungu (Yoane 1,3) | 35 |
| 65 | Mganga mkubwa (Marko 1,2) | 41 |
| 66 | Mwalimu mkubwa (Matayo 5-7) | 47 |
| 67 | Sharti muzaliwe mara ya pili (Yoane 3) | 53 |
| 68 | Mwokozi wa dunia (Yoane 4; Luka 4) | 59 |
| 69 | Amri ya Yesu (Matayo 12; Yoane 5) | 65 |
| 70 | Uwezo wa Yesu (Matayo 12; Yoane 5) | 71 |
| 71 | Mifano mikubwa miwili (Luka 8; Matayo 13) | 77 |
| 72 | Mkate wa Uzima (Marko 6; Yoane 6) | 83 |
| 73 | Yesu analeta matengo (Matayo 15,16; Yoane 7) | 89 |
| 74 | Nuru ya Ulimwengu (Yoane 8,9) | 95 |
| 75 | Bwana wa utukufu (Matayo 16,17) | 101 |
| 76 | Mchungaji Mwema (Yoane 10) | 107 |
| 77 | Moyo wa Mungu (Luka 18,15) | 113 |
| 78 | Ufufuko na Uzima (Yoane 11,12) | 119 |
| 79 | Yesu anaingia Yerusalema (Luka 18-20) | 125 |
| 80 | Masemo magumu na ya kweli (Matayo 22-25) | 131 |
| 81 | Chakula cha mwisho (Matayo 26) | 137 |
| 82 | Yesu anakamatwa (Yoane 14; Matayo 26) | 143 |
| 83 | Yesu anahukumiwa (Matayo 26,27; Yoane 18,19) | 149 |

| *Somo* | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| 84 | Yesu anasulibishwa (Matayo 27; Marko 15; Luka 23; Yoane 19) | 155 |
| 85 | Yesu amefufuka! (Matayo 28; Luka 24; Yoane 20 | 161 |
| 86 | Yesu anapanda mbinguni (Matayo 28; Luka 24; Matendo 1) | 167 |
| 87 | Roho Mtakatifu amekuja! (Matendo 1,2) | 173 |
| 88 | Yesu atarudi tena! (Ufunuo 19-22) | 179 |
| 89 | Habari Njema | 185 |
| 90 | Maulizo ya watu na majibu ya Mungu (#1) | 193 |
| 91 | Maulizo ya watu na majibu ya Mungu (#2) | 199 |
| 92 | Inapasa mwanafunzi wa Kristo kuishi namna gani? | 206 |
| 93 | Ukumbusho #1 Adamu - Neno gumu la zambi (Mwanzo 1-4) | 212 |
| 94 | Ukumbusho #2 Abrahamu - Haki kwa njia ya imani (Mwanzo 6-22) | 218 |
| 95 | Ukumbusho #3: Musa: Sheria takatifu ya Mungu Kutoka 1-20) | 224 |
| 96 | Ukumbusho #4: Yesu Kristo: "Imekwisha!" (Yoane 19, Waebrania 10) | 230 |
| 97 | Hadeze! (Luka 16) | 236 |
| 98 | Paradiso! (Ufunuo 21,22) | 243 |
| 99 | Unafikili nini juu ya Yesu? (#1) | 249 |
| 100 | Unafikili nini juu ya Yesu? (#2) | 255 |

SOMO 29

# NABII MUSA

## KUTOKA 1,2

Salama iwe kwako rafiki msomaji. Tunasalimu nyinyi kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuanza leo *Kitabu 2* cha *Njia ya Haki*.

Kama unavyojua, kuna vitabu vitano ndani ya Tora vilivyo-andikwa na nabii wa Mungu, ndiye Musa. Ndani ya somo la mbele tulimaliza kitabu cha Mwanzo, na tulianza kusoma kitabu cha pili, jina lake *Kutoka*. Tunasihi Mungu aweze kutupa sisi nuru kwa nia na mioyo yetu kwa njia ya maneno yote tunayosoma ndani ya kitabu hiki chenye maana sana na chenye mafundisho mengi ya faida nyingi.

Tumeona ya kwamba kitabu cha pili cha Tora kinaendelea na habari tulizosoma ndani ya kitabu cha kwanza. Hivi tuliona wazao wa Abrahamu, Isaka na Yakobo, ndio **Waisraeli wakikaa katika Misri**, mbali na inchi ya Kanana ambayo Mungu alikuwa ameahidi kuwapa.

Ndani ya sura ya kwanza ya Kutoka tunasoma, kuanza na shairi 1,

> (Kutoka 1) *1 Na haya ni majina ya wana wa Israeli walioingia Misri; kila mtu na nyumba yake wakakuja pamoja na Yakobo. Rubeni, Simeoni, Lawi, na Yuda; Isakari, Zebuluni na Benyamina; Dani na Nafutali, Gadi na Aseri. Na nafsi zote zilizotoka viunoni mwa Yakobo zilikuwa nafsi makumi saba. Na Yosefu alikuwa katika Misri mbele. Yosefu akakufa, na ndugu zake zote, na kizazi kile chote. Wana wa Israeli wakazaa,* ***wakazidi sana, na kuongezeka****, wakakuwa hodari sana sana; inchi ikajaa nao.*
>
> *8 Akakuwa* ***mfalme mpya*** *juu ya Misri, asiyejua Yosefu. Akawaambia watu wake: Tazameni, watu wa wana wa Israeli*

> *wamekuwa wengi, nao ni hodari kuliko sisi; basi tuwatendee kwa akili; wasiongezeke na isiwe wakati vita itakapotokea waungane na adui zetu wapigane nasi na kupanda toka inchi. Kwa hivi wakaweka wasimamizi wa utumwa juu yao* ***kuwatesa kwa mizigo****. Wakajengea Farao miji ya kuwekea akiba, Pitomu na Ramisesi. Lakini hata kadiri walivyowatesa ndivyo wakazidi kuwa wengi na kuenea. Wakachukizwa kwa sababu ya wana wa Israeli. Wamisri wakatumikisha wana wa Israeli kwa nguvu; wakawatia maisha yao uchungu kwa utumwa mkali, na chokaa na matofali, kwa utumwa wote wa mashamba, kila utumwa ambao waliwatumikisha kwa nguvu."* (Kutoka 1:1-14)

Tuache kwanza pale. **Zaidi ya miaka mia tatu ilikuwa imepita** tangu kufa kwa Yosefu. Farao mwingine alitawala juu ya Misri, mfalme aliyesahau maneno yote Yosefu aliyofanya kwa watu wa Misri. Farao huyu alitesa Waisraeli sana, na kuwafanyiza watumwa wake. Aliwatumikisha na nguvu sana sana. Labda Waisraeli walifikiri Mungu alikuwa amesahau ahadi yake kwa mzazi wao Abrahamu ya kwamba watageuka taifa kubwa la uwezo. Lakini Mungu hakusahau! Ndiyo, Mungu alikuwa karibu kutimiza maneno aliyoahidi zamani.

Kweli **Mungu ni mwaminifu**! Anachunga maagano yake! Anafanya neno analoahidi hata kama watu wanafikili hafanyi hivi mbio! **Lilikuwa shauri la Mungu kuumba taifa jipya kwa njia yake manabii na Mkombozi watakuja—na hakuna neno lililoweza kumzuiza asitimize shauri hili!**

Unakumbuka ya kwamba wakati Mungu alipofunua mara ya kwanza shauri lake kufanya taifa jipya, alianza na wazee wawili, Abrahamu na Sara. Abrahamu alizaa Isaka wakati alipokuwa na miaka mia moja; Isaka alizaa Yakobo; na Yakobo alizaa wana kumi na wawili waliogeuka makabila ya Israeli. Walikuwa watu makumi saba wakati walipohama kwenda inchi ya Misri. Lakini sasa, nyuma ya miaka mia tatu mingine, walikuwa wameongezeka sana kuwa makutano makubwa, zaidi ya watu milioni moja! **Mungu alitimiza ahadi aliyotoa zamani?** Mungu alifanya taifa jipya kwa njia ya Abrahamu? Kabisa! Mungu ni mwaminifu, na hawezi kugeuza ahadi ambayo alitoa. Anastahili kupata utukufu kwa milele!

Ndani ya maneno tuliyosoma leo tunaona namna **Farao** alivyotesa makabila ya Israeli, na kuwafanyiza watumwa wake. Lakini tunaona vilevile ya kwamba kila mara Farao alipojaribu kutawala na

kupunguza ukubwa wa makabila ya Israeli, Mungu aliwawezesha kusitawi na kuongezeka. Hivi, Maandiko yanatujulisha ya kwamba Farao alikasirika sana na kutolea Waisraeli agizo hili: *"Kila mtoto mwanamume atakayezaliwa mutatupa mtoni!"* (Kutoka 1:22) Unafikili nini juu ya agizo la namna hii? Nani aliongoza Farao ndani ya shauri hili ovu? **Shetani** tu! Kwa nini Shetani alitaka kutesa na kuharibu Waisraeli? Kwa sababu Shetani alijua ya kwamba Mungu alikuwa ameahidi kutuma Mkombozi duniani atakayeokoa wana wa Adamu toka uwezo wa zambi na hadeze. Na Shetani alijua ya kwamba Mkombozi huyu atafika kwa njia ya **taifa la Israeli!** Kwa sababu hii Shetani alishawishi Farao kutesa watu wa Israeli na hata kuharibu taifa zima kwa njia ya kuagiza watoto wanaume wote watupwe ndani ya mto Nili wazame.

Lakini Mungu, aliye mwenye nguvu kupita Shetani, alikusudi kutumika na mtu mmoja wa makabila ya Israeli kuokoa watu wake wachaguliwa toka mkono wa Farao. Unajua jina la mhodari huyu? Ndiyo, alikuwa nabii wa kujulikana wa Mungu, ndiye **Musa.** Lakini wazazi wa Musa, *Amuramu na Yokebedi*, walikuwa wahodari vilevile kwa sababu *"hawakuogopa amri ya mfalme."* (Waebrania 11:23; Kutoka 6:20). Ndani ya sura ya pili ya Kutoka tunasoma juu ya **miaka ya kwanza ya maisha ya Musa.**

Maandiko yanasema ndani ya sura 2 ya Kutoka, kuanza na shairi 1:

> (Kutoka 2) *1 Akaondoka* ***mtu*** *ya nyumba ya Lawi, akaoa* ***binti*** *ya Lawi. Mwanamke akachukua mimba, akazaa* ***mtoto mwanamume****: na wakati alipomwona ya kwamba yeye ni mtoto mzuri, akamficha miezi mitatu. Na wakati asipoweza kumficha tena, akamtwalia safina ya manyasi, akaipakaa na tope la kunata na lami; akaweka mtoto ndani yake, akaiweka kwa majani kando ya mto.* ***Ndugu yake msichana*** *akasimama mbali ajue ambayo itampata.*
>
> *5* ***Binti ya Farao*** *akashuka aoge mtoni; vijakazi wake wakatembea kando ya mto. Akaona safina katika majani, akatuma kijakazi wake kuitwaa. Na wakati alipoifungua, akaona mtoto; na tazama, mtoto mchanga akalia. Akamhurumia, akasema: Huyu ni mmoja wa wana wa Waebrania."* (Wamisri waliita watu wa Israeli Waebrania.)
>
> *7 Halafu ndugu yake msichana akamwambia binti ya Farao: Niende na kukuitia aya ya wanawake wa Waebrania akunyonyeshee mtoto? Binti ya Farao akamwambia: Kwenda. Msichana akakwenda,*

> *akaita mama ya mtoto. Binti ya Farao akamwambia: Chukua mtoto huyu uninyonyeshee, na nitakupa mishahara yako. Mwanamke akatwaa mtoto, akamnyonyesha. Mtoto akakua, akamleta kwa binti ya Farao, akakuwa mwana wake. Akaita jina lake* ***Musa****, akasema: "Kwa sababu nilimtoa katika maji."* (Kutoka 2:1-10)

Hizi ndizo habari za kuzaliwa kwa Musa. Waza juu ya mshangao huu! Wakati watoto wachanga waume wengine walipokuwa wakiuawa, mtoto Musa alilindwa na kulishwa na mama yake mwenyewe na kuchungwa na Farao, yule mfalme mwovu! **Mungu** alikuwa akiongoza maneno yote yaliyotokea ndani ya maisha ya Musa. Mungu alikusudi kutumika na Musa kuponyesha Waisraeli toka utumwa. Hekima ya Mungu ni kubwa sana; inapita mbali hekima ya Shetani au watu. Unajua pahali gani Musa alipopata nguvu nyuma ya kuacha kunyonya? Alipata nguvu ndani ya nyumba ya Farao, mfalme aliyekuwa akitesa watu wa Israeli! Lakini Mungu alikusudi kutumika na Musa kuponyesha Waisraeli toka mkono wa Farao. Lilikuwa shauri la Mungu kutumika na binti ya mfalme yule mkali kuchunga Musa. Alijua ya kwamba nyumba ya Farao palikuwa pahali pazuri na pa salamu zaidi kwa Musa. Mungu alijua vilevile ya kwamba ilikuwa sharti kwa Musa kujifunza na kufahamu maneno mengi kumtayarisha kwa kazi ya kuongoza wana wa Israeli vizuri. Hivi Maandiko yanasema: *"Musa akafundishwa akili zote za Wamisri; akakuwa hodari kwa maneno na matendo."* (Matendo 7:22) Lakini Musa alihitaji kujifunza maneno mengi kwanza.

Maandiko yanasema, kuanza na Kutoka 2:11:

> (Kutoka 2) *Na ilikuwa kwa siku zile* ***wakati Musa alipokwisha kupata nguvu,*** *akatoka kwa ndugu zake, akaangalia mizigo yao; akaona Mmisri akipiga Mwebrania, mmoja wa ndugu zake. Akatazama huko na huko, na wakati alipoona hapana mtu, akapiga Mmisri, akamficha ndani ya mchanga. Akatoka siku ya pili, na tazama, watu wawili wa Waebrania wakapigana; akamwambia yeye aliyekosa: Kwa nini unapiga jirani yako? Akasema: Nani ambaye alikuweka wewe mkubwa na mwamuzi juu yetu? Unafikili kuniua namna ulivyoua yule Mmisri? Musa akaogopa, akasema: Hakika neno hili limejulikana. Basi wakati Farao aliposikia neno hili, alitaka kuua Musa. Lakini Musa akakimbia toka uso wa Farao; akakaa katika inchi ya Midiani."* (Kutoka 2:11-15)

Hivi tunaona ya kwamba Musu alijaribu kwanza kuponyesha wana wa Israeli kwa uwezo wake mwenyewe. Lakini hili halikuwa mapenzi ya Mungu. Mungu alitaka kutumika na Musa **kama kitu cha kazi** mkononi mwake kufungua wana wa Israeli. **Si Musa ambaye atawaokoa lakini Mungu.** Musa alikuwa mtu tu na hakuwa na uwezo kufungua wana wa Israeli toka mkono wa Farao isipokuwa Mungu alimpa uwezo huu.

Hivi Maandiko yanatujulisha ya kwamba Musa alikaa kwa miaka makumi ine jangwani, katika inchi ya Midani. Kulikuwa na maneno makubwa mengi Mungu aliyotaka kufundisha Musa katika jangwa ile ya kukauka kwa sababu ya jua kali. Kuna shairi moja ndani ya Neno la Mungu linalosema: *"Yeye aliye mwaminifu katika kitu kidogo kabisa ni mwaminifu tena katika kile kilicho kikubwa; naye aliye mzalimu katika kitu kidogo kabisa ni mzalimu tena katika kile kilicho kikubwa."* (Luka 16:10). Mbele ya kupewa kazi kubwa ya kulinda na kuongoza makutano mazima ya Israeli, ilipasa Musa kuonyesha ya kwamba alikuwa mwaminifu ndani ya kazi ndogo. Hivi tunasoma ndani ya Maandiko ya kwamba pale katika inchi iliyokuwa mbali na Misri, Musa aligeuka mchungaji kondoo, akaoa mke na kuzaa watoto wawili. Kwa miaka makumi ine Musa alikuwa mchungaji mwaminifu. Pale jangwani—wakati Musa alipokuwa akichunga kundi la baba ya mkewe—**Mungu alikuwa akitayarisha Musa** kwa siku ile atakapochunga taifa la Israeli. Mungu alikuwa na mashauri makubwa kwa Musa na watu wake Israeli!

Kisha Maandiko yanasema kwa Kutoka 2:23-25:

> *"Na ilikuwa nyuma ya siku nyingi mfalme wa Misri akakufa; wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya utumwa, wakalia, kilio chao kikapanda kwa Mungu kwa sababu ya utumwa.* ***Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake na Abrahamu na Isaka na Yakobo****. Mungu akaona wana wa Israeli, Mungu akawaangalia."*

Wana wa Israeli walikuwa watumwa kwa muda mrefu sana. Waliteswa sana sana! Lakini Mungu hakuwasahau. Alikusudi kuponyesha watu wa Israeli toka utumwa wao. Labda unataka kuuliza: Kwa sababu gani Mungu alikusudi kufungua Waisraeli toka utawala wa Farao? Kwa sababu walikuwa watu wazuri kupita wengine? Sivyo! Waisraeli walikuwa wenye zambi, kama Wamisri, na watu wote wengine. **Basi kwa nini Mungu alikuwa na mashau-**

**ri namna hii kwa wana wa Israeli?** Kwa sababu ya **uaminifu na rehema** yake tu. Tuangalie tena mashairi ya mwisho tuliyosoma. Tulisoma: *"Mungu akasikia kuugua kwao,* ***Mungu akakumbuka agano lake*** *na Abrahamu na Isaka na Yakobo* **(Ona *uaminifu* wa Mungu!).** *Mungu akaona wana wa Israeli,* ***Mungu akawaangalia*** **(Ona *rehema* ya Mungu!)**. (Kutoka 2:24,25)

Ndiyo, Mungu mwaminifu na mwenye rehema, alikumbuka agano lake alilofanya na Abrahamu wakati aliposema naye,

> ***"Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, ... nawe uwe baraka ... na ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa."*** (Mwanzo 12:2,3) *"Uzao wako utakuwa mgeni kwa inchi isiyo yake, na watatumikia watu wale, nao watawatesa kwa miaka mia ine; na vilevile nitahukumu taifa ambao watawatumikia; na nyuma watatoka na mali nyingi."* (Mwanzo 15:13,14)

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaona namna Mungu alivyotokea kwa Musa kwa njia ya ajabu na kumwita kwenda Misri kuponyesha Waisraeli toka utumwa wao, kama alivyoahidi Abrahamu miaka mingi mbele.

Mungu akubariki wakati unapokaa kufikiri juu ya neno hili toka Zaburi:

> ***"Ee shukuruni Bwana, iteni jina lake; julisheni watu matendo yake. ... Amekumbuka agano lake milele, neno aliloamuru vizazi elfu; agano alilofanya na Abrahamu na kiapo chake na Isaka."*** (Zaburi 105:1,8,9)

SOMO 30

# Musa Anakutana na Mungu

KUTOKA 3,4

Salama iwe kwenu, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea leo na mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele tuliona namna Farao, mfalme wa Misri, alitesa wazao wa Abrahamu, ndio Waisraeli, kwa njia ya kuwafanyiza watumwa na kuwatumikisha sana sana. Lakini, tulisoma vilevile ya kwamba *"kwa kadiri walivyowatesa ndivyo wakazidi kuwa wengi na kuenea."* (Kutoka 1:12) Mwishoni Farao alitoa amri watupe kila mtoto mume Mwisraeli atakayezaliwa ndani ya mto azame.

Lakini, Mungu aliye mwenye uwezo kupita Shetani, alikuwa na shauri kuharibu mabaya ambayo Farao alikuwa akifanya. Hivi, tulisoma ya kwamba binti ya Farao alipokea mtoto mchanga wa Waisraeli ambaye alimkuta ndani ya kitunga mtoni. Binti ya Farao alimhurumia na kumpokea kama mtoto wake mwenyewe, akimwita **Musa**. Hivi, Musa alipata nguvu nyumbani mwa Farao—mtu yule aliyetaka sana kuharibu Waisraeli! Mungu, kwa hekima yake alikusudi kutumika na Musa kuponyesha Waisraeli toka mkono wa mfalme yule mwovu. Wakati Musa alipokuwa na miaka makumi ine, alikimbia Farao aliyetaka kumwua. Kwa miaka makumi ine Musa alikaa jangwani, akaoa mke na kulinda kondoo za baba ya mke wake.

Sasa, tuendelee na habari hizi kuona **namna Mungu alivyojifunua kwa Musa** ili aweze kumtuma kwa Farao kuondosha Waisraeli toka Misri. Tunasoma ndani ya Tora, sura ya tatu ya kitabu cha Kutoka, kuanza na shairi 1:

> *Basi, Musa alikuwa akichunga kondoo za Yetoro mkwewe, kuhani wa Midiani; akaongoza kundi nyuma ya jangwa, akakuja kwa mlima wa Mungu, kwa Horebu. **Malaika ya Bwana akaonekana kwake katika ulimi wa moto kati ya kijiti;** akaangalia, na tazama, kijiti kiliwaka kwa moto lakini kijiti hakikuteketea. Musa akasema, nigeuke sasa nione kitu kikubwa hiki kwa nini kijiti hiki hakiteketei.*
>
> *4 Na wakati Bwana alipoona ya kama aligeuka kuona, Mungu akamwita toka kati ya kijiti, akasema: Musa, Musa. Akasema: Mimi ni hapa. Akasema: Usikaribie hapa; ondosha viatu vyako toka miguu yako, maana pahali unaposimama ni **inchi takatifu**. Akasema tena: **Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo**. Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kutazama Mungu. Bwana akasema: **Hakika nimeona teso la watu wangu, walio katika Misri,** na nimesikia kilio chao kwa ajili ya wasimamizi wao wa utumwa; maana ninajua mateso yao; na nimeshuka kuwaponyesha toka mkono wa Wamisri, na kuwapandisha toka inchi ile hata inchi nzuri na kubwa, hata inchi inayojaa maziwa na asali; hata pahali pa Mkanana, na Mhiti, na Mwamori, na Mperezi, na Mhivi, na Myebusi. Na sasa tazama, kilio cha wana wa Israeli kimefika kwangu; na tena nimeona mateso ambayo Wamisri wanawatesa nayo. Basi kuja sasa, na nitakutuma kwa Farao, upate kutoa watu wangu wana wa Israeli toka Misri.*
>
> *11 Musa akamwambia Mungu: Mimi ni nani hata niendee Farao, na nitoe wana wa Israeli toka Misri? Akasema: Hakika nitakuwa pamoja nawe; na hii itakuwa alama kwako ya kama nimekutuma; **wakati utakapokwisha kutoa watu toka Misri, mutatumikia Mungu juu ya mlima huu.** Musa akamwambia Mungu: Tazama, wakati ninapokuja kwa wana wa Israeli, na kuwaambia: Mungu wa baba zenu amenituma kwenu; nao wataniambia: Jina lake nani? nitawaambia nini? Mungu akamwambia Musa: **NDIMI NILIYE**; akasema: Utasema hivi na wana wa Israeli: MIMI NIKO ambaye alinituma kwenu. Mungu akasema tena na Musa: Utasema hivi na wana wa Israeli: Bwana, Mungu wa baba zenu, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo amenituma kwenu; **hili ni jina langu hata milele.***

Tunaweza kujifunza **maneno mane** (na zaidi) juu ya jinsi ya Mungu kwa njia ya maneno Mungu aliyosema na Musa toka kijiti kisichoteketea kwa Mlima Sinai.

1) Kwanza, tunajifunza ya kwamba Mungu ni **mtakatifu**! Musa alishangaa kabisa wakati alipoona ndimu za moto toka kijiti kilichowaka. Alikaribia kuangalia neno hili karibu karibu, akasikia sauti ya Mungu akimwita toka kijiti. Musa alitetemeka kwa woga, akaogopa kuangalia. Musa aliogopa kwa sababu gani? Kwa sababu alikuwa akisimama mbele ya Mungu, Mtakatifu! Mungu alitangaza utakatifu wake kwa njia ya kuagiza Musa: *"Usikaribie hapa; ondosha viatu vyako toka miguu yako, maana pahali unaposimama ni inchi takatifu."*

Ndiyo, Mungu aliyetokea kwa Musa ndani ya ndimi za moto ni **mtakatifu** kweli! Mungu anataka kila mtu kutambua utakatifu wake. Juu ya malaika wanaosimama mbele ya Mungu, Maandiko yanasema: *"Hawapumziki mchana wala usiku wakisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwa, naye yuko, na atakayekuja."* (Ufunuo 4:8) Malaika wanatambua utakatifu wa Mungu. Wewe msomaji, wewe unatambua utakatifu wa Mungu?

Tufikiri juu ya maana ya neno hili. Kama tulivyoona ndani ya masomo ya mbele, kwa sababu ya utakatifu wake Mungu alifukuza Adamu na Hawa toka shamba la Paradiso wakati walipokwisha kufanya zambi. Kwa sababu ya utakatifu wake Mungu alikataa sadaka ya Kaina. Na kwa sababu ya utakatifu wake aliharibu watu wa wakati wa Noa na garika. Na nyuma ya wakati ule Mungu alichanganya lugha za watu wa dunia, na kusambaza watu wa Babeli, ndio wale waliojaribu kuasi Mungu. Na kwa wakati wa Abrahamu, Mungu, kwa sababu ya utakatifu wake, alinyesha moto toka mbingu juu ya watu wa Sodomo, wale ambao walijifurahisha na matendo maovu.

Ni huzuni kubwa kuona ya kwamba hata kwa wakati wa sasa zaidi ya watu hawatambui utakatifu wa Mungu. Hawafahamu kama Mungu ni nani. Hawatambui usafi wake wa kutimia. Tunafahamu neno hili wakati tunapoona namna watu wanavyofanya zambi na kufurahi ndani yao. Tunafahamu vilevile ya kwamba watu wanafikiri juu ya utakatifu wa Mungu kama kitu kidogo wakati wanapovaa dini kama joho, lakini hawasomi Maandiko Matakatifu kufahamu kweli ya Mungu. Ni desturi ya watu wengi kutumia jina la Mungu ndani ya masemo yao kama neno bule. Wanaitia jina la Mungu bule kwa njia ya kusema kwa lugha ya Waarabe, *"kwa jina la Mungu"* ["bi ism Allah'] au *"Mungu akitaka"* ["Insha'a Allah"] lakini kabisa kabisa hawakumbuki Mungu hata kidogo ndani ya mawazo

yao. Tunaona vilevile ya kwamba watu hawafahamu utakatifu wa Mungu kwa namna wanavyojaribu kusimamia haki yao wenyewe mbele ya Mungu na kukataa kupokea njia ya haki ambao Mungu alitayarisha. Wengine wanafikiri wanaweza kujitakasa mbele ya Mungu kwa njia ya kufunga chakula kwa muda mrefu, kusema maneno fulani tena na tena ndani ya maombi, au ibada ya dini. Lakini, kama tulivyoona wazi ndani ya Maandiko ya Manabii, matendo namna hii ya kuonekana hayatoshi kwa **Mungu Mtakatifu** anayetaka mtu kuwa safi katika roho. Rafiki: Mungu ni mtakatifu! Kwa sababu hii alisema na Musa, *"ondosha viatu vyako toka miguu yako, maana pahali unaposimama ni **inchi takatifu**."*

2) Halafu maneno Mungu aliyosema kwa Musa toka kijiti kilichowaka, yanaonyesha ya kwamba Mungu si mtakatifu tu lakini **Mungu Mwaminifu**! Yeye ni mwenye kutimiza maagano yake. Ulisikia maneno Mungu aliyosema kwanza kwa Musa? Alisema, *"Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo."* (Kutoka 3:6) Ingepasa maneno haya kufurahisha mtu ye yote anayetaka kukaribia Mungu na kuwa na upatano mzuri naye. Mungu Mtakatifu ndiye aliyesimamisha agano na Abrahamu, Isaka na Yakobo. Mungu ni mwaminifu; hataacha rafiki zake au kuwatoa kwa adui zao kamwe! Hata nyuma ya mia za miaka hakusahau maneno aliyoahidi Abrahamu, Isaka na Yakobo na wazao wao.

Halafu wewe? Unafurahia uaminifu wa Mungu? Unafurahi ndani ya upatano wa karibu na Mungu yule aliyesemezana na Abrahamu, Isaka, na Yakobo? Hili ndilo ulizo kubwa kwa mtu ye yote anayetaka kukaa na furaha ya kweli hapa duniani na ndani ya uzima unaofuata kufa. Hatuulizi: Unashikana na dini? kwani kutii maagizo ya dini hakuwezi kamwe kufanyiza mtu haki mbele ya Mungu. Neno tunalouliza ndilo hili: Una upatano wa kweli na Mungu? Umeamini habari za njia ya wokovu ambayo Mungu alisimamisha? Umefahamu ya kwamba kufuata **dini** na kuwa na **upatano wa kweli** na Mungu ni maneno mbalimbali?

Kwa wakati wa sasa kuna elfu za dini mbalimbali duniani. Kwa mfano, wenye elimu wanatujulisha ya kwamba ndani ya inchi ya Brazil tu, kuna zaidi ya dini elfu ine! Dini elfu ine?? Ajabu kabisa. Labda kuna miungu elfu ine? Au njia mbalimbali elfu ine zinazoweza kufikisha watu kwa Mungu? Sivyo! Maandiko yanasema:

***"Mungu ni mmoja tu, na mpatanishi katikati ya Mungu na watu ni mmoja"*** (1 Timoteo 2:5) Basi kwa sababu gani kuna elfu za dini duniani leo? Ni kwa sababu zaidi ya wazao wa Adamu waliona bule msingi wa kweli Mungu aliosimamisha na Abrahamu, Isaka, na Yakobo. Hawajui habari za ahadi ambazo Mungu alitolea Abrahamu na wazao wake juu ya Mkombozi atakayekuja duniani kuokoa wana wa Adamu toka azabu na uwezo wa zambi. Hawajui Neno la Mungu asiyegeuka kamwe. Hawamjui **Yule Mwaminifu**!

3) Mungu alijifunua kwa njia nyingine vilevile wakati alipotokea Musa katika moto uliowaka ndani ya kijiti. Alijifunua kama mwenye **rehema**. Mungu si mtakatifu na mwaminifu tu, lakini yeye ni **Mwenye Rehema** vilevile. Kwa sababu hii Mungu alisema na Musa juu ya watu wa Israeli,

> *"Hakika nime**ona** teso la watu wangu walio katika Misri, na nime**sikia** kilio chao kwa ajili ya wasimamizi wao wa utumwa; maana nina**jua** mateso yao; na nime**shuka** kuwaponyesha toka mkono wa Wamisri; na kuwapandisha toka inchi ile hata inchi nzuri na kubwa ."* (Kutoka 3:7,8)

Kwa nini Mungu alikusudi kufungua Waisraeli na kuwafikisha kwa inchi njema? Waisraeli walistahili rehema ya Mungu? Walikuwa wazuri kupita watu wa mataifa mengine? Sivyo, hata kidogo! Kwa sababu gani basi Mungu alikusudi kuwaponyesha na kuwabariki hivi? Kwa sababu ya uaminifu na rehema yake tu. Kama Maandiko yanavyosema: *"Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake na Abrahamu na Isaka na Yakobo. Mungu akaona wana wa Israeli, Mungu akawaangalia."* (Kutoka 2:24,25) Ndiyo, Mungu ni **Mwenye Rehema**!

4) Mwishoni, tunajifunza neno moja lingine juu ya Mungu kwa njia ya habari za kuteketezwa kwa kijiti. Tulisikia Musa akiuliza Mungu kama jina lake ni nani. Itawezekana kweli kuonyesha maneno yote juu ya Mungu kwa njia ya jina *moja*? Mungu huyu aliye mkubwa na mtakatifu, mwaminifu na mwenye rehema; Mungu huyu ambaye watu hawawezi kuona na macho; Mungu huyu aliyeumba vitu vyote, anayeona vitu vyote, anayejua maneno yote, na anayeweza kufanya maneno yote — **jina lake nani?** Watu wengine wanafikiri jina la Mungu ni *"Mungu" {Allah}* tu. Ndiyo, ni kweli, Mungu ni Mungu. Lakini Mungu si **jina** lake. Mungu ndiye

aliye. Mimi ni mtu, lakini *Mtu* si jina langu. Sisi sote tuna jina na watu wanatujua kwa jina hili. Jina la Mungu ni nani? Mungu alijibu Musa nini? Tusome jibu lake tena. Mungu alisema na Musa,

> *"**NDIMI NILIYE**; akasema: Utasema hivi na wana wa Israeli: **MIMI NIKO** ambaye alinituma kwenu. Mungu akasema tena na Musa: Utasema hivi na wana wa Israeli: **BWANA**, Mungu wa baba zenu, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo amenituma kwenu; **hili ni jina langu hata milele**."* (Kutoka 3:14,15)

Nani ndilo jina la Mungu ambalo linatufikirisha namna yake ya milele? Ulilisikia? Ni **BWANA**! Ndani ya Maandiko Matakatifu manabii wanaita Mungu na mia za majina mbalimbali, lakini aliitwa na jina hili, *BWANA*, kupita yote mengine — kupita elfu sita mia tano (6500). Mungu ni BWANA, "NDIMI," yule aliyekuwa, aliye, na atakayekuwa kwa milele! Yeye ni wa milele! Hana mwanzo, hana mwisho. Hakuna mwingine aliye sawasawa naye. Yeye ndiye kwa uwezo wake mwenyewe! Atakuwa kwa milele namna alivyokuwa jana, na namna alivyo leo. Habadiliki kamwe. BWANA ni jina lake!

Rafiki, unajua **BWANA**? Unatambua **utakatifu** wake? Unafurahia **uaminifu** wake (kwa namna anavyochunga upatano wake na maagano yake)? Umepokea **rehema** yake? Unaamini Neno lake? Una upatano wa karibu na Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo? Unajua BWANA aliyesema na Musa toka kijiti kilichowaka kwa moto?

~~~~~~~~~~~~~~~~

Tutaendelea na habari za Musa ndani ya somo la nyuma na kuona namna Mungu alivyomtuma kwa Farao, yule mfalme mwovu wa Misri . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya maneno haya Musa aliyosema na Musa:

> ***"MIMI NDIYE! . . . MIMI NIKO Bwana . . . hili ndilo jina langu kwa milele!"*** (Kutoka 3:14,15; 6:2)
~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 31

# ULIZO LA FARAO: BWANA NI NANI?

## KUTOKA 4-7

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Leo tunaendelea ndani ya kitabu cha pili cha Tora, ndicho Kutoka, ambacho kinatupasha habari za **nabii wa Mungu, ndiye Musa, na watu wa Israeli katika Misri**. Ndani ya masomo ya mbele, tuliona namna Farao, mfalme wa Misri, alivyotesa Waisraeli, na kuwafanyiza watumwa wake. Lakini Mungu alikuwa na shauri lake tayari kuharibu maovu ambayo Farao alitenda. Mungu alikusudi kutumika na Musa, Mwisraeli, kuokoa Waisraeli toka mkono wa Farao.

Tulijifunza ya kwamba Musa alifundishwa maarifa yote ya Misri. Wakati Musa alipokuwa na miaka makumi ine, alijaribu kuponyesha watu wake Waisraeli kwa akili yake mwenyewe, lakini neno hili lilizaa matata tu na ilipasa Musa kukimbia Farao na kujificha jangwani. Ilikuwa lazima kwa Musa kujifunza ya kwamba yeye ni mtu tu na hakuwa na uwezo kuponyesha Waisraeli bila uwezo toka Mungu. Hivi Musa alikaa jangwani kwa miaka makumi ine, akichunga kundi la baba wa mke wake.

Siku moja, **wakati Musa alipokuwa na miaka makumi manane, Mungu alitokea kwake juu ya mlima aliyeitwa Sinai**, ndani ya ndimi za moto za kijiti kilichokuwa kikiwaka. Kijiti kiliwaka kwa moto lakini hakikuteketezwa. Wakati Musa alipoona neno hili, alishangaa. Wakati alipokaribia kutafuta neno hili, alisikia sauti ya Mungu akisema, *"Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu,*

*Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo." Musa alitetemeka na woga, aka-ogopa kuangalia. Halafu Mungu alisema, "Usikaribie hapa; ondosha viatu vyako toka miguu yako, maana pahali unaposimama ni inchi takatifu. Nimeona teso la watu wangu walio katika Misri, na nimesikia kilio chao kwa ajili ya wasimamizi wao wa utumwa. Hivi nimekuja kuwaponyesha na* ***nitakutuma wewe kwa Misri."***

Halafu sasa tuendelee kusoma ndani ya Tora kuona namna Mungu alivyomaliza mazungumzo yake na Musa na kumtuma kwa mfalme wa Misri. Ndani ya sura 3 tulisoma ya kwamba Mungu ali-ahidi kuwa pamoja na Musa, kumpa akili na amri mbele ya Farao na watu wa Misri. Ndani ya sura 4 tutaona ya kuwa hata hivi Musa ali-ogopa kwenda.

Ndani ya kitabu cha Kutoka sura 4 na kuanza na shairi 1 Maandiko yanasema:

> (Kutoka 4) *Musa akajibu, akasema: Lakini tazama, hawataniamini, wala hawatasikia sauti yangu; kwa sababu watasema: Bwana hakuonekana kwako. 2 Bwana akamwambia:* ***Nini ile mkononi mwako?*** *Akasema: Fimbo. 3 Akasema: Uitupe chini. Akaitupa chini na iligeuka kuwa nyoka; Musa akakimbia mbele yake. 4 Bwana akamwambia Musa: Nyosha mkono wako uishike kwa mkia (akanyosha mkono wake, akaishika, ikageuka kuwa fimbo mkononi mwake), 5* ***wapate kuamini ya kama Bwana, Mungu wa baba zao, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo ameonekana kwako."***
>
> *10 "Musa akamwambia Bwana: Ee Bwana, mimi si msemaji, wala zamani wala tangu uliposema na mtumishi wako; kwa maana mimi ni polepole kwa kusema, na mwenye ulimi mzito. 11 Bwana akamwambia:* ***Ni nani aliyeumba kinywa cha mtu?*** *au nani anayefanya mtu bubu, au kiziwi, au mwenye kuona, na kipofu? si mimi Bwana? 12 Kwenda basi sasa, na nitakuwa pamoja na kinywa chako na kukufundisha utakayosema. 13 Akasema: Ee Bwana, tuma, ninakuomba, kwa mkono wake ambaye utamtuma. 14 Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Musa, akasema:* ***Haruni*** *ndugu yako si Mlawi? Ninajua anaweza kusema vizuri. Na vilevile tazama, ametoka kukutana nawe, na wakati atakapokuona, atafurahi moyoni mwake. 15 Na utamwambia na kutia maneno kinywani mwake,* ***nami nitakuwa pamoja na kinywa chako, na kinywa chake, na***

> ***nitawafundisha ninyi ambayo mutayafanya.*** *. . 17 Na utashika fimbo hii utakayofanya alama nayo mkononi mwako.*
>
> *18 "Musa akakwenda, akarudi kwa Yetoro, mkwewe, akamwambia: Uniruhusu, ninakuomba, niende na kurudi kwa ndugu zangu walio katika Misri, nione kama wangali wakiishi. Yetoro akamwambia Musa: Kwenda kwa salama. 19 Bwana akamwambia Musa katika Midiani: Kwenda, na rudi kwa Misri; kwa kuwa watu wote waliotafuta uzima wako wamekufa. 20 Musa akatwaa mke wake na wana wake, akawapandisha juu ya punda,* ***akarudi kwa inchi ya Misri;*** *Musa akatwaa fimbo ya Mungu mkononi mwake. 21 Bwana akamwambia Musa: Wakati utakaporudi kwa Misri, uangalie na kufanya mbele ya Farao maajabu yote niliyotia mkononi mwako . . . 22 Na utamwambia Farao: Bwana anasema hivi: Israeli ni mwana wangu, mzaliwa wangu wa kwanza; 23 na nimekuambia: Acha mwana wangu kwenda anitumikie.*
>
> *27 Bwana akamwambia Haruni: Kwenda jangwani kukutana na Musa. Akakwenda, akakutana naye kwa mlima wa Mungu, akambusu. 28 Musa akamwambia Haruni maneno yote ya Bwana ambayo alimtuma nayo, na alama zote ambazo alimwagiza. 29* ***Musa na Haruni wakakwenda, wakakusanya wazee wote wa wana wa Israeli;*** *30 Haruni akasema maneno yote ambayo Bwana alimwambia Musa, akafanya alama mbele ya watu. 31 Watu wakaamini;* ***na wakati waliposikia ya kama Bwana ameangalia wana wa Israeli, na ya kama ameona mateso yao, halafu wakainama vichwa vyao, wakaabudu.***
>
> (Kutoka 5:1,2) *Basi nyuma Musa na Haruni walikuja, wakamwambia Farao; Bwana Mungu wa Israeli anasema hivi:* ***Ruhusu watu wangu waende*** *na kunifanyia siku kubwa jangwani. Farao akasema:* ***Bwana ni nani****, nisikie sauti yake na kuruhusu Israeli waende?* ***Sijui Bwana, na vilevile sitaruhusu Israeli kwenda!***

Tuache kwanza pale. Tunaona namna Mungu alivyosema kwa Farao kwa njia ya kinywa cha Musa na cha Haruni. Farao aliamini neno la Mungu? Sivyo! Uliona namna alivyojibu Musa na Haruni? Alisema, *"**Bwana ni nani,** nisikie sauti yake na kuruhusu Waisraeli waende? Sijui Bwana, na vilevile sitaruhusu Israeli kwenda!"*

Farao hakujua Bwana, yule aliye tangu milele. Yeye na watu wote wa Misri **walishikana na dini**, lakini **hawakujua Mungu**.

Waliweka roho juu ya kutembea katika dini ya wazazi wao. Hawakufikili ni neno kubwa kujua Mungu aliye hai, Mungu wa kweli—Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo. Farao na Wamisri walitumainia desturi zao, sanamu zao, hirizi zao na viongozi vyao kwa maneno ya dini, lakini **hawa**kutumainia **Bwana na Neno lake la milele.**

Hivi, ndani ya Kutoka 6, kuanza na shairi 1 tunasoma:

> *"Bwana akamwambia Musa: **Utaona sasa nitakayotendea Farao**; kwa maana kwa mkono wa nguvu atawaacha kwenda na kwa mkono wa nguvu atawafukuza toka inchi yake.*
>
> *2 Na Mungu alisema na Musa, akamwambia: **Mimi ni YEHOVA**; 3 nami nilionekana kwa Abrahamu, kwa Isaka na kwa Yakobo, kama Mungu Mwenyezi, lakini sikujulikana kwao kwa jina langu YEHOVA. 4 Na nimesimamisha agano langu pamoja nao, kuwapa inchi ya Kanana, inchi ya kusafiri kwao, pahali waliposafiri. 5 Na tena nimesikia kuugua kwa wana wa Israeli, ambao Wamisri wanawatumikisha kwa utumwa; na nimekumbuka agano langu. 6 Kwa hivi ambia wana wa Israeli: **Mimi ni Bwana**, na nitawatoa ninyi, toka inchi ya mizigo ya Wamisri, na nitawaondosha ninyi katika utumwa wao, na nitawakomboa ninyi na mkono ulionyoshwa, na kwa hukumu zilizo kubwa; 7 nami nitawatwaa ninyi kwangu kuwa watu wangu, na nitakuwa Mungu kwenu; na mutajua ya kama **mimi ni Bwana** Mungu kwenu ambaye anawatoa ninyi toka chini ya mizigo ya Wamisri. Nami nitawaleta ninyi kwa inchi niliyonyanyua mkono wangu juu yake kuwapa Abrahamu na Isaka na Yakobo; na nitawapa ninyi iwe uriti wenu; **Mimi ni Bwana.**"*
>
> (Kutoka 7) *4 Lakini **Farao hatawasikia ninyi**, nami nitaweka mkono wangu juu ya Misri na kutoa majeshi yangu, watu wangu wana wa Israeli, toka inchi ya Misri kwa hukumu zilizo kubwa. 5 Na Wamisri watajua ya kama **mimi ni Bwana** wakati nitakaponyosha mkono wangu juu ya Misri, na kutoa wana wa Israeli kati yao. 6 Musa na Haruni wakafanya hivi; kama Bwana alivyowaagiza, ndivyo walivyofanya. 7 Na Musa alikuwa na miaka makumi manane, na Haruni alikuwa na miaka makumi manane na mitatu wakati waliposema na Farao.*

Hivi tunaona ya kwamba Bwana alikuwa na shauri kuhukumu Farao na watu wa Misri kwa njia ya matendo ya uwezo wa hukumu. Mungu mwenye haki alikusudi kulipiza Wamisri kwa mia za miaka

waliyotesa Waisraeli. Na vilevile, kwa njia ya maajabu Mungu aliyokusudi kutenda kwa mkono wa Musa, Bwana alitaka kuonyesha utukufu na uwezo wake wazi. Hivi, ataonyeshea watu wa Misri na dunia nzima, ya kwamba **Bwana Mungu aliyesema na Abrahamu, Isaka, Yakobo na Musa ni Mungu hai na Mungu wa kweli!**

Kama tulivyojifunza mbele, Mungu ni mwenye rehema naye hataki mtu ye yote kupotea, lakini anataka kila mtu kutubu na kujua na kupokea kweli. Kwa sababu hii alikusudi kufanya maajabu yatakayohakikisha neno alilosema kwa njia ya Musa. Bwana alitaka watu wote kujua **bila shaka** ya kwamba Mungu yule aliyesema kwa njia ya Musa ni **Mungu wa pekee wa kweli!**

Sharti tukumbuke ya kwamba katika Misri kulikuwa na mia za sanamu ambazo Wamisri walifikili ni miungu. Lakini Mungu alitaka wajue ya kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli tu. Mungu alitaka wajue ya kwamba **Mungu mmoja wa kweli ni Mungu aliyesimamisha agano lake na Abrahamu, Isaka na Yakobo**—akiahidi kuwafanyiza taifa kwa njia yake Mungu atawapa dunia manabii, Maandiko, na Mwokozi.

Lakini Farao hakutaka kujua Mungu mmoja wa kweli. Kwa sababu hii, wakati Mungu alipojaribu kusema na Farao kwa njia ya manabii yake, Musa na Haruni, Farao aliwajibu akisema, ***"Bwana ni nani,*** *nisikie sauti yake na kuruhusu Israeli waende? Sijui Bwana, na vilevile sitaruhusu Israeli kwenda"* (Kutoka 5:2)

Farao alisema kweli wakati aliposema hajui Bwana! Hakujua Mungu yule aliyesimamisha agano la milele na Abrahamu, Isaka na Yakobo. Farao alikuwa na **dini**, lakini hakuwa na **upatano** na Mungu. Alifunga roho yake asipokee kweli inayotoka kwa Mungu mmoja wa kweli. Hivi aliona bule maneno Mungu aliyosema naye kwa njia ya Musa na Haruni.

Kufika leo, zaidi ya watu wa dunia wanatembea katika njia ya Farao. Wanasema juu ya Mungu, lakini hawaweki roho juu ya Neno la Bwana. Hivi, **hawajui Mungu**. Wanajua habari nyingine **juu ya Mungu**, lakini hawajui **Mungu mwenyewe**. Wana **dini** waliyopokea toka wazazi wao, lakini hawana **upatano** wa kweli na Mungu aliye hai na ambaye alijifunua kwa Musa.

Na wewe? **Unajua Bwana**? Unajua kweli maneno aliyosema kwa njia ya manabii wake? Umesoma Maandiko ya manabii wa Mungu

na roho ya kweli? Unajua Bwana Mungu kweli kweli? Unampenda na roho yako yote? Una hamu kumtii? Au wewe ni kama Farao, ukifuata tu dini ya wazazi wako?

Eh rafiki wapenzi, hata mmoja wetu asiwe kama Farao aliyekataa kusikiliza na kuamini Neno la Mungu wa milele! Musikilize maonyo haya toka Neno la Mungu: ***"Angalieni, ndugu zangu, asiwe katikati yenu mmoja mwenye moyo mbaya wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai."*** (Waebrania 3:12) Leo, kama ukisikia sauti yake, usifanyize mioyo yenu migumu kama Farao alivyofanya aliyesema, *"Bwana ni nani, nisikie sauti yake?"*

~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kusoma na kujifunza. Mungu akitaka, tutaendelea na habari hizi kwa somo la nyuma na kuona namna Mungu alivyoleta juu ya Farao na Wamisri mapigo kumi ili waweze kujua ya kwamba Yeye ni BWANA!

Mungu awabariki ninyi wakati munapotii maonyo haya toka Neno lake takatifu:

> ***"Leo, kama mukisikia sauti yake, musifanye migumu mioyo yenu!"*** (Waebrania 3:15)
~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 32

# HUKUMU KUMI

### KUTOKA 7-10

Salama iwe kwako kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka ufahamu, kuamini na kupokea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

**"Haifai yayi kushindana na jiwe!"** Mezali hii ya Wawolof, kabila la Senegal inajumlisha maneno tutakayojifunza leo ndani ya Maandiko Matakatifu. Nini inatokea wakati yayi na jiwe yanapogongana? Yayi linavunjika; jiwe haligeuki. Leo tutaona nini ilitokea wakati Farao, mfalme wa Misri, alipojaribu kushindana na Bwana Mungu juu yake nabii Musa aliandika, "*Yeye ni **Mwamba**, kazi yake ni kamilifu; maana njia zake zote ni kamilifu*" (Torati 32:4).

Ndani ya somo la mbele tuliona namna Mungu alivyotuma Musa na Haruni kwa Farao kufungua wana wa Israeli toka utumwa katika Misri. Walisema na Farao: "Bwana, Mungu wa Israeli anasema, 'Ruhusu watu wangu waende na kunifanyia siku kubwa jangwani!'" Lakini, Farao aliwajibu: *"Bwana ni nani, nisikie sauti yake na kuruhusu Israeli waende? Sijui Bwana, na vilevile sitaruhusu Israeli kwenda!"* (Kutoka 5:2) Mungu alikuwa amekusudi kufungua Waisraeli, lakini Farao aliweka roho kabisa juu ya kubaki nao kama watumwa wake. Lakini, "haifai yayi kushindana na jiwe!"

Turudi sasa kwa kitabu cha Kutoka, sura 7, kuona namna Farao alivyojaribu "kushindana" na Mungu. Maandiko yanasema:

> (Kutoka 7:10-12) *Musa na Haruni wakaingia kwa Farao, wakafanya kama Bwana alivyoagiza. Haruni akatupa fimbo yake chini mbele ya Farao, na mbele ya watumishi wake, na iligeuka nyoka. Halafu Farao akaita waakili na wafumu; wao vilevile, wachawi wa Misri, wakafanya hivi kwa uchawi wao. Maana wakatupa chini kila mtu*

> *fimbo yake, zikageuka kuwa nyoka; lakini fimbo ya Haruni ikameza fimbo zao.*

Ona mwanzo wa mashindano katikati ya **Farao na Mungu**. Tunaona kwa ngambo moja Farao na waakili na wachawi wake. Kwa ngambo nyingine tunaona **Musa na Haruni.** Wakati kwa njia ya ajabu fimbo ya Haruni ilipogeuka nyoka, wachawi wa Farao waliiga ajabu hili. *"Maana wakatupa chini kila mtu fimbo yake, zikageuka kuwa nyoka;* ***lakini fimbo ya Haruni ikameza fimbo zao."***

Tunaweza kusema nini juu ya habari hizi? Tunajua ya kwamba maajabu ambayo Musa na Haruni walifanya yalitoka **kwa Mungu** tu. Lakini wachawi wa Farao walifanya maajabu vilevile. Uwezo kwa kufanya maajabu haya ulitoka wapi? Walipata uwezo huu kwa Mungu? Sivyo! Mungu hashindani na yeye mwenyewe. Kama ni hivi, uwezo wao ulitoka wapi? Wachawi wa Farao walitegemea udanganyifu na uwezo unaotoka **kwa Shetani.**

Maandiko Matakatifu yanatujulisha ya kwamba Shetani ni mwenye hila sana na anapenda kudanganya watu; ana uwezo mkubwa vilevile hata anaweza kufanya maajabu. Lakini tunajua kabisa ya kwamba Mungu ana uwezo kupita Shetani. Hivi, fimbo ya Haruni ilimeza fimbo zote za wachawi wa Farao. Lakini maneno haya yote hayakutosha kufanyiza Farao kutubu na kusikia neno la Mungu.

Sikiliza Maandiko tena:

> (Kutoka 7) *14 Bwana akamwambia Musa: Moyo wa Farao ni mzito, anakataa kuruhusu watu kwenda zao. 15 Kwenda kwa Farao asubui: tazama anatoka kwa maji; na utasimama kwa ukingo wa mto kukutana naye, na fimbo iliyogeuzwa kuwa nyoka utaitwaa mkononi mwako. 16 Utamwambia: Bwana Mungu wa Waebrania, amenituma kwako akisema: Acha watu wangu waende, wapate kunitumikia jangwani; na tazama, hata sasa hukusikia. 17 Bwana anasema hivi:* ***Kwa neno hili utajua ya kama mimi ni Bwana;*** *tazama, nitapiga juu ya maji yaliyo ndani ya mto na fimbo iliyo mkononi mwangu, nayo yatageuzwa kuwa damu. . . 20 Musa na Haruni walifanya kama Bwana alivyoagiza; akanyanyua fimbo, akapiga maji yaliyokuwa mtoni mbele ya macho ya Farao na mbele ya macho ya watumishi wake; na* ***maji yote yaliyokuwa mtoni yakageuzwa kuwa damu****. Na samaki waliokuwa katika mto wakakufa; mto ukanuka, wala Wamisri hawakuweza kunywa maji ya mto; damu ikakuwa katika inchi yote ya Misri. 22* ***Wachawi wa Misri wakafanya hivi***

> ***vilevile kwa uchawi*** *wao; moyo wa Farao ukakuwa mgumu, wala hakuwasikia, kama Bwana alivyosema., 23 Farao akageuka, akaingia nyumbani mwake, wala hakufikili hata maneno haya moyoni. 24 Wamisri wote wakachimba karibu na mto wapate maji kunywa; maana hawakuweza kunywa maji ya mto. 25 Siku saba zikatimia, nyuma ya Bwana kupiga mto. 8:1 "Bwana akamwambia Musa: Ingia kwa Farao umwambie: Bwana anasema hivi: Ruhusu watu wangu waende, wanitumikie. 2 Na kama ukikataa kuwaruhusu kwenda, tazama, nitapiga mipaka yako yote na vyula, 3 na mto utajaa vyula, watakaopanda na kuingia nyumbani mwako, na chumbani mwako wa kulala; na juu ya kitanda chako, na nyumbani mwa watumishi wako, na juu ya watu wako, na ndani ya meko yako ...*

Lakini Farao hakusikiliza maonyo toka Musa. Tusome tena toka Kutoka 8:

> *5 Bwana akamwambia Musa: Sema na Haruni: Nyosha mkono wako na fimbo yako juu ya mito, juu ya vijito, na juu ya mashimo, upandishe vyula juu ya inchi ya Misri. 6 Haruni akanyosha mkono wake juu ya maji ya Misri;* ***vyula wakapanda, wakafunika inchi ya Misri. 7 Wachawi wakafanya hivi vilevile kwa uchawi wao, wakapandisha vyula juu ya inchi ya Misri.*** *8 Halafu Farao akaita Musa na Haruni, akasema: Ombeni Bwana aniondoshee vyula, mimi na watu wangu; na nitaacha watu kwenda wapate kutolea Bwana zabihu. . . . 12 Musa akalia kwa Bwana, kwa sababu ya vyula alivyoleta juu ya Farao . . . vyula wakakufa . . . 14 Wakawaokota kwa mafungu; inchi ikanuka. 15 Lakini wakati Farao alipoona ya kama pumziko lilikuwa,* ***akafanya moyo wake mgumu,*** *wala hakuwasikia; kama Bwana alivyosema.*
>
> *16 Bwana akamwambia Musa: Sema na Haruni: Nyosha fimbo yako na piga mavumbi ya inchi, yawe chawa katika inchi nzima ya Misri. 17 Wakafanya hivi; Haruni akanyosha mkono wake na fimbo yake, akapiga mavumbi ya inchi, na* ***chawa walikuwa juu ya mtu, na juu ya nyama,*** *mavumbi yote ya inchi yakakuwa chawa katika inchi nzima ya Misri. 18* ***Wachawi wakafanya hivi kwa uchawi wao kuleta chawa, lakini hawakuweza;*** *chawa walikuwa juu ya mtu, na juu ya nyama. 19 Halafu wachawi wakamwambia Farao: Hiki ni kidole cha Mungu;* ***na moyo wa Farao ulikuwa mgumu*** *wala hakuwasikia; kama Bwana alivyosema.*

Uliona habari za wachawi wa Farao? Tuliona mbele ya kwamba walikuwa na uwezo toka Shetani. Kwa sababu hii waliweza kuiga uwezo wa Mungu na kugeuza nusu ya maji kuwa damu na kufanyiza nusu ya vyula kutokea. (Basi Wamisri walihitaji damu nyingine ndani ya maji yao na vyula ndani ya vitanda vyao kweli?) Ndiyo, walikuwa na uwezo, lakini **ulikuwa uwezo nusu tu.** Wachawi wa Farao hawakuweza kuondosha mapigo ambayo Mwenyezi Mungu alikuwa ameleta juu ya inchi ya Misri. Wakati Haruni alipopiga udongo na fimbo yake na mavumbi yalipogeuka chawa, wachawi walijaribu kugeuza mavumbi kuwa chawa vilevile, lakini walishindwa. Hivi walimwambia Farao, ***"Hiki ni kidole cha Mungu!"***

Ni wazi ya kwamba wachawi walikuwa na uwezo nusu tu. Ndiyo, Shetani ana uwezo na anaweza kutolea watu uwezo vilevile, lakini anaweza kufanya hivi kwa kipimo Mungu alichoamuru tu. Mungu peke yake ni mwenye uwezo wote. Hakuna mipaka kwake! Wachawi wa Farao walianza kujifunza juu ya ukubwa bila kipimo wala mpaka wa Mungu, lakini **Farao alikaa kukataa kunyenyekea** Mungu. Farao alikaa kufanyiza moyo wake mgumu na kufikili ya kwamba ataweza kushindana na Mungu na kushinda!

Hivi Maandiko yanapasha ya kwamba Mungu alileta juu ya Farao na juu ya inchi ya Misri mapigo saba mengine. Kwa **pigo la ine mawingu ya mainzi** yalijaza inchi, hata nyumba za watu, na kuleta uharibifu mkubwa. Kwa sababu ya **pigo la tano ugonjwa mbaya ulipata makundi ya ngombe na kondoo**, na wengi wao walikufa. Lakini hakuna nyama hata mmoja ya makundi ya wana wa Israeli aliyekufa. Hata hivi Farao alifanyiza moyo wake mgumu na alikataa kuruhusu Waisraeli kwenda. Nyuma yake watu na nyama walipatwa na **majipu** mabaya sana. Maandiko yanasema: *"Wala wachawi hawakuweza kusimama mbele ya Musa kwa ajili ya majipu, yaliyokuwa juu ya wachawi, na juu ya Wamisri wote."* (Kutoka 9:11) Kwa **pigo la saba mvua ya mawe**, nzito sana, kama isivyokuwa katika Misri tangu zamani, ilinyesha na kuharibu vyakula ndani ya mashamba. Nyuma ya mvua ile, inchi ilijazwa na **nzige,** zilizokula vyakula nusu vilivyobaki nyuma ya mvua ya mawe. Hili lilikuwa **pigo la nane.**

Ndani ya **pigo la tisa**, Mungu alisema na Musa, *"Nyosha mkono wako mbinguni; giza liwe juu ya inchi ya Misri, hata giza la kugusa."* (Kutoka 10:21) Hivi, kwa siku tatu hakuna mtu aliyeweza kuona

kitu. Lakini pahali Waisraeli walipokaa, kulikuwa na nuru. Hata moja la mapigo haya halikuwagusa. Lakini maneno haya yote hayakusukuma Farao kutubu na kuruhusu Waisraeli kwenda. Maandiko yanasema: *"Farao akamwambia: Toka kwangu, ujiangalie, usione uso wangu tena; kwa sababu siku utakapoona uso wangu utakufa."* (Kutoka 10:28)

Mungu alileta **pigo moja lingine** juu ya Farao na Wamisri, lakini tutangoja somo la nyuma kusema juu yake, kwani saa yetu kwa leo ni karibu kwisha.

Tunaweza kujumlisha somo la leo namna gani? Farao alijaribu kushindana na Bwana Mungu. Farao na wachawi wake waliweza kushinda Mungu Mwenyezi? Walikuwa na uwezo kupita yeye? Sivyo! Hakuna mtu anayeweza kushindana na Mungu na kumshinda! Yayi halipigani na jiwe na kushinda!

Mungu anataka kusema nini nasi kwa njia ya maneno tuliyosoma leo? Maandiko yanasema: *"Maneno haya yote yaliwapata kama **mifano**, yakaandikwa kutu**onya** sisi."* (1 Wakorinto 10:11) Mungu anataka kutuonya. Anataka tutafute hali ya roho zetu na kupokea na kunyenyekea maonyo yake.

Wewe unayesikiliza leo, **unaweka roho juu ya Neno la Mungu?** Unalitii? Au, kama Farao, unashindana na Mungu? Roho yako mwenyewe itakujulisha jibu kwa ulizo hili. Unanyenyekea Neno la Mungu? Unafungana na desturi na dini ya wazazi wako au umepokea na unyenyekevu Neno la Bwana Mungu? Unajaribu kushindana na Mungu?

"Haifai yayi kushindana na mwamba!" **Mtu** ni ***zaifu kama yayi*** linalovunjika nyepesi, na **Neno la Mungu** ni kama **mwamba wa nguvu**. Maandiko yanasema: "Miili yote ni kama majani, na utukufu wao wote kama ua la majani. Majani yanakauka, na ua lake linaanguka; lakini ***Neno la Bwana linadumu kwa milele!"*** (1 Petro 1:24,25) Neno la Mungu wa Milele ni kama Mwamba ulio imara, na kila mtu anayejenga maisha yake juu ya Mwamba huu amechagua msingi wa nguvu kwa maisha yake. Lakini, kama ukikataa kujenga maisha yako juu ya mwamba ule—siku nyingine mwamba wa Neno la Mungu litakuangukia na kukuvunja. Haiwezekani kwa yayi kupigana na mwamba na kushinda. Vivyo hivyo haiwezekani kwa mtu kushindana na Neno la uzima la Mungu bila kuazibiwa.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Inatupasa kuacha hapa kwa leo. Asante kwa kusoma pamoja nasi. Mungu akitaka, ndani ya somo letu la nyuma, tutaona nini Bwana alifanya kufanyiza Farao kuruhusu Waisraeli kuondokea Misri ...

Mungu akubariki wakati unapofikili juu ya maneno nabii Musa aliyoandika ndani ya Tora:

> ***"BWANA Mungu ni Mwamba, kazi yake ni kamilifu; maana njia zake zote ni hukumu; Mungu mwaminifu asiye na uovu, yeye ndiye mwenye haki na adili."*** (Torati 32:4)

## Somo 33

# Mwana-Kondoo ya Pasaka

## (Kutoka 11,12)

Salama iwe kwako. Tunakusalimu kwa jina la Mungu wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea leo na somo lingine la *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele, tuliona namna Farao alivyojaribu kupigana na Mungu. Lilikuwa kusudi la Mungu kuponyesha Waisraeli waliokuwa watumwa katika Misri, lakini mfalme wa Misri aliweka roho sana juu ya kubaki nao kama watumwa wake. Lakini "haifai yayi kushindana na mwamba!" (mezali ya Wawolof, kabila kwa Senegal.) Hivi tuliona ya kwamba Mungu alileta **mapigo tisa** ya kuogofya juu ya Misri kwa agizo la Musa na Haruni. Lakini maalama na maajabu haya yote hayakusukuma Farao kunyenyekea neno la Mungu na kuruhusu Waisraeli kuondokea inchi yake.

Leo tunakusudi kuendelea na habari hizi na tutaona ya kwamba Mungu alileta pigo moja lingine, la kumi na **la mwisho** juu ya Farao kusudi Farao aruhusu Waisraeli kuondokea Misri. Ndani ya somo la mbele, tulisikia Farao akisema na Musa nyuma ya pigo la tisa, *"Toka kwangu, ujiangalie usione uso wangu tena; kwa sababu siku utakapoona uso wangu utakufa."* (Kutoka 10:28) Sasa tusome ndani ya sura 11 na kusikia namna Mungu yeye mwenyewe alivyojibu Farao, kwa njia ya kinywa cha Musa.

Maandiko yanasema:

> (Kutoka 11) *4 Musa akasema: Bwana anasema hivi: Karibu na saa sita ya usiku nitatoka nipite kati ya Misri; 5* ***na wazaliwa wa kwanza wote katika inchi ya Misri watakufa,*** *toka mzaliwa wa*

> *kwanza wa Farao anayekaa juu ya kiti chake cha ufalme, hata mzaliwa wa kwanza wa kijakazi aliye nyuma ya mawe ya kusagia; na wazaliwa wa kwanza wote wa nyama. 6 Na kilio kikubwa kitakuwa katika inchi ya Misri, namna isivyokuwa mbele wala haitakuwa tena. 7 Lakini hata imbwa hatatolea mmoja wa wana wa Israeli ulimi wake, wala mtu wala nyama, mujue ya kama Bwana anaweka tofauti kati ya Wamisri na Israeli. 8 Na watumishi wako hawa wote watashuka kwangu na watajiinama mbele yangu wakisema: Toka wewe na watu wote ambao wanakufuata; na halafu nitatoka. Akatoka mbele ya Farao na hasira kubwa.*

Hivi tunaona ya kwamba Mungu alikusudi kuleta pigo juu ya inchi ya Misri lililokuwa baya kupita mapigo yote yaliyotokea mbele. Mungu alitangaza ya kwamba kila mwana mzaliwa wa kwanza ndani ya inchi ya Misri atakufa. Pigo la kuogofya kabisa! Na nini itapata wazaliwa wa kwanza wa Waisraeli? Watakufa pamoja na wale wa Wamisri? Hawakustahili kuepuka hukumu ya Mungu, kwa sababu wao vilevile walikuwa wenye zambi, kama watu wote wa Misri. Lakini, Mungu aliye mwaminifu na mwenye rehema, alikuwa na **shauri** kuponyesha watu wa Israeli toka pigo lile.

Tuendelee kusoma kuanza na sura 12 na shairi 1 kuona maneno Mungu aliyoagiza Waisraeli kufanya ili wazaliwa wao wa kwanza waepuke kufa. Maandiko yanasema:

> (Kutoka 12) *1 Bwana akamwambia Musa na Haruni katika inchi ya Misri akisema . . . 3 Semeni kwa kusanyiko lote la Israeli mukisema: Kwa siku ya kumi ya mwezi huu watajitwalia kila mtu **mwana-kondoo**, sawasawa na nyumba za baba zao ... 5 Mwana-kondoo yenu atakuwa **pasipo kilema**, ndume ya mwaka wa kwanza; mutamtwaa katika kondoo au katika mbuzi; 6 na mutamchunga hata siku ya kumi na ine ya mwezi ule ule; na kusanyiko lote la makutano ya Israeli watamchinja mangaribi. 7 Na **watatwaa ya damu na kuitia juu ya nguzo mbili za kando ya mlango na juu ya kizingiti cha juu**, katika chumba pahali watakapokula. 8 Watakula nyama usiku ule, imechomwa kwa moto, na mkate pasipo chachu; wataukula na majani machungu. 9 Musiile mbichi, wala ya kupikwa ndani ya maji, lakini imechomwa kwa moto; kichwa chake pamoja na miguu yake na matumbo yake ... 46 Itakuliwa nyumbani moja; hutachukua ya nyama inje ya nyumba; wala hamutavunja mfupa wake hata mmoja."*

> *11 "Na mutaikula hivi: na viuno vyenu vimekwisha kufungwa, viatu vyenu kwa miguu yenu, na fimbo yenu mkononi mwenu; mutaikula kwa haraka; ni* ***pasaka ya Bwana****. 12 Na nitapita katika inchi ya Misri usiku ule, na nitapiga wazaliwa wa kwanza wote katika inchi ya Misri, mtu na nyama vilevile, na juu ya miungu yote ya Misri nitafanya hukumu;* ***mimi ni Bwana.*** *13 Na damu itakuwa alama kwenu juu ya nyumba pahali mutakapokuwa; na* ***wakati nitakapoona damu, nitapita juu yenu,*** *wala pigo halitakuwa juu yenu kuwaharibu ninyi; wakati nitakapopiga inchi ya Misri."*

Tusimame kwanza hapa. Unaona shauri la Mungu kuponyesha wana wazaliwa wa kwanza toka mauti na kukomboa watu wote wa Israeli toka utumwa wao katika Misri? Lilikuwa shauri la kushangaza, shauri lililoonekana pumbavu kwa macho ya watu wa dunia. Alikusudi kuwaokoa na **damu ya mwana-kondoo**—damu ya mwana kondoo bila kilema—damu ambayo watatumia kupakaa nguzo za milango ya nyumba zao. Damu ya mwana-kondoo tu iliweza kuokoa wazaliwa wao wa kwanza toka mauti.

Wakati Mungu alipomaliza kusema na Musa na Haruni, walikusanya wazee wote wa Israeli na kuwaambia maneno Mungu aliyokwisha kusema juu ya zabihu ya mwana-kondoo. Wakati wazee wa Israeli waliposikia namna Mungu alivyokusudi kuponyesha wazaliwa wao wa kwanza toka pigo la mauti, walianguka kifudifudi na kuabudu Mungu. Nyuma yake, wazee na watu wote wa Israeli walifanya maneno yote ambayo Mungu aliyoagiza Musa.

Hivi, Maandiko yanasema:

> (Kutoka 12) *29* ***Kwa saa sita ya usiku Bwana akapiga wazaliwa wa kwanza wote katika inchi ya Misri****, toka mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyekaa juu ya kiti chake cha ufalme, hata mzaliwa wa kwanza wa mfungwa aliyekuwa nyumbani mwa kifungo, na wazaliwa wote wa kwanza wa nyama. 30 Farao akaamka usiku, yeye na watumishi wake wote, na Wamisri wote, na kilikuwa kilio kikubwa katika Misri maana* ***hakuna nyumba pasipo mfu.***

Ulisikia nini ilitokea usiku ule wa kuogofya? Mungu alihukumu inchi ya Misri kama alivyosema atafanya? Ndiyo! Kwa saa sita ya usiku, malaika ya uharibifu alipita katika inchi ya Misri, akiua wazaliwa wa kwanza wote, toka mzaliwa wa kwanza wa mfalme, ndiye Farao hata wazaliwa wa kwanza wa wale waliokuwa gerezani.

Usiku ule kulikuwa na malamiko na maombolezo makubwa katika inchi nzima, kwa sababu hakuna nyumba ya Wamisri isiyokuwa na mfu!

Lakini nini ilitokea ndani ya nyumba za Waisraeli? Mungu aliponyesha wazaliwa wao wa kwanza toka pigo la mauti? Unafikili nini? Mungu alikuwa ameahidi mbele akisema, ***"Wakati nitakapoona damu, nitapita juu yenu."*** Watu wa Israeli walikuwa wamepakaa milango ya nyumba zao na damu ya mwana-kondoo, namna Mungu alivyoagiza. Hivi **hakuna hata mmoja wa wazaliwa wao wa kwanza aliyekufa**. Lakini ndani ya nyumba za Wamisri, **kila mzaliwa wa kwanza alikufa** kwa sababu hawakushiriki ndani ya njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha, njia ya damu ya kondoo.

Hivi, Maandiko yanasema:

> (Kutoka 12) *31 (**Farao**) akaita Musa na Haruni usiku, akasema: **Ondokeni, mutoke katika watu wangu, ninyi na wana wa Israeli vilevile**; kwendeni mutumikie Bwana, kama mulivyosema. 32 . . . na munibariki mimi vilevile!* 33 ***Wamisri wakasukuma watu, kuwatoa kwa haraka toka inchi;*** *kwa sababu wakasema: "Sisi sote ni wafu!"*

Mwishoni Farao alilazimishwa kunyenyekea na kuruhusu Waisraeli kwenda. Tumeona mbele ya kuwa kwanza Farao alisema na Musa na Haruni, *"Bwana ni nani nimtii na kuruhusu Israeli kwenda? Sijui Bwana na sitawaacha kwenda!"* Lakini, mwishoni, ilikuwa sharti kwa Farao na Wamisri wote kukubali ya kwamba Mungu wa Abrahamu, Isaka na Israeli ni Mungu Mwenyezi, mwenye uwezo kupita sanamu na wachawi wao wote! "Haifai yayi kupigana na mwamba!" Haiwezekani kwa mtu ye yote kupigana na Mungu na kushinda!

Usiku ule ule, Waisraeli walitoka Misri, wakakwenda na mali nyingi waliyopewa na Wamisri. Maandiko yanasema:

> (Kutoka 12) *35 Wana wa Israeli wakafanya kama neno lile la Musa, wakaomba Wamisri vyombo vya feza na vyombo vya zahabu, na mavazi. 36 Bwana akawapa upendeleo kwa macho ya Wamisri, hata waliwapa walivyoomba. Watu wakateka Wamisri. ... 40 Basi kukaa kwa wana wa Israeli walipokaa katika Misri, kulikuwa miaka mia ine makumi tatu.*

Maneno haya yote yalitokea kutimiza ahadi Mungu aliyotolea Abrahamu mia za miaka ya mbele, akisema,

> *"Jua kabisa ya kwamba uzao wako utakuwa mgeni kwa inchi isiyo yake, na watatumikia watu wale, nao watawatesa miaka mia ine; na vilevile nitahukumu taifa ambao watawatumikia;* ***na nyuma watatoka na mali nyingi.****"* (Mwanzo 15:13,14)

Habari tulizosoma leo, habari za Pasaka, ni kama bahari inayokwenda chini sana na inayojaa na hazina nyingi zinazofichwa ndani yake. Tungeweza kusema maneno mengi sana juu ya Pasaka, lakini hatuna saa kueleza kweli zote ndani ya habari hizi. Lakini lazima tukae kukumbuka kweli kubwa moja. Ni ahadi ya Mungu kwa Waisraeli: ***"Wakati nitakapoona damu, nitapita juu yenu!"***

Kwa nini wazaliwa wa kwanza wa Waisraeli hawakufa pamoja na wale wa Wamisri? Hawakufa kwa sababu Mungu aliwafungulia **njia ya wokovu kwa njia ya damu ya mwana-kondoo.** Mungu alikusudi kwa mzaliwa wa kwanza **kupona** ndani ya kila nyumba pahali damu ya mwana-kondoo ilipopakaliwa kwa mlango. Lakini mzaliwa wa kwanza ndani ya kila nyumba i**liyokosa damu** kwa mlango **atakufa**!

Kijana mzaliwa wa kwanza mmoja wa Israeli akiuliza baba yake, akisema, "Baba, kwa nini inapasa mwana-kondoo yetu asiyefanya neno baya kufa?" Baba atamjibu namna hii: "Mwana wangu, unajua ya kwamba Mungu amehukumu kila mwana mzaliwa wa kwanza inchini. Kwa sababu ya zambi zetu, sisi sote tunastahili kuhukumiwa na Mungu. Lakini Mungu, kwa rehema yake, alitujulisha ya kwamba tukitoa zabihu ya mwana-kondoo asiye na kilema, na kupakaa damu yake kwa milango ya nyumba yetu, pigo hili halitatugusa. Ni lazima kwa mwana-kondoo kufa, kwa sababu malipo ya zambi ni mauti. Mungu ni mwenye haki na hawezi kuona zambi bule. Mwana-kondoo atakukomboa wewe. Tutamtoa kwa pahali pako, kama babu yetu Abrahamu alivyotoa kondoo-ndume kuwa sadaka kwa pahali pa mwana wake. Mungu wetu ni mwenye haki na haoni zambi kama kitu kidogo. Alituambia waziwazi ya kwamba **damu** ikiwa kwa mlango wetu atapita nyumba yetu!"

Rafiki, inatupasa kufahamu ya kwamba kwa macho ya Mungu, wazao wote wa Adamu ni kama wana wazaliwa wa kwanza wa watu wa Misri na Israeli. **Sheria takatifu ya Mungu inatuhukumu**

**sisi sote mmoja mmoja** kufa na kupata hukumu ya haki ya Mungu. Maandiko Matakatifu yanasema hivi: *"hapana tofauti; kwa sababu **wote wamefanya zambi na kupungukiwa** na utukufu wa Mungu"* (Waroma 3:22,23) Malipo ya zambi ni hukumu ya milele, *"kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake!"* (2 Watesalonika 1:9)

Basi, inatupasa kufanya nini tuweze kuokolewa? Namna gani Mungu anaweza kuokoa wenye zambi toka zambi zao pamoja na kuwa mwenye haki? Hatuwezi kujibu ulizo hili zima leo, lakini sharti tujue ya kwamba **wana-kondoo** ambao Waisraeli walitoa kuwa sadaka kuepuka pigo la mauti ni **mfano wa Mkombozi** atakayekuja na kumwanga damu yake kulipa deni ya zambi kwa wazao wote wa Adamu. Juu ya Mkombozi, Maandiko yanasema ya kwamba: *"Kristo aliteswa mara moja kwa ajili ya zambi, **mwenye haki kwa ajili yao wasio haki**, ili atulete kwa Mungu . . .[**kama mwana-kondoo** aliyetolewa kwa Mungu kama sadaka siku ya Pasaka]."* (1 Petro 3:18; 1 Wakorinto 5:7). Hivi, damu ya mwana-kondoo wana wa Israeli waliyopakaa kwa milango yao kuokoa wazaliwa wao wa kwanza wasife ni **mfano.** Ni mfano wa damu ambayo Mwokozi alimwanga juu ya msalaba miaka mingi nyuma, ili mtu ye yote anayemwamini aweze kuepuka azabu ya milele ya Mungu.

Rafiki, habari zako nini? **Unajua** maneno manabii wa Mungu waliyoandika juu ya damu ya Mkombozi? Mkombozi alimwanga damu yake ili Mungu aweze kukusamehe wewe zambi zako bila kuacha kuwa mwenye haki. **Unaamini** maneno yaliyoandikwa juu ya damu hii iliyo na uwezo kukuokoa toka azabu ya uharibifu wa milele na kuhakikisha kwamba utakuwa na nafasi kwa milele mbele ya Mungu mbinguni? Siku ya hukumu, hukumu ya kuogofya ya Mungu itapita juu yako? Au itakupata kama ilivyopata Wamisri?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Saa yetu imekwisha. Ndani ya somo la nyuma, tutaendeleo na habari za Waisraeli na kuona namna Mungu alivyofungua njia katikati ya bahari.

Mungu akubariki, na kufunua kwa roho yako maana ya ndani ya maneno aliyosema na Waisraeli:

***"Wakati nitakapoona damu nitapita juu yenu!"*** (Kutoka 12:13)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 34

# Njia Katikati ya Bahari

### Kutoka 13–15

Salama iwe kwako, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kukutana tena leo na kujifunza somo lingine la mfulizo *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele, tuliona namna Mungu alivyoponyesha Waisraeli toka utumwa kwa njia ya kuua wazaliwa wa kwanza wote wa Wamisri. Lakini aliponyesha wazaliwa wa kwanza wa Waisraeli nao hawakufa kwa sababu ya damu ya mwana-kondoo waliyopakaa juu ya milango ya nyumba zao. Maana Mungu alikuwa amesema yeye mwenyewe, *"Damu itakuwa* ***alama*** *kwenu juu ya nyumba pahali mutakapokuwa; na* ***wakati nitakapoona damu, nitapita juu yenu."*** (Kutoka 12:13)

Hivi, usiku ule, makabila yote ya Israeli walitoka Misri. Usiku ule wa Pasaka ulikuwa usiku wa furaha kubwa kwao. Fikili kwanza! Kwa mia za miaka watu wa Misri walikuwa wamewatesa na kazi ngumu sana hata hawakujuana na furaha tena. Lakini sasa . . . walikuwa **huru**! Usiku ule wa Pasaka, Bwana Mungu aliwaokoa! Minyororo yao ya utumwa ilivunjwa! Na sasa Mungu **aliahidi** kuwaongoza katika jangwa na **kuwafikisha tena kwa inchi ya Kanana.** Unajua ya kwamba hii ndiyo inchi ambayo Mungu aliahidi mbele kuwapa wazao wa Abrahamu, Isaka na Yakobo. Kanana ndiyo inchi pahali Yakobo na wana wake walipokaa mbele ya kuhama kwenda Misri kukaa pamoja na Yosefu. Sasa inchi hii inaitwa *Palestina* au *Israeli*.

Leo tutaona **namna Mungu alivyoponyesha Waisraeli toka majeshi ya Farao**. Tutasoma zaidi ndani ya sura 14 ya kitabu cha Kutoka. Sikiliza habari ambazo nabii Musa alitujulisha ndani ya Tora:

> (Kutoka 12) *37 Wakasafiri wana wa Israeli toka Ramese hata Sukoti, karibu na* ***watu elfu mia sita wakikwenda kwa miguu, wanaume, wanawake, na tena watoto. Nao wengine walio-***

> ***changanyika nao**, wakapanda vilevile pamoja nao; na ngombe na kondoo, na nyama wengi sana. 13:19 Musa akachukua **mifupa ya Yosefu** pamoja naye; maana kuapiza akaapiza wana wa Israeli akisema: Hakika Mungu atawaangalia ninyi, na mutapandisha mifupa yangu toka hapa pamoja nanyi.". . . 21 Bwana akakwenda mbele yao, mchana kwa nguo ya wingu, kuwaonyesha njia, na usiku kwa **nguzo ya moto**, kuwaangazia waende mchana na usiku; 22 nguzo ya wingu kwa mchana, wala nguzo ya moto usiku haikuondoka mbele ya watu.*
>
> *(Kutoka 14) 1 Bwana akamwambia Musa akisema: 2 Sema na wana wa Iaraeli wageuke na kupiga kambi ... karibu na [Bahari Nyekundu] ... 3 Na Farao atasema juu ya wana wa Israeli: Wametatanishwa inchini, jangwa limewafunga. 4 Na nitafanya moyo wa Farao mgumu, naye atawafuata; **na nitajipatia heshima juu ya Farao na juu ya jeshi lake lote; na Wamisri watajua ya kama mimi ni BWANA**. Wakafanya hivi.*
>
> *5 Mfalme wa Misri akaambiwa ya kama watu wamekimbia; **moyo wa Farao na wa watumishi wake ukageuka** juu ya watu, wakasema: Nini hili tulilofanya, tukiwa tumeacha Israeli wasitutumikie? 6 Akatayarisha gari lake, akachukua watu wake pamoja naye; akachukua magari machaguliwa mia sita, na magari yote ya Misri, na kila moja na akida lake.*
>
> ***Wamisri ... farasi na magari yote ya Farao, na wapandaji farasi yake, na jeshi lake,** wakawapata kwa kambi karibu na bahari [nyekundu] ... 10 Na wakati Farao alipokaribia, wana wa Israeli wakanyanyua macho yao, na tazama, Wamisri walikuwa wakikuja nyuma yao; **wakaogopa sana,** wana wa Israeli wakalia kwa Bwana. 11 Wakamwambia Musa, Kwa sababu hapana makaburi katika Misri, umetutoa katika Misri? 12 Si hili neno ambalo tulikuambia katika Misri tukisema: Utuache, tutumikie Wamisri? Maana ni afazali tutumikie Wamisri kuliko kufa jangwani.*

Waisraeli walikuwa wakisema nini? Kwa nini hawakuamini Mungu? Mungu yule ambaye aliwafungua toka utumwa katika Misri hakuweza kuwaponyesha tena toka majeshi ya Farao? Aliweza! Lakini Waisraeli hawakukumbuka neno hili kwa sababu waliogopa sana. **Bahari** ilikuwa mbele yao. **Milima** ilikuwa kwa upande wao wa kuume na kwa kushoto. Nyuma yao **majeshi** ya Farao yalikuwa yakikaribia kuwafunga tena au hata kuwaua!

Iliwapasa kufanya nini? Waliweza kufanya nini basi? Wataweza kupona namna gani? Tusikilize maneno Musa aliyosema na kuona nini Mungu alifanya.

> (Kutoka 14) *13 Musa akawaambia watu:* ***Musiogope; simameni tu, mwone wokovu wa Bwana ambao atawafanyia ninyi leo****; kwa maana Wamisri ambao muliwaona leo, hamutawaona tena hata milele. 14 Bwana atawapigania ninyi, nanyi mutanyamaza kimya.*
>
> *15 Bwana akamwambia Musa: Kwa nini unalia kwangu? Sema na wana wa Israeli waendelee mbele. Nawe nyanyua fimbo yako, na nyosha mkono wako juu ya bahari uitenge, na wana wa Israeli watakwenda katikati ya bahari kwa inchi kavu. Nami, tazama, nitafanya mioyo ya Wamisri migumu, na wataingia nyuma yao; na nitajipatia heshima juu ya Farao, na juu ya jeshi lake lote, juu ya magari yake, na juu ya wapandaji farasi wake.* ***Nao Wamisri watajua ya kama mimi ni BWANA ..."*** *19 Malaika ya Mungu aliyekwenda mbele ya kambi ya Israeli akaondoka, akakwenda nyuma yao; nguzo ya wingu ikaondoka mbele yao, ikasimama nyuma yao; 20 na ilikuwa katikati ya kambi ya Misri na kambi ya Israeli; yatakuwa wingu na giza, hata hivi likaangaza usiku; wala hawakukaribiana usiku mzima.*
>
> *21 Musa akanyosha mkono wake juu ya bahari; Bwana akaendesha bahari kwa upepo wa mashariki wa nguvu usiku mzima, akafanya bahari kuwa inchi kavu,* ***maji yakatengwa****. 22 Wana wa Israeli wakakwenda kati ya bahari juu ya* ***inchi kavu****; maji yakakuwa ukuta kwao kwa mkono wao wa kuume, na kwa kushoto.*
>
> *23 Wamisri wakafuata, wakaingia nyuma yao kati ya bahari, farasi zote za Farao, magari yake, na wapandaji farasi yake. 24 Na ilikuwa kwa kesha la asubui, Bwana akaangalia jeshi la Wamisri. Akaondosha magurudumu ya magari yao, yawe nguvu kuendesha, hata Wamisri wakasema: Tukimbie mbele ya uso wa Israeli; kwa kuwa Bwana anawapigania juu ya Wamisri.*
>
> *26 Bwana akamwambia Musa: Nyosha mkono wako juu ya bahari maji yarudi juu ya Wamisri, juu ya magari yao, na juu ya wapandaji farasi wao. 27 Musa akanyosha mkono wake juu ya bahari, bahari ikarudi na nguvu zake kwa mapambazuko ya asubui; Wamisri wakakimbia mbele yake; Bwana akaangusha Wamisri kati ya bahari. 28 Maji yakarudi, yakafunika magari na wapandaji farasi;* ***hata jeshi lote la Farao*** *lililoingia nyuma yao baharini;* ***hakubaki hata mmoja wao****. 29 Lakini wana wa Israeli wakakwenda juu ya inchi*

> *kavu kati ya bahari; maji yalikuwa ukuta kwao kwa mkono wao wa kuume, na wa kushoto. Hivi Bwana akaponyesha Israeli siku ile toka mkono wa Wamisri; Israeli wakaona Wamisri wamekufa juu ya pwani. 31 I**sraeli akaona kazi kubwa Bwana aliyofanya juu ya Wamisri, watu wakaogopa Bwana, wakaamini Bwana na mtumishi wake Musa.***

Halafu Musa na Waisraeli waliimba wimbo huu kwa Bwana: *"Nitaimbia Bwana kwa maana ameshinda kwa utukufu; farasi na mpandaji wake ametupa baharini. Bwana ni nguvu yangu, yeye ni wimbo wangu; vilevile amekuwa wokovu wangu."* (Kutoka 15:1,2) Hivi, walianza kuimba, na kushukuru Mungu kwa **wokovu mkubwa** ambao aliwafanyia. Miriamu, ndugu mke wa Haruni na Musa alitwaa toazi, wanawake wote wakamfuata wakipiga matoazi na kuimba na kucheza. Miriamu alianza wimbo huu: *"**Imbeni kwa Bwana, kwa sababu ameshinda kwa utukufu**; farasi na mpandaji wake ametupa baharini!"* (Kutoka 15:21)

Rafiki, hizi ndizo habari za kweli na za ajabu za namna Mungu alivyofanya njia katikati ya bahari kwa watu wa Israeli. Halafu tunaweza kumaliza somo la leo namna gani? Labda tunaweza kumaliza na ulizo hili: **Nani aliweza kuponyesha Waisraeli toka majeshi ya Farao?** Waliweza kujiokoa wenyewe? Tuliona ya kwamba **bahari** ilikuwa mbele yao. **Milima** ilikuwa kando yao kwa kuume na kushoto. Na **majeshi ya Farao** yalikuwa nyuma yao. Waisraeli waliweza kujiokoa wenyewe? Waliweza kukausha bahari? Au kuondosha milima? Au labda waliweza kushindana na majeshi ya Farao? Sivyo, hata kidogo! Basi nani aliweza kuwaokoa? **Mungu tu!** Bwana tu aliweza kuwaokoa. Kwa sababu hii Musa aliwaambia, *"Musiogope, simameni tu, mwone **wokovu wa Bwana ambao atawafanyia ninyi** leo!"* Mungu tu aliweza kuwaokoa! Na aliwaokoa kweli. Kwa sababu hii, nyuma ya kufikia ngambo ya bahari, waliimba, *"Bwana ni nguvu yangu, na wimbo wangu, yeye vilevile amekuwa **wokovu wangu.**"*

**Mungu yeye mwenyewe** amekuwa wokovu wao. Waisraeli hawakuweza kufanya hata neno moja kujiokoa toka majeshi ya Farao — ila kufuata njia ambayo Mungu alikuwa amewafungulia katikati ya bahari, kisha kumshukuru na kumwabudu kwa kuwaokoa toka mauti!

Rafiki, Mungu anataka watu wote kujua ya kwamba wana wote wa Adamu ni sawasawa na wana wa Israeli. Kama Waisraeli hatuna

njia kuepuka uharibifu ambao utatuangukia nyuma kidogo isipokuwa Mungu anatuokoa! Labda bahari si mbele yetu, lakini **mauti na hadeze** zinatungojea. Labda milima si kando kando yetu, lakini **utakatifu wa Mungu** ni kama ua kwetu na kutuhukumu. Farao na majeshi yake si nyuma yetu, lakini **Shetani na zambi zetu** ni karibu kutuharibu kwa milele!

Nani anayeweza kuokoa wana wa Adamu toka hukumu ya haki ya Mungu? Nani anayeweza kuokoa mwenye zambi toka moto usiozimika kamwe? Nani anayeweza kuokoa mtu toka uwezo wa Shetani? Nani anayeweza kutuokoa toka maneno haya yote? Nani anayeweza kutufikisha ngambo ya bahari ya zambi na kutuleta kwa pahali patakatifu panapoitwa Paradiso? Mungu tu! Mungu yeye mmoja anaweza kutuokoa! Mtu hana njia kujiokoa mwenyewe au kuokoa mtu mwingine. Hili ndilo neno ambalo Maandiko yanatangaza: *"**Mumeokolewa kwa neema** kwa njia ya imani, wala **neno hili halikutoka ndani yenu wenyewe**, ni zawadi ya Mungu, si kwa matendo, asiwe mtu atakayejisifu."* (Waefeso 2:8,9)

Mungu, mwenye rehema kubwa, amefungua njia ya wokovu kwa wana wote wa Adamu, kutuokoa toka uwezo wa Shetani na zambi na hadeze. Mungu anataka tuepuke hukumu ya moto unaowaka milele na unaongojea wote wanaokufa ndani ya zambi zao, **lakini sharti tufike kwa njia ya wokovu ambayo alitufungulia!** Unajua njia ya wokovu ambayo Mungu alikufungulia ili uweze **kuepuka** uwezo wa **Shetani**, matunda ya kuogofya ya **zambi** na azabu ya **hadeze**? Umeingia njia ya haki ambayo Mungu alitayarisha ili uweze kubarikiwa katika ukaribu wake mtakatifu kwa milele?

Njia ya haki ambayo Mungu alifungulia wana wa Adamu si kwa sababu ya matendo mema ambayo mtu anaweza kufanya, wala kwa sababu ya kutii maagizo ya dini fulani. Mungu anasema ya kwamba *"**si** kwa njia ya matendo, **asiwe mtu** atakayejisifu."* Njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha kwa sisi ni nini? Ni **njia ya Mkombozi,** aliyeshuka toka mbinguni kufa kwa zambi zetu na kufufuliwa tena —kufungua wote ambao wanamwamini—sisi tuliokuwa **kama watumwa** kwa sababu ya uwezo wa zambi na woga wa mauti. Maandiko Matakatifu yanasema juu ya Mkombozi huyu mwenye uwezo: *"**Hakuna wokovu katika mwingine,** kwa maana **hakuna jina lingine** chini ya mbingu walilopewa watu tupate kuokolewa nalo."* (Matendo 4:12)

Ndiyo, Mungu alikufungulia njia ndani ya "bahari ya zambi" ili uweze kuepuka azabu ya zambi na kufika ngambo—karibu na Mungu mtakatifu pahali hatari isipokuwa tena. Lakini lazima uvuke kwa njia ambayo Mungu alikufungulia. Juu ya njia hii ya wokovu, Mkombozi alisema,

> *"**Mimi ndimi njia**, na kweli, na uzima: mtu hakuji kwa baba, ila kwa mimi. . . Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye **anayesikia** neno langu na kumw**amini** yeye ambaye alinituma ana uzima wa milele; hafiki kwa hukumu, lakini **amepita kutoka mauti kuingia uzima.**"* (Yoane 14:6; 5:24)

Rafiki, *umepita ku**toka mauti kuingia uzima?**"*

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mara ya nyuma tutaona namna gani Mungu alikulisha Waisraeli jangwani . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya neno la Musa kwa Waisraeli:

> ***"Musiogope, simameni tu, mwone wokovu wa Bwana ambao atawafanyia ninyi leo!"*** (Kutoka 14:13)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 35

# CHAKULA JANGWANI

## KUTOKA 16,17

Salama iwe kwako, rafiki yetu. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kujifunza somo lingine leo la mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele, tuliona namna **Mungu alivyoponyesha** Waisraeli toka mkono wa Farao na majeshi yake. Wakati Waisraeli walipofika kwa pwani ya Bahari Nyekundu hawakuwa na njia kukimbia jeshi la Farao. Lakini tuliona ya kwamba Mungu alisukuma maji kando ili waweze kutambuka katikati ya bahari wakitembea juu ya inchi kavu. Lakini wakati majeshi ya Misri walipojaribu kuvuka, walizama. Hivi, siku ile Bwana aliokoa Waisraeli toka mkono wa Wamisri. Na wakati walipoona uwezo mkubwa wa Bwana, walimwogopa na kumwimbia, *"Nitaimbia Bwana kwa maana ameshinda kwa utukufu."*

Tunasoma sasa ndani ya kitabu cha Kutoka, pahali Waisraeli walipokuwa jangwani **katikati ya Misri na Kanana.** Kanana ndiyo inchi ambayo Mungu aliahidi kumpa mzazi wao Abrahamu na wazao wake, iwe inchi yao. Leo tutaona **namna gani Mungu alilisha Waisraeli jangwani.** Maandiko yanaonyesha namna Mungu yeye mwenyewe "alitembea" mbele yao, ndani ya wingu kubwa kwa mchana na ndani ya ulimi wa moto usiku. Kuna neno moja tunalojua hakika, ya kwamba kama Mungu asipowaongoza na kuwalinda, wangalikufa jangwani.

Waza kwanza juu ya hali ya Waisraeli. Walikuwa watu wengi sana, karibu milioni mbili! Walikuwa wakipita ndani ya jangwa ya kukauka kabisa—hakuna maji wala chakula. Jeshi lile kubwa walikuwa wakipita katika jangwa ya mchanga na michongoma! Makabila ya Israeli watapona namna gani? Nani atakayeweza kuwaponyesha toka njaa na kiu? Pahali gani makundi yao mengi

watapata maji na vyakula vya kutosha kukaa hai jangwani? Waliweza kujikulisha wenyewe? Sivyo! Basi nani aliweza kuwalisha? Kuna jibu moja tu kwa ulizo hili. **Mungu peke yake** aliweza kuwalisha na kuwalinda!

Waisraeli **waliamini Mungu?** Walimtegemea kuwalinda, au walikaa kusumbuka kama watakula na kunywa nini? Bila shaka ingalipasa Waisraeli kuamini BWANA Mungu. Mungu alikuwa amewafanyia maneno makubwa mengi. Aliwafungua toka utumwa wao kwa njia ya mapigo kumi. Aliokoa wazaliwa wao wa kwanza toka kufa, kwa njia ya damu ya mwana-kondoo. Alifungua njia iliyokauka katikati ya bahari. Na sasa alikuwa akienda mbele yao katika wingu kuwafikisha tena kwa inchi ya Kanana, kama alivyoahidi tata yao, Abrahamu zamani. Unafikili nini? Watu hawa waliamini Mungu wao? Waliamini ya kwamba Mungu atatimiza ahadi yake? Tusome Maandiko sasa kupata jibu kwa maulizo haya.

Tunasoma ndani ya sura 16 ya Kutoka, katika Tora ya Musa. Maandiko yanasema:

> (Kutoka 16) *1 Wakasafiri toka Elimu, kusanyiko lote la wana wa Israeli, wakafika kwa jangwa la Sinai iliyo kati ya Elimu na Sinai, siku ya kumi na tano ya mwezi wa pili nyuma ya kuondoka kwao toka inchi ya Misri. 2 Kusanyiko lote la wana wa Israeli waka**nungunikia** Musa na Haruni jangwani; 3 wana wa Israeli wakawaambia: Afazali tungalikufa kwa mkono wa Bwana katika inchi ya Misri, wakati tulipokaa karibu na sufuria za nyama, wakati tulipokula mkate na kushiba. Kwa sababu **mumetutoa katika jangwa hili kuua kusanyiko hili lote kwa njaa.***

Unafikili mataifa ya Israeli walitumainia Mungu? Sivyo, hawakumtumainia. Walikuwa wakimnungunikia yeye na nabii wake Musa. Sikia namna Mungu alivyowajibu.

> (Kutoka 16) *11 Bwana akamwambia Musa akisema: 12 Nimesikia manunguniko ya wana wa Israeli; uwaambie ukisema: Mangaribi mutakula nyama, na asubui mutashibishwa na mkate; **na mutajua ya kwamba mimi ni Bwana, Mungu wenu.** ... 4 Halafu Bwana akamwambia Musa: Tazama, nitawanyeshea ninyi mkate toka mbingu; watu watatoka na kuokota sehemu ya kila siku, nipate kuwapima kama watatembea kwa sheria yangu au sivyo. ...*

*13 Na ilikuwa mangaribi kanga wakapanda, wakafunika kambi; asubui umande umelala kuzunguka kambi. 14 Na wakati umande uliolala ulipopanda, tazama, juu ya uso wa jangwa kitu kidogo cha mviringo, kidogo kama sakitu juu ya inchi. 15 Na wakati wana wa Israeli walipokiona wakasema wao kwa wao:* ***Hiki ni nini?*** *kwa maana hawakujua kama ni nini. Musa akawaambia: Ni mkate ambao Bwana aliwapa ninyi kula. ... 31 Nyumba ya Israeli wakaita jina lake mana; na ilikuwa kama mbegu za giligilani; nyeupe; na utamu wake ulikuwa kama mkate mdogo wembamba pamoja na asali.*

Mungu alikulisha makabila ya Israeli hivi jangwani, kufika siku walipofikia inchi ya Kanana. Ulisikia kama chakula chenyewe kilitoka wapi? **Kilitoka mbinguni**. Kilitoka **kwa Mungu**. Waisraeli walistahili kupokea vyakula ambavyo Mungu alituma kwao? Sivyo! Hawakustahili kupokea kitu toka Mungu ila hukumu yake kwa sababu ya kutokuamini kwao na ukosefu wao wa asante. Ilikuwa kwa sababu ya rehema ya Mungu tu hawakufa kwa njaa jangwani.

Sasa tuendelee kusoma nini ilitokea siku nyingine, **wakati Waisraeli walipokosa maji.** Tutasoma ndani ya sura 17. Maandiko yanasema:

(Kutoka 17) *1 Kusanyiko lote la wana wa Israeli wakasafiri toka jangwa la Sini, kwa safari zao, kwa amri ya Bwana. Wakapiga kambi kwa Refidimu, maji hayakuwa kwa watu kunywa. 2 Kwa hivi watu* ***wakagombana*** *na Musa, wakasema: Utupe maji tupate kunywa. Musa akawaambia: Kwa nini munagombana nami? Kwa nini munajaribu Bwana? 3 Watu wakaona kiu pale; watu wakanungunikia Musa, wakasema: Kwa nini umetupandisha toka Misri, kutuuasi sisi na wana wetu na nyama zetu kwa kiu? 4 Musa akalia kwa Bwana, akisema: Nitafanyia watu hawa nini? Wao ni karibu kunitupia mawe.*

*5 Bwana akamwambia Musa: Pita mbele ya watu, na twaa wazee wa Israeli pamoja nawe; na twaa fimbo yako uliyopiga mto nayo mkononi mwako uende. 6 Tazama, nitasimama mbele yako pale juu ya mwamba kwa Horebu; na utapiga mwamba, na maji yatatoka ndani yake, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivi mbele ya macho ya wazee wa Israeli."*

Halafu maji mengi yalitoka kwa mwamba na kushuka kwa jangwa, watu wote wakakunywa, wao pamoja na makundi yao.

Tuwaze kwanza kidogo juu ya habari tulizosoma leo. Nyuma ya

maneno yote ambayo Mungu alikuwa amefanyia Waisraeli, walikuwa na imani? Walimwamini? Mioyo yao ilijaa sifa na mashukuru kwa sababu ya yote ambayo aliwafanyia? Sivyo! Hawakuamini Mungu. Kwa pahali pa kumtegemea walinungunika na kusema maneno yasiyofaa juu ya Mungu yule aliyekwisha kuwaokoa toka hatari nyingi sana.

Halafu Mungu alifanya nini? BWANA Mungu, mwenye saburi na wema, aliwapa vyakula na maji jangwani. Watu walistahili kupokea wema wa Mungu? Sivyo, walistahili hukumu tu. Kwa nini Mungu aliwaonyeshea wema wake? Kwa sababu Mungu ni **mwaminifu** na **mwenye rehema**. Yeye ni Mungu, Mwaminifu. Kwa sababu ya **rehema yake** alipatia Waisraeli vyakula na maji, hata wakati walipokuwa wenye zambi wasiokuwa na asante! Kama wokovu toka njaa na kiu ungalitegemea wema wao, bila shaka Mungu angaliwaacha kufa jangwani.

Vivyo hivyo ingetupasa kufahamu ya kwamba Mungu hakulinda watu wake kwa sababu ya rehema yake tu, lakini kwa **kutimiza ahadi yake**. Mungu ni mwaminifu na anatimiza ahadi zake zote— naye alikuwa ametoa ahadi kubwa kwa maneno ya Israeli. Tumejifunza ya kwamba **Mungu alikuwa ameahidi kubariki mataifa yote ya dunia kwa njia ya taifa la Israeli,** kwa sababu kwa njia ya manabii Maandiko Matakatifu yatakuja, na Mwokozi wa dunia vilevile. Ndiyo, Mungu ni mwaminifu na mwenye rehema tele! Yeye ni **Mungu wa kweli** na **Mungu wa mapendo**. Kweli mataifa ya Israeli hawakustahili mapendo ya Mungu. Hata hivi wakati walipomwasi na kusema maneno mabaya juu yake, alihakikisha uaminifu na mapendo yake kwa njia ya kuwapa vyakula toka mbiguni.

Labda unauliza, "Habari hizi za Waisraeli zina faida gani kwa sisi leo?" Neno la Mungu linasema ya kwamba *"Maneno haya yote yaliwapata **kama mifano,** yakaandikwa kutuonya **sisi** tuliofikiliwa mwisho wa siku."* (1 Wakorinto 10:11) Kama Mungu alivyookoa wana wa Israeli toka uwezo wa jangwa, vivyo hivyo Mungu anataka kuokoa kila mtoto wa Adamu toka **uwezo wa zambi.**

Tunakuuliza: Ilipasa Waisraeli kufanya nini ili wasiharibiwe jangwani? Iliwapasa tu **kuokota na kula vyakula ambavyo Mungu alituma toka mbinguni.** Wokovu wao ulitoka wapi? Kwa kazi na masumbuko yao wenyewe? Sivyo, wokovu wao ulitoka kwa Mungu. Hawakuwa na uwezo kujiokoa wenyewe toka njaa na mauti.

Hawakuweza kufanya neno ila **kuokota na kula vyakula ambavyo Mungu alikuwa amewaletea.**

Maandiko Matakatifu yanaonyesha ya kwamba sisi sote ni wenye zambi kama watu wa Israeli na **hatuna njia kujiokoa wenyewe**—toka uwezo wa zambi au toka hukumu ya haki ya Mungu. Labda hatutembei ndani ya jangwa ya kukauka kama Waisraeli, lakini kivuli cha mauti ni juu yetu namna kilivyokuwa juu yao. Neno la Bwana ni wazi: Mtu ye yote anayekataa kupokea njia ya wokovu ambayo Mungu aliweka tayari atakufa ndani ya zambi zake na kuanguka ndani ya moto wa milele. Haya si mafikili ya kupendeza. Kufa ndani ya zambi! Kuhukumiwa na Mungu! Kuanguka ndani ya hadeze! Haya ni **mambo ya kuogofya sana!** Lakini **habari njema** ndizo hizi: Si lazima kwa mtu ye yote, mume au mke au mtoto, kufa ndani ya zambi yake. Kama Mungu alivyopatia Waisraeli vyakula ili waweze kuishi na kutokufa kwa njaa jangwani, vivyo hivyo Mungu amewapa sisi "vyakula" ili tuweze kubarikiwa katika maisha yetu ya sasa na ndani ya maisha ya kuja yatakayoendelea kwa milele!

"Chakula" kinacholeta uzima wa milele ni nini? Tunaweza kununua chakula fulani kwa soko kinachoweza kutupa sisi uwezo kuishi kwa milele? Sivyo, hakuna chakula namna hii kinachopatikana kwa soko! Basi "chakula" hiki kinacholeta uzima wa milele ni nini na kinapatikana wapi?

Rafiki, vizuri ujue ya kwamba karibu miaka 1500 nyuma ya wakati Waisraeli walipokula mana (chakula) jangwani, Mungu alituma **Mkombozi** toka mbinguni, Mwokozi wa dunia. Yeye ndiye "Chakula" ambacho Mungu alileta kuokoa watu wa dunia toka uwezo wa zambi, mauti, hukumu na hadeze. Tusikilize na kuwaza sana juu ya maneno ambayo Mkombozi alisema juu yake mwenyewe wakati alipokuwa hapa duniani. Alisema,

> *"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye mwenye kuniamini mimi ana uzima wa milele. Mimi ni mkate (ndicho chakula) wa uzima. Baba zenu walikula mana katika jangwa, wakakufa. Huu ni mkate unaoshuka toka mbinguni, ili mtu apate kuukula, asife.* ***Mimi ni mkate wa uzima ulioshuka toka mbinguni . . . yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa!"*** (Yoane 6:47-51,35)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Sharti tuache hapa kwa leo. Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaanza kuona namna Mungu alivyotolea Israeli Amri Kumi . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maneno Mkombozi aliyosema,

> ***"Mimi ni mkate wa uzima. Yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa!"*** (Yoane 6:35)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 36

# MLIMA SINAI

KUTOKA 19,20

Salama iwe kwako, rafiki msomaji, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ameitayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya somo la mbele, tuliona namna Mungu alivyolinda makabila katika jangwa la kukauka kwa njia ya kuwapa **vyakula toka mbinguni** ili wasife kwa njaa. Tuliona vilevile namna Waisraeli walivyochukiza Mungu tena na tena kwa sababu ya kutoamini kwao na kutoaminifu kwao.

Leo tutaona namna Mungu alivyoonekana kwa watu wa Israeli jangwani na kuwapa **sheria yake takatifu.** Tunasoma ndani ya Tora, kitabu cha Kutoka sura 19. Sura hii inaanza hivi: *"Kwa mwezi wa tatu nyuma ya kutoka kwa wana wa Israeli katika Misri, siku yenyewe wakafika kwa jangwa la Sinai."* (Kutoka 19:1) Musa na Waisraeli walikuwa wamefika wapi sasa kwa safari yao jangwani? Walikuwa wamefikia jangwa la **Sinai**. Unakumbuka pahali Musa alipokuwa wakati Mungu alipomwita kwanza kwa njia ya kijiti kisichoteketea? Alikuwa pahali pale tu, kwa Sinai, ndio Horebu. Unakumbuka habari hizi? Tulisikia Mungu akisema na Musa,

> *"Hakika nimeona teso la watu wangu katika Misri . . . na nimeshuka kuwaponyesha . . . Basi kuja sasa, na nitakutuma kwa Farao . . . Hakika nitakuwa pamoja nawe; na hii itakuwa alama kwako ya kama nimekutuma;* ***wakati utakapokwisha kutoa watu toka Misri, mutatumikia Mungu juu ya mlima huu!"*** (Kutoka 3:7,8,10,12)

Mungu alifanyia Musa neno aliloahidi? Ndiyo! Ndani ya masomo yetu ya leo Musa ni wapi? Tunaona Musa na makundi ya Israeli

kwa **upande wa chini ya Mlima Sinai, kama Mungu alivyoahidi Musa miaka makumi ine mbele** wakati aliposema naye toka kijiti kisichoteketea ya kwamba: *"wakati utakapokwisha kutoa watu toka Misri, mutatumikia Mungu juu ya **mlima huu!"***

Sasa tuendelee kusoma kuona namna Mungu alivyoonekana kwa Musa na kusema na watu wote wa Israeli kwa Mlima Sinai. Maandiko yanasema:

> (Kutoka 19) *3 Musa akapanda kwa Mungu, Bwana akamwita toka mlima akisema: Utasema hivi na nyumba ya Yakobo, na kuwaambia wana wa Israeli: 4 Mumeona ambavyo nilifanyia Wamisri, na namna nilivyowabeba ninyi juu ya mabawa ya tai na kuwaleta ninyi kwangu. 5 **Kwa hivi basi kama kweli mutasikia sauti yangu, na kuchunga agano langu, halafu mutakuwa mali yangu mwenyewe kuliko mataifa yote;** maana dunia nzima ni yangu; 6 na mutakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu. Haya ni maneno ambayo utawaambia wana wa Israeli. 7 Musa akakuja, akaita wazee wa watu, akaeleza mbele yao maneno haya yote ambayo Bwana alimwagiza. 8 Watu wote wakajibu pamoja, wakasema: "**Yote Bwana aliyosema tutafanya!"***

Ulisikia namna Waisraeli walivyojibu Mungu? Walisema, ***Yote** Bwana aliyosema tutafanya!"* Neno walilosema lilikuwa kweli? Waliweza kushika maagizo **yote** ya Mungu? Mungu alijua vizuri ya kwamba Waisraeli hawataweza kufanya maneno yote ambayo aliwaagiza. Neno Mungu alilotaka lilikuwa kwa watu kufahamu ya kwamba hawakuweza kupendeza Mungu, kukubali zambi zao mbele yake, na kuamini Habari Njema juu ya Mkombozi atakayekuja duniani kuokoa wenye zambi. Mungu alikuwa amesamehe zambi za wazazi wao Abrahamu, Isaka na Yakobo kwa sababu **waliamini ahadi za Mungu**. Mungu alitaka kusamehe watu wa Israeli vilevile kwa njia ya imani peke yake. Tangu zamani njia ya wokovu ya Mungu ni kwa njia ya **imani peke yake**—imani ndani ya Mungu na njia yake ya wokovu. Maandiko yanasema: *"Ni wazi ya kwamba hakuna mtu anayehesabiwa haki kwa sheria katika macho ya Mungu, kwa sababu wenye haki wataishi **kwa imani.**"* (Wagalatia 3:11)

Lakini, kufika sasa, Waisraeli walitaraji ya kwamba wataweza kuwa na haki mbele ya Mungu kwa njia ya **kazi zao wenyewe**. Upumbavu kabisa! Walikuwa wamesahau mara ngapi walikuwa

wamekosea Mungu! Hawakufahamu ukubwa wa zambi zao mbele ya Mungu! Kwa mawazo yao zambi haikuwa neno kubwa, lakini kwa macho ya Mungu anayepaswa kuzihukumu zambi ni **neno baya kabisa! Mungu ni mtakatifu na mkamilifu**; hawezi kukubali kazi zisizo kamilifu kabisa! Lakini kufika wakati ule Waisraeli hawakufahamu neno hili. Kwa sababu hii walisema (na kiburi), *"Yote Bwana aliyosema tutafanya."* (Kutoka 19:8) Lakini Mungu alikuwa na shauri kuwaonyesha ya kwamba **hawakuweza** kufanya *"yote Bwana aliyosema!"* Sasa tuendelee kusoma Maandiko kuona namna Mungu alivyoshuka juu ya Mlima Sinai, akafunua utukufu na utakatifu wake, na alitolea makabila ya Israeli **Amri Kumi.**

Maandiko yanasema:

> (Kutoka 19) *10 Bwana akamwambia Musa: Kwenda kwa watu . . . (na kuwaambia ya kwamba) siku ya tatu Bwana atashuka kwa macho ya watu wote juu ya mlima Sinai. 12 Na* ***utaweka mipaka*** *kwa watu pande zote ukisema: Mujiangalie wenyewe musipande mlima wala kugusa mpaka wake; mtu anayegusa mlima, hakika* ***atauawa****; 13 mkono hautaugusa, lakini hakika atatupiwa mawe, au kutobolewa; akiwa nyama au mtu, hakika hataishi; . . . 16 Na ilikuwa siku ya tatu, wakati ilipokuwa asubui, zilikuwa* ***radi*** *na* ***lalo****, na* ***wingu zito*** *juu ya mlima,* ***sauti ya baragumu nguvu sana;*** *watu wote waliokuwa kambini wakatetemeka. 17 Musa akatoa watu toka kambi kukutana na Mungu; wakasimama kwa upande wa chini wa mlima. 18 Mlima Sinai mzima* ***ukatoa moshi****, kwa sababu Bwana alishuka juu yake katika* ***moto****;* ***moshi wake ukapanda kama moshi wa tanuru, mlima mzima ukatetemeka sana.*** *19 Na* ***wakati sauti ya baragumu ilipozidi kulia nguvu sana*** *. . .20* ***Bwana akashuka*** *juu ya mlima Sinai . . .*
>
> (Kutoka 20) *1 Mungu akasema maneno haya yote akisema: 2* ***Mimi ni Bwana*** *Mungu wako ambaye alikutoa katika inchi ya Misri, toka nyumba ya utumwa.*
>
> **1)** ***Usiwe na miungu mingine*** *ila mimi. (sh.3)*
>
> **2)** ***Usijifanyie sanamu ya kuchonga*** *. . . kwa kuwa mimi ni Bwana Mungu wako (mash. 4,5)*
>
> **3)** ***Usitaje jina la Mungu wako bule****; maana Bwana hatamhesabu ya kuwa hana kosa mwenye kutaja jina lake bule. (sh.7)*
>
> **4)** ***Kumbuka siku ya sabato*** *uitakase. (sh.8)*

**5)** ***Heshimu baba yako na mama yako***. *(sh.12)*

**6)** ***Usiue***. *(sh.13)*

**7)** ***Usizini.*** *(sh.14)*

**8)** ***Usiibe***. *(sh.15)*

**9)** ***Usishuhudie jirani yako uwongo***. *(sh.16)*

**10)** ***Usitamani*** *nyumba ya jirani yako, usitamani mke wa jirani yako, wala mtumishi wake, wala kijakazi wake, wala ngombe yake, wala punda yake wala cho chote kilicho cha jirani yako. (sh.17)*

*18 Watu wakaona radi na lalo, na sauti ya baragumu, na mlima ukitoa moshi; . . .* ***wakatetemeka, wakasimama mbali.*** *19 Wakamwambia Musa: Sema wewe nasi na tutasikia; lakini Mungu asiseme nasi tusife. 20 Musa akawaambia watu: Musiogope; Mungu amekuja kuwapima ninyi, na* ***woga wake*** *uwe mbele yenu musikose. 21* ***Watu wakasimama mbali. . .***

Tutaacha hapa leo kusoma Maandiko**.** Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaangalia Amri Kumi zote moja moja ambazo Mungu aliwapa Waisraeli juu ya Mlima Sinai. Lakini mbele ya kuagana leo, kuna neno lingine ambalo Mungu anataka kutufundisha kwa njia ya maneno ambayo tulisoma sasa tu. Lazima tufahamu neno hili: **Mungu ni Mtakatifu na hatuwezi kamwe kumkaribia kamwe kwa njia ya kazi yetu wenyewe.** Maandiko yanasema ya kwamba *"Miili yote ni kama **majani**"* (1 Petro 1:24) na *"Mungu wetu ni **moto wa kuteketeza!**"* (Waebrania 12:29) Sisi sote tunajua nini inatokea juu ya moto unaowaka!

Kwa mwanzo wa somo letu leo, tulisikia Waisraeli wakisema na Musa, *"Yote Bwana aliyosema tutafanya!"* Walisema hivi kwa sababu **hawakutambua utakatifu wa Mungu.** Walifikili waliweza kupendeza Mungu kwa njia ya kazi zao wenyewe. Lakini, wakati Mungu alipokwisha kuwatokea juu ya Mlima Sinai, mafikili yao yaligeuka kabisa! Wakati Waisraeli walipoona lalo na mangurumo na mlima ukiwaka kwa moshi na kusikia sauti ya Bwana, ***wakatetemeka,*** *wakasimama mbali. Wakamwambia Musa: Sema wewe nasi na tutasikia; lakini Mungu asiseme nasi* ***tusife***.

Hivi Waisraeli walianza kufahamu utakatifu wa Mungu na ya kuwa hawakuweza kumkaribia kwa nguvu na uzuri wao wenyewe. Pale kwa mguu wa Mlima Sinai walianza kutambua kweli ya Maandiko ya kwamba *"Miili yote ni kama majani"* (1 Petro 1:24) na

*"Mungu wetu ni moto wa kuteketeza!"* (Waebrania 12:29) Wakisimama pale mbele ya Mungu Mtakatifu, Waisraeli waliweza kusema kweli "Si neno. Tutafanya maneno yote ambayo Bwana alisema!"? Sivyo, hata kidogo! Sasa Waisraeli walifahamu ya kwamba **neno gumu sana** lilikuwa limewapata! Walifahamu kidogo utakatifu wa Mungu na ya kwamba ilikuwa lazima kwao kutii amri zake; walifahamu vilevile ya kwamba wao si watakatifu na hawataweza kushika sheria kamilifu ya Mungu. Walifahamu ya kwamba **walifanana na majani ya kukauka mbele ya moto unaowaka!**

Basi wewe? Unafahamu utakatifu wa Bwana? Unafahamu ya kwamba Mungu na sheria yake ni haki na takatifu? Unafahamu ya kwamba moyo wako na kazi zako si haki na hazitimii mbele ya Mungu? Au wewe ni kama Waisraeli waliofikili, "Si neno; tutaweza kufanya neno lo lote Mungu analotaka. Tutakaribia Mungu na matendo yetu mema!" Kweli mawazo namna hii hayapatani na mafikili ya Mungu. Watu walio wachafu rohoni na kuchafuwa na zambi wanaweza kukaa pamoja na Yule aliye safi na mtakatifu? Sivyo, haiwezekani. Mungu anaweza kukubali maneno yaliyo mema kwa sehemu na mabaya kwa sehemu? Sivyo, hatafanya hivi; ndiyo **hawezi** kufanya hivi. Mungu ni mtakatifu naye hawezi kukubali mambo yasiyo matakatifu. Anataka ukamilifu. **Umefahamu neno hili?** Au unataraji ya kwamba, siku nyingine, siku ya hukumu, matendo yako **"mema"** yatazima matendo yako **maovu**? Kama ingalikuwa hivi, **Mungu asingalikuwa mwamuzi wa haki**! Kwa mfano, utafikili nini juu ya mwamuzi anayemwambia mwuaji, "Umetenda uuaji, lakini kwa sababu ya matendo yako mema uliyofanya mbele, sitakuhukumu. Wewe ni huru." Tungesema nini juu ya mwamuzi anayefanya hivi? Tungesema yeye ni mzalimu na hahukumu kwa haki.

Rafiki, **Mungu ni Mwamuzi wa haki!** Hawezi kuona zambi bule! Ni lazima kwa Bwana Mungu anayehukumu dunia kutenda yaliyo haki! **Haki ya Mungu inalazimisha malipo kwa zambi.** Na malipo yale ni **mauti na kutengwa na Mungu kwa milele!** Matendo yetu mema hayawezi kuzima deni yetu ya zambi. Maandiko Matakatifu yanasema juu ya matendo yetu mema: *"Sisi sote tumekuwa kama kitu kichafu, na haki zetu zote ni kama vitambaa vya kupasukapasuka!"* (Isaya 64:6) **Mungu** ni **moto wa kuteketeza** na **matendo mema** ya wana wa Adamu ni kama **majani ya kukauka**. Hatuwezi kusimama mbele ya moto wa kuwaka wa hukumu takatifu ya Mungu na haki yetu wenyewe!

Waisraeli walijasiri kukaribia moto wa Mungu ulioshuka juu ya mlima Sinai? Walijaribu kupanda mlima kufika kwa pahali Mungu alipokuwa? Walikaribia na ukaramisu mlima uliotetemeka na kunguruma na ngurumo na lalo, ule mlima toka ndani yake ulitoka moshi kama kutoka tanuru? Sivyo, hawakuukaribia! **Walisimama mbali na kutetemeka kwa woga!** Hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa na ukaramisu kukaribia mlima kwa sababu waliogopa sana utakatifu wa Bwana Mungu na uwezo wa kuogofya. Lakini woga hili lililikuwa vizuri, kwa sababu Neno la Mungu linasema: ***"Kuogopa Bwana ni mwanzo wa maarifa!"*** (Mezali 1:7).

Saa inakwisha kwa leo. Lakini tunakusihi kukaa kukumbuka maneno uliyosoma sasa tu: ya kwamba

**Mungu ni mtakatifu** na **ni lazima kwake kuhukumu watu** sawasawa na **kipimo chake** cha utakatifu.

**Mungu ni mtakatifu** na hawezi kuona zambi bule.

**Mungu ni mtakatifu** na hatuwezi kumkaribia kwa njia ya kazi zetu wenyewe!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaangalia na kueleza Amri Kumi ambazo Mungu aliwapa Waisraeli pale juu ya mlima Sinai.

Mungu akubariki na kukaa kukufundisha wakati unapowaza juu ya kweli hii kubwa toka Neno lake:

***"Woga wa Bwana ni mwanzo wa maarifa!"*** (Mezali 1:7)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 37

# AMRI TAKATIFU

### KUTOKA 20

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na somo lingine la mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele, tuliona ya kwamba **mlima mzima wa Sinai ulitoa moshi** kwa sababu Bwana alikuwa ameshuka juu yake ndani ya moto, na mangurumo na lalo kutoa Amri Kumi kwa watu wa Israeli. Mungu alionya Waisraeli wasiguse mlima pahali alipokuwa wasife. Mungu alitaka kuwafundisha **utakatifu** wake!

Leo tunataka kuangalia Amri Kumi hizi moja moja pamoja na kufikili juu ya maisha yetu wenyewe tuweze kufahamu hali yetu mbele ya Mungu Mtakatifu. Tutasoma ndani ya Kutoka 20. Wakati Mungu alipokwisha kushuka juu ya Mlima Sinai katikati ya moto na moshi, alisema maneno haya: *"Mimi ni Bwana Mungu wako ambaye alikutoa katika inchi ya Misri, toka nyumba ya utumwa."* (Kutoka 20:1,2)

1) ***"Usiwe na miungu mingine ila mimi."*** (Kutoka 20:3) Hii ni amri ya kwanza. Bwana Mungu alisema, *"Usiwe na miungu mingine ila mimi."* Sharti yeye pekee awe Mungu wetu. Hataacha mwingine kushiriki ndani ya utukufu wake. Sharti tuabudu Mungu Mwumba tu. Hatuoni neno hili ndani ya inchi yetu au dunia pia. Watu wanatukuza mtu kwa pahali Mungu tu anapostahili kupewa. Jina lake tu ni takatifu na la kuogopesha. Yeye tu anastahili tumaini na kuabudu kwetu. Lakini wakati watu wanapopata matata, hawageuki kwa Mungu na kuomba kwake aliyeumba vitu vyote na anayeweza kufanya maneno yote. Sivyo, lakini wanatumainia watu wengine kama wao wenyewe na kuwapa heshima inayotosha kwa Mungu tu. Wale wanaofanya hivi wana mungu mwingine. Ni zambi kuwa na mungu mwingine!

2) Ndani ya amri ya pili Mungu alisema: ***"Usijifanyie sanamu ya kuchonga . . . usiiname mbele yao kuzitumikia; kwa kuwa mimi Bwana Mungu wako ni Mungu mwenye wivu!"*** (Kutoka 20:4,5) Ndani ya agizo hili, Mungu anasema nasi kukaa mbali na sanamu. Sanamu si mifano tu inayochorwa na kuabudiwa kwa pahali fulani. Sanamu ni **kitu cho chote** ambacho kinatutenga na Mungu. Kwa watu wengine sports ni mungu wao kwa sababu sports ni neno kubwa kupita Mungu ndani ya maisha yao. Kwa watu wengine television inawagawa na Mungu. Hawaweki roho juu ya kusoma Neno la Mungu na kujaribu kulifahamu; hawana saa kwa kitu cho chote ila kuangalia television. Na kuna wengine wanaovaa hirizi zinazoonyesha ya kamba Mungu hatoshi kwa kuwalinda. Ndani ya maisha ya wengine mali ni kwa pahali pa kwanza. Wanafanya hata maneno yasiyopendeza Mungu kwa kupata faida kupita. Kwa watu namna hii mali ni mungu wao. Neno lo lote linaloondosha Mungu kwa pahali pake pa kwanza ni sanamu.

3) Ndani ya agizo la tatu, Mungu alisema: ***"Usitaje jina la Mungu wako bule; maana Bwana hatamsamehe ya kuwa hana kosa mwenye kutaja jina lake bule."*** (Kutoka 20:7) Ndiyo, Mungu hataki tutaje jina lake takatifu bule. Lakini karibu kila siku unaweza kusikia mtu akitolea jirani yake ahadi akisema, Mungu akitaka nitafanya neno fulani au kwenda pahali fulani, lakini rohoni mwake hakusudi hata kidogo kufanya hivi. Hakumbuki mapenzi ya Mungu hata kidogo. Anatumia tu jina la Mungu ili jirani yake aweze kuamini wongo zake. Neno hili ni zambi. Wengine wanasema, "Mungu anajua sikufanya neno lenyewe", hata kama wakijua kwamba walilifanya! Labda mtu mwingine atasema, "Mungu anajua ya kwamba siwezi kufanya neno namna hii," lakini ni uwongo. Watu namna hii wanataja jina la Mungu bule. Neno la Mungu linasema, *"Maneno yenu yawe, 'Ndiyo, ndiyo'; 'siyo, siyo', kwa maana neno zaidi ya haya linatoka kwa yule mwovu."* (Matayo 5:37)

4) Ndani ya amri ya ine, Mungu alisema na wana wa Israeli: ***"Kumbuka siku ya sabato uitakase. Siku sita utatumika na kufanya kazi zako zote . . . Maana kwa siku sita Bwana akafanya mbingu na inchi, bahari na vyote vilivyo ndani yao, akapumzika siku ya saba."*** (Kutoka 20:8,9,10) Amri hii inaonyesha ya kwamba Mungu alitaka wana wa Israeli kupumzika kila siku ya saba **kumheshimu yeye.**

5) Ndani ya amri ya tano Mungu aliyotoa, alisema: ***"Heshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika inchi ambayo Bwana Mungu wako anakupa wewe."*** (Kutoka 20:12) Hapa tunaona ya kwamba wazazi wetu wanastahili kupokea **heshima** toka kwetu. Hatuoni neno hili kwa wakati wa sasa. Tunaona watoto wakisema na wazazi wao bila adabu na kuzarau masemo ya wazazi wao. Hawaheshimu wazazi; wanawakasirisha tu. Haya si mafundisho ya amri ya tano. Ni mapenzi ya Mungu kwa watoto kupenda wazazi wao, kuwaheshimu na kuwatii ndani ya maneno yote yanayopendeza Mungu na kupatana na kutaka kwake.

6) Ndani ya amri ya sita, Mungu alisema: ***"Usiue."*** (Kutoka 20:13) Hapa Mungu anasema: Mtu anayeua mtu mwingine, anakosea Mungu, kwa sababu Mungu ndiye anayeleta uzima na nafsi kwa kila mtu. Kuua mtu ni kuchukia Mungu, kwa sababu Mungu alifanya mtu kwa sura yake mwenyewe. Neno la Mungu linaonyesha vilevile uuaji si kuondoa uzima wa mtu tu, kwani Maandiko yanasema: *"Kila mtu anaye**chukia** ndugu yake ni mwuaji."* (1 Yoane 3:15) Watu wengi hawakumbuki ya kwamba Mungu hahukumu mtu tu kwa neno alilofanya, lakini kwa neno analotaka kufanya, maana yake anamhukumu kwa makusudi yake! Mungu anatazama roho na hivi kuchukia na uuaji ni zambi sawasawa machoni mwake.

7) Ndani ya amri ya saba Mungu alisema: ***"Usizini."*** (Kutoka 20:14) Ndoa ni zawadi ya damani toka Bwana. Mungu anajua nini ni nzuri zaidi kwa sisi, na kwa sababu hii, wakati anapokwisha kumpa mtu mke awe mke wake, anataka mtu huyu kubaki na mke huyu mmoja na kukataa kutamani hata kidogo wanawake wo wote wengine. Neno la Mungu linasema ya kwamba *"inafaa waume kupenda wake wao wenyewe kama miili yao wenyewe"* (Waefeso 5:28), na ya kwamba *"kila mtu ambaye ataondosha mke wake ila kwa sababu ya uasherati, na kuoa mwingine, anazini."* (Matayo 19:9) Wakati watu wanapoasi sheria ya Mungu na kufanya neno linalokatazwa, mara nyingi wanavuna ndani ya miili yao matunda mabaya ya matendo yao. Kwa sababu hii watu wanapata gonjwa mbaya sana wakati wanapotenda uzini. Vizuri ujue vilevile ya kwamba uzini si tendo la mwili tu, lakini tunaweza kuzini na nia zetu vilevile. Maandiko yanasema: *"Kila mtu anayetazama mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake."* (Matayo 5:28)

8) Ndani ya Amri ya nane Mungu alisema: ***"Usiibe."*** (Kutoka 20:15) Agizo hili ni wazi. Lakini, sharti tufahamu ya kwamba, kwa macho ya Mungu Mwamuzi wetu, kuiba si **kukamata** tu mali au vitu visivyo vyako. Hata kama uki*taka* tu kukamata vitu vya mtu mwingine, lakini huvikamati, wewe ni mwizi moyoni mwako. Mungu anaangalia moyo. Tunaweza kuwa mwizi kwa njia mbali-mbali. Kwa mfano, bwana wako wa kazi anakupa kazi fulani kufanya, na anakulipa mshahara kufanya kazi ile, naye anafikili unatumika kazi wakati unapopoteza saa bule, basi wewe ni mwizi. Ndiyo, umeiba faida ambayo bwana wako ya kazi angaliweza kupata. Halafu azabu kwa wizi na kwa zambi zote nyingine ni nini? Ni kufa na kuingia moto usiozimika kamwe!

9) Amri ya tisa inasema: ***"Usishuhudie jirani yako uwongo."*** (Kutoka 20:16) Agizo hili ni wazi kabisa vilevile. Bwana Mungu ni Mungu wa kweli na hawezi kukubali wongo. Watu wanafikili si neno kusema wongo ndogo kuepuka matata na kuchunga salama. Lakini kwa macho ya Mungu wa kweli hakuna "uwongo mdogo!" Mungu anasema: Kila mtu anayesema uwongo ni wa **Shetani**, *"yeye ni mwongo, na baba ya wongo"* (Yoane 8:44) Shetani alisema wongo kwa wazazi wetu, Adamu na Hawa, na anakaa kudanganya watu na wongo zake! Mtu ye yote anayesema uwongo ni wa Shetani.

10) Ndani ya amri ya kumi Mungu anasema: ***"Usitamani nyumba ya jirani yako, usitamani mke wa jirani yako, wala mtumishi wake, wala kijakazi wake, wala ngombe yake, wala punda yake, wala cho chote kilicho cha jirani yako."*** (Kutoka 20:17) Agizo hili linaonyesha wazi ya kwamba Mungu anajua kabisa uovu wa moyo wa mtu. Tamaa na choyo zinapatikana ndani ya **mioyo** ya wana wa Adamu. Mioyo yetu miovu inatufanyiza kutamani mke wa mtu mwingine au kukaza macho juu ya kitu cho chote cha mtu mwingine tusicho nacho. Neno hili ni zambi, kwa sababu Neno la Mungu linasema: *"Hatukuleta kitu duniani, tena ni kweli ya kuwa hatuwezi kutoka na kitu; lakini tukiwa na chakula na nguo, kwa vitu hivi tufurahi."* (1 Timoteo 6:7,8)

Hizi ndizo Amri Kumi ambazo Mungu alitolea Musa na wana wa Israeli.

Basi tumalize somo letu la leo namna gani? Labda tunaweza kulimaliza na ulizo. Ulizo lenyewe ni hili: "**Mimi** nimetii Amri Kumi

**zote**? Labda umejifunza mbele ya kwamba wakati Mkombozi wetu mtakatifu alipokuja duniani, alijumliza Amri Kumi na masemo mafupi mawili. Alisema:

1) ***"Upende Bwana wako na moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote!*** na

2) ***Penda jirani yako kama wewe mwenyewe.*** *Katika amri hizi mbili inategemea torati yote na manabii."* (Matayo 22:37,39,40)

Halafu ukitaka kujipima mwenyewe kuona kama ulishika Amri Kumi ambazo Mungu alitolea Musa, unaweza kujiuliza maulizo mawili:

1) **Ninapenda Mungu na akili yangu yote?**

2) **Ninapenda jirani yangu kama mimi mwenyewe?**

Jibu ulizo la kwanza na roho ya kweli. Unapenda **Mungu** na akili yako yote? Unampenda na moyo wako wote? Mungu na Neno lake ni kwa pahali pa kwanza ndani ya maisha yako?

Basi jibu lako kwa ulizo la pili ni nini? Jibu na roho ya kweli. Unapenda **jirani** yako kwa kipimo unachojipenda mwenyewe? Unaweka faida ya watu wengine mbele ya faida yako mwenyewe ndani ya maneno yote unayofanya? Unalinda wenzako namna unavyojilinda mwenyewe? Unatendea wengine maneno unayotaka wakutendee wewe?

Kama usipoweza kujibu maulizo haya na "ndiyo", vizuri ufahamu ya kwamba mbele ya Mungu wewe ni **mwenye kuvunja sheria**. Kazi zako njema zote haziwezi kukupatia kitu ila laana ya milele ya hukumu ya haki ya Mungu. Maandiko yanasema: *"Wenye woga, na wasioamini, na wenye machukio, na wauaji, na wazini, na wachawi, nao wanaoabudu sanamu, na wawongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa linalowaka moto na kiberiti."* (Ufunuo 21:8)

Mungu ni mtakatifu na hawezi kuvumilia maneno maovu. Yeye ni mkamilifu na hawezi kupokea kazi zo zote zisizo kamilifu. Kwa sababu hii Maandiko yanasema: *"**Mtu anayeshika sheria yote, lakini akakosa katika neno moja tu, amekosa juu ya yote!**"* (Yakobo 2:10) Kujaribu kushika Amri Kumi hakuwezi kusaidia mtu *kuhesabiwa haki mbele ya Mungu*. Kwa sababu *"**wote** wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu!"* (Waroma 3:20,23) Ndiyo, Neno la Mungu linasema wazi: *"**Wote** wamefanya zambi"* na *"**Wote** walio wa matendo ya sheria ni chini ya laana."* (Wagalatia 3:10)

Labda mtu mmoja atauliza, "Basi **kwa sababu gani Mungu alitolea watu Amri Kumi** kama hakuna mtu anayeweza kuzitii?" Hili ni ulizo kubwa na, Mungu akitaka, tutasikia jibu la Mungu ndani ya somo la nyuma.

Mungu akubariki na kukufunulia kweli kubwa ya shairi hili:

> ***"Mtu anayeshika sheria yote, lakini akakosa katika neno moja tu, amekosa juu ya yote!"*** (Yakobo 2:10)

## Somo 38

# Kusudi la Amri Kumi

## Kutoka 20

Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na mfulizo wetu.

Ndani ya masomo mawili ya mbele, tuliona ya kwamba Mungu alishuka juu ya Sinai ndani ya moto, ngurumo na lalo kuwapa makabila ya Israeli amri zake takatifu kumi. Ndani ya amri ya kwanza Mungu alisema nao: **Usiwe na miungu mingine ila mimi.** Ndani ya amri ya pili: **Usijifanyie sanamu ya kuchonga**. Ya tatu: **Usitaje jina la Mungu wako bule.** Ya ine: **Kumbuka siku ya sabato uitakase**. Ya tano: **Heshimu baba yako na mama yako**. Ya sita: **Usiue**. Ya saba: **Usizini**. Ya nane: **Usiibe**. Ya tisa: **Usishuhudie jirani yako uwongo.** Ya kumi: **Usitamani cho chote kilicho cha jirani yako.**

Hizi ndizo Amri Kumi Mungu alizotolea Musa na Waisraeli. Mungu aliweka mzigo mzito juu yao na kuwaambia: Mtu ye yote anayeweza kufanya **kabisa kila kitu** kinachoagizwa na amri hizi kumi anaweza kukaa pamoja na Mungu kwa milele. Lakini mtu ye yote anayeshika sheria nzima lakini anaanguka kwa **neno moja**, ni kama anaanguka kwa maneno yote, na atatengwa nami **kwa milele!**

Hii ndiyo njia ya utakatifu ambayo Mungu alitolea makabila ya Israeli juu ya Mlima Sinai. Mungu aliagiza wamtii ndani ya maneno **yote**! Ndiyo, ndani ya **kila kitu**! Wenye zambi wanaweza kushika amri zote za Mungu? Sivyo, hawawezi! Hata hivi, hili ndilo neno Mungu, Mungu Mtakatifu analotaka kabisa! Hivi **neno kubwa tunalouliza** leo ndilo hili: **Kwa nini Mungu alitolea wana wa Israeli Amri hizi Kumi kama alijua hakuna mtu hata mmoja atakayeweza**

**kuzishika kabisa?** Kwa nini Mungu aliweka mzigo mzito namna hii juu ya wazao wa Adamu?

Tuliona ya kwamba wana wa Israeli walisema, *"Yote Bwana aliyosema tutafanya!"* Lakini Mungu alijua ya kwamba hawataweza kufanya yote aliyoagiza. Waisraeli hawakufahamu ya kwamba walikosa nguvu kutimiza mapenzi ya Mungu kabisa. Hawakutambua ya kwamba walikuwa mbali sana na Mungu na utukufu wake mkubwa. Ni kwa sababu ya neno hili tu Mungu aliwapa Waisraeli amri hizi kumi kamilifu, akiwaambia: **Muzishike zote, kama mukiweza! Lakini mtu ye yote anayeanguka hata kwa neno moja atatengwa nami kwa milele!**

Kwa njia ya amri hizi nzito Mungu alikusudi **kufahamisha makabila ya Israeli ya kwamba hawakuweza kumpendeza**. Mungu alijua ya kwamba wana wa Israeli hawakuweza kutii maagizo yake yote, lakini Waisraeli walikuwa hawajafahamu neno hili. Walikuwa kama zaidi ya watu wa dini kwa wakati wa sasa wanaofikili ya kwamba Mungu anataka sisi kujaribu kutenda mema tu na ya kwamba Siku ya Hukumu, kama hesabu ya matendo yetu mema inapita ile ya matendo yetu mabaya, Mungu atasema nasi, "Kuja na kukaa karibu nami kwa milele!" Lakini watu wanaofikili hivi wanaanguka na hawajui Maandiko Matakatifu au utakatifu wa Mungu. Mungu ni mkamilifu, na hawezi kuona bule hata zambi moja!

Kwa kueleza, babu yetu Adamu alifanya zambi ngapi mbele ya kufukuzwa na Mungu toka Paradiso? Zambi kumi? Au mia moja? Labda elfu moja? Sivyo! Zambi moja tu! Kwa sababu ya **zambi moja** tu ilipasa Adamu kuondokea Paradiso!

Nyuma ya zambi moja tu Adamu hakuwa mkamilifu tena mbele ya Mungu!

Kwa sababu ya zambi ile moja hakuweza kukaribia Mungu tena!

Kwa sababu ya zambi ile moja ilimpasa kufa!

Zambi ile moja ilimpatia nafasi ndani ya moto wa milele!

Ndiyo, Mungu ni mtakatifu na hawezi kuona zambi kama kitu kidogo! Kwa sababu hii aliwaambia wana wa Israeli: *"Mtu anayeshika sheria yote, lakini akakosa katika **neno moja** tu, amekosa juu ya **yote**."* (Yakobo 2:10)

Basi kama utakatifu wa Mugu ni hivi, tunataka kujua neno hili: **Kwa sababu gani Mungu alitolea Waisraeli Amri Kumi kama ali-**

**jua ya kwamba hakuna mtu hata mmoja wao atakayeweza kuzitii kabisa?** Sikiliza jibu la Mungu: *"Kwa kazi ya sheria hapana mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele yake; kwa sababu* ***kwa njia ya sheria zambi inajulikana****."* (Waroma 3:20) Hivi kusudi la Amri Kumi ni nini? Kuondosha zambi? "Sivyo," Mungu anasema, "kusudi la Amri Kumi ni **kufunua** zambi!"

Ulifahamu neno hili? Kwa nini Mungu alitolea Musa na wana wa Israeli amri zake kumi? Aliwatolea amri hizi ili kwa njia ya kuzitii waweze kujipatia njia kuingia Paradiso? Sivyo! Neno hili haliwezekani kwa sababu Mungu anasema, "Kama musipotii **zote**, mumehukumiwa!" Wana wa Adamu wanaweza kutii Mungu ndani ya maneno **yote** ambayo aliagiza? Inawezekana kuteka maji safi toka chungu cha maji machafu? Haiwezekani hata kidogo!

Basi kusudi la Amri Kumi ni nini? Maandiko yanasema: "Kusudi la maagizo ni **kufunua zambi!"** Mungu hakutoa maagizo haya kutuokoa toka hukumu yake. Mungu aliyatoa kutuonyeshea ya kwamba tuko **wenye zambi waliohukumiwa** na ya kwamba t**unahitaji Mwokozi!** Neno hili ni wazi kwa mafikili yako?

Amri kumi ni kama machine ya **X-ray** ndani ya hopital. Kama mimi nina ugonjwa na sijui kama ni nini ambayo inanitesa, labda mganga atajaribu kuangalia ndani ya mwili wangu kwa njia ya X-ray. Kazi ya photo ya X-ray ni nini? Ni kuonyesha **nini ni mbaya ndani ya mwili wangu**. Vivyo hivyo, maagizo matakatifu Mungu aliyotolea Musa ni kama machine ya X-ray ndani ya hopital. Kazi yao ni kuonyesha ubaya, ndiyo **zambi ndani ya nafsi na roho yangu**. Namna gani Amri Kumi zinaweza kufunua zambi ndani ya roho yangu? Inawezekana hivi: Nikisawanisha mwenendo wangu na sheria takatifu ya Mungu, ninafahamu ya kwamba mimi ni mbali sana na Mungu—kwa njia ya mafikili yangu, masemo yangu na matendo yangu. Wakati **ninapoangalia sheria ya Mungu** na halafu **ninajiangalia mwenyewe**, ninajua nimekosea Mungu, na watu vilevile, na ya kwamba **siwezi kupata ruhusa kutokea mbele ya Mungu mtakatifu!**

Kama machine ya X-ray ikiwa na faida **kuonyesha** neno gani ni baya ndani ya mwili wa mtu, vivyo hivyo Amri Kumi zina faida **kuonyesha** maneno yaliyo mabaya rohoni mwa mtu. Lakini, kama X-ray **haiwezi kuponyesha** mgonjwa, vivyo hivyo Amri Kumi **haziwezi kuponyesha** roho yangu inayojaa zambi. Kwa roho yangu

kuponyeshwa inanipasa kurudi karibu na Mganga Mkubwa , maana yake Mungu. Mungu tu ana shauri kuniokoa toka mauti na hukumu ambazo zinaningojea kwa sababu ya zambi rohoni mwangu.

Labda mtu mwingine anasema: "Ngoja kwanza, rafiki! Mimi ni mtu mzuri. Mimi si kama watu wale wengine wanaoiba, kudanganya watu na kutenda uzini!" Ukifikili hivi, ni kama hujafahamu bado utakatifu wa Mungu! Sharti ujue ya kwamba siku ya hukumu **Mungu hatakusawanisha na jirani yako mwenye zambi. Atakusawanisha na sheria yake takatifu,** inayosema: *"Mtu anayeshika sheria yote, lakini anakosa katika **neno moja** tu, amekosa **juu ya yote**!"* (Yakobo 2:10) Mungu yule anayesema: "Usizini" anasema vilevile, "Usiseme uwongo!" Hivi, hata kama hukutenda uzini, lakini ulisema uwongo mmoja tu, umevunja sheria nzima (ona Yakobo 2:11) na huwezi kutokea mbele ya Mungu katika Paradiso, kwa sababu Maandiko yanasema: *"**Ndani yake hakitaingia kabisa kitu cho chote kilicho kichafu**, wala yeye anayefanya machukizo na uwongo."* (Ufunuo 21:27) Fahamu neno moja kabisa: Hatuwezi kamwe kupendeza Mungu kwa njia ya kazi zetu wenyewe! Maandiko ya Mungu yanatangaza neno hili wazi:

> *"Sisi sote tumekuwa kama **kitu kichafu** na haki zetu zote ni kama **vitambaa vya kupasukapasuka vya taka**."* (Isaya 64:6) Mungu anahukumu watu wote kama wenye zambi. *"Hakuna mwenye haki, hata mmoja. Wote wametoka kwa njia, wote wamekuwa pasipo faida; hakuna mwenye kufanya mema, hata mmoja. Hapana tofauti; kwa sababu wote wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."* (Waroma 3:10,12,22,23)

Basi kama hii ndiyo hali yetu mbele ya Mwamuzi wetu, namna gani tutaweza kuepuka azabu yake? Inatupasa kufanya nini kwa kuokolewa? Tuna tumaini gani? Hatuna tumaini kama tukitegemea **kazi zetu wenyewe.** Lakini Mungu ashukuriwe, ametayarisha **njia kuokoa** wana wa Adamu toka azabu ya zambi!

Tuendelee sasa ndani ya Tora, na kusoma toka Kutoka sura 20. Utaona pale njia Mungu aliyotayarisha kwa wana wa Israeli kuokolewa toka laana iliyo juu yao kwa sababu ya sheria yake takatifu. Wakati Mungu alipokwisha kutolea Waisraeli Amri Kumi Maandiko yanaendelea kusema:

> (Kutoka 20) *18 Watu wakaona radi na lalo na sauti ya baragumu, na*

> *mlima ukitoa moshi; na wakati watu walipoona maneno yale wakatetemeka, wakasimama mbali . . . 21 Musa akakaribia giza zito pahali Mungu alipokuwa. 22 Bwana akamwambia Musa: Utasema hivi na wana wa Israeli: Ninyi wenyewe mumeona ya kama nimesema nanyi toka mbingu . . . 24* ***Mazabahu*** *ya udongo utanifanyia na* ***kutoa sadaka*** *zako za kuteketezwa juu yake, na sadaka zako za salama, kondoo zako na ngombe zako juu yake;* ***kwa kila pahali nitakapokumbusha jina langu nitakuja kwako na kukubariki.****"*

Hivi, Musa aliandika maneno yote ambayo Mungu alikuwa amemwagiza. Kisha, asubui mapema Musa alisimamisha mazabahu kwa mguu wa Mlima Sinai kama Mungu alivyokwisha kuagiza. Wakati alipokwisha kuifanya, aliagiza vijana wengine wa wana wa Israeli kutoa sadaka za ngombe ndume, kukusanya damu yao ndani ya mabakuli, na kuteketeza nyama juu ya mazabahu. Kisha Musa alinyunyiza damu ya ngombe ndume juu ya mazabahu, juu ya kitabu cha agano ndani yake aliandika Amri Kumi, na juu ya makutano, akasema, *"Tazameni* ***damu ya agano*** *Bwana alilofanya pamoja nanyi."* (Kutoka 24:4-8)

Hivi tunaona Musa, akiagizwa na Mungu, akifanya mazabahu, akitoa sadaka za nyama, na kunyunyiza damu yao juu ya makutano ya Israeli. Sababu yake nini? Mungu alitaka kukumbusha Waisraeli neno alilofundisha wazazi wao, ndio Adamu, Abeli, Noa, Abrahamu, Isaka na Yakobo, ya kwamba ***"pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo."*** (Waebrania 9:22) Sharti kila mtu aliyetaka kukaribia Mungu afanye hivi na sadaka isiyo na kipako.

Kwa nini Mungu aliagiza sadaka hizi zote za nyama kutolewa? Kwa sababu yeye ni mwenye haki, na sheria yake takatifu inasema ya kwamba **azabu** hata kwa zambi ndogo sana ni mauti na hukumu ya milele, mbali na Mungu na utukufu wake mkubwa. Na kwa sababu wana wa Israeli hawakuweza kushika amri zake takatifu zote, iliwapasa kuletea Mungu zabihu pasipo kipako, ili nyama hawa **wasiokuwa na kosa** waweze kukomboa **wenye hatia**. Lakini, kama tulivyojifunza mbele, sadaka za nyama hazikuweza kuondoa zambi, ziliweza kufunika tu zambi za mtu, kufika wakati Mungu alipotuma **Mkombozi mtakatifu** duniani. Mkombozi huyu atajitoa na roho tayari kama Sadaka ya mwisho kwa zambi.

Leo tunafurahi sana kwa sababu Mwokozi huyu alikuja na kulipa kwa zambi zetu mara moja kwa milele. Unajua jina lake? Ndiyo,

ni **Yesu.** Maana ya jina hili Yesu ni ***Bwana anaokoa.*** Yesu hakuwa na baba ya dunia. Alikuja toka mbinguni. Hakuriti tabia ya zambi inayopatikana ndani ya wazao wote wa Adamu. Yesu alitii Amri Kumi kabisa bila kuanguka ndani ya neno hata moja. Kwa sababu hakuwa na zambi, aliweza kutoa uzima wake kama sadaka kuondoa zambi za wote ambao wanamwamini. Kwa sababu ya sadaka kamilifu ya Mkombozi, Mungu anaweza kututangazia wewe na mimi haki, kwa sababu yule asiyekuwa na zambi, alivumilia azabu kwa zambi zako na zangu.

Rafiki, nyuma ya kujifunza maneno haya leo, tukumbuke maneno makubwa mawili:

1) Tujue kabisa ya kwamba **hakuna mtu anayeweza kujiokoa mwenyewe kwa njia ya kutii Amri Kumi!** Sikia tena maneno Maandiko yanayosema juu ya neno hili: Wote walio wa matendo ya sheria ni chini ya laana, maana imeandikwa: *"Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati ayafanye."* (Wagalatia 3:10) *"Maana mtu anayeshika sheria yote, lakini akakosa katika neno moja tu, amekosa juu ya yote."* (Yakobo 2:10) Hakuna mtu atakayeokolewa kwa njia ya kujaribu kushika Amri Kumi! Kusudi la amri hizi ni kufunua zambi.

2) Neno la pili ambalo inatupasa kukumbuka ni ya kwamba **Mungu tu ana shauri kuokoa wenye zambi!** Sikiliza maneno Maandiko yanayosema: *"Mungu ni mmoja tu, na mpatanishi katikati ya Mungu na watu ni mmoja, yule mtu Kristo Yesu, ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote!"* (1 Timoteo 2:5,6) Kweli, Mungu tu ana shauri kuokoa wenye zambi.

Hivi, rafiki, tunakuacha na mawazo haya mawili: **Hakuna mtu** atakayeokolewa kwa njia ya kushika Amri Kumi! Na: **Mungu tu** ana shauri kuokoa wenye zambi!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki na akusaidie kufahamu vizuri maneno tuliyojifunza leo, kwani Neno lake linasema:

> ***"Kwa maana kwa kazi ya sheria hapana mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele yake; kwa sababu kwa njia ya sheria zambi inajulikana."*** (Waroma 3:20)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 39

# AMRI ZINAZOVUNJWA

## KUTOKA 32

Salama iwe kwako, rafiki msomaji wa mfulizo *Njia ya Haki*. Ndani ya masomo matatu ya mbele, tuliona ya kwamba Mungu alisema na Waisraeli toka Sinai ndani ya moto, ngurumo na lalo kuwapa amri zake **takatifu** kumi. Tuliona vilevile ya kwamba Mungu aliagiza watu wa Israeli kusimamisha **mazabahu** kwa mguu wa Mlima Sinai na kutoa sadaka za nyama wasiokuwa na kipako.

Kwa nini Mungu aliagiza sanamu hizi za nyama? Mungu aliziagiza kwa sababu yeye ni mwenye haki na sheria yake takatifu inatangaza: *"Mtu anayeshika sheria yote, lakini akakosa katika neno moja tu, ame**kosa** juu ya yote."* Mtu ye yote anayevunja sheria ya Mungu amekosa . . . na malipo ya zambi ni mauti! (Yakobo 2:10; 1 Yoane 3:4; Waroma 6:23). Kwa sababu Waisraeli hawakuweza kushika amri zote za Mungu, iliwapasa kutolea Mungu sadaka bila kipako, ili nyama asiyekuwa na kosa aweze kufa **badala ya** mwenye zambi. Nyama alipotewa na uzima wake ili isiwe lazima kwa mwenye zambi kufanya hivi. Kwa njia hii Mungu alihakikisha ya kwamba yeye ni mwenye haki na ya kwamba hawezi kuona zambi bule kwa sababu ya kazi za mtu. Mungu anaweza kusamehe zambi kwa sababu ya damu ya zabihu kamilifu tu.

Somo letu leo linaitwa **"Amri Zinazovunjwa."** Kwa saa hii nabii Musa na makabila ya Israeli walikuwa ndani ya kambi yao mbele ya Mlima Sinai jangwani. Sasa turudi kwa Maandiko Matakatifu kuona nini ilitokea nyuma, wakati Mungu alipokwisha kuwapa Amri Kumi. Tunasoma ndani ya sura 24 ya Kutoka. Maandiko yanasema:

> (Kutoka 24) *12 Bwana akamwambia Musa:* ***Panda kwangu*** *mlimani, uwe pale; na nitakupa wewe mbao za mawe, na torati na amri,*

> *nilizoandika uwafundishe. 13 Musa* ***akaondoka, na Yosua mtumishi wake; Musa akapanda mlimani kwa Mungu.*** *14 Akawaambia wazee: Mutungoje hapa, hata tutakaporudi kwenu; na tazama, Haruni na Huri ni pamoja nanyi; mtu aliye na neno awaendee. 15 Musa akapanda mlimani, wingu likafunika mlima. 16 Utukufu wa Mungu ukakaa juu ya mlima Sinai, wingu likaufunika siku sita; siku ya saba akaita Musa toka kati ya wingu. 17 Na kuonekana kwa utukufu wa Bwana kulikuwa kama moto wa kuteketeza juu ya kichwa cha mlima kwa macho ya wana wa Israeli. 18 Musa akaingia kati ya wingu, akapanda mlimani; Musa akakuwa mlimani* ***siku makumi ine, mchana na usiku.****"*

Tusimame kwanza hapa. Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutajifunza maneno ambayo Mungu alimwambia Musa juu ya Mlima Sinai kwa muda ule wa siku makumi ine. Lakini leo tutaona nini ilifanyikana na Waisraeli waliokuwa ndani ya kambi kwa mguu wa mlima wakingojea kurudi kwa Musa. Sisi sote tunajua ya kwamba kungojea Mungu si nyepesi kwa wana wa Adamu. Ni nyepesi kupita kwa sisi kuacha kumngojea, kusahau Neno la Mungu na kufanya kutaka kwetu. Hivi, maneno tutakayosoma juu ya Waisraeli sasa ni maneno makubwa kwasi leo—makubwa sana. Mungu anataka **kutuonya** kwa njia ya habari hizi mbaya sana.

Ndani ya Sura 32 ya Kutoka tunasoma:

> *1 Na wakati watu walipoona ya kama Musa amekawa kushuka mlima, watu wakakusanyikia Haruni, wakamwambia:* ***Simama, utufanyie miungu itakayokwenda mbele yetu;*** *kwa maana huyu Musa ambaye alitutoa katika inchi ya Misri, hatujui neno gani ambalo lilimpata. 2 Haruni akawaambia: Vunjeni pete za zahabu zilizo katika masikio ya wake wa wana wenu na ya binti zenu; na kuzileta kwangu. 3 Watu wote wakavunja pete za zahabu zilizo masikioni mwao, wakazileta kwa Haruni. 4 Akazipokea mikononi mwao, akazitengeneza kwa patasi, akazifanya kuwa sanamu ya ndama kwa kuziyeyusha. Wakasema: Hii ni miungu yako, Ee Israeli, ambayo ilikutoa katika inchi ya Misri.*

Unaona maneno Waisraeli waliyofanya? Muda mfupi tu nyuma ya kusema, "Kila neno ambalo Bwana amesema tutafanya!" tunawaona wakiasi amri ya kwanza na ya pili ambazo Mungu aliwatolea sasa tu juu ya Mlima Sinai! Mungu alikuwa amesema nao:

1) *"Usiwe na miungu mingine ila mimi!"*, na 2) *"Usijifanyie sanamu!"* Lakini Waisraeli walifanya nini? Waligeuzia Mungu mgongo, wakajifanyia sanamu kwa mfano wa ndama ya ngombe namna ya sanamu walizoona katika Misri.

Kwa nini Waisraeli walikwenda mbio hivi mbali na Mungu na Neno lake? Kwa sababu walitaka **mungu ambao waliweza kuona na kugusa**. Walikuwa kama watu wa wakati wa sasa wanaochagua kuona bule Neno la Mungu na kufuata watu na mafundisho yao. Kufuata **mtu** ambaye tunaweza kuona na macho ni nyepesi kupita kufuata **Mungu** asiyeonekana na macho. Kwa sababu hii zaidi ya wana wa Adamu wanakomboa **Neno la kweli la Mungu** na **mawazo ya watu** yasiyo na msingi.

Sasa tuone nini ilitokea wakati Waisraeli walipokwisha kujifanyia ndama ya zahabu. Maandiko yanasema katika Kutoka sura 32:

> *5 Wakati Haruni alipoiona, akajenga mazabahu mbele yake. Haruni akatangaza, akasema: "Kesho itakuwa siku kubwa kwa Bwana." 6 Wakaamka asubui mapema kesho yake, wakatoa sadaka za kuteketezwa na kuleta sadaka za salama; watu wakaketi kula na kunywa, wakasimama kucheza.*

Uliona neno Haruni alilofanya? Maandiko yanasema kwamba *alijenga mazabahu mbele ya ndama na kutangaza, "Kesho itakuwa siku kubwa kwa Bwana!"* Neno hili lilikuwa kweli? Waisraeli waliweza kuabudu Bwana hivi? Sivyo, hata kidogo! Tunajua ya kwamba **Mungu hakuwa na ushirika na siku kubwa yao.** Hawakuvunja amri ya kwanza na ya pili tu lakini amri ya tatu vilevile inayosema: *"Usitaje jina la Mungu wako bule."* Walisema "Mungu Bwana! Mungu, Mungu, Mungu" na vinywa vyao, lakini walikuwa mbali sana naye mioyoni mwao. Kuabudu kwao kulikuwa bule. Maombi yao na kuinama kwao kulikuwa bule na kuliweza kukasirisha tu Mungu.

Sasa tumalize habari hizi kwa Kutoka 32:

> *7 Bwana akamwambia Musa: "Kwenda, shuka. Kwa sababu watu wako ambao uliwatoa katika inchi ya Misri wamejiharibu nafsi zao, 8 wamegeuka* ***mbio kuacha njia*** *ambayo niliwaamuru; wamejifanyia ndama ya kuyeyusha, wakaiabudu na kuitolea zabihu, wakasema: Hili ni miungu yako, Ee Israeli, ambayo ilikutoa katika inchi ya Misri. 9 Bwana akamwambia Musa: Nimeona watu hawa, na tazama, ni watu*

*wenye shingo ngumu; 10 basi uniache sasa, hasira yangu iwake juu yao, niwaharibu; na nitakufanya wewe uwe taifa kubwa."*

*11 Musa akasihi Bwana Mungu wake, akasema: Bwana, kwa nini hasira yako inawaka juu ya watu wako ambao uliwatoa katika inchi ya Misri kwa uwezo mkubwa na kwa mkono wa nguvu? 12 Kwa nini Wamisri waseme: Amewatoa kuwatendea mabaya, na kuwaua juu ya milima, na kuwaharibu toka uso wa inchi? Geuka katika hasira yako kali utubu uovu huu ulio nao juu ya watu wako. 13 Kumbuka Abrahamu, Isaka na Israeli, watumishi wako ambao uliwaapia kwa wewe mwenyewe na kuwaambia: Nitazidisha kizazi chenu kama nyota za mbingu, na inchi hii yote niliyosema juu yake nitawapa kizazi chenu, nao watairiti kwa milele. 14 Bwana akatubu ule uovu ambao alisema atatendea watu wake.*

*15 Musa akageuka, akashuka katika mlima, na zile mbao mbili za ushuhuda mkononi mwake: mbao zilizoandikwa pande zao mbili; ziliandikwa kwa upande huu na kwa upande ule. 16 Na mbao zilikuwa kazi ya Mungu, na maandiko yalikuwa maandiko ya Mungu yaliyochorwa katika zile mbao. 17 Na wakati Yosua aliposikia kelele la watu wakati walipokuwa wakipiga kelele, akamwambia Musa: Kelele la vita ni katika kambi. 18 (Musa) akasema: Hii si sauti yao wanaopiga kelele kwa sababu ya kushinda vitani, wala si sauti yao wanaolia kwa sababu ya kushindwa; lakini ninasikia sauti yao wanaoimba.*

*19 Na ilikuwa wakati alipokaribia kambi, mara moja aliona ile ndama na michezo; hasira ya Musa ikawaka, akatupa zile mbao mikononi mwake,* ***akazivunja*** *chini ya mlima. 20 Akatwaa ile ndama waliyofanya na kuichoma kwa moto, akaisaga kuwa mavumbi, akainyunyiza juu ya maji, akakunywesha wana wa Israeli nayo. 21 Musa akamwambia Haruni: Watu hawa walikufanyia nini, hata umeleta kosa hili kubwa juu yao? 22 Haruni akasema: Hasira ya bwana wangu isiwake; unajua watu hawa ya kuwa wanaweka roho zao juu ya kufanya mabaya. 23 Maana waliniambia: Utufanyie miungu itakayokwenda mbele yetu; kwa maana mtu huyu Musa ambaye alitutoa katika inchi ya Misri, hatujui nini ilimpata. 24 Nikawaambia: Kila mtu aliye na zahabu, aivunje; basi wakanipa, nikaitupa katika moto, akatoka ndama huyu.*

*25 Na wakati Musa alipoona ya kama watu hawa wameasi; maana Haruni amewaacha waasi ili wawe zihaka katika adui zao; 26 halafu Musa akasimama katika mlango wa kambi, akasema: Yeye aliye*

> *upande wa Bwana, aje kwangu. Wana wote wa Lawi wakamkusanyikia. 27 Akawaambia: Bwana, Mungu wa Israeli anasema hivi: Kila mtu ajifungie upanga wake pajani mwake, na apite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya kambi, na achinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenzake, na kila mtu jirani yake. 28 Na wana wa Lawi walifanya kama Musa alivyosema,* ***wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu.*** *. . . 35 Bwana akapiga watu wale, kwa kuwa walifanya ndama ambayo Haruni alifanya.*

Huu ndio mwisho wa sura 32. Nyuma ya maneno haya Mungu aliagiza Musa kutayarisha **mbao mbili nyingine za mawe** kukomboa zile alizokwisha kuvunja. Bwana aliandika juu yao maagizo ambayo Waisraeli walikwisha kuvunja. Kweli Waisraeli walikuwa wamefanya zambi kubwa! Walikuwa **wamevunja** sheria takatifu ya Mungu. Uovu wa moyo wa mtu ulionekana tena. Hata nyuma ya maneno yote ambayo Bwana alifanyia wana wa Israeli, tunaona ya kwamba walikuwa wameacha mbio njia ya haki ambayo Mungu alikuwa ametayarisha. Walichagua kufuata njia nyingine, na kujisimamishia **dini yao wenyewe**. Walichagua njia ya kazi ambayo wao wenyewe waliweza kufanya. Waligeuza mgongo kwa njia Mungu aliyosimamisha na walifurahi na dini ambayo walijichagulia. Walitaja jina la Mungu na midomo yao, lakini mioyo yao ilikuwa mbali naye! Kwa sababu hii walifanya ndama ile ya zahabu, wakafurahia kazi ya mikono yao wenyewe, na kugeuzia Mungu mgongo wao.

Mungu anataka kutufundisha nini kwa njia ya habari hizi mbaya? Mungu anataka tuwaze juu ya hali yetu mbele yake. Labda kuna watu wanaofikili: "Mimi si kama Waisraeli. Sikugeuzia Mungu mgongo kamwe na kuabudu sanamu." Wewe unayefikili hivi, unajua kabisa ya kwamba hujaabudu sanamu kamwe? Labda hukuabudu sanamu ambayo ulifanya na mikono yako mwenyewe. Lakini watu wanaabudu sanamu nyingine vilevile. Sanamu ni kitu cho chote kinachoingia katikati yetu na Mungu. Labda **sanamu** yako ni mali, mavazi, television, kazi, rafiki, desturi za wazazi, vivi hivi. Wengine wanashikamana na hirizi na talasimu. Wengine wanaweka roho sana juu ya kuabudu sanamu zao; wanaweka roho juu ya maombi na kufunga chakula kupita juu ya kusikia Neno la Mungu. **Kitu cho chote kinachokomboa Mungu Mwumba na Neno lake la kweli ndani ya maisha na mawazo yetu ni sanamu.**

**Mungu wako ni nani?** Ni nani ambaye unaabudu kweli kweli, Bwana Mungu au sanamu? Jina la Mungu ni juu ya midomo yako tu au ni kweli kweli ndani ya moyo wako? Kuna tofauti katikati ya wale wanaoabudu Mungu na roho ya kweli na wale wanaoabudu sanamu. Ni **Neno la Mungu**. Unafikili nini juu ya Neno la kweli la Mungu? Unajua Neno la Mungu? Unaliamini? Unalipenda na roho yako yote? Au wewe ni kama Waisraeli? Mungu alisema juu yao: *"Watu hawa wananiheshimu na midomo yao; lakini moyo wao ni mbali nami. Wananiabudu **bule**, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya watu."* (Matayo 15:8,9)

Basi wewe? Unaabudu nani kweli kweli, Bwana Mungu aliyetoa sheria yake ya haki kwa Musa? Unaamini Neno lake? Au unatumainia kazi zako mwenyewe za dini kama Waisraeli? Maandiko yanasema:

> (1 Yoane 5*) "Maneno haya yote yaliwapata kama mifano, yakaandikwa kutuonya sisi . . . Sababu hii wapenzi wangu, **kimbieni kuabudu sanamu** . . . Ninasema kwa watu wenye akili."* (1 Wakorinto 10:11,14,15) *"Lakini wenye woga, na wasioamini, na wenye machukio . . . na wachawi , na **wanaoabudu sanamu** . . . sehemu yao ni katika lile ziwa linalowaka moto na kiberiti."* (Ufunuo 21:8). *"Kama tukipokea ushuhuda wa watu, ushuhuda wa Mungu ni mkubwa zaidi; kwa maana ushuhuda wa Mungu ndio huu, kwamba ameshuhudia Mwana wake . . . amekwisha kuja, naye ametupa sisi akili ili tumjue yeye aliye wa kweli. . . Watoto wadogo, **mujilinde nafsi zenu kwa sanamu**."* (1 Yoane 5:9,20,21)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutawaza juu ya shauri la namna nyingine ambayo Mungu alitayarisha ili aweze kupanga katikati ya Waisraeli wenye zambi bila kuharibu haki yake mwenyewe.

Mungu akubariki wakati unapokumbuka agizo hili kubwa:

***"Mujilinde nafsi zenu kwa sanamu."*** (1 Yoane 5:21)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 40

# Hema ya Kusanyiko

## Kutoka 24–40, Walawi 16

Tuanze somo letu leo na sifa kwa Mungu anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele, tuliona namna Waisraeli walivyoacha Bwana ambaye aliwakomboa toka utumwa katika Misri. Wakati Musa alipokuwa akipokea Neno la Mungu juu ya Mlima Sinai, Waisraeli walifanya ndama ya zahabu waiabudu kama sanamu. Lakini leo tutasikia habari za kufurahisha kabisa. Sharti tusikilize vizuri kwa sababu zina mafundisho ya ndani ndani kabisa. Tutaona ya kwamba Mungu aliwaambia Musa na Waisraeli kufanya hema ya namna nyingine kusudi aweze kuwafundisha namna gani waliweza kumkaribia, kukutana naye na kumwabudu. Hivi somo la leo linaitwa **"Hema ya Kusanyiko."**

Tukisoma ndani ya Tora, kitabu cha Kutoka kuanza na sura 24 na shairi 16, Maandiko yanasema:

> (Kutoka 24) *16* ***Utukufu wa Bwana ukakaa juu ya mlima Sinai,*** *wingu likaufunika siku sita; siku ya saba (Mungu) akaita Musa toka kati ya wingu. 17 Na kuonekana kwa utukufu wa Bwana kulikuwa kama moto wa kuteketeza juu ya kichwa cha mlima kwa macho ya wana wa Israeli. 18 Musa akaingia kati ya wingu, akapanda mlimani; Musa akakuwa mlimani siku makumi ine, mchana na usiku.*
>
> (Kutoka 25) *1 Bwana akamwambia Musa, akisema: 2 Sema na wana wa Israeli wanitwalie sadaka; toka kila mtu aliye tayari moyoni mwake mutatwaa sadaka yangu. 3 Na hii ni sadaka ambayo mutawatwalia: zahabu na feza na shaba; 4 na samawi, na zambarau, na rangi*

> *nyekundu, kitani nzuri na nyole za mbuzi; na ngozi za kondoo ndume zilizotiwa rangi nyekundu, na ngozi za pomboo, na mti wa mshita; 6 mafuta kwa taa, manukato kwa mafuta ya kupakaa, na kwa uvumba mtamu; 7 vito vya shohamu na vito vya kutiliwa, kwa efodi na kwa kifua. 8* ***Na wanifanyie pahali patakatifu, nipate kukaa katikati yao.*** *9* ***Sawasawa na maneno yote ambayo nitakuonyesha, mfano wa hema, mfano wa vyombo vyake vyote, ndivyo mutakavyofanya."***

Ulisikia maneno Mungu aliyosema na Musa? Alimwambia kufanya kitu cha ajabu kabisa! Lilikuwa kusudi la Mungu kukaa katikati ya Waisraeli, katikati ya wale ambao walimkosea mara nyingi sana! Kwa nini Mungu, aliye mkubwa na mtakatifu sana alitaka kukaa pamoja na wenye zambi namna hii? Kwa nini Mungu, aliye roho na asiyehitaji kitu alikubali kusema na wazao wa Adamu waliokuwa wamekwenda mbali naye? Kama tulivyoona mbele, Mungu aliumba mtu kwa sura yake mwenyewe kwa sababu alitaka kuwa na ushirika na mtu. Zambi ya mtu iliharibu ushirika huu, lakini Mungu alitengeneza njia ya haki kwa kuwezesha mtu kurudi kwake. Kwa sababu ya rehema yake kubwa kwa wenye zambi Bwana alifanya shauri kwa utukufu wake kukaa katikati ya Waisraeli. Kwa njia ya **hema na sheria speciales**, Mungu alitaka kuonyesha kwa njia ya mfano namna wazao wa Adamu waliweza kumkaribia. Kama tulivyojifunza mbele, kwa sababu Mungu ni mtakatifu, wenye zambi hawawezi kumkaribia kwa njia yo yote wao wanayochagua. Kwa sababu hii Mungu aliagiza Waisraeli kumfanyia hema ile ili aweze kukaa katikati yao namna ilivyofaa kwa utakatifu na utukufu wake. Vilevile, kwa njia ya hema hii, Mungu alikusudi kufundisha watu watakaozaliwa nyuma maneno makubwa mengi juu yake mwenyewe na juu ya Mwokozi ambaye alikusudi kutuma duniani.

Mbele ya kufikiri maneno Mungu aliyoagiza Musa juu ya kao ambalo alitaka Waisraeli kumjengea, inatupasa kufahamu kwanza ya kwamba Mungu hakuwaambia kumjengea hema kwa sababu alihitaji pahali pa kupanga! Sivyo! Mungu, Mjuu sana, aliyeumba dunia na vitu vyote ndani yake, hapangi ndani ya nyumba zinazofanywa na watu! Ndani ya Maandiko ya Manabii, Bwana yeye mwenyewe anatangaza: *"Mbingu ni kiti changu cha ufalme, na dunia ni kiti changu cha miguu; mutanijengea nyumba ya namna gani? na pahali pangu pa*

*kupumzika ndani yake ni pahali gani? Maana mkono wangu umefanya vitu hivi vyote, na vitu vyote vimekuwa."* (Isaya 66:1,2; Mateno 7:48,49)

Basi kwa sababu gani Mungu aliagiza Waisraeli kufanya hema kwa Roho yake na utukufu wake kukaa ndani yake? Kama tulivyosema mbele, Mungu alitaka Waisraeli na wazao wote wa Adamu kujua ya kwamba ana hamu kubwa kwa **ushirika** nao. Mungu alitaka vilevile kuwapa **mfano** wa namna gani watu wanaweza kusamehewa zambi zao na kuwa na ruhusa kukaa pamoja na Mungu mbinguni kwa milele!

Hivi, Mungu aliagiza Musa na Waisraeli kumfanyia hema ili aweze kukaa katikati yao. Lakini Hema ya Kusanyiko itakuwa namna nyingine na hema nyingine. Kuna sura makumi tano ndani ya Maandiko Matakatifu kueleza kazi ya kufanya hema hii! Sura hizi zina mafundisho ya ndani ndani na hatuna saa kusema juu ya maneno yote yanayoandikwa ndani yao. Tunaweza kujaribu kujumlisha maneno makubwa makubwa tu.

Neno la kwanza ambalo inatupasa kujua ni ya kwamba ilipasa Hema hii ya Kusanyiko kuwa na **vyumba viwili.** Hema ya Kusanyiko ilikuwa hema moja, lakini **pazia** zito na la mapambo lilifanywa kuigawa kuwa vyumba viwili.

Chumba cha kwanza kiliitwa ***Pahali Patakatifu***. Hakuna mtu aliyekuwa na ruhusa kuingia chumba kile ila makuhani. Makuhani ndio wale waliochaguliwa na Mungu wa wazao wa Haruni kuchinja nyama kama sadaka kwa kuondoa (au kufunika) zambi. Kulikuwa na vitu vitatu ndani ya chumba kile: meza ya zahabu juu yake waliteketeza uvumba, taa au kinara ya mafuta, na meza juu yake wakaweka mikate namna nyingine mbele ya Mungu kwa kuabudu.

Chumba cha pili kiliitwa ***Patakatifu pa Patakatifu*** au ***Pahali Patakatifu Sana.*** Kiliitwa Pahali Patakatifu Sana kwa sababu wakati kazi ya kufanya hema itakapokwisha, Mungu atashuka na kujaza chumba kile na utukufu wake. Pahali Patakatifu Sana palikuwa mfano wa mbingu (Paradiso). Hivi, pahali pale palikuwa kwa Mungu tu. Kwa sababu hii Mungu alimwambia Musa ya kwamba mtu ye yote akijaribu kuingia Pahali Patakatifu Sana atakufa! Kuhani mkubwa tu ataingia Pahali Patakatifu Sana, mara moja tu katika mwaka mmoja. Na vilevile, ilimpasa kuingia na damu ya sadaka kwa zambi zake mwenyewe na zambi za watu, kama Mungu alivyoagiza.

Mungu aliagiza Musa kuweka ndani ya Pahali Patakatifu Sana sanduku iliyofanywa kwa mshita na kufunikwa na zahabu safi. Sanduku hii iliitwa ***Sanduku ya Agano***. Waliagizwa kuchunga ndani ya sanduku ya agano, mbao mbili za mawe juu yao Amri Kumi ziliandikwa. Juu ya sanduku waliweka kifuniko cha zahabu. Ilipasa kuhani mkubwa kunyunyizia kifuniko damu ya nyama mara moja kila mwaka ili Mungu aweze kusamehe zambi za Waisraeli. Kwa sababu hii Mungu aliita kifuniko hiki ***kiti cha rehema.***

Nyuma yake, Mungu alionyeshea Musa namna gani kufanya pazia la juu sana kuzunguka Hema ya Kusanyiko. Ukuta ule, ndio **ukuta wa kiwanja**, utakuwa pazia jeupe. Watafanya **mlango mmoja** ndani ya pazia lile. Hivi hakuna mtu aliyeweza kuingia kiwanja cha Hema ya Kusanyiko bila kupita kwa mlango wa kiwanja. Ndani ya kiwanja, mbele ya mlango wa kiwanja, Mungu aliagiza Musa na Waisraeli kuweka **mazabahu** ya shaba. Hivi ilipasa kila mtu aliyeingia mlango wa kiwanja kupita kwanza kwa mazabahu. Mungu alitaka kufundisha Waisraeli na wazao wote wa Adamu kwa njia gani inawapasa kukaribia Mungu. Waisraeli watakaribia Mungu namna gani? Kwa njia ya sadaka ya damu.

Ilipasa kila mtu aliyetaka kuingia kiwanja cha "kao la Mungu" kuingia na sadaka ya nyama kama malipo kwa zambi. Mungu alikuwa akifundisha ya kwamba **hakuna mtu anayeweza kumkaribia ila kwa njia ya sadaka ya damu.** Kwa sababu hii Mungu alimwambia Musa, *"Uhai wa mwili ni katika damu; na nimewapa ninyi damu hii juu ya mazabahu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwa maana* ***ni damu inayofanya upatanisho kwa ajili ya nafsi."*** (Walawi 17:11)

Hivi mtu ye yote akitaka kuabudu Mungu, ilimpasa kutoa sadaka ya nyama kwanza kwa usamehe wa zambi yake. Sharti mwabudaji alete ngombe ndume, au kondoo, au ndege ndani ya kiwanja cha Hema ya Kusanyiko. Mbele ya mazabahu, ilimpasa kuweka mikono yake juu ya kichwa cha sadaka aliyoleta, na kukiri kwa Mungu ya kwamba alikuwa mwenye zambi aliyestahili kufa kwa zambi zake. Nyuma yake, kuhani alikamata damu ya sadaka, aliinyunyiza juu ya mazabahu na juu ya udongo uliozunguka mazabahu, kisha kuteketeza sadaka juu ya mazabahu. Kwa njia hii Mungu alisamehe (au *kufunika*) zambi ya mtu huyu, kwa sababu nyama asiyekuwa na zambi alikufa kwa pahali pake.

Ilipasa Waisraeli kutoa sadaka hizi tena na tena kila mwaka. **Sadaka za nyama hazikuweza kutosha kwa utukufu wa Mungu milele**. Zilikuwa **mifano kwa wakati tu ya Mkombozi** atakayekuja na kufa kwa pahali pa wenye zambi — ili Mungu aweze kusamehe **kwa milele** wazao wa Adamu deni yao ya zambi pamoja na kuwa mwenye haki.

Kama mfano wa kazi ambayo Mkombozi atafanyia wenye zambi, Mungu aliweka siku moja kila mwaka kwa Waisraeli saa Kuhani Mkubwa atakapoingia chumba cha pili, Pahali Patakatifu Sana, pa Hema ya Kusanyiko. Siku ile iliitwa ***Siku ya Upatanisho*** (ndiyo siku *Mungu alipofunika zambi*). Siku ile, (katika mwezi wa kumi), Kuhani Mkubwa alikuwa na amri au ruhusa kuingia Pahali Patakatifu Sana, na kunyunyiza damu juu ya kiti cha rehema juu ya sanduku ya agano. Hakuweza kamwe kuingia Pahali Patakatifu Sana bila kuleta damu ya nyama asiyekuwa na kipako na kuitoa kwa Mungu kwa zambi zake mwenyewe na zambi za Waisraeli wote. Kwa njia hii Mungu alikuwa akionyesha namna Mkombozi atavyokuja na atamwanga damu yake ili Mungu aweze kusamehe wenye zambi, na kuwakaribisha kwake milele!

Kweli, wasomaji wenzetu, somo letu leo ni la ajabu sana. Kuna maneno mengi mengine ambayo tungependa kusema, lakini nafasi haiko. Lakini mbele ya kumaliza somo hili, kuna neno moja lingine ambalo inawapasa ninyi kufahamu juu ya Hema ya Kusanyiko. Ndani ya sura ya mwisho ya kitabu cha Kutoka, Maandiko yanasema:

> *"Sawasawa na yote Bwana aliyoamuru Musa, ndivyo walivyofanya wana wa Israeli kazi yote. Musa akaona kazi hii yote, na tazama, walikuwa wameimaliza; kama Bwana alivyoamuru, ndivyo walivyofanya; Musa akawabariki . . . Kisha wingu lilifunika hema ya kusanyiko na* ***utukufu wa Bwana ukajaza Hema.*** *Wala Musa hakuweza kuingia katika hema ya kusanyiko kwa sababu wingu lilikaa juu yake na utukufu wa Bwana ulijaza Hema."* (Kutoka 39:42,43; 40:34,35)

Unaona nini ilitokea? Wakati Hema ya Kusanyiko ilipokuwa tayari, utukufu wa Mungu ulishuka juu ya hema na kujaza Pahali Patakatifu Sana, na nuru ya utukufu wa Mungu ilingaa, hata kupita nuru ya jua! Inatupasa kukumbuka ya kwamba ndani ya maneno haya yote Mungu alileta mfano wa baraka kubwa zaidi za wakati wa kuja saa Mkombozi wa dunia atakaposhuka toka mbinguni na

kupanga katikati ya wana wa Adamu. **Mkombozi mwenyewe ndiye "Hema ya Kusanyiko" ya kweli** ambaye Mungu alitoa ili tuweze kuwa na upatano wa karibu na mzuri sana naye kwa milele! Kama ilivyoandikwa ndani ya Habari Njema (Injil):

> *"Katika mwanzo alikuwa Neno, na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na Neno alikuwa Mungu . . . Na* ***Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu,*** *tukatazama utukufu wake! . . . [Yeye ni] Mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu!"* (Yoane 1:1,14,29)

Ndiyo, Mkombozi ndiye anayetimiza **mifano yote** ya Hema ya Kusanyiko na sadaka za nyama, kwani yeye hakufika ndani ya dunia yetu tu na **kuishi katikati ya watu**, lakini **alimwanga damu yake** vilevile kama Sadaka Kamilifu kwa wenye zambi ili tuweze kuwa na ushirika wa karibu na Mungu kwa milele!

Labda unafikili maneno tuliyojifunza leo ni nguvu kufahamu na hata nguvu kupita kuamini? Halafu tukumbuke ya kwamba mara nyingine kuna maneno ndani ya Neno la Mungu ambayo ni nguvu kufahamu, lakini ni kweli hata hivi! Tusisahau kamwe ya kwamba Bwana mwenyewe anasema: *"Mafikili yangu si mafikili yenu, wala njia zenu si njia zangu! . . . kama vile mbingu ni juu sana kuliko dunia, hivi* ***njia zangu ni juu sana kuliko njia zenu, na mafikili yangu juu kuliko mafikili yenu!"*** (Isaya 55:8,9)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Tumefikia mwisho wa somo 40. Mungu akubariki. Tunaagana nawe na mashairi haya toka Maandiko Matakatifu:

> ***"Tazameni namna ya utajiri wa akili na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazivumbulikani, na njia zake hazitafutikani! Maana ni nani aliyejua nia ya Bwana? au ni nani aliyekuwa mshauri wake? . . . Kwa maana vitu vyote vinatoka kwake, na viko kwa uwezo wake. Utukufu uwe kwake milele. Amina."*** (Waroma 11:33-36)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 41

# Kutoamini kwa Waisraeli

### Hesabu 13, 14

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza tena kujifunza tena ndani ya mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Tunaendelea kusoma ndani ya Tora. Kama unavyojua, Tora ni sehemu ya kwanza ya Maandiko ya Manabii na ina vitabu vitano ndani yake. Ndani ya kitabu cha kwanza, kinachoitwa **Mwanzo**, tulijifunza namna zambi iliingia duniani, na kuleta mateso, mauti na hukumu. Lakini tuliona vilevile ya kwamba Mungu alitayarisha njia kuokoa Adamu na wazao wake toka azabu ya zambi, ndio moto wa milele. Tulijifunza ya kwamba Mungu aliahidi kutuma Mkombozi kufa kwa wenye zambi ili Mungu aweze kusamehe zambi zao bila kuacha kuwa mwenye haki. Kitabu cha Mwanzo kilitufundisha vilevile namna Mungu alivyochagua Abrahamu na kuahidi kufanya taifa kubwa kwa njia yake na ya kwamba manabii watakuja kwa njia ya taifa hili, na mwishoni Mwokozi wa dunia.

Ndani ya kitabu cha pili cha Tora, ndicho **Kutoka**, tuliona namna Mungu alivyookoa wazao wa Abrahamu, ndio Waisraeli, toka utumwa inchini mwa Misri, akitumika na Musa, nabii wake. Mungu alitoa makabila ya Israeli katika Misri na kuwaleta jangwani, akiwafundisha kwa Mlima Sinai pahali alipowatolea maagizo yake na kuwafundisha juu ya sadaka ya damu kwa njia yake aliweza kusamehe zambi zao.

Ndani ya somo la mwisho tuliona Mungu akiagiza Musa na Waisraeli kumjengea kao zuri sana, ndilo **Hema ya Kusanyiko** ili aweze kukaa katikati yao. Wakati vitu vyote vilipokuwa tayari

*"wingu lilifunika hema ya kusanyiko, na utukufu wa Bwana ukajaza Hema."* (Kutoka 40:34) Mungu alikuwa akionyeshea Waisraeli ya kwamba alitaka kuwa na ushirika wa ajabu kabisa nao, lakini hakuna mtu aliyeweza kumkaribia ila kwa njia ya damu ya sadaka iliyotolewa juu ya mazabahu ya Hema ya Kusanyiko. Hema ya Kusanyiko na sadaka zake za nyama zilikuwa **vivuli na mifano tu ya Mkombozi** atakayekuja toka mbinguni na kumwanga damu yake kama sadaka kuondoa zambi.

Ndani ya **sehemu ya tatu ya Tora**, kitabu cha **Walawi** (ndizo *sheria za kabila la Lawi*), Mungu aliongoza Musa kuandika sheria zinazoeleza namna gani ilipasa Waisraeli kutolea Mungu zabihu zinazofunika zambi. Mafundisho ya kitabu hiki ni ya ndani ndani sana na hatuna saa kuangalia maneno yote yanayoandikwa ndani yake. Ukikisoma na kujifunza peke yako, utaona maneno mawili yanayoonekana karibu mara mia mbili. Maneno haya mawili yanajumlisha mafundisho makubwa ya kitabu kizima. Maneno yenyewe ni ***"Takatifu"*** na ***"Damu."*** Kwa nini maneno haya mawili yanaonekana tena na tena ndani ya kitabu hiki? Kwa sababu maneno makubwa mawili zaidi mtu anayoweza kufahamu ni ya kwamba **Mungu ni mtakatifu,** na ya kwamba *"pasipo kumwanga **damu** hakuna ondoleo (la zambi)!"* (Waebrania 9:22) Kazi ya kitabu cha tatu cha Tora ilikuwa kufundisha Waisraeli namna gani mtu anayechafuwa na zambi anaweza kukaribia Mungu safi na mwenye utukufu na aliye safi. Mungu alionyesha waziwazi ya kwamba hakuna mtu anayeweza kumkaribia, ila kwa njia ya damu ya sadaka, sadaka iliyo mfano wa Mkombozi mtakatifu atakayekuja duniani na kufa kwa wenye zambi, kulipa deni yao ya zambi.

Ndani ya baki la somo hili tuendelee na **sehemu ya ine** ya Tora, ndiyo kitabu cha **Hesabu**. Ndani ya kitabu hiki tunaona ya kwamba Waisraeli walikaa kwa mguu wa Mlima Sinai kwa karibu mwaka mmoja. Ndani ya mwaka ule, Mungu aliwafundisha maneno mengi, na aliongoza Musa kuandika sehemu kubwa ya Tora tunayosoma ndani yake leo. Lakini Mungu hakukusudi kwa Waisraeli kukaa jangwani daima. Kwa sababu hii, siku moja, Mungu aliwaongoza kufunga vitu vyao na kuanza safari kwenda kwa inchi ya kusitawi ambayo aliahidi kuwapa, ndiyo inchi ya Kanana. Maandiko yanatuambia ya kwamba siku ilipowapasa kuondokea Sinai, wingu la utukufu wa Mungu lililofunika Hema ya Kusanyiko, liliondokea Hema na kuanza kwenda mbele yao. **Bwana Mwenyewe** alikuwa

akiwaongoza, ndani ya **wingu** mchana kuwaonyeshea njia, na ndani ya **nguzo ya moto** usiku.

Hivi Waisraeli walifuata wingu kwa wakati wa mchana na nguzo ya moto usiku kufika wakati walipofikia mpaka wa inchi ya Kanana, inchi ambayo Mungu aliahidi kuwapa Abrahamu na wazao wake miaka mingi mbele. Mungu hakusahau ahadi zake. **Kwa sababu ya uaminifu na uwezo wa Mungu, Waisraeli walikuwa wamefikia mpaka wa inchi ya Kanana,** ndiyo inchi inayoitwa Palestina au Israeli kwa wakati wa sasa.

Lakini Kanana ilijaa na watu. Wenyeji wa Kanana walikuwa wengi na wenye uwezo. Basi namna gani Waisraeli wataweza kukamata inchi yao? Kulikuwa na njia moja tu: **Mungu atawapa inchi yenyewe**. Hakuna neno linaloshinda Mungu! Mungu aliahidi Abrahamu: *"Inchi hii ya Kanana nitawapa wazao wako!"* Mungu alikusudi kuharibu kabisa watu wa Kanana na kuwapa wazao wa Abrahamu, ndio Waisraeli, inchi yao. Ni neno kubwa kufahamu ya kwamba zambi za watu wa Kanana zilikuwa kubwa sana. Walikuwa wazalimu kabisa na walitoa hata watoto wao kwa miungu yao. Mungu alikuwa na saburi nyingi kwa watu wa Kanana, lakini waliendelea ndani ya zambi zao na njia zao za haya. Kwa sababu hii Mungu alikusudi kuwapa makabila ya Israeli inchi yao.

Sasa tusome ndani ya sehemu ya ine ya Tora kuona nini ilitokea wakati Waisraeli walipofikia mpaka wa inchi ya Kanana. Ndani ya Hesabu 13 Maandiko yanasema:

> (Hesabu 13) *1 Bwana akamwambia Musa akisema: 2 Tuma watu wapeleleze inchi ya Kanana ambayo* ***ninawapa wana wa Israeli;*** *tumeni mtu mmoja wa kila kabila la baba zao . . . 3 Musa akawatuma toka jangwa la Parani kama Bwana alivyoagiza . . . Basi wakapanda, wakapeleleza inchi . . .*
>
> *25 Wakarudi nyuma ya kupeleleza inchi kwa mwisho wa siku makumi ine. 26 Wakapanda, wakakuja kwa Musa na kwa Haruni na kwa makutano yote ya wana wa Israeli kwa jangwa la Parani, kwa Kadesi. Wakawaletea habari, wao na makutano yote, na kuwaonyesha matunda ya inchi. 27 Wakamwambia Musa wakisema: Tulifika kwa inchi ulipotutuma, na hakika* ***inajaa maziwa na asali****; na haya ni matunda yake. 28* ***Lakini watu wanaokaa inchini ni wenye nguvu*** *na miji yao ni yenye maboma, na ni mikubwa sana; na tena tuliona wana wa Anaki pale! . . .*

*30 Halafu **Kalebu** (mmoja wa watu waliopeleleza inchi) alinyamazisha watu mbele ya Musa, akasema: Tupande mara moja na kuikamata; maana tunaweza kuishinda! 31 **Lakini watu** waliopanda kwenda pamoja naye wakasema: Hatuwezi kupigana na watu wale, kwa kuwa wao wana nguvu kupita sisi. 32 Wakaleta habari mbaya kwa wana wa Israeli toka inchi ambayo walipeleleza, wakisema: "inchi tuliyopita kati yake kwa kuipeleleza, ni inchi inayokula wenyeji wake, na watu wote tulioona ndani yake ni watu warefu sana. 33 Na tuliona pale Wanefili . . . tulikuwa kama mapanzi machoni mwetu na machoni mwao vilevile."*

(Hesabu 14) *1 Makutano yote wakapaza sauti zao, wakalia; watu **wakatoa machozi** usiku ule. 2 Wana wote wa Israeli **wakanungunikia** Musa na Haruni; makutano yote wakawaambia: ingekuwa heri kama tungalikufa katika inchi ya Misri! au ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili! 3 Na kwa nini Bwana anatuleta kwa inchi hii, ili tuanguke kwa upanga? Wake wetu na watoto wetu watakuwa mateka, si afazali turudi Misri? 4 Wakasemezana wao kwa wao: Tuweke mtu mmoja kuwa akida, halafu turudi Misri. 5 Halafu Musa na Haruni wakaanguka kifudifudi mbele ya kusanyiko la makutano ya wana wa Israeli.*

*6 Na **Yosua** mwana wa Nuni na **Kalebu** mwana wa Yefune waliokuwa kati yao waliopeleza inchi wakapasua nguo zao; 7 wakawaambia makutano yote ya wana wa Israeli wakisema: Inchi tuliyopita kati yake kwa kuipeleleza ni inchi nzuri sana. 8 Kama Mungu akitufurahia, atatuingiza katika inchi hii, na kutuletea sisi iwe inchi yetu, inchi inayojaa maziwa na asali. 9 Lakini musiasi juu ya Bwana, wala musiogope watu wa inchi; maana wao ni chakula chetu, ulinzi wao umeondoshwa juu yao, na **Bwana ni pamoja nasi,** musiwaogope.*

*10 **Lakini makutano yote wakaamuru wapigwe kwa mawe**. Na utukufu wa Bwana ulionekana hemani mwa kusanyiko kwa wana wote wa Israeli. 11 Bwana akamwambia Musa: "**Hata wakati gani watu hawa watanizarau? Na hata wakati gani hawataniamini,** hata ikiwa nikifanya alama hizi zote katikati yao?"*

Tusimame kwanza hapa. Unasikia namna Israeli walivyokosea na kuchukiza Mungu? Unaona kutoamini kwao? Unaona namna walivyoshitaki Mungu kusema hakutimiza ahadi zake? Ndiyo, siku ile Waisraeli walikosa sana kwa sababu **hawakuamini** ahadi ya

Mungu ya kwamba atawapa inchi ya Kanana. Hawakuamini ahadi ya Mungu kwa Abrahamu, Isaka, Yakobo, na Musa. Walikuwa namna ya watu wengi kwa wakati wa sasa wanaosema, "Tunaamini Mungu na manabii!" lakini hawaamini Mungu kweli kweli, na hawaamini manabii, kwa sababu hawaamini maneno ambayo Mungu aliahidi kwa njia ya manabii wake ndani ya Maandiko Matakatifu. Kutoamini ni zambi mbaya sana mbele ya Mungu.

Basi tuendelee na habari hizi ndani ya Hesabu 14.

> (Hesabu 14) *26 Bwana akawaambia Musa na Haruni akisema: 27 Hata wakati gani nitavumilia makutano haya mabaya ambao wananinungunikia? Nimesikia manunguniko ya wana wa Israeli ambayo wananinungunikia. 28 Muwaambie: Kama ninavyoishi, Bwana anasema, Hakika kama ninyi mulivyosema masikioni mwangu, ndivyo nitakayowatendea ninyi; 29* ***maiti zenu zitaanguka katika jangwa hili;*** *na wote waliohesabiwa katikati yenu, kama jumla ya hesabu yenu, toka miaka makumi mbili na zaidi ambao walininungunikia, 30 hakika hamutaingia katika inchi, niliyonyosha mkono wangu kwa ajili yake ya kuwa nitawafanya ninyi kukaa ndani yake, ila* ***Kalebu*** *mwana wa Yefune, na* ***Yosua*** *mwana wa Nuni. 31* ***Lakini watoto wenu*** *muliosema watakuwa mateka, wao nitaleta ndani, na watajua inchi ambayo mulikataa. 32 Lakini ninyi, maiti zenu zitaanguka katika jangwa hili . . . 35 Mimi Bwana nimesema, hakika nitafanya hivi kwa makutano maovu haya yote,* ***wanaokusanyika juu yangu****; katika jangwa hili wataharibiwa na pale watakufa."*
>
> *36 Na watu ambao Musa alituma kupeleleza inchi, na waliorudi na kufanya makutano yote kumnungunikia kwa sababu ya kuleta habari mbaya juu ya inchi, 37 hata watu wale walioleta habari mbaya juu ya inchi, wakakufa kwa tauni mbele ya Bwana. 38 Lakini Yosua ... na Kalebu . . . wakabaki hai wa watu wale waliokwenda kupeleleza inchi (kwa sababu waliamini neno la Bwana).*

Hivi tunaona ya kwamba Waisraeli walikataa kuamini Bwana hata kama alikuwa amewaokoa toka mkono wa Farao na kuwaleta kwa mpaka wa inchi ya Kanana. Mungu alifanya nini juu ya wale wasioamini Neno lake? Aliwahukumu kufa jangwani! Kwa nini kizazi hiki cha Waisraeli hawakuingia inchi ya Kanana? **Kwa sababu walikataa kuamini Neno la Mungu!**

Rafiki, kukataa kuamini Neno la Mungu ni hasara kubwa. Ni la-

zima kwa Mungu kuazibu kila mtu ambaye anayekataa kumwamini! Mtu ye yote anayekataa au kuona bule maneno Mungu anayosema ndani ya Neno lake takatifu anaita Mungu mwongo na hawezi kushiriki ndani ya ufalme wake wa milele! Si kutaka kwa Mungu kwa mtu ye yote kufa katika kutoamini. Anataka watu wote kuamini Habari Njema juu ya njia ya wokovu ambayo alitayarisha. Lakini inapasa kila mtu kuchagua kwa yeye mwenyewe. Wote wanaokataa kuamini Neno la Mungu watapotea. Sikia maonyo haya ya Roho Mtakatifu kwa njia ya manabii:

> *"Leo, kama mutasikia sauti yake, musifanye migumu mioyo yenu, kama katika jangwa . . . Angalieni, ndugu zangu, asiwe katikati yenu mmoja mwenye **moyo mbaya wa kutokuamini** kwa kujitenga na Mungu aliye hai!"* (Waebrania 3:7,8,12; Zaburi 95:7-11)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kusoma pamoja nasi. Ndani ya somo la nyuma, tutaona namna watu wale wote waliokataa kuamini Mungu walikufa jangwani, kama Mungu alivyosema . . .

Mungu akubariki wakati unapoweka roho juu ya maonyo haya toka Maandiko:

> ***"Angalieni, ndugu zangu, asiwe katikati yenu mmoja mwenye moyo mbaya wa kutokuamini kwa kujitenga na Mungu aliye hai!"*** (Waebrania 3:12)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 42

# Nyoka ya Shaba

### Hesabu 20, 21

Tunakusalimu tena leo kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa kujifunza juu ya *Njia ya Haki*.

Kwa somo la mbele, ndani ya sehemu ya ine ya Tora, ndicho kitabu cha Hesabu, tuliona namna Waisraeli walivyofikia mpaka wa Kanana, inchi Mungu aliyoahidi kwa Abrahamu, Isaka, Yakobo na wazao wao. Mungu alikusudi kufukuza watu warefu sana waliokaa ndani ya inchi ile na kutia inchi nzima kwa mikono ya Waisraeli. Lakini zaidi ya Waisraeli waliogopa watu wale warefu sana na **walikataa kuamini ahadi ya Mungu** kuwapa inchi ya Kanana.

Hivi tulisoma namna Mungu alivyohukumu Waisraeli kwa sababu ya kutoamini kwao. Alisema nao,

> ***"Hakika hamutaingia katika inchi, niliyonyosha mkono wangu kwa ajili yake ya kuwa nitawafanya ninyi kukaa ndani yake, ila Kalebu . . . na Yosua . . . kwa sababu wao walikuwa na roho ya namna nyingine na walinifuata na roho moja.*** *Watoto wao watairiti. Na vilevile, watoto wenu muliosema watakuwa mateka, wao nitaleta ndani wafurahi na inchi ambayo mulikataa! Lakini ninyi, maiti zenu zitaanguka katika jangwa hili!"*
> (Hesabu 14:30-32)

Sharti tufahamu ya kwamba Mungu alitaka kubariki Waisraeli sana, lakini **hakuweza kuwabariki kwa sababu ya kutoamini kwao.** Kwa sababu walikataa kuamini ahadi za Bwana, Mungu aliwahukumu kuhangaika jangwani kwa miaka makumi ine, kufika wakati watu wote wenye miaka zaidi ya makumi mbili ambao hawakumwamini walikufa.

Sasa, tuendelee ndani ya kitabu cha Hesabu kuona nini ilitokea kwa mwisho wa miaka makumi ine ambayo Waisraeli walipoteza jangwani kwa sababu ya kutoamini kwao. Ndani ya sura 20 tunasoma:

> (Hesabu 20) *1 Kisha wana wa Israeli, hata makutano yote, wakakuja kwa jangwa la Sini . . . watu wakakaa kwa Kadesi (pahali walipokataa mbele kuamini Mungu na kuingia inchi ya Kanana ambayo aliahidi kuwapa). Miriami (ndugu mke na mkubwa wa Musa) akakufa pale, akazikwa pale.*
>
> *2 Na maji hayakuwa kwa makutano; wakajikusanya juu ya Musa na juu ya Haruni. 3 Watu **wakashindana** na Musa, wakasema: Ingalikuwa heri kama tungalikufa wakati ndugu zetu walipokufa mbele ya Bwana! 4 Na kwa nini mumeleta makutano ya Bwana katika jangwa hili, ili tufe pale, sisi na ngombe zetu? 5 Na kwa nini mumetupandisha toka Misri, ili kutuleta kwa pahali pabaya hapa? Si pahali pa mbegu wala tini wala zabibu wala makomamanga; wala hapana maji ya kunywa!"*

Unasikia maneno Waisraeli waliyosema? Nyuma ya maneno yote ambayo Mungu aliwatendea na baba zao katika Misri na jangwani, mioyo yao ilijaa asante na tumaini? Sivyo! Walifanya neno lile lile ambalo baba zao walifanya. Walinungunika! Ndiyo, walichoka sana na jangwa, lakini ingaliwapasa kukumbuka ya kwamba kwa sababu ya kutoamini kwao walikuwa hawajaingia inchi ya Kanana! Ndiyo, Waisraeli walikosa maji kweli. Lakini kwa sababu gani hawakuomba Mungu? Yule ambaye aliwalinda kwa miaka makumi ine katika jangwa lile la kukauka hakuweza kuwapa maji sasa? Aliweza! Mungu alitaka kuwapa vyote walivyohitaji! Lakini Waisraeli hawakuamini Bwana Mungu wao kabisa!

Tuendelee ndani ya sura 20 kuona nini ilitokea.

> (Hesabu 20) *6 Musa na Haruni wakatoka katika makutano, wakakwenda hata mlangoni mwa hema ya kusanyiko, wakaanguka kifudifudi; na utukufu wa Bwana ulionekana kwao. 7 Bwana akamwambia Musa akisema: 8 Twaa fimbo na kusanya makutano, wewe na Haruni ndugu yako na **museme na mwamba** mbele ya macho yao, ili utoe maji yake; nawe utawatokezea maji toka mwamba; hivi utanywesha maji makutano na ngombe zao.*
>
> *9 Musa akatwaa fimbo kutoka mbele ya Bwana, kama alivyomwagiza. 10 Musa na Haruni wakakusanya makutano mbele ya mwamba,*

*akawaambia: Sikieni sasa, ninyi waasi; sisi tutawatokezea ninyi maji toka mwamba huu? 11 Musa akanyosha mkono wake,* ***akapiga mwamba*** *mara mbili kwa fimbo yake; maji yakatoka mengi, makutano wakakunywa, na ngombe zao. 12 Bwana akawaambia Musa na Haruni: Kwa sababu hamukuniamini, kwa kunitakasa machoni mwa wana wa Israeli, kwa hivi hamutaingiza kusanyiko hili ndani ya inchi ambayo ninawapa.*

Ulifahamu neno lililotokea? Mungu aliagiza Musa kufanya nini ili makutano ya Israeli wapate maji kwa kunywa? Alisema: *"Museme na mwamba."* Musa alitii agizo la Mungu kwa njia ya kusema na mwamba? Sivyo! Musa alikasirika, akapiga mwamba mara mbili. Kuasi kwake hakukuzuiza Mungu, kwa wema wake, kufanyiza maji kutoka ndani ya mwamba, lakini neno Musa alilofanya lilichukiza Mungu. Kwa sababu hii Mungu alimwazibu, akisema: *"Kwa sababu hamukuniamini, kwa* ***kunitakasa*** *machoni mwa wana wa Israeli, kwa hivi* ***hamuta****ingiza kusanyiko hili ndani ya inchi ambayo niliwapa."*

Labda unafikili azabu ya Mungu kwa Musa ilikuwa kali zaidi. Lakini sharti tukumbuke ya kwamba neno linalopendeza Mungu ni kwa watu kuamini na kutii Neno lake. Mungu hawezi kukubali neno lo lote lisilopatana na Neno lake—hata kama likitoka kwa Musa, nabii wa Mungu!

Mungu haonyeshi upendeleo. Musa alikuwa nabii mkubwa, lakini alikuwa mtu tu kama sisi sote. Kwa sababu hii, alikuwa mwenye zambi kama wazao wote wa Adamu. Hata nabii wa Mungu, **Musa, hakuweza kujiponyesha mwenyewe** kwa sababu ya kazi zake njema. Kama wazao wote wa Adamu Musa alianguka kwa maneno mengine na hakutimiza haki ya sheria kwa maneno yote. Ilikuwa sharti kwa nabii Musa, kama Waisraeli wote, kufikia Mungu kwa njia yeye aliyotayarisha kwa watu kupata wokovu, ndiyo njia ya sadaka ya damu. Kwa njia ya zambi ya Musa, Mungu anataka kutukumbusha ya kwamba **wote** wamefanya zambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. (Waroma 3:23) Wote wana hatia mbele ya Mungu. Kila mtu amefanya zambi. Hakuna mtu aliye mwenye haki! Hakuna asiyekwenda mbali na njia ya Mungu—ila Mkombozi mwenye haki aliyekuja toka mbingu kuokoa wenye zambi!

Tukiendelea na habari zetu, tunasoma kwa mwisho wa sura 20 ya kwamba Haruni, mkubwa wa Musa, alikufa juu ya mlima unaoitwa Hori, na watu wa Israeli walimwombolea kwa siku makumi tatu.

Nyuma yake, ndani ya sura 21, kuanza na shairi 4, Maandiko yanasema:

> (Hesabu 21) *4 Wakasafiri toka mlima Hori kwa njia ya Bahari Nyekundu . . . roho za watu zilitiwa* ***mashaka sana*** *kwa sababu ya njia. 5 Watu wakanungunikia Mungu na Musa: Kwa nini mumetuleta sisi toka Misri ili tufe katika jangwa? maana hapana mkate na hapana maji; na nafsi yetu inachukia chakula hiki bule.*
>
> *6 Na Bwana alituma* ***nyoka za moto*** *kati ya watu, wakauma watu; watu wengi katika Israeli wakakufa. 7 Watu wakakuja kwa Musa, wakasema: Tumekosa kwa sababu tumenungunikia Bwana na wewe; omba kwa Bwana aondoshe nyoka hawa kati yetu. Musa akaombea watu. 8 Bwana akamwambia Musa: Ujifanyie nyoka ya shaba na kumweka juu ya mti; na itakuwa kila mtu aliyeumwa, wakati anapomwona, ataishi. 9 Musa akafanya nyoka ya shaba, akamweka juu ya mti; na ilikuwa nyoka akiuma mtu ye yote, wakati alipo****angalia*** *nyoka ya shaba, aka****ishi****."*

Tuwaze juu ya habari hizi za kushangaza. Kwa nini Mungu alituma nyoka za sumu katikati ya Waisraeli? Alituma nyoka kwa sababu ya **zambi** zao. Tulisikia maneno mabaya waliyosema juu ya Mungu na Musa, na walikataa chakula ambacho Mungu aliwapa toka mbinguni. Kwa sababu hii Mungu alituma nyoka za sumu kuwauma, na kufanyiza wengi wao **kufa**.

**Ilipasa Waisraeli kufanya nini kwa kuepuka mauti?** Waliweza kujiokoa wenyewe toka tauni mbaya ile ya nyoka? Waliweza kujiponyesha wenyewe toka sumu ya mauti ya nyoka? Hawakuweza hata kidogo! Basi wafanye nini? Waliweza kulilia Mungu! Wakafanya hivi. Tuliona ya kwamba Waisraeli walitubu na walifikia Musa wakimwambia, "Tumekosa! Tulikukosea wewe na tulikosea Mungu! Omba Bwana aweze kutuhurumia na kuondosha nyoka hizi."

Mungu aliwaondolea nyoka? Alifanya neno hata zuri kupita. Mungu aliagiza Musa kufanya nyoka ya shaba na kuinyanyua juu ya fimbo ili *"mtu ye yote aliyeumwa na nyoka aweze* ***kuiangalia na kuishi.****"* Hii ndiyo njia **ya kuponya ya Mungu**. Nyoka akiuma mtu ye yote, ilipasa mtu huyu kufanya neno moja tu, ndilo kutazama nyoka ya shaba juu ya fimbo, na ataponyeshwa! Hii ndiyo njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha: **Tazama na ishi!**

Mungu aliahidi kuponyesha **mtu ye yote** aliyeangalia nyoka ya

shaba ambayo Musa alinyanyua juu ya fimbo. Nini ilitokea juu ya wale **waliokataa kuangalia**? Walikufa na maumivu machungu. Lakini mtu ye yote aliyeamini Mungu na kuangalia nyoka ya shaba aliponyeshwa toka mauti, kwa sababu Mungu alikuwa ameahidi akisema, *"**mtu ye yote** aliyeumwa anaweza **kuiangalia na kuishi.**"*

Kweli hizi ni habari nzuri kabisa. Ziliandikwa kwa kutufundisha sisi. Mungu anataka kutuonyesha ya kwamba **sisi sote** ni sawasawa na Waisraeli. Sisi vilevile ni wenye zambi, na kwa sababu hii tunanungunikia Mungu na watu mara nyingi na kukosea Mungu ndani ya mawazo yetu, masemo yetu na matendo yetu. **Shetani** ni kama nyoka za sumu zilizouma Waisraeli. Na **zambi** ni kama sumu ambayo iliwaua. Shetani ameuma wana wote wa Adamu, na sumu ya zambi itatuharibu kwa milele, isipokuwa Mungu anatupatia **njia ya kuponyeshwa**! Malipo kwa zambi ni kufa ndani ya moto wa milele, na sisi watu hatuna njia kujiponyesha. Lakini tunasifu Mungu, kwani namna alivyotayarisha njia kuponyesha Waisraeli wasife kwa sababu ya **sumu ya nyoka**, vivyo hivyo alitayarisha njia kuokoa wana wa Adamu toka **sumu ya zambi**!

Rafiki, unajua neno Mungu alilofanya kukuokoa toka laana ya zambi? **Soma neno Mkombozi mtakatifu alilosema** karibu miaka elfu moja mia tano nyuma ya wakati Musa aliponyanyua nyoka ya shaba juu ya mti jangwani. Alisema, *"Kama Musa alivyonyanyua nyoka jangwani, vivyo hivyo sharti Mwana wa watu anyanyuliwe. . . ili kila mtu akimwamini asipotee lakini awe na uzima wa milele!"* (Yoane 3:14,16)

Shairi hili toka Habari Njema {*Injil*} linatufundisha ya kwamba nyoka ya shaba ambayo Musa alinyanyua jangwani, ilikuwa **mfano** wa Mkombozi atakayekuja na kufa msalabani ili aweze kushinda Shetani aliyekuwa na nguvu za kufa. (Waebrania 2:14) Ni habari za ajabu, habari nzuri kabisa! Tutaona ndani ya masomo ya nyuma ya kwamba, kwa njia ya mauti na ufufuko wa Mkombozi, Mungu amefunulia wana wa Adamu mlango wa wokovu, salama na furaha kwa milele! Mungu anataka ukubali tu ya kwamba huwezi kujiokoa mwenyewe toka uweo wa zambi, na kuamini moyoni mwako maneno Mungu aliyosema juu ya Mwokozi aliyekufa juu ya msalaba kulipa deni ya zambi zako. Mungu anasema: **Tazamia Mkombozi nawe utaishi!** Umwamini na Mungu atakuponyesha, kukuokoa toka sumu ya zambi na kukutayarishia pahali pa kukaa milele mbele yake mbinguni!

Wazee na vijana, wanaume na wanawake, wenye mali na wamasikini, Mungu anasema na kila mtu: **Angalia na kuishi!** Tazamia Mkombozi mwenye uwezo aliyetumwa na Mungu na **utaokolewa**! Lakini Mungu anasema vilevile: **Kama ukikataa kuangalia,** kama usipoamini Mwokozi kwa njia yake Mungu alitayarisha njia ya pekee kukuokoa toka zambi, *"utakufa katika zambi zako!"* (Yoane 8:24) Sheria ya haki ya Mungu inasema ya kwamba mtu ye yote asiyepokea njia ya kupona ambayo alitayarisha **ataharibiwa**. Mungu hana njia nyingine kuokoa wana wa Adamu toka sumu ya zambi. Umetazamia Mwokozi juu yake manabii wote waliandika? Atakusafisha na kukupa uzima wa milele kama ukimwamini na kumtegemea yeye tu. Sikia tena neno Maandiko yanayosema: *"Kama Musa alivyonyanyua nyoka jangwani, vivyo hivyo sharti Mwana wa watu (Mkombozi wa dunia) anyanyuliwe . . .* ***ili kila mtu akimwamini asipotee, lakini awe na uzima wa milele!"*** (Yoane 3:14,16)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutafikili juu ya masemo ya mwisho ya nabii Musa na kumaliza masomo yetu ndani ya Tora takatifu . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya ahadi hii ya Mungu:

***"Muniangalie, na mwokolewe!"*** (Isaya 45:22)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 43

# MANENO YA MWISHO YA MUSA

### KUMBUKUMBU LA TORATI

Salama iwe kwako, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na somo lingine la mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya masomo 40 ya mbele tuliangalia kitabu cha kwanza ndani ya Maandiko Matakatifu, kitabu cha Tora. Kama unavyojua, ni Mungu aliyetia maneno yake ndani ya nia ya nabii Musa na kumwongoza kuyaandika ndani ya kitabu. Karibu miaka elfu tatu mia tano imepita tangu Musa aliandika Tora, lakini hata leo ina faida nyingi kwa sisi. Tora ni **msingi** uliowekwa na Mungu mwenyewe, ili tuweze kupima kila neno tunalosikia na **kufahamu kama linatoka kwa Mungu** au sivyo. Mafundisho ndani ya Tora ni **kweli kabisa** toka Mungu. Mafundisho yo yote yasiyopatana nayo ni **uwongo**. Kweli nzima ya Mungu inapatana kabisa na maneno yanayoandikwa ndani ya Tora. Kuna neno moja ambalo Mungu Mwenyezi hawezi kufanya. Ni neno gani? Ndiyo, **Mungu hawezi kujikana mwenyewe!** Ndani ya Hesabu 23:19 Musa aliandika maneno haya, ***"Mungu si mtu aseme uwongo; wala mwana wa mtu, ajute; anasema naye hatalifanya? au amenena naye hatalitimiza?"***

Kwa njia ya kujifunza maandiko ya Tora ya Musa, Mungu ametufunulia siri nyingi za ndani. Leo tunataka kumaliza mafundisho yetu toka Tora takatifu. Lakini mbele ya kuangalia sura za mwisho, tufanye ukumbusho wa maneno tuliyoona tangu mwanzo kufika leo.

Ndani ya sura ya kwanza ya Tora, Mwanzo 1, tuliona namna Mungu alivyoumba mtu wa kwanza kwa sura yake mwenyewe.

Mungu alitaka kuwa na **upatano** wa ajabu, wa maana sana na mtu ambaye alimwumba. Kwa sababu hii aliweka ndani ya nafsi ya mtu nia (roho) ili aweze kujua Mungu, alimpa roho aweze kupenda Mungu na alimpa mtu njia kuwa na kutaka kwake mwenyewe ili aweze kuchagua yeye mwenyewe kama atatii Mungu au kumwasi.

Ndani ya sura ya tatu, tuliona ya kwamba mtu wa kwanza, Adamu alichagua kutii Shetani na alikula ya mti Mungu aliokataza. Hivi, Maandiko yanasema: *"Kwa mtu mmoja **zambi** iliingia ulimwenguni, na **kufa** kwa njia ya zambi; na hivi kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi."* (Waroma 5:12) Azabu kwa zambi ni Mauti na kutengwa na Mungu kwa milele.

Hivi, tuliona ya kwamba Mungu alifukuza Adamu na Hawa toka Shamba la Paradiso kwa sababu ya zambi yao. Lakini mbele ya kuwafukuza, Mungu alitangaza ya kwamba alikusudi kutuma **Mkombozi** duniani siku nyingine, kufungua mlango wa wokovu kwa wazao wa Adamu; kuwafungua toka utawala wa Shetani na azabu ya zambi.

Nyuma yake tulijifunza ya kwamba Mungu aliita Abrahamu, akiahidi kumfanyiza baba ya **taifa lisilo na kifano** kwa njia yake manabii na Mkombozi watazaliwa. Hivi, Abrahamu alizaa Isaka; Isaka alizaa Yakobo; na Yakobo alizaa wana kumi na wawili. Nyuma, Mungu aligeuza jina la Yakobo kuwa **Israeli**. Wana kumi na wawili wa Israeli walikuwa mwanzo wa taifa jipya ambalo Mungu aliahidi Abrahamu. Wana kumi wa kwanza waliuza mdogo wao, Yosefu, kuwa mtumwa aliyepelekwa kwa Misri. Lakini, *"yo yote mtu anayopanda, ndiyo atakayovuna."* (Wagalatia 6:7) Hivi, tuliona ya kwamba wana wote wa Israeli waligeuka watumwa katika inchi ya Misri. Hata hivi, Mungu hakusahau ahadi yake kwa Abrahamu na wazao wake. Ndani ya kitabu cha Kutoka tulijifunza namna Mungu alivyotimiza ahadi yake kwa Abrahamu kwa njia ya kuita Musa kufungua Waisraeli toka utumwa wao.

Habari za Musa zilitujulisha ajabu kubwa la namna Mungu alivyoponyesha makutano ya Israeli toka utumwa wa Farao na watu wa Misri. Tunasoma vilevile namna Mungu alivyowachunga jangwani na kuwafikisha kwa mpaka wa Kanana, ndiyo inchi ambayo aliahidi kumpa mzazi wao Abrahamu miaka mingi mbele. Lakini zaidi ya Waisraeli waliogopa watu warefu sana waliokuwa inchini mwa Kanana na hawakuamini Mungu atatimiza ahadi yake ambayo

aliwatolea. Kwa sababu hii hawakuingia inchi ya Kanana kwa wakati ule.

Kwa sababu ya kutokuamini kwao, Waisraeli walizunguka jangwani kwa miaka makumi ine, kufika wakati wote wasioamini ahadi ya Mungu juu ya inchi ya Kanana walikuwa wamekufa. Hii ilikuwa azabu ya Mungu kwa kutokuamini kwao. Kweli yeye ni *"Mungu mwaminifu, asiye na uovu, yeye ndiye mwenye haki na adili."* (Torati 32:4)

Sasa **tumalize safari yetu ndani ya Tora.** Kumbuka ya kwamba Waisraeli walikuwa jangwani kwani Mungu alikuwa akiwaazibu kwa sababu ya kuasi kwao. Kila mmoja wa wale waliokuwa na miaka kupita makumi mbili na aliyekataa kuamini ahadi ya Mungu juu ya inchi ya Kanana alikuwa amekufa. Hata mmoja wao (ila Yosua na Kalebu) alikuwa hai. Sasa watoto wao walifika tena kwa mpaka wa Kanana. Nyuma ya miaka mirefu makumi ine jangwani, walikuwa na hamu sasa kuingia inchi ambayo wazazi wao walikosa kuingia na kupanga pale!

Mafundisho yetu leo ni toka sehemu ya tano ya Tora, kitabu cha **Torati** (maana yake *Sheria ya Pili*). Ndani ya sehemu hii ya mwisho Musa alifanya ukumbusho wa sheria takatifu ya Mungu na kuifundisha kwa makabila ya Israeli. Ndani ya Torati tunapata vilevile **hotuba ya mwisho** ya Musa kwa watu kuwatayarisha kuingia inchi ambayo Mungu aliahidi kuwapa. Hatuna saa kusoma hotuba nzima ya Musa leo, lakini tunaweza kuijumlisha na neno moja tu: **"Musisahau!"**

Kwa ufupi, Musa alisema maneno kama haya kwa Waisraeli: Mwangalie musisahau ya kwamba mulikuwa watumwa katika Misri! Musisahau maneno yote ambayo Mungu aliwafanyia njiani, nyuma ya kutoka Misri na kufikia inchi mpya mutakayoingia. Musisahau namna mulivyokosea Mungu wenu! Musisahau namna Bwana alivyohukumu wazao wenu kwa sababu ya kutoamini kwao na maiti zao zinabaki jangwani. Musisahau ya kwamba Mungu alitendea wazazi wenu mema, lakini walikuwa na kichwa kigumu na walikataa kumwamini. **Musisahau maneno haya!**

Leo, wakati munaposikia sauti ya Mungu, musifanyize mioyo yenu migumu, kama wazazi wenu walivyofanya jangwani. Mutakuwa kama wazazi wenu waliokataa kuamini Neno la Mungu, au mutaamini Bwana Mungu wenu? Kama mukikataa kuamini Neno

la Mungu kama wazazi wenu walivyofanya, Mungu atawaazibu ninyi namna alivyoazibu wazazi wenu. **Musisahau neno hili!**

Bwana Mungu atawaingiza ninyi ndani ya inchi inayojaa maziwa na asali ambayo aliahidi kuwapa wazazi wenu. Musisahau Mungu ambaye aliwapa ninyi inchi hii, kwa sababu mtu haishi kwa mkate tu lakini kwa kila neno linalotoka kinywa cha Bwana! **Musisahau neno hili!**

Nyuma ya kumaliza hotuba yake, Bwana alisema na Musa:

> (Torati 32) *49 Panda katika mlima huu wa Abarimu . . . kuelekea Yeriko; na angalia inchi ya Kanana ambayo ninawapa wana wa Israeli kuwa uriti; 50 na kufa katika mlima pahali unapopanda . . . 51 kwa sababu mumenikosea katikati ya wana wa Israeli kwa maji ya Meriba ya Kadesi, katika jangwa . . . kwa sababu hamukunitakasa katikati ya wana wa Israeli. 52 Kwani utaona inchi mbele yako; lakini hutakwenda kule kuingia katika inchi ambayo ninawapa wana wa Israeli.*
>
> (Torati 34) *1 Musa akapanda kutoka inchi sawa za Moabu mpaka mlima Nebo . . . Bwana akamwonyesha inchi yote . . . inchi yote ya Yuda mpaka bahari ya mangaribi . . . 4 Bwana akamwambia: Hii ni inchi ambayo niliapia Abrahamu, Isaka na Yakobo nikisema: Nitawapa wazao wako: nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka kule. 5 Hivi **Musa mtumishi wa Bwana akakufa pale katika inchi ya Moabu,** sawasawa na neno la Bwana. 6 Akamzika bondeni katika inchi ya Moabu . . . lakini hakuna mtu anayejua kaburi lake hata leo. 7 Musa alikuwa na miaka mia moja makumi mbili wakati alipokufa; jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka. 8 Wana wa Israeli wakalilia Musa katika inchi sawa za Moabu siku makumi tatu. Basi siku za kulia kwa kuomboleza Musa zikakwisha. 9 Na **Yosua** (aliyekomboa Musa kama kiongozi cha Waisraeli) . . . alijaa roho ya akili; maana Musa alikuwa ameweka mikono yake juu yake; na wana wa Israeli walimsikiliza, kama Bwana alivyoamuru Musa.*
>
> *10 Wala hakusimama tena katika Israeli nabii kama Musa, ambaye Bwana alijua uso kwa uso; 11 katika alama zote na maajabu, ambaye Bwana alituma kufanya katika inchi ya Misri, kwa Farao, na kwa watumishi wake wote, na kwa inchi yake yote; na katika ule mkono wa nguvu wote na katika yale maogopesho makubwa yote ambayo Musa aliyatenda mbele ya macho ya Israeli wote."* Amina.

Basi, rafiki, tumefikia mwisho wa Tora. Maneno yote ndani ya Tora yaliandikwa ili tuweze kuongezeka katika kujua, na kuongozwa kuamini njia ya wokovu wa Mungu. Kweli, Musa alikuwa **nabii mkubwa**. Alijua Bwana Mungu uso kwa uso. Kwa uwezo wa Mungu alifanya maajabu. Kwa mkono wa Musa, Mungu aliokoa Waisraeli toka mateso ya Farao. Na kwa mkono wake, Mungu ametupa sisi Tora, kitabu cha kwanza cha Maandiko Matakatifu. Inapasa kila mtu kujua maneno Musa aliyoandika. Mtu ye yote asiyejua Tora ya Musa atadanganywa ndani ya maneno mengi naye ni katika hatari kubwa ya kupotea katika njia ya uzalimu. Kumbuka, Tora ni msingi ambao Mungu mwenyewe aliweka, msingi juu yake Mungu, kwa njia ya manabii wote wengine atajenga baki la kitabu chake kitakatifu.

Kweli, nabii Musa aliandika maneno ya kushangaza, maneno magumu kwa kufahamu. Lakini ya maneno yote Musa aliyofanya na kuandika, neno lililokuwa na maana kubwa zaidi ni neno alilosema ndani ya sehemu ya tano ya Tora, Torati sura 18. Pale Musa aliwaambia Waisraeli ya kwamba Mungu **alikusudi kuleta nabii mwingine, hata mkubwa kupita Musa, atakayesema kwa ajili ya Mungu.** Sikia maneno Musa aliyowaambia watu wa Israeli:

> (Torati 18) *15* ***Bwana Mungu wako atakusimamishia nabii toka katikati yako, mmoja wa ndugu zako, sawasawa nami; mumsikilize yeye;*** *16 kama maneno yote uliyotaka kwa Bwana Mungu wako katika Horebu kwa siku ya kusanyiko, ukisema: Nisisikie tena sauti ya Bwana Mungu wangu, wala nisione tena moto huu mkubwa nisife. 17 Bwana akaniambia:* ***Wametenda vema kusema walivyosema.*** *18* ***Nitawasimamishia nabii toka katikati ya ndugu zao sawasawa nawe; na nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote ambayo nitamwagiza.*** *19* ***Na itakuwa mtu ye yote asiyetaka kusikiliza maneno yangu atakayosema kwa jina langu, nitalitaka kwake.***

Kwa njia ya masemo haya ya Musa Mungu alitangaza ya kwamba nabii mwingine atakuja kwa njia ya taifa la Waebrania (mash. 15,18), Mtu atakayesema Neno la Mungu zima (mash. 18,19), Nabii atakayekuwa Mpatanishi katikati ya Mungu na watu (mash. 16,17). Unajua kama Nabii huyu alikuwa nani? Unajua Nabii gani aliyesema na amri kupita Musa? Unajua Nabii gani alifanya kazi zilizokuwa kubwa kupita hata zile za Musa? Ndiyo, Nabii ambaye Musa alise-

ma juu yake ni **Mkombozi mwenye haki,** aliyezaliwa na bikira Myuda. Hata mbele, wakati Musa alipoonya taifa la Israeli, alisema na nguvu: ***"Sharti mumsikilize!*** . . . ***mtu ye yote asiyetaka kusikiliza maneno yangu atakayosema kwa jina langu, nitalitaka kwake."***

Rafiki, mafundisho yetu juu ya Tora inakwisha hapa. Tumalize na maneno Musa yeye mwenyewe aliyotangaza kwa Waisraeli siku alipokufa. Ndani ya sura 32 Musa alisema:

> ***"Sikilizeni, ninyi mbingu, na nitasema; na inchi isikie maneno ya kinywa changu . . . nitatangaza jina la Bwana. Muhesabie Mungu wetu ukubwa . . . Yeye ni mwamba, kazi yake ni kamilifu; maana njia zake zote ni hukumu; Mungu mwaminifu asiye na uovu, yeye ndiye mwenye haki na adili!"*** (Torati 32:1,3,4)

Na masemo haya ya Mungu kwa kinywa cha Musa tunamaliza somo hili 43. Ndani ya somo linalofuata tutaanza kitabu kitakatifu kinachofuata Tora ya Musa na tutaona namna Mungu alivyoingiza Waisraeli ndani ya inchi inayojaa maziwa na asali kama alivyoahadi zamani . . .

~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu wa pekee anayestahili utukufu na enzi kwa milele, akubariki! Nabii Musa alisema vizuri:

> ***"Bwana . . . ni . . . Mungu mwaminifu asiyetenda mabaya! Yeye ndiye mwenye haki na adili!"*** (Torati 32:4) Amina!
~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 44

# YOSUA NA INCHI YA KANANA

### YOSUA

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunafurahi kwa sababu leo tunaanza kujifunza habari za kitabu cha Yosua.

Ndani ya masomo ya mbele tulimaliza Tora ya Musa, kitabu cha kwanza cha Maandiko ya Manabii. Ndani ya Tora tulijifunza namna gani zambi iliingia dunia na kuleta laana. Lakini tulijifunza vilevile ya kwamba Bwana Mungu alikuwa na shauri la ajabu, akaahidi kutuma Mwokozi duniani atakayekomboa wana wa Adamu toka laana ya zambi. Kwa kuanza kutimiza shauri hili, Mungu aliita Abrahamu kuondokea nyumba ya baba yake na inchi yake na kuhama kwa inchi ya mbali, ndiyo Kanana. Mungu alikusudi kuanza taifa jipya na Abrahamu kwa njia yake Mkombozi atazaliwa. Wakati Abrahamu alipofikia inchi ya Kanana, Mungu alionekana kwake tena, akamtolea ahadi akisema, *"Inchi ya Kanana ndani yake wewe ni mgeni, nitawapa wazao wako kuwa inchi yao kwa milele!"* Leo tutaona **namna Mungu alitimiza ahadi hii ambayo alitolea Abrahamu zamani,** na **alitoa inchi ya Kanana kwa wazao wa Abrahamu**, ndio Waisraeli. Kanana ndiyo inchi inayoitwa **Israeli** kwa wakati wa sasa.

Ndani ya somo la mbele na sura ya mwisho ya Tora, tulisikia namna **Musa** alivyokufa juu ya mlima, nyuma ya kuona Kanana toka kichwa chake. Nyuma ya kufa kwa Musa, **Yosua,** msaidizi wake, aligeuka kiongozi cha Waisraeli. Ni Mungu aliyechagua Yosua kukomboa Musa. Tulisoma juu ya Yosua mbele. Yosua alijulikana kwa sababu aliamini ahadi zote za Mungu, hata wakati zaidi ya Waisraeli wasipoamini. Yosua alikuwa mmoja wa wapelelezi walioamini Mungu wakati Waisraeli walipofikia mpaka wa inchi ya Kanana mara ya kwanza. Waisraeli walikuwa tayari kumtupia mawe na kumwua kwa sababu aliamini na aliwaonya kuamini Bwana vilevile na kwenda kukamata inchi. Leo tutaona ya kwamba Yosua

huyu aliyekataliwa na Waisraeli miaka makumi ine mbele aligeuka kiongozi ambaye alichaguliwa na Mungu kuingiza Waisraeli ndani ya inchi!

Kitabu cha Yosua tunachosoma leo, ni ndani ya Maandiko Matakatifu katikati ya Tora na kitabu cha Zaburi. Ndani ya kitabu cha Yosua tunasoma juu ya Mungu akitimiza ahadi aliyotolea Abrahamu zamani wakati aliposema naye: *"Nitakupa wewe na uzao wako inchi yote ya Kanana, kwa uriti wa milele!"* (Mwanzo 17:8)

Kwa wakati ule Waisraeli hawayakuwa bado na inchi yao wenyewe. Walikuwa wenye kutembeatembea jangwani. Na vilevile inchi ile ya Kanana watakayokaa ndani yake ilijaa na watu warefu sana waliokuwa askari za uwezo sana. Lakini Mungu Mwenyezi alikusudi kufukuza wenyeji wa Kanana na kuwaharibu kwa sababu ya zambi zao nyingi za kuchukiza na kuweka inchi yao nzuri mikononi mwa Waisraeli.

Sasa tuone namna gani Yosua na Waisraeli waliingia inchi, walishinda na kuikamata kuwa inchi yao wenyewe. Ndani ya sura ya kwanza ya Yosua tunasoma:

> (Yosua 1) *1 Nyuma ya kufa kwa Musa, mtumwa wa Bwana, Bwana akamwambia Yosua, mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akisema: 2 Musa, mtumwa wangu amekufa; ondoka sasa uvuke Yorodani huu, wewe na watu hawa wote, mukaende kwa inchi ambayo ninawapa wana wa Israeli. 3* ***Kila pahali miguu yenu itakapokanyaga, nimekwisha kuwapa nyinyi sawasawa nilivyomwambia Musa.*** *4 Toka jangwani, na Lebanoni hii, hata mto mkubwa . . . na hata bahari kubwa . . . itakuwa mipaka yenu. 5 Hakuna mtu atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; sawasawa nilivyokuwa pamoja na Musa, nitakuwa pamoja nawe vilevile; sitakupungukia wala sitakuacha. 6 Kaa na nguvu na uwe hodari, maana ni wewe utakayeritisha watu hawa, inchi ambayo niliapia baba zao ya kwamba nitawapa. . . 9* ***Sikukuagiza? Kaa na nguvu na uwe hodari, usiogope, na usifazaike, kwa kuwa Bwana Mungu wako ni pamoja nawe pahali po pote unapokwenda.***
>
> *10 Halafu Yosua akaagiza wasimamizi wa watu akisema: 11 Piteni katikati ya kambi; mwagize watu, mukisema: Tengenezeni chakula kwa maana kwa siku tatu mutavuka Yorodani huu, kwa kuingia na kumiliki inchi ambayo Bwana Mungu wenu anawapa ninyi mupate kuimiliki."*

Kisha, Maandiko yanatupasha ya kwamba Yosua alituma **wapelelezi wawili** na kuwaagiza, "Kwendeni mutazame inchi, hata **Yeriko**." Wapelelezi wawili walikwenda na kuangalia Yeriko na kuta za juu na nguvu sana zilizozunguka mji. Usiku walifichama ndani ya Yeriko, wakaingia nyumba ya kahaba jina lake **Rahaba**. Lakini watu wengine wa Yeriko waliona wapelelezi Waisraeli wakiingia nyumba ya Rahaba. Wakamwambia mfalme habari mara moja, wakimwambia, "Kuna Waisraeli hapa kupeleleza mji." Mfalme alituma askari kwa nyumba ya Rahaba kuwafunga, lakini Rahaba aliwaficha juu ya dari.

Nyuma ya kuondoka kwa askari Rahaba aliita wapelelezi, akasema nao: "Ninajua ya kwamba Bwana, Mungu wenu, ni Mungu wa kweli. Ninajua vilevile ya kuwa Mungu wenu atatoa kwa mikono yenu mji wangu na inchi nzima ya Kanana. Watu wote wa inchi wanawaogopa ninyi sana, kwa sababu wamesikia namna Mungu alivyofungua Bahari Nyekundu mbele yenu na kuharibu adui zenu zote. Ninaamini ya kwamba Bwana Mungu wenu ni Mungu wa kweli! Kwa sababu hii, ninawaomba ninyi kunitolea kiapo ya kwamba wakati munapokuja kushinda mji wetu, mutanilinda mimi pamoja na jamaa yangu, na kutuponyesha toka mauti." Wapelelezi wawili walijibu: "Wakati Mungu anapotoa mji wenu mikononi mwetu, tutakulinda wewe na wote walio nyumbani pamoja nawe."

Ndani ya sura 3, Maandiko yanapasha habari za watu wa Israeli wakivuka **mto Yorodani** kwa kuingia inchi ya Kanana, lakini mto ulikuwa mpana na maji yake yalikwenda chini sana. Namna gani milioni mbili au tatu za watu waliweza kuvuka ule mto mpana? Si nguvu kujibu ulizo hili, kwa sababu Bwana Mungu ambaye aliwafungulia njia katika Bahari Nyekundu hakubadilika! Mungu alifungua njia kwa Waisraeli vilevile, lakini mara hii ilikuwa kuvuka Mto Yorodani. Hivi walipita katika mto, wakitembea juu ya inchi kavu. Waisraeli wote walivuka mto, wakitokea mbele ya mji mkubwa wa Yeriko. Watu wa Yeriko walikuwa wamefunga malango ya mji. Hakuna mtu aliyeweza kuingia mji, na hakuna mtu aliyeweza kutoka.

Ndani ya sura 5, Maandiko yanatupasha ya kwamba wakati Yosua alipokuwa karibu na Yeriko, alinyanyua kichwa chake, akaona mtu mwenye upanga mkononi mwake. Yosua alimwuliza, "Wewe ni rafiki au adui yetu?" Alijibu, "Mimi nimefika kama **kapiteni ya jeshi** la Bwana!" Yosua akaanguka kwa uso wake kwa

udongo. Halafu yule aliyeitwa kapiteni la jeshi la Bwana alisema na Yosua, "Ondosha viatu vyako kwa miguu yako, kwa kuwa pahali unaposimama ni patakatifu."

Rafiki, unajua nani alikuwa akisema na Yosua? Alikuwa Bwana mwenyewe ambaye alimtokea kwa muda mfupi. Tuliona mbele ya kwamba Mungu alitokea kwa Abrahamu kama mtu na kusema naye, na alitokea kwa Musa ndani ya kijiti kisichoteketea. Na sasa tunaona Mungu akitokea kwa Yosua kama kapiteni mkubwa akishika upanga!

Hivi, Bwana Mungu alisema na Yosua,

> *"Tazama, nimetia Yeriko katika mkono wako pamoja na mfalme wake, na watu wa nguvu na uhodari. Mutazunguka mji, watu wote wa vita, mutazunguka mji mara moja. Utafanya hivi siku sita. Makuhani saba watabeba mabaragumu saba ya pembe za kondoo ndume mbele ya sanduku. Na siku ya saba mutazunguka mji mara saba, na watapiga mabaragumu. Na itakuwa wakati watakapopiga pembe za kondoo ndume kwa nguvu, na watakaposikia sauti ya baragumu, watu wote watapiga kelele na sauti kubwa sana, na ukuta wa mji utaanguka chini, na watu watapanda, kila mtu akiendelea mbele yake."* (Yosua 6:2-5)

Wakati Bwana alipokwisha kusema na Yosua, alikwenda zake.

Yosua alikwenda karibu na Waisraeli mara moja na kuwaambia maneno yote ambayo Bwana alimwagiza. Kisha Yosua aliwaagiza kukamata sanduku ya agano na kuzunguka mji mara moja wakitembea kwa miguu. Aliwaambia vile, "Musiseme neno kufika siku nitakapotoa agizo kulalamika. Saa yenyewe mutaweza kupiga kilele." Wakati walipomaliza kuzunguka mji mara moja walirudia kambi yao na kushinda pale usiku. Siku ya pili walizunguka mji na kurudia kambi. Walifanya hivi kwa siku sita.

Lakini siku ya saba, kwa mapambazuko ya asubui walitoka kambi na kuzunguka mji mara saba. Wakati walipozunguka mji mara ya saba, makuhani walipiga mabaragumu. Halafu Yosua aliagiza makutano: "*Pigeni kelele, kwa sababu Bwana amewapa ninyi mji!*" (Yosua 6:16)

Wakati Waisraeli waliposikia sauti ya baragumu, walilalamika na nguvu, na kuta za mji zilianguka! Wanaume wa Israeli waliingia mji. Hivi tunaona namna gani Yosua na Waisraeli walishinda mji wa kwanza inchini mwa Kanana. Siku ile watu wote wa Yeriko walikufa, ila Rahaba na jamaa yake, kama wapelelezi wawili walivyomwahidi.

Nyumba ya Rahaba haikuanguka, kwa sababu alikuwa ameacha kuabudu sanamu na aliamini na kutegemea Mungu wa Israeli.

Kwa sababu gani Yosua na Waisraeli waliweza kushinda mji ule ulioimarishwa sana, na kuingia inchi ambayo Mungu aliahidi kuwapa? Walishinda kwa sababu waliamini Neno la Mungu. Mungu ni pamoja na wale wanaoamini Neno lake. Kwa sababu gani Rahaba hakufa pamoja na watu wa Yeriko wakati mji ulipoharibiwa? Alipona kwa sababu hakushangaa tu juu ya uwezo wa Mungu; **alimwamini** na alifungana na watu wa Mungu. Hili ndilo neno Maandiko yanayotangaza:

> *"Kwa **imani** kuta za Yeriko zilianguka, zikikwisha kuzungukwa siku saba. Kwa **imani** Rahaba, yule kahaba hakuangamia pamoja nao walioasi, kwa sababu alipokea wapelelezi kwa salama . . . Lakini **pasipo imani haiwezekani kupendeza Mungu;** kwa maana mtu anayekuja kwa Mungu, sharti **aamini** ya kuwa yeye yuko, naye anawapa zawabu wale ambao wanamtafuta."* (Waebrania 11:30,31,6)

Tungefurahi kushiriki nanyi habari nyingine tunazosoma ndani ya kitabu cha Yosua, lakini saa haitoshi. Kwa kujumlisha, inakupasa kujua ya kwamba habari ndani ya kitabu hiki zinaonyesha wazi namna Mungu alikuwa pamoja na Yosua na Waisraeli, na namna alivyowapa inchi ya Kanana na miji yake, kama alivyoahidi. Halafu, ndani ya sura 22, Maandiko yanasema: *"Basi Mungu akawapa Israeli inchi nzima . . . Bwana akatoa adui zao zote mkononi mwao!"* (Yosua 21:43,44)

Rafiki, Mungu alitimiza ahadi aliyotolea Abrahamu na wazao wake miaka mingi mbele? Alileta inchi ya Kanana kwa Waisraeli kama alivyosema atafanya? Ndiyo! Mungu ni mwaminifu na anachunga maagano yake! Kila neno analoahidi atalifanya, hata kama mara nyingine hafanyi hivi mbio. Bwana Mungu alitaka sana kutendea wana wa Israeli kwa neema na kuwapa inchi ya Kanana, inchi ya vyakula vingi, lakini alingoya wamwamini. Kama tulivyoona, Waisraeli **walipoteza miaka mingi mbele ya kuanza kuamini** ahadi ya Mungu. Wazazi wao hawakuriti baraka za inchi ya Kanana, kwa sababu hawakuamini ahadi za Mungu.

Na wewe? Unaamini Mungu? Hatuulizi kama ukiamini Mungu yuko au kama Mungu ni mmoja. Shetani yeye mwenyewe anaamini

kwamba Mungu yuko na ya kwamba yeye ni Mmoja! Ulizo ambalo inakupasa kujibu leo ni: **Unaamini Mungu?** Unam**penda?** Unategemea **Neno la Mungu** na roho yako yote? Una**jua** maneno ambayo Mungu aliweka akiba kwa wale ambao wanamwamini? **Una** uzima wa milele na Roho Mtakatifu ambaye Mungu anampa kila mtu anayeamini Habari Njema yake? Zaidi ya wana wa Adamu wanaamini ya kwamba Mungu yuko. Lakini ni huzuni kwa sababu wachache tu wana**jua** na ku**amini** ahadi kubwa na za damani za Mungu. Rafiki unayesikiliza, Mungu anakupenda sana na anataka kukubariki kupita yote unayoweza kufikili, lakini sharti u**jue** Neno lake, kuli**amini** na kuli**pokea**! Maandiko yanasema:

> *"Jicho halikuona, wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa mtu maneno Mungu aliyotengenezea wenye kumpenda."* (1 Wakorinto 2:9) *"Musiwe wavivu, lakini wafuata wa wale walioriti ahadi kwa **imani na uvumilivu**!"* (Waebrania 6:12)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maonyo haya toka Neno lake:

> ***"Musiwe wavivu, lakini wafuata wa wale walioriti ahadi kwa imani na uvumilivu!"*** (Waebrania 6:12)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 45

# Waamuzi na Ruta

### Waamuzi na Ruta

Ndani ya somo la mbele tulijifunza juu ya Yosua, mtumishi wa Musa, akiongoza Waisraeli kuingia inchi ya Kanana. Tulisoma ya kwamba Mungu alikwenda mbele ya Yosua na Waisraeli kufukuza adui zao na kuwaleta ndani ya inchi ya Kanana, ndiyo inchi iliyojaa vyakula, kama alivyoahidi mzazi wao Abrahamu miaka mingi mbele. Leo tutaangalia vitabu viwili vinavyofuata kitabu cha Yosua, ndivyo vitabu vya **Waamuzi na Ruta**. Vitabu hivi vinaonyesha nini ilitokea katikati ya wakati wa **nabii Yosua** na wakati wa **nabii Daudi**.

Mbele ya kuanza na kitabu cha Waamuzi, vizuri tusome hotuba ya Yosua kwa Waisraeli mbele ya kufa kwake. Ndani ya sura ya mwisho ya kitabu cha Yosua, Yosua alikutana na viongozi wote wa Israeli kuwaonya na kusema nao kupenda na kutii Bwana Mungu wao ambaye aliwafungua toka Misri na kuwapa inchi nzuri ambayo walikaa ndani yake sasa. Ndani ya hotuba hii ya mwisho Yosua alisema nao,

> *"Kama ni vibaya machoni mwenu kutumikia Bwana, **chagueni siku hii ni nani ambaye mutamtumikia**, kama ni miungu baba zenu walitumikia ngambo ya Mto, au miungu ya Waamori munaokaa katika inchi yao. **Lakini mimi na nyumba yangu, tutatumikia Bwana.**" Halafu makutano ya Israeli walijibu Yosua wakisema, "Sisi vilevile tutatumikia Bwana kwa sababu yeye ni Mungu wetu!"* (Yosua 24:15,18)

Sasa tuone nini ilitokea. Ndani ya Waamuzi, sura 2, Maandiko yanasema:

> (Waamuzi 2) *7 **"Watu wakatumikia Bwana siku zote za Yosua,** na siku zote za wazee walioishi kuliko Yosua, walioona*

> *matendo makubwa yote ya Bwana ambayo alitendea Waisraeli. 8 Yosua . . . mtumishi wa Bwana, akakufa, mwenye miaka mia moja na kumi. 9 Wakamzika . . . katika inchi ya vilima vya Efuraimu. . . 10 Kizazi kingine wakasimama nyuma yao wasiojua Bwana wala matendo aliyotendea Israeli. 11* ***Wana wa Israeli wakafanya uovu mbele ya macho ya Bwana****, wakatumikia Mabali. 12 Wakaacha Bwana Mungu wa baba zao, ambaye aliwapandisha toka inchi ya Misri, wakafuata miungu mingine, ya miungu ya mataifa kwa pande zao zote, wakainama mbele yao, wakakasirisha Bwana. 13 Wakaacha Bwana, wakatumikia Bali na Astaroti.*

Hivi Waisraeli walisahau Bwana, wakamgeuzia mgongo na **walianza kufuata dini za mataifa ambayo waliwazunguka.** Lakini, mataifa haya hawakujua Mungu wa kweli na hawakuwa na Neno lake. Waliabudu Bali. Bali ilikuwa sanamu lakini watu wa Kanana walisema ni Mungu. Walijifanyia mifano ya Bali na kuiabudu. Mataifa waliosifu Bali **walifikili walikuwa wakiabudu Mungu**. Lakini kabisa kabisa, walikuwa wakiabudu maneno wao wenyewe waliyotaka na Shetani; lakini hawakujua neno hili kwa sababu Shetani alikuwa amewadanganya. Shetani alidanganya Waisraeli wengi; ni kwa sababu hii walikwenda mbali na Bwana Mungu na walianza kuabudu Bali kama mataifa ambao waliwazunguka walivyofanya.

Zaidi ya Waisraeli waliacha njia Mungu aliyosimamisha, ndiyo njia ya sheria ya Musa na sadaka ya nyama juu ya mazabahu kufunika zambi. Kwa pahali pa kufuata njia ya haki ya Mungu, walifuata njia ya uwongo, ndiyo, dini ya Bali. Amri ya kwanza ya Amri kumi ambazo Mungu alimpa Musa kwa Mlima Sinai inasema:

> *"Usiwe na miungu mingine ila mimi . . . kwa kuwa mimi Bwana Mungu wako ni Mungu mwenye wivu; nikipatiliza wana uovu wa baba zao, hata kizazi cha tatu na cha ine cha wale wambao wananichukia; na nikihurumia elfu elfu zao ambao wananipenda, na kuchunga amri zangu."* (Kutoka 20:3,5,6)

Lakini zaidi ya Waisraeli hawakuheshimu Bwana Mungu, na kwa sababu hii Mungu aliwaazibu.

Tukiendelea na sura 2 ya kitabu cha Waamuzi, Maandiko yanasema:

> (Waamuzi 2) *11* ***Wana wa Israeli wakafanya uovu*** *mbele ya macho ya Bwana, wakatumikia Mabali . . . 14 Hasira ya Bwana iliwaka juu ya Israeli;* ***akawatia kwa mikono ya wanyanganyi*** *walionyanganya vitu vyao,* ***akawauza kwa mikono ya adui zao***

> *pande zote; hivi hawakuweza kusimama tena mbele ya adui zao. 15 Pahali po pote walipotoka, mkono wa Bwana ulikuwa juu yao kwa ubaya, sawasawa Bwana alivyosema na kuwaapia, wakafazaika sana.*

Hivi ndani ya kitabu cha Waamuzi tunaona namna Waisraeli walivyofunga roho zao tena na tena na kugeuka mbali na Bwana. Kwa sababu hii Mungu aliwatoa kwa mikono ya adui zao tena na tena, kuwaazibu, ili waweze kukubali zambi yao na kutubu na kuponyeshwa toka uharibifu. Kila mara Waisraeli walipotubu na roho ya kweli, Mungu aliwasimamishia kiongozi (mwamuzi) kuwaokoa toka adui zao. Tungependa kukupasha habari za watu wahodari kama Gideoni aliyeshinda jeshi kubwa na la uwezo sana na watu mia tatu tu, za Samusoni aliyeshinda watu elfu moja peke yake, lakini hatuna saa kufanya hivi. Labda utasoma habari zao wewe mwenyewe ndani ya kitabu cha Waamuzi.

Kwa kujumlisha, kitabu cha Waamuzi kinatuonyesha ya kwamba kila mara Waisraeli walipokwenda mbali na Mungu na Neno lake, Bwana aliwaazibu kusudi waweze kuachana na zambi yao na kurudi kwake. Wakati walipotubu, Mungu aliwasimamishia kiongozi kuwaponyesha toka adui zao. Hizi ndizo habari za **kitabu cha Waamuzi** kwa ufupi.

Ndiyo, Waisraeli walikosea Mungu tena na tena. Lakini kutoaminifu kwao kuliweza kuzuiza uaminifu wa Mungu? **Sivyo!** Ndiyo, Mungu aliazibu kila mtu aliyefanya zambi, lakini alilinda *taifa* la Israeli, kwa sababu Mungu hakuweza kusahau ahadi ambayo alitolea Abrahamu zamani wakati aliposema naye: *"Ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa."* Mungu alikusudi kufanyiza wazao wa Abrahamu taifa litakaloleta duniani **Mwokozi wa dunia**. Hakuna neno lililoweza kuzuiza shauri hili la ajabu la Mungu: si zambi za Waisraeli, si Farao, si watu wa Misri, si watu wa Kanana, si dini ya uwongo kama ile ya Bali, si Shetani mwenyewe! **Hakuna neno lililoweza kuzuiza shauri la Mungu kutuma Mwokozi wa dunia kwa njia ya Israeli!**

Sasa tuangalie habari ndani ya kitabi kifupi kinachofuata kitabu cha Waamuzi: **kitabu cha Ruta**. Habari za kitabu hiki ni habari za ajabu. Ni kama ua la mapambo sana likiota katikati ya kilima cha kunuka cha yalala, kwa sababu ni **habari za mwanamke aliyependa Mungu hata katika kizazi cha jeuri na ubishi.**

Hatuwezi kusoma kitabu kizima cha Ruta ndani ya somo hili, lakini tunaweza kujumlisha maneno yanayoandikwa ndani yake. Tunaona ya kwamba **Ruta** alikuwa mjane na ya kwamba hakuwa

mtu wa kabila la Israeli. Alikuwa mtu wa kabila la **Moabu** na alikaa inchini mwa Moabu iliyokuwa kwa upande wa kusini wa Israeli. Na inakupasa kujua vilevile ya kwamba watu wa Moabu walikuwa waabudaji sanamu na walizarau Mungu wa Israeli na Waisraeli.

Ndiyo, Ruta alikuwa mwanamke wa Moabu, lakini neno hili halikumsukuma kuzarau Mungu wa Israeli. Sivyo, **aliamini Mungu wa Israeli na moyo wake wote**! Ruta alikuwa amesikia namna Bwana Mungu alikuwa amefanya maajabu ya kushangaza sana kuponyesha makutano makubwa ya Israeli toka mikono ya Wamisri. Na vilevile Ruta alikuwa amesikia maneno nabii Musa aliyoandika ndani ya Tora juu ya njia ya wokovu ambayo Mungu alisimamisha. Ruta aliamini Mungu na roho yake yote, na alipokea habari alizotuma kwa Waisraeli.

Maneno mengine ambayo inatupasa kujua ni ya kwamba Ruta alikaa katikati ya waabudaji sanamu inchini mwa Moabu. Wazazi wa Ruta walikuwa waabudaji sanamu. Hivi Ruta alizaliwa katikati ya waabudaji sanamu. Lakini **Ruta hakuamini tena dini ya baba yake**. Alikuwa ameamini Mungu wa Israeli. Hivi tunaona ya kwamba ilimpasa kuchagua. Ilikuwa nguvu. Vizuri Ruta abaki nyumbani mwa baba yake, aendelee na dini yake na kuoa mwanamume asiyejua Mungu wa Israeli? Au ageuzie nyumba na dini ya baba yake mgongo na kuhama kwa Israeli? Kweli lilikuwa chaguo la nguvu!

Mbele ya kuona kama Ruta alichagua njia gani, inakupasa kujua vilevile ya kwamba ndugu ya mume wa Ruta alikuwa na mke Mwoabu vilevile, jina lake **Orupa**. Orupa vilevile alikuwa amesikia maneno mengi juu ya Mungu wa Israeli. Hivi **ilipasa Orupa kuchagua** vilevile, au kuendelea ndani ya dini ya baba yake au kufuata Bwana Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo.

Ruta na Orupa walichagua njia gani? Orupa alichagua **njia iliyokuwa nyepesi,** ndiyo kubaki nyumbani mwa baba yake na kuoa mtu aliyefuata dini ya baba yake. Lakini Ruta alichagua **njia ya nguvu,** maana yake kuondokea nyumba ya baba yake na kuhama kwa inchi ya Israeli. Ruta alijua ya kwamba hakuna mtu anayeweza kuabudu miungu miwili. Haiwezekani kuchanganya kuabudu Mungu wa Israeli na kuabudu sanamu za Moabu. Kwa sababu hii Ruta aligeuzia dini ya baba yake mgongo. Alifahamu ya kwamba **kutii Mungu ni vizuri kupita kutii mtu**. Alichagua kufuata Mungu wa kweli aliye hai hata kama ndugu zake na rafiki zake hawakuweza kufahamu vizuri. Hivi Ruta aliondokea nyumba ya baba yake, akahama kwa inchi ya Israeli, kwa mji mdogo jina lake ***Betelehemu.***

Mtu mmoja aliishi kwa Betelehemu, jina lake **Boazi**. Boazi alikuwa **mwana wa Rahaba,** mwanamke aliyepona wakati uharibifu ulipopata Yeriko (kama tulivyoona ndani ya somo la mbele. Boazi alikuwa mtu wa haki aliyeheshimu Neno la Mungu sana. Boazi alikuwa mtu wa mali vilevile na mashamba mengi, lakini hakuoa mke kwanza.

Maandiko yanapasha ya kwamba Ruta, aliyekaa katika mji wa Betelehemu sasa, alikuwa na desturi kutoka nyumbani asubui mapema kila siku kutumika ndani ya mashamba kuokota shayiri wavunaji waliyoacha kuanguka chini. Ruta alikuwa mkulima masikini na sheria Mungu aliyotolea Musa kwa Waisraeli iliruhusu watu masikini kufanya hivi, kusaidia njaa yao. Maandiko yanatupasha vilevile ya kwamba Mungu aliongoza Ruta kwenda na kuokota ndani ya shamba la Boazi, mwana wa Rahaba.

Boazi aliona Ruta akiokota ndani ya shamba lake, akasemezana naye. Boazi alitambua mbio uzuri na usafi wa roho ya Ruta. Boazi alikuwa mtu wa haki, akaona kwamba Ruta alikuwa mwanamke mtawa. Halafu unafikili nini ilitokea? Ndiyo, Boazi na Ruta walianza kupendana na nyuma ya wakati walioana. Ruta aliweka Mungu na Neno lake kwanza ndani ya maisha yake na kwa sababu hii Mungu alimbariki. Maandiko yanatujulisha ya kwamba Boazi na Ruta walikuwa na mwana jina lake **Obedi**. Obedi alikuwa baba ya **Yese**, na Yese aligeuka baba ya nabii Daudi. Nabii Daudi aligeuka mfalme mkubwa wa taifa la Israeli, na aliandika **Zaburi** nyingi. Na kwa njia ya wazao wa Daudi **Mkombozi** mkubwa alikuja, ndiye Mwokozi wa dunia. Manabii wote walikuwa wametabiri juu yake.

Hivi tunaona leo namna Mungu alivyotumika ndani ya maisha ya Ruta, mwanamke asiyekuwa wa taifa la Israeli. **Wakati Waisraeli walipogeuzia Bwana Mungu wao mgongo na kufuata dini za mataifa** kando kando yao, **Ruta aligeuzia dini ya baba yake mgongo kufuata Mungu wa Israeli!** Hivi Mungu aliongoza Ruta kuishi kwa Betelehemu katika Israeli, kuolewa na Boazi, na kuwa mzaa bibi ya Daudi, mfalme wa Israeli. Ndani ya maneno haya yote tunaona Mungu akiendelea mbele na shauri lake kuleta **Mkombozi** duniani, kwa sababu Mwokozi atazaliwa kwa njia ya **wazao wa Daudi** na **katika mji wa Betelehemu.**

Ndani ya somo la nyuma tutaanza kusoma ndani ya kitabu kinachopasha juu ya maisha ya nabii Daudi aliyezaliwa katika Betelehemu, mzao wa Ruta na Boazi. Leo tunakulaga na ulizo hili: **Unafanana zaidi na nani?** Unafanana na Orupa, mjane wa ndugu ya

mume wa Ruta, aliyechagua **njia nyepesi**? Au wewe ni mhodari kama Ruta, aliyegeuzia dini ya baba yake mgongo na kufuata **Mungu wa pekee wa kweli**?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapokumbuka maneno ambayo Yosua aliwaambia Waisraeli mbele ya kufa kwake:

> ***"Chagueni siku hii ni nani ambaye mutamtumikia . . . Lakini mimi na nyumba yangu, tutatumikia Bwana!"*** (Yosua 24:15)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SEHEMU 2

# ZABURI
# NA
# MANABII

### MASOMO JUU YA WATU HAWA:

| | |
|---|---|
| SAMWELI | YONA |
| SAULO | ISAYA |
| DAUDI | YEREMIA |
| GOLIATA | DANIELI |
| BATI-SEBA | ZEKARIA |
| SOLOMONO | MALAKI |
| ELIA | |

***"Unaamini manabii?"***

*MATENDO 26:27*

Somo 46

# Samweli, Saulo na Daudi

1 Samweli 1-16; Zaburi 8, 23

Salama iwe kwako, rafiki msomaji, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele, tuliona ya kwamba **wakati wa giza na ubovu** ulifuata muda wa nabii Yosua. Lakini hata kwa wakati ule wa giza tuliona nuru ya uaminifu wa Mungu. Bwana hakusahau ahadi yake kwa Abrahamu na wazao wake juu ya Mkombozi atakayekuja toka taifa la Israeli.

Hivi tuliona kazi ya Mungu ndani ya maisha ya mwanamke mmoja jina lake **Ruta**. Ruta hakuwa Mwisraeli, lakini aliamini Mungu wa Israeli na roho yote. Na wakati Waisraeli wengi walipokwenda mbali na Bwana Mungu wao kufuata dini za mataifa kando kando, Ruta alichagua kuacha dini ya baba yake kufuata Mungu wa Israeli. Ruta alihama kwa inchi ya Israeli, akakaa katika mji wa Betelehemu pahali alipoolewa na Mwisraeli, jina lake Boazi. Boazi na Ruta walizaa mwana, jina lake Obedi; Obedi alizaa Yese, baba ya nabii **Daudi**. Hivi shauri la Mungu kukomboa wana wa Adamu toka zambi zao liliendelea mbele, kwa sababu **Mkombozi** atakuja duniani kwa njia ya **wazao wa Daudi. Mwokozi** huyu atazaliwa katika **Betelehemu**, ndio mji wa Daudi. Ndani ya masomo ya nyuma, tutaona namna manabii ya Mungu walitabiri maneno haya yote na ya kwamba Mkombozi aliyatimiza nyuma ya mia za miaka. Mungu tu aliweza kufanya neno namna hii!

**Nabii Daudi** (*Dawud* kwa lugha ya Waarabe) anajulikana sana ndani ya Maandiko Matakatifu. Jina lake linatajwa kupita mara elfu

moja. Wewe unajua nini juu ya nabii Daudi? Labda unajua ya kwamba ndiye kijana aliyeua yule mtu mrefu sana, ndiye Goliata, na kombeo na jiwe tu. Na labda unajua vilevile ya kwamba Daudi alikuwa mfalme mkubwa wa Israeli, na nabii aliyeandika sehemu kubwa ya kitabu cha Zaburi. Asante kama unajua maneno haya, lakini kuna maneno mengine ambayo inakupasa kujua juu yake. Tukijua ya kwamba Daudi alikuwa mfalme mkubwa, bila kujua **nini ilimfanyiza kuwa mkubwa**—faida yake nini? Au kama tukijua kwamba Daudi aliandika neno la Mungu ndani ya kitabu cha Zaburi, lakini hatujui kama **aliandika nini**—faida yake nini kwa sisi?

Rafiki, kama ukitaka kujua zaidi juu ya **nabii Daudi** na kusikia mengine ya maneno ya uwezo aliyoandika ndani ya **Zaburi**, tunakuomba kufungana nasi kwa somo la leo na masomo matano yanayofuata.

Unajua jina la nabii wa Mungu aliyetangulia nabii Daudi? Ni nabii **Samweli.** Mungu alichagua Samweli kurudisha Waisraeli karibu na Bwana, Mungu wao, kwa sababu mioyo yao ilikuwa mbali sana na Mungu. Leo tutasoma toka **kitabu cha Samweli**. Kitabu hiki kitakatifu kina nafasi kubwa katikati ya maandiko ya Manabii, kwa sababu ndani yake tunasoma habari toka maisha ya Samweli na ya wafalme watatu wa kwanza wa Israeli: Saulo, Daudi na Solomono.

Kama tulivyoona, Mungu aliwapa Waisraeli **viongozi** kama Musa, Yosua, na Samweli kuwaongoza na kuwahukumu. Lakini Mungu yule ambaye aliwafungua toka utumwa katika Misri, alikuwa **Mfalme wao wa hakika**. Mungu, ambaye aliwaagiza kufanya hema ili aweze kukaa katikati yao, alitaka kuwa Mtawala wao. Alitaka wamtii na kumfuata yeye tu. Lakini, zaidi ya Waisraeli hawakufurahi kuwa na Bwana tu kama Mfalme wao. **Walitaka kuwa sawasawa na mataifa yote** ya dunia na kuwa na mwana wa Adamu kutawala juu yao kama mfalme wao!

Ndani ya sura 8 ya kitabu cha kwanza cha Samweli, Maandiko yanasema:

> (1 Samweli 8) 4 *Kisha wazee wote wa Israeli wakajikusanya pamoja, wakafikia Samweli kwa Rama;* 5 *wakamwambia: Tazama, wewe ni mzee, na wana wako hawakwendi katika njia zako, **utufanyie mfalme atuhukumu kama mataifa yote.*** 6 *Lakini neno hili halikupendeza Samweli wakati waliposema: Utupe mfalme, atuhukumu. Samweli akaomba Bwana.*

> *7 Bwana akamwambia Samweli: Sikiliza sauti ya watu katika yote ambayo wanakuambia: kwa maana hawakukukataa wewe, lakini wamenikataa mimi nisiwe mfalme juu yao. 8 Kwa namna ya matendo yote ambayo waliyatenda tangu siku nilipowaleta toka Misri hata siku hii ya leo, wameniacha, wakatumikia miungu mingine, ndivyo wanavyokutendea wewe vilevile. 9 Basi sasa usikilize sauti yao; lakini uwashuhudie sana na kuwaonyesha namna ya mfalme ambaye atawatawala.*

Hivi Mungu alisema na Samweli kuwapa watu neno walilotaka na kuwawekea mfalme. Mungu hakutaka Waisraeli kuwa na mfalme mwingine pamoja naye, lakini kwa sababu walikuwa wamekataa utawala wa Mungu, hivi hatatawala juu yao kwa nguvu. Ndani ya sura ya nyuma, tunaona ya kwamba Samweli aliwekea Waisraeli mtu mmoja jina lake Saulo kuwa mfalme wao. Maandiko yanasema: *"Pale Samweli akatwaa kichupa cha mafuta, akayamimia juu ya kichwa chake* (cha Saulo)." (1 Samweli 10:1) Hili ndilo neno Waisraeli walilofanya kuweka mtu kwa kazi fulani. Walimwanga mafuta juu ya kichwa cha nabii, kuhani au mfalme kuwaweka mbali kwa kazi fulani. Nyuma ya kumwanga mafuta juu ya kichwa cha Saulo, Samweli alisema na watu wote, *"Mumtazame yeye ambaye Bwana alimchagua, ya kuwa hakuna mtu kama yeye katikati ya watu wote. Watu wote wakapiga kelele, wakasema: Mungu aokoe mfalme!"* (1 Samweli 10:24)

Kwa wakati Waisraeli walifurahi sana na mfalme wao, ndiye Saulo. Alikuwa mtu wa nguvu, mhodari, kijana na mwenye kuonekana vizuri, mrefu kupita Waisraeli wote wengine. Kwa kuonekana kwa macho ya watu, ingalipasa Saulo kuwa mfalme mzuri sana. Lakini Mungu haangalii maneno namna watu wanavyoyaangalia. Mtu anaangalia **kuonekana kwa inje**, lakini Bwana anatazama **moyo**. Mfalme alianza vizuri, lakini nyuma ya wakati aligeuka mwenye wivu, mtu asiyetafuta kusaidiwa na mtu. Saulo aliheshimu Mungu na midomo yake, lakini roho yake ilikuwa mbali naye. Hakuheshimu wala kutii Neno la Mungu. Alifanya mapenzi yake mwenyewe, si mapenzi ya Mungu.

Miaka michache nyuma ya mwanzo wa utawala wa Saulo,

> (1 Samweli 15) *Neno la Bwana lilikuja kwa Samweli likisema: Ninajuta kwa kusimamisha Saulo kuwa mfalme; maana* ***amerudi nyuma asinifuate wala hakufanya amri zangu.*** *Samweli akaka-*

> *sirika; akalilia Bwana usiku mzima. Samweli akaamka mapema kukutana na Saulo . . .* (1 Samweli 15:10-12)
>
> Hatuna saa kusoma habari nzima ya namna Samweli alivyohamakia Saulo, lakini hata hivi sharti tusome shairi hili moja: *"Kuasi ni kama kosa la ufumu, na kichwa nguvu ni kama kuabudu sanamu na terafi.* ***Kwa sababu umekataa neno la Bwana, yeye vilevile amekukataa wewe, usiwe mfalme."*** (1 Samweli 15:23)

Hivi, Samweli alimwambia Saulo ya kwamba mtu mwingine atapewa ufalme. Nyuma, ndani ya sura 16, maandiko yanasema,

> (1 Samweli 16) *1 Bwana akamwambia Samweli: Hata wakati gani utaomboleza kwa sababu ya Saulo, ikiwa nimemkataa asiwe mfalme juu ya Israeli? Jaza pembe yako mafuta, uende, nami nitakutuma kwa* ***Yese*, *mtu wa Betelehemu***; *maana nimejipatia mfalme* ***katikati ya wana wake****. 2 Samweli akasema: Nitakwenda namna gani? Saulo akisikia ataniua. Bwana akasema: Ujitwalie ndama pamoja nawe na sema: Nimekuja kutolea Bwana zabihu. 3 Na ita Yese kwa zabihu, na nitakuonyesha nini utakachofanya; na utanipakalia yeye ambaye nitamtaja kwako. 4 Samweli akafanya maneno Bwana aliyosema, akakuja kwa Betelehemu. Wazee wa mji wakakuja kukutana naye wakitetemeka, wakasema: Umekuja na salama? 5 Akasema: Na salama. Nimekuja kutolea Bwana zabihu. Mujitakase, na kujeni pamoja nami kwa zabihu. Akatakasa Yese na wana wake, akawaita kwa zabihu. 6 Na ilikuwa wakati walipofika, akatazama Eliabu, akasema: Hakika mpakaliwa wa Bwana ni mbele yake. 7 Lakini Bwana akamwambia Samweli: Usiangalie uso wake, wala urefu wa mwili wake; kwa maana nimemkataa.* ***Kwa maana Bwana haoni kama mtu anavyoona, maana mtu anaangalia kuonekana kwa inje, lakini Bwana anatazama moyo.***
>
> *8 Halafu Yese akaita Abinadabu, akampitisha mbele ya Samweli. Akasema: Wala Bwana hakuchagua huyu. 9 Halafu Yese akapitisha Shama. Akasema: Wala Bwana hakuchagua huyu. 10 Yese akapitisha saba wa wana wake mbele ya Samweli. Samweli akamwambia Yese: Bwana hakuchagua hawa. 11 Samweli akamwambia Yese: Wana wako wote ni hapa? Akasema: Mmoja anabakia,* ***mdogo*** *wa wote, na tazama, anachunga kondoo. Samweli akamwambia Yese: Tuma kumwita: kwa sababu hatutaketi hata atakapokuja hapa. 12 Akatuma, akamleta ndani. Naye alikuwa mwekundu, mwenye macho mazuri,*

*na ya kupendeza kwa kumtazama. Bwana akasema: Simama umpakae; kwa maana huyu ni yeye. 13 Halafu Samweli akachukua pembe ya mafuta, akampakaa kati ya ndugu zake; na roho ya Bwana alikuja na uwezo juu ya* ***Daudi*** *tangu siku ile.*

Hivi tunaona ya kwamba Mungu alichagua **Daudi** kuwa mfalme wa Israeli nyuma ya Saulo. Lakini tufahamu ya kwamba Daudi hakugeuka mfalme wa Israeli siku ile ile. Daudi alikuwa kijana tu na saa Mungu aliyotaka kwa Daudi kuanza kutawala juu ya taifa la Israeli ilikuwa haijafika bado. Ndiyo, miaka kumi itapita mbele ya kuketi kwa Daudi juu ya kiti cha ufalme cha Israeli.

Hivi Daudi alirudi kwa mashamba yaliyozunguka Betelehemu na kazi ya kulinda makundi ya baba yake. Daudi alikuwa mchungaji mwema na mwaminifu. Hakuogopa kitu kwa sababu **alitegemea Bwana**. Kwa mfano, siku moja, wakati Daudi alipokuwa akichunga kondoo za baba yake, simba alifika, akaiba mmoja wao. Daudi alifuata simba, akampiga na kuponyesha kondoo toka kinywa chake. Wakati simba alipogeuka kuua Daudi, Daudi alimkamata kwa nyole za ndevu zake, akampiga na kumwua. (1 Samweli 17:35)

Daudi hakuwa mchungaji tu; alijua kupiga kinubi na kuimba vilevile. Roho ya Mungu alimwongoza kutunga nyimbo nyingi na kuziandika ndani ya kitabu cha **Zaburi**. Kweli Daudi alipenda Bwana Mungu na Neno lake sana!

Tunataka kumaliza somo la leo na sehemu nyingine za kitabu cha Zaburi cha Daudi. Jaribu kuwaza juu ya Daudi ndani ya mashamba ya majani mazuri, katikati ya kondoo, akisifu Mungu na nyimbo na mashukuru zilizotungwa na Roho ya Mungu. Sikiliza:

***"Ee Bwana, Bwana wetu, jina lako ni lenye utukufu duniani mwote!*** *. . . Wakati ninapofikiri mbingu zako, kazi ya vidole vyako, mwezi na nyota ambazo uliziamuru, mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na mwana wa watu, hata umwangalie? Kwa kuwa umemfanya chini kidogo kupita malaika, na umemvika taji ya utukufu na heshima . . . Ee Bwana, Bwana wetu, jina lako ni lenye utukufu duniani mwote!"* (Zaburi 8:1,3-5,9)

*"**Neno lako ni taa** kwa miguu yangu na nuru kwa njia yangu. Nimeficha neno lako moyoni mwangu, nisikukosee."* (Zaburi 119:105,11) *"Sheria ya Bwana ni kamilifu, inaburudisha nafsi; ushuhuda wa Bwana ni wa kweli, unatia mjinga akili. Maagizo ya*

*Bwana ni ya haki, yanafurahisha moyo; amri ya Bwana ni safi, inatia macho nuru . . . Ni za kutamanika kupita zahabu, ndiyo, kupita wingi wa zahabu safi. Ni tamu kupita asali na sega la asali. Tena mtumishi wako anaonywa kwa njia zao; katika kuzishika kuna zawabu nyingi."* (Zaburi 19:7,8,10,11)

***"Bwana ni mchungaji wangu****; sitapungukiwa na kitu. Ananilalisha katika malisho ya majani mabichi; ananiongoza kando ya maji matulivu. Anarudisha nafsi yangu; ananiongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Ndiyo, hata nikipita kati ya bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe ni pamoja nami; gongo lako na fimbo yako zinanifariji. Unanitengenezea meza mbele ya adui zangu; umenipakalia mafuta kichwani; kikombe changu kinafurika. Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu; na nitakaa nyumbani mwa Bwana, milele."* (Zaburi 23) Amina!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, tunakusudi kuendelea na habari za Daudi na kuona ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye wakati alipopigana na Goliata, mtu mrefu sana . . .

Mungu akubariki wakati unapofikili juu ya maneno Mungu aliyosema na Samweli:

***"Bwana haoni kama mtu anavyoona, maana mtu anaangalia kuonekana kwa inje, lakini Bwana anatazama moyo."***

(1 Samweli 16:7)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 47

# Daudi na Goliata

1 Samweli 17; Zaburi 27

Kwa somo la mbele, tulianza kusoma juu ya nabii Daudi. Sikia maneno Mungu aliyosema juu yake: *"Nimeona **Daudi,** mwana wa Yese, mtu anayependeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote."* (Matendo 13:22) Tuliona namna gani Mungu aliweka Daudi kuwa mfalme wa pili wa Israeli, kwa sababu mfalme wa kwanza, Saulo, hakutii Neno la Mungu. Lakini Daudi hakugeuka mfalme wa Israeli mara moja siku Mungu alipomweka. Alikuwa kijana kwanza, na saa ya Mungu kwa yeye kupokea ufalme ilikuwa haijafika bado. Nyuma ya kupakaliwa kuwa mfalme, Daudi alirudi kwa mashamba inje ya mji wa Betelehemu kuchunga makundi ya baba yake.

Leo tutasoma habari za ajabu zinazoonyesha ya kwamba Mungu alikuwa pamoja na Daudi, kwa sababu Daudi alitembea pamoja na Mungu. Somo letu linaitwa **"Daudi na Goliata**." Tuendelee sasa ndani ya kitabu cha kwanza cha Samweli, sura 17. Maandiko yanasema:

> (1 Samweli 17) *1 Basi **Wafilistini** [adui wakali zaidi za Israeli] wakakusanya majeshi yao kwa vita . . . 2 **Saulo na watu wa Israeli** wakakusanyika, wakapiga kambi katika bonde la Ela, wakatayarisha vita juu ya Wafilistini. 3 Wafilistini wakasimama juu ya mlima kwa upande mmoja; Israeli wakasimama juu ya mlima kwa upande mwingine.*
>
> *4 Mpigaji akatoka kwa kambi ya Wafilistini, jina lake **Goliata,** wa Gati, urefu wake mikono sita na shibiri moja. 5 Na alikuwa na kofia ya shaba juu ya kichwa chake, akavalishwa na kanzu ya madini; uzito wa kanzu ulikuwa shekeli elfu tanu za shaba. 6 Akavaa shaba kwa miguu yake na mkuki mfupi wa shaba kati ya mabega yake. 7 Na mti wa mkuki wake ulikuwa kama mti wa mfuma; na uzito wa kichwa cha*

*mkuki wake ulikuwa shekeli mia sita za chuma; mwenye kubeba ngabo yake akakwenda mbele yake.*

*8 Goliata akasimama, akalia kwa majeshi ya Israeli na kuwaambia: Kwa nini mumetoka kujitayarisha kwa vita? Mimi si Mfilistini nanyi watumishi wa Saulo? Mujichagulie mtu, ashuke kwangu. 9 Kama akiweza kupigana nami na kuniua, sisi tutakuwa watumishi wenu; lakini mimi nikimshinda na kumwua, ninyi mutakuwa watumishi wetu na kututumikia sisi. 10 Yule Mfilistini akasema: Ninatukana leo majeshi ya Israeli; munipe mtu tupigane naye. 11 Na wakati Saulo na Israeli wote waliposikia maneno yale ya Mfilistini,* ***wakafazaika, wakaogopa sana.***

Saa Goliata alipozihaki Waisraeli, **Daudi** alikuwa akichunga makundi ya baba yake na salama, mbali na pahali pa vita, akiwaza juu ya Neno la Mungu, akipiga kinubi na kuimbia Bwana. Lakini Daudi alikuwa na ndugu wakubwa watatu waliokuwa askari ndani ya jeshi la Israeli. Siku moja baba ya Daudi alimfikia na kusema, "**Kwenda kuangalia ndugu zako** pahali pa vita na kuniletea habari zao." Hivi Daudi aliomba mchungaji mwingine kuangalia kondoo zake, akaondoka asubui mapema kwenda pahali pa vita.

Wakati Daudi alipokuwa akisalimu wakubwa wake na kusemezana nao, Goliata, mpigaji mwenye uwezo wa Wafilistini alitoka katikati ya askari za Wafilistini, alisimama mbele yao na kuwatia hofu, namna alivyofanya kwa siku makumi ine zilizopita. Wakati askari Waisraeli walipomwona, walikimbia na woga. Halafu mtu mmoja alisema na Daudi, "Unaona mtu yule? Anakaa kutaka vita nasi. Mtu ye yote ambaye anamwua, mfalme Saulo atampa mali nyingi na kumpa vilevile binti yake kuwa mke wake na jamaa ya baba yake hawatahitaji kulipa kodi tena."

Halafu Daudi alisema, "Yule Mfilistini asiyetahiriwa, yeye ni nani hata atakaa kutaka vita na majeshi ya Mungu aliye hai?" Wakati aliposema hivi, mkubwa wa Daudi alimkasirikia sana, akasema, "Umeshuka kwa sababu gani? Na kondoo wale wachache uliacha na nani jangwani? Ninajua majivuno yako na uovu wa moyo wako; maana umeshuka ili upate kutazama vita!" Lakini mmoja wa askari za Israeli walisikia masemo ya uhodari ya Daudi juu ya mpigaji Mfilistini, akakwenda na kuyapasha kwa mfalme Saulo. Halafu Saulo alituma kuita Daudi na kuulizana naye.

Hivi, Maandiko yanasema:

(1 Samweli 17) *32* ***Daudi akamwambia Saulo: Moyo wa mtu ye yote usizimie*** *kwa ajili ya huyu; mtumishi wako atakwenda kupigana na Mfilistini huyu. 33 Saulo akamwambia Daudi: Huwezi kupanda juu ya Mfilistini huyu kupigana naye, kwa maana wewe ni kijana tu, naye ni mtu wa vita tangu ujana wake. 34 Daudi akamwambia Saulo: Mtumishi wako amechunga kondoo za baba yake; na wakati simba alipokuja, au dubu, na kukamata mwana-kondoo toka kundi, 35 nilitoka nyuma yake na kumpiga na kumponyesha toka kinywani mwake, na wakati aliposimama juu yangu, nikampata kwa ndevu yake, nikampiga, na kumwua. 36 Mtumishi wako ameua simba na dubu vilevile; na Mfilistini huyu asiyetahiriwa atakuwa sawasawa na mmoja wao, kwa sababu ametukana majeshi ya Mungu wa uzima. 37 Daudi akasema: Bwana ambaye aliniponyesha na mkono wa simba, na mkononi mwa dubu, ataniponyesha na mkono wa Mfilistini huyu. Saulo akawambia Daudi: Kwenda, na Bwana atakuwa pamoja nawe. 38 Saulo akavika Daudi na mavazi yake ya vita, akatia kofia ya shaba juu ya kichwa chake, akamvika kanzu la madini. 39 Daudi akafunga upanga wake juu ya mavazi yake, akapima kwenda, maana alikuwa hajavijaribu. Na Daudi alimwambia Saulo: Siwezi kwenda na vitu hivi, kwa sababu sikuvijaribu.*

*40 Daudi akaviondosha, akachukua gongo lake mkononi mwake, akajichagulia* ***mawe laini matano*** *toka kijito, akayaweka ndani ya mfuko wa mchungaji kondoo alio nao, hata ndani ya mkoba, na* ***kombeo*** *lake lilikuwa mkononi mwake; akakaribia Mfilistini. 41 Mfilistini akajongea, akakaribia Daudi, na mtu aliyebeba ngabo yake akakwenda mbele yake. 42 Na wakati Mfilistini alipotazama na aliona Daudi, akamzarau; kwani alikuwa kijana tu, na mwekundu, na mwenye macho mazuri. 43 Mfilistini akamwambia Daudi: Mimi ni imbwa hata unakuja kwangu na magongo? Mfilistini akatukana Daudi kwa miungu yake. 44 Mfilistini akamwambia Daudi: Kuja kwangu, na nitatoa mwili wako kwa ndege za anga, na kwa nyama za poli.*

*45 Halafu Daudi akamwambia Mfilistini: Unakuja kwangu na upanga na mkuki mfupi, lakini* ***ninakuja kwako kwa jina la Bwana wa majeshi,*** *Mungu wa majeshi ya Israeli ambaye ulimzarau. 46 Siku hii Bwana atakutoa mkononi mwangu, nami nitakupiga na kukuondolea kichwa chako; na nitatoa maiti za majeshi ya Wafilistini kwa ndege za anga siku hii na kwa nyama za poli za inchi; ulimwengu wote wajue ya kwamba Mungu ni katikati ya Israeli. 47 Kusanyiko hili lote wajue ya kama Bwana haponyeshi kwa upanga na mkuki, kwa maana* ***vita ni ya Bwana****, naye atawatoa ninyi mkononi mwetu.*

> *48 Na ilikuwa wakati Mfilistini aliposimama na alikuja na kukaribia kukutana na Daudi, Daudi akafanya mbio, akapiga mbio kwa jeshi kukutana na Mfilistini. 49 Daudi akatia mkono wake mfukoni mwake, akatwaa jiwe, akalitupa kwa kombeo na kupiga Mfilistini kwa paji la uso, jiwe likaingia ndani ya paji la uso wake, akaanguka chini kifudifudi. 50 Hivi* ***Daudi akashinda*** *Mfilistini yule kwa kombeo na jiwe, na kupiga Mfilistini, na kumwua, lakini upanga haukuwa mkononi mwa Daudi. 51 Halafu Daudi akapiga mbio, akasimama juu ya Mfilistini, akachukua upanga wake, na kuuondosha alani mwake, akamwua na kumwondolea kichwa nao. Na wakati Wafilistini walipoona ya kama mpigaji wao amekufa, wakakimbia. 52 Watu wa Israeli na Wayuda wakasimama na kupiga kelele, wakafuata nyuma ya Wafilistini hata unapofika kwa bonde na mpaka malango ya Ekuroni.*

Hivi tunaona leo namna Daudi, kijana alivyoponyesha kabila lake toka adui zao na **kombeo, jiwe**, na **imani ya nguvu ndani ya Mungu aliye hai**. Kweli habari hizi za Daudi na Goliata ni habari za ajabu na zinatufundisha maneno mengi.

Tuliona ya kwamba Saulo na Waisraeli waliogopa Goliata sana. Wao wote waliogopa kupigana naye, lakini Daudi hakuogopa yule mtu mrefu sana; akampiga hata alianguka, akamwua. Kwa nini Saulo na askari zake waliogopa lakini Daudi hakuogopa? Tofauti katikati yao ilikuwa nini? Tunaweza kujumlisha tofauti yenyewe hivi: Daudi hakuogopa mtu mrefu sana, kwa sababu **aliamini Bwana Mungu**. Saulo na askari zake hawakutumainia Mungu. Kwa sababu hii waliogopa yule mtu mrefu sana.

Saulo na askari zake waliona **Goliata tu**. Daudi aliona **Mungu Mwenyezi**! Saulo na askari Waisraeli walikuwa na dini lakini hawakuwa na upatano wa kweli na Mungu. Mtu anaweza kuwa mtu wa dini bila kuwa mtu wa Mungu kweli. Saulo na askari walijua vizuri ya kwamba Mungu yuko, ya kwamba Mungu ni mmoja, na ya kwamba yeye ni mkubwa na mwenye uwezo. Lakini kujua tu maneno haya hakukuweza kuwaponyesha ndani ya vita na Goliata. Lakini Daudi alijuana na Mungu kabisa kabisa na alitembea pamoja naye. Daudi aliamini ahadi za Mungu. Kwa sababu hii Daudi hakuogopa Goliata.

Wewe unafanana na nani zaidi? Na Daudi? Au na Saulo na askari zake?

Unajuana na Mungu wewe mwenyewe? Au umesikia tu habari chache juu yake?

Unajua Neno la Mungu sana hata linajaza roho yako na furaha? Au unajaribu kutimiza tu utaratibu wa dini yako?

Una upatano wa nguvu na wa furaha na Mungu aliye hai? Au una dini ya kukauka tu?

Soma maneno nabii wa Mungu, Daudi aliyoandika ndani ya Zaburi, juu ya upatano wake na Mungu. Alisema:

> *"**Bwana ni mchungaji wangu**; sitapungukiwa na kitu... Ndiyo, hata nikipita kati ya bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe ni pamoja nami . . . Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu; na nitakaa nyumbani mwa Bwana milele."* (Zaburi 23:1,4,6)

Basi wewe? Una upatano wa karibu na Bwana Mungu? Unamjua kama Mchungaji wako? Unajua kabisa ya kwamba utakaa nyumbani mwake mbinguni kwa milele? Daudi alijua maneno haya, kwa sababu alijua ahadi za ajabu na za damani za Bwana Mungu. Na hakuzijua **kwa nia yake** tu; aliziamini **moyoni mwake**.

Daudi alikuwa na imani ya kweli. Msingi wa imani yake haukuwa masemo ya watu yasiyo ya kutumainiwa. Imani yake ilisimama juu ya Neno aminifu la Bwana Mungu asiyeacha watu wake kamwe! Sikia maneno Daudi aliyoandika ndani ya Zaburi:

> ***"Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu; nitaogopa nani?*** *Bwana ni nguvu ya uzima wangu, nitakuwa na woga kwa sababu ya nani? . . . Kama jeshi likipanga juu yangu, moyo wangu hautaogopa. Kama vita ikitokea juu yangu, hata hivi nitakaa na imani. Kitu kimoja niliomba na Bwana, ndicho nitakachotafuta, nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, nitazame uzuri wa Bwana, nikauliza kwa hekalu lake. . . . Usikie, Bwana; na sauti yangu ninalia, unirehemu ukanijibu. Wakati uliposema: Tafuta uso wangu, moyo wangu ukakuambia: **Uso wako, Ee Bwana, nitautafuta.**" (Zaburi 27:1,3,4,7,8)*
>
> *"**Ninakupenda, Ee Bwana, nguvu yangu**. Bwana ni Mwamba wangu na boma langu, na mwokozi wangu; Mungu wangu, mwamba wangu, ambaye ninamkimbilia. Yeye ni ngabo yangu . . . Kwa sababu yako ninakimbia katika jeshi; na kwa sababu ya Mungu wangu ninaruka ukuta. Mungu, **njia yake ni kamilifu, Neno la Mungu limejaribiwa; yeye ni ngabo kwao ambao wanamwekea tumaini lao**." (Zaburi 18:1,2,29,30)*

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kujifunza pamoja nasi. Ndani ya somo letu la nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea na habari za nabii Daudi na kusoma juu ya mwanzo wa utawala wake kama mfalme wa Israeli.

Mungu akubariki. Tunakulaga na masemo haya toka Daudi ndani ya kitabu cha Zaburi:

> ***"Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni mwema; Heri mtu ambaye anamwekea tumaini lake."*** (Zaburi 34:8)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 48

# Mfalme Daudi na Ahadi ya Mungu

### 1 Samweli 18 – 2 Samweli 7

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Leo tunaendelea na habari za **nabii Daudi.** Masomo mawili mbele tuliona ya kwamba Mungu alichagua Daudi, kijana, kuwa mfalme wa pili wa Israeli, hata kama hakuanza kutawala siku ile ile Mungu alipomweka kuwa mfalme. Mungu alikataa Saulo, mfalme wa kwanza, kwa sababu hakuweka roho juu ya kufanya mapenzi ya Mungu. Lakini Mungu alishuhudia Daudi akisema, *"Nimeona Daudi, mwana wa Yese, mtu anayependeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote."* (Matendo 13:22) Tumesoma mbele juu ya Daudi akiua mtu mrefu sana, ndiye Goliata, akimshinda na kombeo na jiwe na **imani ya nguvu ndani ya Mungu aliye hai.** Sasa tuendelee na habari za Daudi na kuona namna Daudi alivyokomboa Saulo kama mfalme wa Israeli.

Tukiendelea ndani ya 1 Samweli sura 18 tunasoma:

> *6 Na ilikuwa wakati [watu] walipokuja, wakati Daudi aliporudi toka uuaji wa Mfilistini, wanawake walitoka katika miji yote ya Israeli, wakiimba na kucheza, kukutana na mfalme Saulo, na matoazi, kwa furaha, na vinanda. 7 Wanawake wakaimbana mmoja kwa mwenzake, katika michezo yao, wakasema: Saulo ameua* ***elfu zake****, na Daudi* ***elfu zake kumi****. 8 Saulo akakasirika sana wala maneno haya hayakumpendeza; akasema: Wameandikia Daudi elfu kumi, na mimi wameniandikia elfu tu; naye anaweza kupata nini zaidi, isipokuwa ni ufalme? 9 Na tangu siku ile Saulo* ***alimwonea Daudi wivu****."*

Hivi Maandiko yanatupasha ya kwamba Waisraeli walipenda Daudi sana. Lakini kwa kipimo mapendo yao kwa Daudi yaliongezeka, kwa kipimo kile Saulo alizidi kumchukia. **Roho ya Saulo ilijaa wivu** hata alifikili juu ya neno moja tu, ndilo ya kwamba ni sharti kwake kuua Daudi. Hivi Daudi alikimbia, akafichama ja-

ngwani, pamoja na askari mia ine za Israeli waliofungana naye. Saulo na askari zake walitafuta Daudi na watu wake jangwani. Saulo alifanya kila kitu alichoweza kukamata Daudi na kumwua, lakini alishindwa, kwa sababu Bwana alikuwa pamoja na Daudi. Hata hivi Saulo alitaabisha Daudi sana. Kwa miaka mirefu minane Daudi na watu wake walilazimishwa kukimbia kasirani ya Mfalme Saulo.

Lakini hata kama Daudi aliweza kuona wivu na kasirani ya Saulo, neno hili halikumfanyiza kumchukia. Kwa nini Daudi hakuua Saulo, mtu ambaye alitaka kumwua? Daudi hakuweza kuchukia Saulo, kwa sababu **Daudi alitembea pamoja na Mungu anayefanyiza jua yake kuwaka juu ya wenye haki na wazalimu**. Kama Maandiko yanasema:

> *"Kila mtu anayependa amezaliwa na Mungu, naye anajua Mungu. Yeye asiyependa, hakujua Mungu, kwa maana* ***Mungu ni mapendo****. Sisi tunampenda kwa sababu yeye alitupenda sisi kwanza. Kama mtu akisema: Ninapenda Mungu, naye anachukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyependa ndugu yake ambaye alimwona, hawezi kupenda Mungu ambaye hamwoni."* (1 Yoane 4:7,8,19,20)

Hatuna saa kusoma habari zote zilizotokea katikati ya Saulo na Daudi, lakini tunataka kuwaza juu ya neno moja na kuona **unyenyekevu na mapendo ya Daudi.** Tukisoma ndani ya 1 Samweli na sura 24, kuanza na shairi 1, Maandiko yanasema:

> (1 Samweli 24) *1 Na ilikuwa wakati Saulo aliporudi toka kufuata Wafilistini, aliambiwa kusema: Tazama, Daudi ni jangwani mwa Engedi. 2* ***Saulo*** *akatwaa watu wachaguliwa elfu tatu toka Israeli wote,* ***akakwenda kutafuta Daudi*** *na watu wake juu ya miamba ya mbuzi za mwitu. 3 Na alikuja kwa mazizi njiani palipokuwa pango; Saulo akaingia kufunika miguu yake. Basi Daudi na watu wake walikuwa wakikaa kwa pande za ndani za pango.*
>
> *4 Watu wa Daudi wakamwambia: Tazama, hii ni siku ile ambayo alikuambia Bwana: Tazama, nitatoa adui yako mkononi mwako na utamtendea sawasawa itakavyokupendeza. Daudi akasimama,* ***akakata upindo wa vazi la Saulo kwa maficho****. 5 Na ilikuwa nyuma, moyo wa Daudi ulimpiga kwa sababu amekata upindo wa vazi la Saulo. 6 Akawaambia watu wake: Bwana akataze nisifanye kitu hiki juu ya bwana wangu mpakaliwa wa Bwana, kunyosha mkono wangu juu yake, kwa maana yeye ni mpakaliwa wa Bwana. 7 Hivi Daudi akazuiza watu wake na maneno haya, wala hakuwaacha kusimama juu ya Saulo. Saulo akaondoka pangoni, akakwenda zake.*

*8 Daudi vilevile akasimama nyuma, akatoka pangoni, akalia nyuma ya Saulo akisema: Bwana wangu mfalme. Na wakati Saulo alipoangalia nyuma yake, Daudi aliinama kwa uso wake kwa udongo, akainamisha kichwa. 9 Daudi akamwambia Saulo: Kwa nini unasikiliza maneno ya watu wanaosema: Tazama Daudi anatafuta kukuumiza? 10 Tazama, siku hii macho yako yameona namna Bwana alivyokutia mkononi mwangu pangoni leo, na wengine waliniambia nikuue, lakini nilikuachilia; nikasema: Sitanyosha mkono wangu juu ya bwana wangu; kwa maana yeye ni mpakaliwa wa Bwana. 11 Na tena, baba wangu, tazama, ndiyo tazama, upindo wa vazi lako mkononi mwangu; kwa maana ikiwa nimekata upindo wa vazi lako wala sikukuua, jua na ona ya kama ubaya wala kosa si mkononi mwangu wala sikukosa juu yako, hata kama ukiwinda nafsi yangu kuikamata. 12 Bwana ahukumu katikati yangu nawe; Bwana anilipie kisasi kwako; lakini mkono wangu hautakuwa juu yako. 13 Kama mezali ya wazee inavyosema: Toka mwovu uovu unatoka; lakini mkono wangu hautakuwa juu yako.*

*16 Na ilikuwa wakati Daudi alipomaliza kumwambia Saulo maneno haya, Saulo akasema: Hii ni sauti yako, mwana wangu Daudi? Saulo akapaza sauti yake, akalia. 17 Akamwambia Daudi: Wewe ni haki kuliko mimi, maana umenitendea mema, lakini mimi nimekutendea mabaya. 18 Na umeonyesha leo namna ulivyonitendea mema; kwa maana wakati Bwana aliponitoa mkononi mwako, hukuniua. 19 Maana mtu akipata adui yake, atamwacha kwenda zake kweli? Kwa hivi Bwana akulipie mema kwa maneno haya ambayo ulinitendea leo. 20 Na sasa, tazama, ninajua ya kama hakika utakuwa mfalme, na ya kama ufalme wa Israeli utasimamishwa katika mkono wako."*

Nyuma ya maneno haya Saulo alirudi kwake, lakini nyuma ya muda mfupi tu wivu ulifunga roho yake tena na kumsukuma kurudia jangwa na kuendelea kutafuta Daudi. Saulo alifanya hivi kwa miaka minane, kwa sababu ya **wivu**! Hata hivi, kila mara Mungu aliponyesha Daudi toka mikono ya Saulo. Mwishoni, Saulo alivuna ubaya aliopanda. Sikia maneno yaliyoandikwa ndani ya sura 31:

*1 Basi Wafilistini wakapigana na Israeli; watu wa Israeli walikimbia mbele ya Wafilistini; wakaanguka wameuawa katika mlima Gilboa. 2 Wafilistini wakafuata na nguvu nyuma ya Saulo na nyuma ya wana wake; Wafilistini wakaua Yonatana, na Abinadabu, na Malki-Sua, wana wa Saulo. 3 Vita ilikuwa nzito juu ya Saulo, wenye upinde*

> *wakampata; akataabishwa sana kwa sababu ya wenye upinde. 4 Halafu Saulo akamwambia mwenye kubeba silaha zake: Ondosha upanga wako unichome nao; wasiotahiriwa hawa wasije na kunichoma, na kunitendea mabaya. Lakini mwenye kubeba silaha zake akakataa, kwa sababu aliogopa sana. Basi* ***Saulo akatwaa upanga wake, akauangukia****.*

Siku ile Saulo na wana wake watatu walikufa. Hivi, wazao wa Saulo waliharibiwa kabisa, kama Mungu alivyosema mbele. Ndani ya sura zinazofuata, tunasoma ya kwamba **Mungu aliweka ufalme wa Israeli kwa mkono wa Daudi**. Daudi alikuwa mfalme wa haki aliyependa haki na kuchukia uzalimu. Daudi alipenda Bwana na moyo wake wote. Neno la Mungu na utukufu wa Mungu zilikuwa kwa pahali pa kwanza ndani ya mafikili ya Daudi. Hivi wakati Daudi alipoanza kutawala juu ya Israeli, neno la kwanza alilotaka kufanya lilikuwa kuleta hema ya kusanyiko na sanduku ya agano kwa Yerusalema. Yerusalema ulikuwa mji mkubwa wa Israeli. Kwa sababu hii Daudi alitaka kusimamisha hema ya kuabudu na mazabahu kwa sadaka pale.

Wakati Daudi alipokwisha kuhamisha hema ya kuabudu kwa Yerusalema, tunasoma ndani ya Maandiko ya kwamba alifanya shauri kujenga hekalu zuri kuheshimu jina la Bwana. Daudi alitaka kujenga hekalu ili sanduku ya agano iwekwe ndani yake na liwe pahali wenye zambi watakapoweza kutolea Mungu zabihu kufunika zambi zao. Lakini Bwana alijulisha Daudi ya kwamba yeye hatajengea Mungu nyumba, lakini Mungu atamjengea yeye nyumba, maana, **wazao watakaoendelea milele!** Sikiliza **agano Mungu alilofanya na Daudi**. Alisema naye ndani ya 2 Samweli 7, kuanza na shairi 12:

> *12 Wakati siku zako zitakapotimia, na utalala pamoja na baba zako, nitasimamisha mzao wako nyuma yako atakayetoka viunoni mwako, nami nitasimamisha ufalme wake. 13 Atajenga nyumba kwa jina langu, na nitasimamisha kiti cha ufalme chake milele. 14 Nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwana wangu. ... 16* ***Na nyumba yako na ufalme wako zitasimama imara mbele yangu milele; kiti cha ufalme chako kitasimamishwa milele."***

Unafahamu agano Mungu alilosimamisha na Mfalme Daudi siku ile? Ilikuwa ahadi kubwa sana inayoshinda sisi watu kufahamu! Mungu aliahidi Daudi, *"Na nyumba yako na ufalme wako zitasimama imara mbele yangu milelele;* ***kiti cha ufalme chako kitasimamishwa milele."***

Kweli? Namna gani ufalme wa Daudi utaendelea **milele**? Namna gani Daudi, aliyekuwa mtu tu, aliweza kuwa na utawala utakaoendelea milele? Ona jibu kwa ulizo hili: Mungu aliahidi Daudi ya kwamba **mmoja wa wazao wake** atasimamisha utawala wa milele. Mtu atazaliwa ndani ya kizazi cha kifalme chake atakayepokea amri kutawala mbinguni na duniani milele. Ataitwa Mfalme wa wafalme, Bwana wa wabwana, Mkubwa wa salama. Mia za miaka nyuma ya wakati wa Daudi, na karibu miaka mia saba mbele ya kuzaliwa kwa Mfalme huyu wa wafalme, nabii Isaya aliandika maneno haya:

> *"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na* ***utawala utakuwa juu ya bega lake; na jina lake litaitwa Mwenye ajabu, Mwenye shauri, Mungu Mwenye uwezo, Baba ya milele, Mkubwa wa salama. Kuongezwa kwa utawala wake na salama hakutakuwa na mwisho****, juu ya kiti cha ufalme cha Daudi, na juu ya ufalme wake, kuusimamisha, na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi utafanya maneno haya."* (Isaya 9:6,7)

Unajua nani, katikati ya wazao wa Daudi, alipewa amri kusimamisha ufalme wa milele? Unajua nani atakayehukumu wana wa Adamu siku ya hukumu na kutawala kwa milele? Ndiyo, ni **Mkombozi, Mfalme toka mbingu**, aliyezaliwa na bikira, bikira aliyekuwa mmoja wa wazao wa Daudi. Maandiko yanasema juu ya Mfalme huyu: ***"Mungu alimtukuza sana, na kumpa jina lililo juu ya kila jina!"*** (Wafilipi 2:9)

Wakati Daudi alipofahamu shauri la Mungu kutuma Mkombozi kwa njia ya kizazi chake, Daudi alipiga magoti na kuabudu Bwana akisema,

> (2 Samweli 7) *18* ***"Mimi ni nani, Ee Bwana Mungu, na nyumba yangu ni nini hata umenileta hata hapa?*** *19 Na neno hili lilikuwa dogo tu mbele ya macho yako, Ee Bwana Mungu; lakini umesema juu ya nyumba ya mtumishi wako kwa* ***miaka mingi ya kuja*** *vilevile; na hili kwa namna ya watu, Ee Mungu! . . . 22 Kwa hivi* ***wewe ni mkubwa, Ee Bwana Mungu; kwa maana hakuna aliye kama wewe, wala hakuna Mungu mwingine ila wewe*** *sawasawa na yote tuliyosikia kwa masikio yetu. . . 28 Na sasa, Ee Bwana Mungu, wewe ni Mungu, na* ***maneno yako ni kweli,*** *na umeahidi mtumishi wako* ***kitu hiki kizuri***, *29 basi sasa ikupendeze kubariki nyumba ya mtumishi wako, ipate kudumu mbele yako* ***milele;*** *kwa*

*maana wewe, Ee Bwana Mungu, uliisema; nyumba ya mtumishi wako ibarikiwe* ***milele*** *kwa baraka yako."* (2 Samweli 7:18,19,22,28,29)

Haya ndiyo mashukuru ya Daudi kwa Bwana kwa ahadi yake juu ya **Mfalme** atakayekuja kwa njia ya wazao wake. Ninyi munaojua Maandiko Matakatifu munajua ya kwamba Mungu ametimiza sehemu ya ahadi hii. Kwani ndani ya Habari Njema {*Injil*} tunasoma ya kwamba miaka elfu moja nyuma ya wakati wa Daudi, Mungu alituma malaika karibu na wachungaji waliokuwa wakilinda makundi yao ndani ya vilima vile vile pahali Daudi alipolinda kundi la baba yake. Malaika ya Bwana alisema na wachungaji, *"Ninawaletea ninyi Habari Njema ya furaha kubwa itakayokuwa* ***kwa watu wote.*** *Kwa sababu leo amezaliwa kwenu katika* ***mji wa Daudi,*** *Mwokozi, ndiye* ***Kristo Bwana.****"* (Luka 2:10,11) Ndiyo, **Mfalme** ambaye Mungu aliahidi kuleta kwa njia ya kizazi cha Daudi amezaliwa. Kwa wakati wa sasa yeye ni mbinguni tena, akingoja siku ya kuogofya na ya utukufu wakati atakaporudi kuhukumu dunia na haki. Siku ile, watu wote watajua ya kwamba ahadi Mungu aliyofanya kwa Daudi juu ya **ufalme wake wa milele** ni kweli. Siku ile itasemwa, *"Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake,* ***naye atatawala hata milele na milele.****"* (Ufunuo 11:15)

Habari za kushangaza kabisa. Mara ya nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea na habari za Mfalme Daudi na kusikia juu ya neno lingine ambalo litakushangaza sana.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya shairi hili toka Maandiko Matakatifu:

***"Tazameni namna ya utajiri wa akili na maarifa ya Mungu! . . . Kwa maana vitu vyote vinatoka kwake, na viko kwa uwezo wake, na viko kwa yeye. Utukufu uwe kwake milele. Amina.***
(Waroma 11:33,36)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 49

# Mfalme Daudi na Bati-Seba

2 Samweli 11,12; Zaburi 51,32

Salama iwe kwako, rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Asante kwa kufika tujifunze pamoja somo lingine la mfulizo la *Njia ya Haki*.

Ndani ya somo la mbele tuliona namna Daudi alivyogeuka Mfalme wa Israeli. Daudi alikuwa mfalme wa haki, mwenye huruma aliyependa Neno la Mungu sana. Lakini leo tutasoma **neno la huzuni juu ya Daudi**. Daudi alifanya neno la kuchukiza machoni mwa Mungu; alitamani mke wa jirani yake, akazini naye, kisha aliongeza zambi nyingine kujaribu kufunika zambi hii ya kwanza. Labda watu wengine wanataka kuuliza: "Kwa sababu gani habari mbaya namna hii zinaandikwa ndani ya Maandiko Matakatifu?" Maandiko yanajibu ulizo hili: *"Yote yaliyoandikwa, yameandikwa **kwa mafundisho kwetu**."* (Waroma 15:4) *"Maneno haya yote . . . yakaandikwa **kutuonya sisi** . . . Basi, yeye anayezania anasimama, aangalie asianguke!"* (1 Wakorinto 10:11,12) Ndani ya Maandiko Matakatifu, Mungu hafichi zambi za manabii kwa sababu Mungu anataka kutupa sisi mafundisho ya faida.

Sasa turudi kwa kitabu cha pili cha Samweli na kuona namna Daudi alivyoanguka na kutenda zambi. Tusome kwa 2 Samweli 11 kuanza na shairi 1:

> (2 Samweli 11) *1 Na ilikuwa kwa mwanzo wa mwaka mpya wakati wafalme wanapotoka kwenda vitani, **Daudi** akatuma **Yoabu** na watumishi wake pamoja naye, na Israeli wote; wakaharibu wana wa Amoni, wakazunguka Raba kwa vita. Lakini Daudi akakaa kule Yerusalema.*

*2 Na ilikuwa mangaribi, Daudi akaondoka kitandani, akatembea juu ya dari ya nyumba ya mfalme; toka dari akaona mwanamke akioga; na huyu mwanamke alikuwa mzuri sana kutazama. 3 Daudi akatuma na kuuliza habari za yule mwanamke. Mmoja akasema: Huyu si* ***Bati-Seba*** *. . . mke wa Uria Mhiti? 4 Daudi akatuma wajumbe, akamtwaa, akakuja kwake, akalala pamoja naye . . . akarudi nyumbani mwake. 5 Mwanamke akachukua mimba; akatuma kumwambia Daudi, akasema: "Nina mimba."*

Halafu Maandiko yanaonyesha namna Daudi alivyojaribu kufunika zambi yake. Wakati Daudi aliposikia ya kwamba Bati-Seba alikuwa na mimba, alituma barua kwa Yoabu, kiongozi cha jeshi lake, akamwagiza kutuma kwake Uria, mume wa Bati-Seba. Basi Uria alikuwa mtu mwenye uwezo ndani ya jeshi la Israeli. Hivi Yoabu alituma Uria kwa Daudi.

(2 Samweli 11) *7 Wakati Uria alipokuja kwake, Daudi alimwuliza habari za Yoabu, na habari za watu, na habari za vita. 8 Daudi akamwambia Uria: Shuka kwa nyumba yako na nawa miguu yako. Uria akaondoka nyumbani mwa mfalme, zawadi ya chakula ilimfuata toka mfalme. 9 Lakini Uria akalala kwa mlango wa nyumba ya mfalme pamoja na watumishi wote wa bwana wake, wala hakushuka kwa nyumba yake. 10 Na wakati walipomwambia Daudi wakisema: Uria hakushuka kwa nyumba yake, Daudi akamwambia Uria: Wewe hukutoka safari? Kwa nini hukushuka kwa nyumba yako? 11 Uria akamwambia Daudi: Sanduku, na Israeli, na Yuda wanakaa vibandani; na bwana wangu Yoabu na watumishi wa bwana wangu wamepiga kambi waziwazi; basi nitashuka nyumbani mwangu, nile na kunywa na kulala na mke wangu? Sawasawa unavyoishi . . . sitafanya neno hili.*

*12 Daudi akamwambia Uria: Kawa hapa leo vilevile na kesho nitakuruhusu kwenda. Basi Uria akakaa kule Yerusalema siku ile na kesho yake. . . 14 Na ilikuwa asubui Daudi akaandikia Yoabu barua, akaituma kwa mkono wa Uria. 15 Akaandika ndani ya barua akisema: Weka Uria pamoja na watu wa mbele pahali vita ni kali zaidi, kisha mumwondokee, hata apigwe na kufa. 16 Na ilikuwa wakati Yoabu alipolinda mji, akaweka Uria pahali alipojua watu hodari walipokuwa. 17 Watu wa mji wakatoka, wakapigana na Yoabu; wengine wa watu wakaanguka, hata wa watumishi wa Daudi; na Uria Mhiti alikufa vilevile. 18 Halafu Yoabu akatuma na kumwambia Daudi maneno yote ya vita; 21 . . . Mtumishi wako Uria Mhiti amekufa vilevile.*

*26 Wakati mke wa Uria aliposikia ya kuwa Uria bwana wake amekufa, akafanyia bwana wake ombolezo. 27 Na wakati ombolezo lilipokwisha, Daudi akatuma na kumtwaa kwake nyumbani, akakuwa mke wake, akamzalia mwana.* ***Lakini neno Daudi alilofanya halikupendeza Bwana.***

(2 Samweli 12) *1 Bwana akatuma [nabii mmoja jina lake]* ***Natana*** *kwa Daudi. Akakuja kwake, akamwambia: Watu wawili walikuwa mjini mmoja; mmoja alikuwa tajiri, mwingine alikuwa masikini. 2 Tajiri alikuwa na kondoo na ngombe wengi sana; 3 lakini masikini hakuwa na kitu ila mwana-kondoo mmoja mdogo ambaye alimnunua na kumlea; na alipata nguvu pamoja naye na pamoja na watoto wake; akakula ya chakula chake mwenyewe na kunywa toka kikombe chake mwenyewe, akalala kifuani mwake na alikuwa kwake kama binti. 4 Na msafiri alifikia tajiri, naye hakutwaa za kondoo zake mwenyewe, na ngombe zake mwenyewe kutayarisha kwa msafiri aliyekuja kwake, lakini akatwaa mwana-kondoo wa masikini huyu, akamtayarisha kwa mtu aliyekuja kwake.*

*5 [Wakati Daudi aliposikia habari hizi] hasira yake iliwaka sana juu ya mtu yule; akamwambia Natana: Sawasawa Bwana anavyoishi,* ***mtu aliyefanya neno hili anastahili kufa****; 6 naye atarudisha mwana-kondoo mara ine, kwa sababu ametenda neno hili na kwa sababu hakuwa na huruma. 7 Natana akamwambia Daudi:* ***Wewe ni mtu yule****. Bwana, Mungu wa Israeli, anasema hivi: Nilikupakaa mafuta, uwe mfalme juu ya Israeli, na kukuponyesha toka mkononi mwa Saulo; 8 . . . nikakupa nyumba ya Israeli na ya Yuda na kama maneno haya yangalikuwa machache, ningalikuongezea maneno mengine hivi na hivi. 9 Kwa nini umezarau neno la Bwana, na kufanya yaliyo mabaya mbele ya macho yake? Umepiga Uria Mhiti kwa upanga na umetwaa mke wake kuwa mke wako, na kuua Uria kwa upanga wa wana wa Amoni. 10 Kwa hivi basi upanga hautaondokea nyumba yako kwa sababu umenizarau, na kutwaa mke wa Uria kuwa mke wako. 11 Bwana anasema hivi: Tazama, nitasimamisha uovu juu yako toka nyumbani mwako mwenyewe, na nitaondosha wake wako mbele ya macho yako, na kumpa jirani yako, naye atalala na wake wako mbele ya jua. 13 Daudi akamwambia Natana:* ***Nimekosea Bwana****. Natana akamwambia Daudi:* ***Bwana ameondoa zambi yako vilevile, hutakufa****. 14 Lakini kwa sababu ya tendo hili uliwapa adui za Bwana nafasi kubwa kwa kutukana, hakika mtoto aliyezaliwa kwako atakufa. 15 Natana akatoka kwenda nyumbani mwake.*

Ndani ya sura zinazofuata Maandiko yanatuonyesha ya kwamba zambi ya Daudi ilizaa taabu na masikitiko mengi ndani ya jamaa yake. Lakini Neno la Mungu linasema vilevile: "*Pahali zambi zilipozidi, **neema** ilizidi zaidi sana*." (Waroma 5:20) Hivi, ndani ya nusu ya saa inayobaki leo, tutaona namna Mungu alivyoonyeshea Daudi **neema** yake, na kusamehe **zambi** zake zote.

**Kwa nini Mungu alisamehe Daudi zambi zake?** Ulisikia neno Daudi alilojibu Natana wakati Natana aliposema na Daudi, "***Wewe ni mtu yule!***"? Nabii wa Mungu, Natana, alikuwa na uhodari mkubwa wakati aliposema neno namna hii kwa mfalme mkubwa wa Israeli! Daudi alijibu Natana namna gani? Alimfunga gerezani, au aliagiza auawe, kama wafalme wengi walivyofanya? Sivyo, hakufanya hivi. Daudi alijaribu kuhakikisha zambi zake kwa njia ya kusema, "Mungu alitaka hivi!" au "Mungu ni mwema, labda atazima matendo yangu mabaya kwa sababu ya matendo yangu mazuri!"? Daudi alijibu Natana namna hii? Sivyo. Daudi hakusema hivi! Basi Daudi alijibu namna gani? Daudi alijibu na kusema, "Nimekosa!" "***Nimekosea Bwana****!*"

Kwa kufahamu vizuri namna Daudi alivyokiri zambi yake mbele ya Mungu, inatupasa kusoma ndani ya Zaburi maneno Daudi aliyoandika wakati nabii wa Mungu alipokwisha kumhamakia juu ya zambi yake na Bati-Seba. Ndani ya Zaburi 51 Daudi alisema:

> (Zaburi 51) *1* ***Unirehemu, Ee Mungu, sawasawa na wema wako;*** *sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. 2 Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi zangu, 3 maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. 4 Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako; ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema. 5 Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. 6 Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima. 7* ***Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. . .*** *10 Umba moyo safi ndani yangu, Ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. . . 17* ***Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, Ee Mungu.***

Hii ndiyo namna Daudi alivyotubu. Daudi alihuzunishwa sana kwa sababu ya zambi yake. Roho yake ilivunjika mbele ya Mungu. **Daudi hakuwa kama wale walio na dini, lakini wanaoendelea ndani ya zambi kila siku.** Ndiyo, Daudi alianguka kabisa ndani ya

zambi, lakini hakuweza kuendelea ndani ya zambi ile kwa sababu alipenda Mungu, na alijua ya kwamba *"Mungu ni nuru; wala giza si ndani yake kabisa."* (1 Yoane 1:5)

Hivi wakati Daudi alipokwisha kutubu, Mungu alisema nini naye kwa njia ya kinywa cha nabii Natana? Mungu alisema naye, "Kwenda na kufanya kazi njema kusudi nizime zambi zako!"? Sivyo, Mungu hakusema hivi! Natana alisema naye, *"Bwana ameondoa zambi yako vilevile, hutakufa."* (2 Samweli 12:13)

Nyuma ya maneno haya, Daudi aliandika ndani ya Zaburi juu ya heri ya mtu **anayesamehewa na Mungu, bila kufanya kazi yeye mwenyewe**. Alisema: *"Heri yeye aliye**samehewa** makosa yake na zambi yake ime**funikwa**. Heri mtu ambaye Bwana hamhesabu uovu na ndani ya roho yake hila haiko."* (Zaburi 32:1,2; Waroma 4:7,8) Ndiyo, Mungu alisamehe Daudi na alimhesabu kuwa mwenye haki! Lakini Mungu hakuondosha taabu na huzuni zambi ya Daudi ilizozaa. Maana yake ndiyo hii: Mungu hatakumbuka zambi za Daudi siku ya hukumu. Alikuwa amezizima toka kitabu chake!

**Mungu aliweza kufanya hivi namna gani?** Namna gani Mungu aliweza kusamehe zambi zote za Daudi pamoja na kuwa mwamuzi wa haki? Mungu aliweza kusahau tu uovu wote Daudi aliotenda? Sivyo! Mungu ni mwamuzi wa haki, na hawezi kufunga macho tu kwa maneno ya zambi za wana wa Adamu. Basi, namna gani Mungu aliweza kusamehe Daudi, pamoja na kubaki mwenye haki?

Unakumbuka ombi la Daudi wakati alipokwisha kutambua zambi yake? Aliomba: "*Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi zangu . . . Unisafishe kwa **hisopo** na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji."* (Zaburi 51:2,7) Mungu alikuwa ameagiza Waisraeli kutumia tawi la pando lililoitwa hisopo kunyunyiza damu ya sadaka. Damu iliyonyunyizwa ilikuwa mfano wa sadaka kubwa ya **Mkombozi atakayekuja** na atakayekufa kwa kutaka kwake mwenyewe, akimwanga damu yake kuwa **malipo kwa zambi.**

Mungu aliweza kusamehe Daudi zambi zake kwa sababu Daudi alikuwa **ametubu** (kuacha zambi yake na kugeuka kwa Mungu) na **aliamini** uwezo wa Mungu kumsafisha kwa sababu ya kazi ya Mkombozi atakayekuja. Daudi alitolea Mungu maombi namna hii: "Ee Mungu, ninahuzunishwa kwa sababu ya zambi yangu na ninakuomba kunisamehe! Ninajua unaweza kusamehe zambi zangu, kwa sababu siku nyingine utatuma Mkombozi, asiye na zambi, na

yeye mwenyewe atabeba azabu ya zambi zangu kwa ajili yangu. Hivi, Bwana, unirehemu, mimi mwenye zambi! Unioshe ndani ya damu ya Mkombozi mtakatifu, nami nitakuwa safi kabisa!"

Mungu, kwa neema yake, alisamehe Daudi zambi zake zote? Mungu alisafisha moyo wa Daudi na kumhesabu kuwa mwenye haki? Ndiyo, alifanya hivi! Aliweza kufanya hivi kwa sababu gani? Mungu alisamehe Daudi kwa sababu Daudi **alikiri** hali yake ya zambi mbele ya Mungu na aliamini ahadi ya Mungu juu ya Mkombozi atakayekuja na kubeba azabu kwa zambi. Kwa sababu ya imani yake ndani ya ahadi za Mungu Daudi aliweza kufurahi, na kuandika ndani ya Zaburi: ***"Heri yeye aliyesamehewa makosa yake na zambi zake zimefunikwa. Heri mtu ambaye Bwana hamhesabu uovu, na ndani ya roho yake hila haiko!"*** (Zaburi 32:1,2)

Rafiki, asante kwa kujifunza pamoja nasi. Ndani ya masomo mawili ya nyuma, Mungu akitaka, tutasoma ndani ya kitabu kitakatifu cha Zaburi kuona ushuhuda wa Daudi juu ya Mkombozi, atakayebeba azabu yetu, ili Mungu aweze kusamehe zambi zetu kwa milele . . .

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya shairi hili Daudi aliloandika ndani ya Zaburi juu ya moja ya baraka kubwa zaidi za Mungu:

> ***"Heri yeye aliyesamehewa makosa yake na zambi zake imefunikwa. Heri mtu ambaye Bwana hamhesabu uovu, na ndani ya roho yake hila haiko!"*** (Zaburi 32:1,2)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 50

# Nabii Daudi na Masiya

### Zaburi 1, 2

Tunakusalimu, rafiki, kwa jina la Mungu, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Asante kwa sababu tunaweza kuendelea na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya masomo mane ya mbele tulisoma juu ya maisha ya **nabii Daudi**. Tuliona ya kwamba Daudi alikuwa mchungaji, mpiga kinubi, mwandishi wa nyimbo, mwenye kujifunza Neno la Mungu, mwenye kushinda vitani, mfalme wa Israeli, na nabii wa Mungu. Ndani ya somo lililotangulia lile la sasa, tuliona ya kwamba Daudi alikuwa **mwenye zambi** vilevile, na ya kwamba alitenda neno lililohuzunisha Mungu sana. Lakini, tuliona namna Mungu alivyosamehe Daudi zambi zake, kwa sababu Daudi aliachana na zambi hizi kabisa na toba ya kweli na aliamini maneno Mungu aliyoahidi juu ya Mkombozi atakayekuja duniani na kubeba azabu kwa zambi za dunia nzima.

Leo tunataka kuwaza juu ya kitabu cha ajabu kilicho katikati ya Maandiko Matakatifu. Unajua jina la kitabu hiki? Ndiyo, ni **Zaburi**. Ndani ya kitabu cha Zaburi kuna sura au nyimbo mia moja na makumi tano. Ndani ya muda wa miaka zaidi ya mia moja, Mungu alitumia manabii kuandika zaburi. Wengine walikuwa Musa, Solomono, Asafu, na wana wa Kora. Lakini Daudi aliandika zaburi nyingi kupita nabii ye yote mwingine. Leo tunataka kuangalia zaburi (nyimbo au sura) mbili za kwanza karibu karibu.

Wimbo wa kwanza unaonyesha kwamba kuna watu wa namna mbili duniani: Wale wanaotembea ndani ya **njia ya haki,** na wale wanaotembea ndani ya **njia ya uzalimu.** Ndani ya zaburi ya kwanza (Zaburi 1) imeandikwa:

> *1* ***Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la waovu,*** *wala haketi barazani mwa wenye kuzarau. 2 Lakini furaha yake ni katika sheria ya Bwana; na katika sheria yake anawaza mchana na usiku. 3*

> *Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, unaozaa matunda yake kwa wakati wake, wala majani yake hayakauki; na yo yote anayofanya yatabarikiwa. 4* ***Waovu si hivi;*** *lakini wao ni kama makanda yanayopeperushwa na upepo. 5 Kwa hivi waovu hawatasimama katika hukumu, wala wenye zambi katika makutano ya wenye haki.* ***6 Kwa kuwa Bwana anajua njia ya wenye haki; lakini njia ya waovu itapotea.*** (Zaburi 1)

Tunaona hapa **njia ya wale wanaobarikiwa** na **njia ya wale wanaoharibiwa.** Kila mtu anataka kubarikiwa. Hakuna mtu anayetaka kuharibiwa. Mungu anataka kila mtu kubarikiwa. Lakini sharti kwa mtu kuja kwa njia ya baraka Mungu aliyotayarisha. Njia ile ni nini? Wimbo wa kwanza (ndiyo zaburi ya kwanza) unajumlisha njia hii na mawazo mawili. **La kwanza:** Usifuate njia ya wale wanaozarau Neno la Mungu. **La pili:** Waza juu ya Neno la Mungu na kusudi la kufahamu, kuamini na kupokea njia ya wokovu Mungu aliyotayarisha.

Ukiamini na kufuata njia ya haki ya Mungu, Maandiko yanasema utakuwa *"kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji";* maisha yako yatasimamishwa ndani ya Mungu mwenyewe, na kuzaa matunda *"kwa wakati wake"* kama mapendo, furaha, na salama. Lakini kama usipofuata njia ya haki, utaharibiwa kama *"makanda yanayopeperushwa na upepo".*

Sasa tuendelee na zaburi ya pili. Ndani ya sura hii Mungu aliongoza Daudi kuandika juu ya **Mkombozi** atakayefika duniani. Tusikilize karibu karibu neno Mungu alilosema nasi kwa njia ya nabii wake Daudi. Maandiko yanasema:

> (Zaburi 2) *1 Kwa nini mataifa wanafanya ukali, na makabila wanafikili ubatili? 2 Wafalme wa dunia wanajipanga, na watawala wanafanya shauri pamoja juu ya Bwana, na juu ya* ***mpakaliwa wake (Masiya),*** *wakisema: 3 Tuvunje vifungo vyao na kutupa mbali nasi kamba zao. 4 Yeye anayeketi mbinguni atacheka; Bwana atawafanyiza zihaka. 5 Kisha atawaambia katika hasira yake, na kuwafazaisha katika uchungu wake; 6 nami nimeweka* ***mfalme wangu*** *juu ya Sayuni mlima wangu mtakatifu. 7 Nitahubiri amri; Bwana aliniambia: Wewe ni* ***mwana wangu****; leo nimekuzaa. 8 Uniombe, na nitakupa mataifa kuwa uriti wako, na miisho ya dunia kuwa miliki yako. 9 Utawaponda kwa fimbo ya chuma, utawavunja vipande vipande kama chombo cha mfinyanzi. 10 Na sasa ninyi wafalme, fanyeni akili; na mufundishiwe, ninyi waamuzi wa dunia. 11 Tumikieni Bwana kwa woga, na furahini pamoja na kutetemeka.*

> *12* ***Busuni mwana asikasirike, nanyi munapotea njiani, kwa kuwa hasira yake itawaka upesi. Heri wote ambao wanamkimbilia***.

Unafahamu maneno Bwana Mungu aliyotangaza ndani ya Zaburi 2? Ni maneno makubwa sana! Ndani ya wimbo huu Mungu anatujulisha **majina matatu ya ajabu ya Mkombozi** atakayekuja duniani kuleta wokovu kwa wana wa Adamu. Ulisikia majina haya matatu? Ni **Masiya, Mfalme**, na **Mwana**. Tuwaze kidogo juu ya majina haya matatu Mungu anayoita Mwokozi wa dunia.

1) Kwanza, tunaona ya kwamba Mungu aliita Mkombozi **"Masiya."** Masiya ni neno kwa Kiebrania, maana yake *Yule anayechaguliwa na Mungu*. Kwa njia ya jina hili Masiya, Mungu alikuwa akitangaza kwa wana wa Adamu ya kwamba inapasa kila mtu kuamini na kupokea Mkombozi atakayekuja duniani, kwa sababu huyu ndiye aliyechaguliwa na Mungu mwenyewe kuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia. Lakini, ndani ya mashairi matatu ya kwanza ya wimbo huu, Mungu alitabiri ya kwamba zaidi ya wana wa Israeli watakataa Masiya ambaye Mungu atatuma duniani. Tusome mashairi haya tena.

> *"Kwa nini mataifa wanafanya ukali, na makabila wanafikili ubatili? Wafalme wa dunia wanajipanga, na watawala wanafanya shauri pamoja juu ya Bwana, na juu ya mpakaliwa wake (Masiya), wakisema: Tuvunje vifungo vyao na kutupa mbali nasi kamba zao."* (Zaburi 2:1-3)

Kwa sababu gani watu wa dunia watakataa Masiya ambaye Mungu alituma? Watakataa Masiya kwa sababu atakuwa mtakatifu, bila kipaku cha zambi, na Maandiko yanatupasha ya kwamba *"kila mtu anayefanya mabaya anachukia nuru, wala hafiki kwa nuru,* ***matendo yake yasikemewe****."* (Yoane 3:20) Hivi Mungu alitabiri ndani ya mashairi haya namna Wayuda na mataifa ya dunia watafungana pamoja kujaribu kuharibu yule Mtu mtakatifu ambaye Mungu alichagua kuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia. Lakini Mungu alijua kila neno ambalo watu waovu watajaribu kufanya. Mungu alikusudi mashauri maovu ya watu kutimiza shauri lake la haki kukomboa wenye zambi. Kwa sababu hii tunasoma: *"Yeye anayeketi mbinguni atacheka; Bwana atawafanyiza zihaka!"* (Zaburi 2:4) Hivi, jina la kwanza ambalo Mungu alimpa Mkombozi ndani ya sura hii ni ***Masiya***. Utapenda kujua ya kwamba neno hili *Masiya* kwa Kiebrania ni *Kristo* kwa Kiyunani. Maana ya majina haya mawili ni *"Yule ambaye Mungu alichagua."*

2) Jina la pili ni "**Mfalme**." Masiya ni Mfalme vilevile. Kwa njia ya jina hili, Mungu anataka watu wote kujua ya kwamba mwishoni Masiya atakuwa Mwamuzi na Mtawala wa dunia hata kama zaidi ya watu watamkataa. Siku ile kubwa ya hukumu, watu wote watapiga magoti mbele yake, kwa sababu yeye ndiye aliyechaguliwa na Mungu kuwa Mfalme wa wafalme, Bwana wa wabwana. Hivi, Masiya atakuwa au **Mwokozi au Mwamuzi wako**—kwa sababu **yeye ni Mfalme** ambaye Mungu alichagua kutawala milele!

3) Jina la tatu tuliloona ndani ya sura hii ambalo Mungu anampa Masiya ni jina ambalo inatupasa kufikili sana juu yake. Ni **"Mwana"**. Mbele ya kueleza maana ya jina hili, tujikumbushe ya kwamba maneno yote Daudi aliyoandika ndani ya Zaburi, aliyaandika kwa hekima aliyopewa na Mungu. Tukumbuke vilevile ya kwamba ndani ya maandiko ya Manabii kuna maneno mengine yaliyo magumu kufahamu, lakini maneno haya ni kweli hata hivi! Mungu anatuonya ndani ya Neno lake akisema: "*Katika barua hizi [Maandiko] ni maneno yaliyo magumu kwa kufahamu, watu wasio na elimu, wasio imara wanayogeuza . . . kwa uharibifu wao wenyewe!"* (2 Petro 3:16) Ujinga ni neno mabaya kabisa, zaidi kama ni ujinga juu ya Masiya ambaye Mungu alichagua kuokoa wana wa Adamu toka uharibifu wa milele. Kama watu wa kabila moja wanavyosema kwa mfano, "Ujinga unaua mbio!" Tukumbuke wazo hili wakati tunapowaza juu ya jina la tatu ambalo Mungu yeye mwenyewe alimpa Masiya.

Sasa turudi kwa Zaburi 2. Ndani ya shairi 7 tunasoma ya kwamba Masiya anasema: *"Nitahubiri amri; Bwana aliniambia: "Wewe ni **mwana** wangu; leo nimekuzaa."* (Zaburi 2:7) Ulisikia neno Bwana alilosema na Masiya? Alisema: *"Wewe ni **mwana wangu** . . . **nimekuzaa**."* Unajua **kwa nini** Mungu aliita Masiya **Mwana wake**? Unafahamu maana ya jina hili? Tunataraji ya kwamba ninyi wote munajua ya kwamba maana yake ***haiko*** ya kwamba Mungu alioa mke kuzaa mtoto kwa njia yake! Sivyo, hata kidogo! Wazo namna hii ni ukufuru! Mungu ni roho naye hazai mwana namna mtu anavyozaa.

Basi, kwa sababu gani Mungu alisema na Masiya, *"Wewe ni **Mwana wangu!**"*? Tunaweza kushukuru Mungu kwa sababu Bwana Mungu mwenyewe alitujulisha kwa sababu gani alifanya hivi. Hatuna saa kutafuta neno hili sana leo, lakini tunataka kuonyesha **sababu tatu** toka Maandiko ya Manabii **kwa sababu gani** Mungu aliita Masiya **Mwana wake.**

1. Sharti ujue ya kwamba Mungu aliita Masiya *Mwana wake,* kwa sababu **Masiya alikuja kutoka juu,** toka mbingu. Kila mtu

anayeamini maandiko ya Manabii anajua ya kwamba Masiya hakuja toka mtu lakini toka mbele ya Mungu. Kama munavyojua, **Masiya hakuwa na baba ya dunia**. Kwa maisha yake hapa duniani, alikuja kwa njia ya wazao wa Daudi, kwa sababu Masiya alizaliwa na bikira aliyekuwa mzao wa mfalme Daudi. Lakini kwa maneno ya Baba yake, Masiya alitoka kwa Roho ya Mungu. Kwa sababu hii Mungu aliweza kusema naye: *"Wewe ni **Mwana wangu;** leo nimekuzaa!"*

2. Mungu aliita Masiya *Mwana wake* kwa sababu maandiko yanasema ya kwamba **wanashiriki tabia takatifu**. Ilikuwa lazima kwa Mkombozi ambaye Mungu aliahidi kutuma kuwa safi na mtakatifu kama Mungu mwenyewe ni safi na mtakatifu. Hatuwezi kueleza neno hili zaidi sasa, lakini wakati tutakapojifunza juu ya vitabu vya Habari Njema {Injil}, tutaona ya kwamba Masiya hakuwa kama wana wa Adamu wenye zambi! Kama tulivyoona, hata manabii wa kujulikana zaidi walifanya zambi. Lakini, Masiya hakufanya zambi kamwe. Alifanya mapenzi ya Mungu kila mara. Ilikuwa sharti kwa Masiya kuwa bila zambi kwa sababu alikuja duniani kuokoa wenye zambi! Watu wenye deni kubwa wanaweza kulipa deni za watu wengine? Hawawezi hata kidogo! Masiya hakuwa na deni ya zambi. Maandiko yanamwita *"mtakatifu, pasipo uovu, wala alama ya uchafu, aliyetengwa na wenye zambi, aliyekuwa juu kuliko mbingu."* (Waebrania 7:26) **Ndiyo, Mkombozi alikuwa mtakatifu, kama Mungu ambaye alimtuma ni mtakatifu!** Kwa sababu hii Mungu hakuwa na haya kumwita **Mwana wake**.

3. Inakupasa kujua ya kwamba Mungu aliita Masiya *Mwana wake* **kumweka mbali na manabii wote wengine**. Tumeona mbele ya kwamba Abrahamu aliitwa *"rafiki ya Mungu."* Nabii Musa aliitwa *"mtu wa Mungu."* Juu ya Daudi, Mungu alisema, *"Nimeona Daudi . . . mtu anayependeza moyo wangu."* Lakini Mungu alisema na nabii gani, *"Wewe ni **Mwana wangu**; leo **nimekuzaa**"*? Aliweza kusema neno hili juu ya Masiya tu, kwa sababu Masiya ndiye wa pekee aliyetoka juu, aliyezaliwa na bikira, na asiyechafuwa na zambi.

Msomaji, unajua **Masiya, Mfalme** ambaye Mungu anaita **Mwana wake**? Mungu anataka kila mtu kumjua, kumsikiliza, kumwamini na kumpokea. Kwa sababu hii nabii Daudi alimaliza sura hii na maneno haya:

> *"Na sasa ninyi wafalme, **fanyeni akili;** na mufundishiwe, ninyi waamuzi wa dunia. Tumikieni Bwana kwa woga, na furahini pamoja na kutetemeka. Busuni Mwana asikasirike, nanyi munapotea njiani,*

> *kwa kuwa hasira yake itawaka upesi.* ***Heri wote ambao wanamkimbilia***." (Zaburi 2:10-12)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Tumefikia mwisho wa somo hili. Ndani ya somo 51 tutawaza juu ya wimbo mzuri mwingine ambao Daudi aliandika ndani ya kitabu cha Zaburi . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya maneno nabii Daudi aliyoandika ndani ya Zaburi akisema:

> "***Fanyeni akili . . . Tumikieni Bwana kwa woga, na furahini pamoja na kutetemeka. Busuni Mwana asikasirike, nanyi munapotea njiani, kwa kuwa hasira yake itawaka upesi. Heri wote ambao wanamkimbilia***." (Zaburi 2:10-12)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 51

# Mafundisho Mengine toka Zaburi

(Zaburi 22)

Salama iwe kwako, rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea tena kusoma pamoja mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Mara ya mbele tulisoma sura 1 na 2 toka **kitabu cha Zaburi**. Ingekuwa vizuri kama ndani ya masomo haya tungalikuwa na saa kusoma na kusemezana juu ya kila sura ndani ya Zaburi, lakini kitabu kile kina sura 150, hivi neno hili haliwezekani.

Lakini mbele ya kuacha kitabu cha Zaburi, tunataka kuangalia wimbo mmoja mwingine ambao Mungu aliongoza Daudi kuandika, ndiyo **Zaburi 22**. Zaburi hii ni sura kubwa sana, kwa sababu **inatabiri ya kwamba Masiya atakufa katika maumivu makali kulipa deni ya zambi** kwa wana wote wa Adamu. Ndani ya sura hii, Daudi aliyeishi miaka elfu moja mbele ya kuja kwa Masiya, alitabiri maneno karibu 30 yaliyotokea siku Masiya alipokufa. Wakati tutakaposoma Habari Njema {Injil} inayopasha habari za Masiya, tutaona ya kwamba **maneno yote yalitokea namna nabii wa Mungu, ndiye Daudi alivyotabiri.** Hivi tunajua ya kwamba wimbo huu si mawazo ya mtu tu, lakini unatoka nia ya Mungu. Mungu tu anaweza kutabiri maneno yatakayotokea kwa wakati wa kuja.

Sasa tusikilize maneno nabii Daudi aliyoandika ndani ya Zaburi 22 miaka elfu moja mbele ya kuzaliwa kwa Masiya. Ndani ya sura hii, Daudi aliandika mafikili ya Masiya siku alipomwanga damu yake kama malipo kwa zambi. Alisema:

> (Zaburi 22) *1 Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? Kwa nini wewe ni mbali na kunisaidia, na kwa maneno ya kuugua kwangu? 2 Ee Mungu wangu, ninalia mchana, lakini hujibu; na*

> *wakati wa usiku, wala sinyamazi. 3 Lakini wewe ni mtakatifu, Ee wewe unayeketi juu ya sifa za Israeli. 6 Lakini mimi ni mdudu wala si mtu; laumu ya watu, na mwenye kuzarauliwa na watu. 14 Nimemwangika kama maji, na mifupa yangu yote imeteguka, moyo wangu ni kama nta; umeyeyuka ndani ya matumbo yangu. 15 Nguvu zangu zimekauka kama kipande cha chungu, na ulimi wangu unaambatana na kinywa changu; umenileta katika mavumbi ya mauti. 16 Kwa maana imbwa wamenizunguka; kusanyiko la waovu wamenisonga;* ***wametoboa mikono yangu na miguu yangu.***

Tuache pale kwanza kidogo. Ulifahamu maneno nabii Daudi aliyoandika juu ya Masiya? Miaka elfu moja mbele ya kuzaliwa kwa Masiya duniani Daudi aliandika: *"Kusanyiko la waovu wamenisonga;* ***wametoboa mikono yangu na miguu yangu."*** Na maneno haya Daudi alitabiri namna wana wa Adamu watakavyotoboa mikono na miguu ya Masiya kwa njia ya kumfunga juu ya msalaba. Kwa nini nabii Daudi aliandika ndani ya Zaburi ya kwamba watu waovu watatoboa mikono na miguu ya Masiya? Kwa sababu gani Masiya atakufa mauti ya maumivu namna hii? Kwa nini Mungu ataacha watu kuua Mkombozi mtakatifu ambaye alituma?

Majibu kwa maulizo haya ni ndani ya Neno la Mungu. Ilikuwa lazima kwa Mkombozi kupata maumivu makubwa na kufa mauti ya kuogofya namna hii, ili aweze **kutukomboa** sisi na kubeba azabu ya Mungu kwa ajili yetu. Kwa sababu malipo kwa zambi ni mauti na hukumu kwa milele katika hadeze, ilikuwa sharti kwa Masiya kuonja maumivu mabaya ya hadeze ambayo ilitupasa sisi kupata kwa sababu ya zambi zetu. Mungu, kwa sababu ya neema yake, alikusudi kutuma Mkombozi asiyekuwa na zambi, ili aweze, kwa kutaka kwake mwenyewe, *"kuonja kufa kwa ajili ya kila mtu."* (Waebrania 2:9) Kwa njia hii Mungu aliweza kufungulia wana wa Adamu njia kupata usamehe kwa zambi na mlango wazi kupokea uzima wa milele, bila kuacha kuwa mwenye haki yeye mwenyewe! Masiya atapata azabu kwa zambi zetu. Kwa sababu ya **mauti ya Masiya mwenye haki**, Mungu, Mwenye Haki, **anaweza kuhesabu kama haki kila mtu ambaye anamwamini**.

Maneno haya ambayo nabii Daudi aliandika juu ya mauti ya Masiya yanatushangaza kabisa. Miaka elfu moja mbele ya kuzaliwa kwa Masiya, Daudi aliandika maneno mengi, moja moja juu ya namna Masiya atakavyoumia juu ya msalaba pahali atakapofungwa na misumari. Labda neno ambalo inatupasa kufahamu na kukumbuka ndilo hili: Waroma ndio taifa walioanza desturi ya kuua watu kwa

njia ya kufunga mtu juu ya msalaba na misumari, mauti ya maumivu mingi. Lakini wakati Daudi alipoandika juu yake ndani ya Zaburi, taifa la Waroma halikuwa kwanza, na hakuna mtu aliyejua juu ya kuua mtu kwa njia ya kumfunga juu ya msalaba na misumari. Lakini Mungu alitia habari za kufa kwa Masiya juu ya msalaba ndani ya nia ya Daudi, na kumwongoza kuziandika ndani ya Zaburi, **ili tuweze kujua hakika** ya kwamba mauti ya Masiya juu ya msalaba ilikuwa **shauri la Mungu** kutuokoa toka azabu ya zambi zetu.

Kweli tunayosoma ndani ya sura hii ni wazi kabisa, na sharti tuweke roho juu yake. Lakini, **si kila mtu anayepokea habari hizi toka Mungu**. Hata leo, watu wengine wanakana maneno ambayo nabii wa Mungu, Daudi, aliandika ndani ya Zaburi juu ya kufa kwa Masiya juu ya msalaba. Wanasema, "Mungu hawezi kukubali Masiya kufa mauti ya maumivu mengi hivi!" Lakini wale wanaosema hivi hawajui Maandiko ya Manabii na njia ya Mungu kuokoa wenye zambi. Rafiki, kaa na ange usione njia ya wokovu ya Mungu bule! Kwa Waebrania 2:3 tunasoma, *"Tutapona namna gani **tusipochunga** wokovu mkubwa namna hii?"* Na 1 Wakorinto 1:18 linatujulisha ya kwamba *"neno la msalaba kwao wanaopotea ni upumbavu; lakini kwetu sisi tunaookolewa ni uwezo wa Mungu!"*

Sasa tuangalie maneno mengine Daudi aliyoandika juu ya kufa kwa Masiya juu ya msalaba. Tunasikia Masiya akisema ndani ya Zaburi 22:

> *1 **Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? 7 Wote ambao wananiona wananicheka sana; wanatoa mdomo, wanatikisa vichwa vyao, wakisema: 8 Ametegemea Bwana; yeye amponyeshe; amponyeshe maana anapendezwa naye.** 14 Nimemwangika kama maji, na mifupa yangu yote imeteguka. Moyo wangu ni kama nta; umeyeyuka ndani ya matumbo yangu. 15 Nguvu zangu zimekauka kama kipande cha chungu, na **ulimi wangu unaambatana na kinywa changu**; umenileta katika mavumbi ya mauti. 16 Kwa maana imbwa wamenizunguka; kusanyiko la waovu wamenisonga; wametoboa mikono na miguu yangu. 17 Ninaweza kuhesabu mifupa yangu yote; **wananitazama na kunikazia macho;** 18 **wamegawa nguo zangu katikati yao, na vazi langu wanalipigia kura.**"*

Na maneno haya, Daudi alitabiri ya kwamba nyuma ya kufunga Masiya juu ya msalaba na misumari, watu watamzarau na kumzihaki, kumkazia macho na kupiga kura kwa kanzu yake. Neno hili lili-

tokea miaka elfu moja nyuma ya saa Daudi alipoliandika. Sikia habari zinazoandikwa ndani ya Habari Njema {Injil} juu ya kufa kwa Masiya. Maandiko yanasema:

> *"Wakati walipokwisha kumsulibisha, waligawa mavazi yake katikati yao wakipiga kura . . . wakaketi kumlinda pale. . . . Nao waliopita njiani wakamtukana wakitikisha vichwa vyao wakisema . . . kama ukiwa Mwana wa Mungu, shuka msalabani. Vile wakubwa wa makuhani wakimzihaki pamoja na waandishi na wazee wakasema: Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni Mfalme wa Israeli; ashuke sasa msalabani na tutamwamini. Anaamini Mungu; amwokoe sasa kama anamtaka; kwa sababu alisema: Mimi ni Mwana wa Mungu."* (Matayo 27:35,36,39-43)

Hivi maandiko ndani ya kitabu cha Habari Njema yanaonyesha namna maneno ya nabii wa Mungu, ndiye Daudi, yalivyotimizwa.

Tumesoma leo vilevile juu ya unabii wa Daudi ya kwamba Masiya atakuwa na kiu na kuteswa sana mwilini mwake na ndani ya nafsi na roho yake. Kwa sababu hii Masiya alilalamika ndani ya shairi la kwanza akisema: *"Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?"* Wakati tunaposoma vitabu vya Habari Njema tunaona ya kwamba maneno Daudi aliyotabiri yalitimia kweli. Kwa nini Masiya alilalamika juu ya msalaba akisema, *"Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?"* Kwa sababu Mungu ni *mtakatifu* (Zaburi 22:3) na hawezi kuvumilia zambi. Ilipasa Mungu kugeuza mgongo kwa Masiya aliyefungwa juu ya msalaba, na kujitenga naye, kwa sababu **Mungu aliweka azabu kwa zambi zetu zote juu yake.** Kwa sababu hii Maandiko yanasema: *"Yeye [Masiya] asiyejua zambi [Mungu] alimfanya kuwa zambi kwa ajili yetu, ili sisi tuwe haki ya Mungu katika yeye."* (2 Wakorinto 5:21)

Mungu asifiwe, kwani kuna neno lingine ambalo nabii Daudi alitabiri ndani ya Zaburi—habari nzuri kabisa! Ndani ya Zaburi 16, Daudi aliandika juu ya Masiya akisema: *"Kwa sababu **hutaachia Hadeze nafsi yangu, wala hutaacha mtakatifu wako kuona uharibifu.** Utanionyesha njia ya uzima."* (Zaburi 16:10,11) Kwa njia hii Daudi alitabiri ya kuwa Mungu alikusudi kufufua Masiya toka kaburi, ili mtu ye yote ambaye anamwamini aweze kuishi pamoja naye mbele ya Mungu mtakatifu kwa milele! Hivi Habari Njema ndiyo hii: *"Kristo [Masiya] **alikufa kwa sababu ya zambi zetu** kama maandiko yanavyosema . . . **alizikwa, akafufuka** siku ya tatu, kama Maandiko yanavyosema!"* (1 Wakorinto 15:3,4)

Daudi alitabiri vilevile ya kwamba nyuma ya ufufuko wa Masiya toka mauti, Mungu atampeleka mbinguni, na kusema naye kuketi kwa mkono wake wa kuume, kufika wakati atakaporudi kuhukumu watu wa dunia. Haya ndiyo maneno Daudi aliyoandika ndani ya Zaburi 110:1 wakati aliposema: *"Bwana anamwambia bwana wangu: Uketi kwa mkono wangu wa kuume hata nifanye adui zako kuwa kiti cha miguu yako."*

Kwa mwisho wa Zaburi 22 Daudi aliandika:

> *27 Miisho yote ya dunia itakumbuka na kugeuka kwa Bwana; na jamaa zote za mataifa wataabudu mbele yake . . . 30 Wazao watamtumikia; habari za Bwana zitasimuliwa kwa kizazi kitakachokuja. 31 Wao watakuja na kuhubiri haki yake kwa watu watakaozaliwa, ya kwamba* ***ndiye ambaye aliyafanya****.*

Maneno ya mwisho ya zaburi hii ni ***"Ndiye ambaye aliyafanya!"*** Masiya atafanya nini? Atakufa kwa pahali pa wenye zambi wote! Atatimiza maneno yote ambayo Mungu aliahidi Adamu na Hawa juu ya Mkombozi ambaye atawaokoa na wazao wao toka zambi zao. Masiya atakufa kama sadaka ya mwisho. Kwa njia ya mauti yake juu ya msalaba Masiya atatimiza na kuondosha sadaka za nyama zilizokuwa mfano wa mauti yake, sadaka Mungu alizotaka wenye zambi kutoa katika miaka iliyopita. Kama kondoo aliyekufa kwa pahali pa mwana wa Abrahamu, Mkombozi atakufa kwa pahali pa wenye zambi kama sadaka ya mwisho, sadaka kamilifu—kwa wote—kwa milele! Hizi ndizo Habari Njema ya Mungu kwa dunia: Masiya alikufa **kwa pahali pako**! Umwamini na utaokolewa toka hukumu ya Mungu. Njia ya wokovu ni wazi kwa wote ambao wanaiamini. Kwa sababu hii, saa ndogo mbele ya kufa kwake Masiya alilia, ***"Imekwisha!"*** (Yoane 19:30) ***"Ameyafanya!"*** (Zaburi 22:31) Na Mungu aliyakinisha sadaka kamilifu ya Masiya kwa njia ya kumfufua toka wafu siku ya tatu. Tutasoma zaidi juu ya maneno haya wakati tutakaposoma kitabu cha Habari Njema.

Tukae kukumbuka neno hili: **Miaka elfu moja mbele ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, nabii Daudi alitabiri ya kwamba wenye zambi watatoboa mikono na miguu ya Masiya!** Na tusisahau sababu kwa mauti ya maumivu ya Masiya. Alikufa kwa **wewe** na kwa **mimi,** na kwa **wenye zambi wote**, ili mtu ye yote ambaye anamwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele! Masiya aliruhusu watu waovu kutoboa mikono na miguu yake kwa sababu alitaka kufanya mapenzi ya Mungu—na kwa sababu ya mapendo

yake makubwa kwa **wewe** na **mimi**. Sikiliza maneno Yesu Masiya anayosema ndani ya Habari Njema {*Injil*}:

> ***"Ninatoa uzima wangu, ili niutwae tena. Hakuna mtu anayeuondoa kwangu, lakini mimi mwenyewe ninautoa.*** *Nina uwezo kuutoa, na nina uwezo kuutwaa tena. Agizo hili nililipokea kwa Baba yangu."* (Yoane 10:17,18)

Rafiki unayesoma maneno haya, unasifu na kushukuru Mungu kwa sababu alituma Masiya kukuokoa toka zambi zako? Maandiko Matakatifu yanasema: *"[Yesu Masiya] aliteswa kwa ajili **yenu**! . . . Yeye mwenyewe alichukua zambi zetu katika mwili wake juu ya mti, hata sisi, tukiwa wafu kwa maneno ya zambi, tuwe hai kwa maneno ya haki; na kwa kupigwa kwake muliponyeshwa . . . aliyetolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tuhesabiwe haki . . . **ili kila mtu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele!**"* (1 Petro 2:21,24; Waroma 4:25; Yoane 3:16)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Tunaomba Mungu aweze kukufahamisha wazi kila neno ambalo tulisoma leo. Mungu akitaka, tutaendelea ndani ya Maandiko ya Manabii na kusoma juu ya mwana wa Daudi, ndiye Solomono. . .

Mungu akubariki wakati unapowaza kwa sababu gani aliongoza nabii Daudi kutabiri habari hizi juu ya Masiya:

***"Wametoboa mikono yangu na miguu yangu!"*** (Zaburi 22:16)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 52

# NABII SOLOMONO

1 WAFALME 2-10; ZABURI 72

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Mungu akitokea kwako na kusema nawe, "Omba neno lo lote unalotaka, na nitakupa," utaomba nini? Maisha marefu? Mali nyingi? Sifa kubwa? Au neno lingine? Siku moja Mungu alitokea kwa Solomono, mwana wa Daudi, ndani ya ndoto, akasema naye, ***"Omba neno lo lote unalotaka mimi kukupa."*** Unajua kama Solomono alichagua nini? Tutasikia leo namna gani alijibu Mungu.

Ndani ya masomo sita tuliyomaliza sasa tu tulisoma habari za nabii wa Mungu, Daudi. Tulisoma nyingine za nyimbo alizoandika ndani ya kitabu cha **Zaburi**. Ndani ya somo tulilomaliza sasa tu tuliona ya kuwa Daudi alitabiri kwamba wana wa Adamu wataua Masiya kwa njia ya kutoboa mikono na miguu yake. Daudi alitabiri vilevile ya kwamba Mungu atafufua Masiya toka wafu. Leo tunakusudi kuacha habari za Daudi na kuendelea kwa habari za mwana wake **Solomono** [*Suliman* kwa Kiarabe]**.**

Ndani ya sura 2 ya kitabu cha kwanza cha Wafalme, Maandiko Matakatifu yanasema:

> (1 Wafalme 2) *1 Siku ya kufa kwa Daudi ilikaribia; naye aliagiza Solomono mwana wake, akisema: 2 Mimi ninakwenda njia ya watu wote wa dunia; basi uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume; 3 ushike maagizo ya Bwana Mungu wako,* ***kutembea katika njia zake, kushika amri zake na sheria zake . . . sawa ilivyoandikwa katika torati ya Musa, upate kusitawi katika yote unayofanya, na katika pahali pote unapogeuka****. 10 Basi Daudi alilala na baba zake, akazikwa katika mji wa Daudi. 11 Na siku Daudi alizotawala juu ya Israeli zilikuwa miaka makumi ine . . . 12 Basi Solomono alikaa katika kiti cha ufalme cha Daudi baba yake, na ufalme wake ulisimama imara sana.*

(1 Wafalme 3) *3 Solomono akapenda Bwana, akitembea katika amri za Daudi baba yake . . . 5 Bwana alitokea Solomono katika ndoto ya usiku; Mungu akasema:* ***Omba unalotaka nikupe****. 6 Na Solomono alisema: . . . 7 Ee Bwana, Mungu wangu, umeweka mtumwa wako awe mfalme pahali pa Daudi baba yangu; na mimi ni mtoto mdogo tu; sijui namna gani ya kutoka wala kuingia. . . 9* ***Kwa sababu hii, umpe mtumwa wako moyo wa akil****i nihukumu watu wako, nipate kutambua mema na mabaya; kwa maana ni nani anayeweza kuhukumu watu wako walio wengi? 10 Na* ***neno hili lilipendeza Bwana****, ya kuwa Solomono ameomba neno hili. 11 Naye Mungu alimwambia: Kwa sababu umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha ya siku nyingi, wala hukutaka utajiri kwa wewe mwenyewe, wala hukuomba kufa kwa adui zako, lakini uliomba akili kwa wewe mwenyewe, upate kujua kuhukumu; 12 tazama, nimefanya kama ulivyosema. Tazama, nimekupa moyo wa akili na ufahamu; hata mbele yako hakuwa mtu kama wewe, wala nyuma yako hatasimama mtu kama wewe. 13 Na mambo yale usiyoomba nimekupa vilevile, mali na heshima, hata hatakuwa mtu katikati ya wafalme kama wewe siku zako zote. 14 Na kama ukitembea katika njia zangu, kushika amri zangu na maagizo yangu, kama baba yako Daudi alivyokwenda, basi nitafanya siku zako kuwa nyingi. 15 Naye Solomono aliamka, na tazama, ilikuwa ndoto; naye alifikia Yerusalema, akasimama mbele ya sanduku la agano la Bwana, akatoa sadaka za kuteketezwa, akatoa sadaka za salama, akafanyia watumishi wake wote karamu.*

*16 Kisha wanawake wawili, makahaba, walikwendea mfalme, wakasimama mbele yake. 17 Kisha mwanamke mmoja akasema: Ee bwana wangu, mimi na mwanamke huyu tunakaa katika nyumba moja; nami nilizaa mtoto, wakati nilipokuwa pamoja naye nyumbani. 18 Kisha, siku ya tatu nyuma ya kuzaa kwangu, mwanamke huyu alizaa vilevile; na sisi tulikuwa pamoja; hakuna mgeni tena pamoja nasi katika nyumba, ila sisi wawili tu. 19 Na mtoto wa mwanamke huyu alikufa usiku, kwa kumlalia. 20 Akaamka kati ya usiku, akatwaa mtoto wangu ubavuni mwangu, wakati kijakazi wako alipolala usingizi, akamweka kwa kifua chake, na mtoto wake mfu aliweka katika kifua changu. 21 Wakati nilipoamka asubui kunyonyesha mtoto wangu, kumbe! amekufa. Lakini wakati asubui nilipomtazama sana, kumbe! si mtoto wangu ambaye nilimzaa. 22 Na mwanamke yule wa pili alisema: Sivyo, lakini mtoto wangu ndiye mwenye uhai, na mtoto wako ndiye aliyekufa. Na mwenzake alisema: Sivyo, lakini mtoto wako*

*ndiye aliyekufa, na mtoto wangu ndiye mwenye uhai. Hivyo wakabishana mbele ya mfalme.*

*23 Kisha mfalme alisema: Mmoja anasema: Mtoto huyu aliye hai ni wangu, naye aliyekufa ni mtoto wako. Na mwingine anasema: Sivyo; lakini mtoto aliyekufa ni wako, na mtoto aliye hai ni wangu. Naye mfalme alisema: 24 Muniletee upanga. Wakaleta upanga mbele ya mfalme. 25 Mfalme akasema: Kata mtoto aliye hai vipande viwili, mumpe huyu nusu na huyu nusu.*

*26 Pale mwanamke aliyekuwa mama ya mtoto aliye hai alimwambia mfalme, kwa sababu ndani yake aliona mtoto wake kwa huruma, akasema: Ee Bwana wangu, umpe huyu mtoto aliye hai, wala usiue mtoto kamwe. Lakini yule mwingine alisema: Asiwe wangu wala wako; akatwe. 27 Ndipo mfalme akajibu, akasema: Mumpe yule wa kwanza mtoto aliye hai, maana yeye ni mama yake. 28 Na Israeli wote walisikia habari za hukumu ile aliyohukumu mfalme;* ***wakaogopa mfalme; kwa maana waliona ya kuwa akili ya Mungu ilikuwa ndani yake ili afanye hukumu.***

(1 Wafalme 4) *29 Mungu alimpa Solomono hekima na akili nyingi sana, na moyo mwema, kama mchanga kwa pwani. 30* ***Akili ya Solomono ilipita*** *akili ya wana wote wa mashariki, na akili zote za Misri. 31 Kwa kuwa alikuwa na akili kuliko watu wote . . . sifa zake zikaenea kati ya mataifa yote pande zote. 32 Akasema mifano elfu tatu, na nyimbo zake zilikuwa elfu moja na tano. . . . 34 Na watu walikuja wa mataifa yote kusikia akili ya Solomono, toka wafalme wote wa dunia, waliopata habari za akili yake.*

Kisha Maandiko yanapasha ya kwamba kwa wakati ule malkia mmoja, **malkia ya Sheba,** alisikia habari za akili kubwa na enzi ya Solomono. Malkia alijitayarisha kwa safari kwenda Yerusalema kuonana na Solomono, na aweze kujua kama habari alizosikia juu yake zilikuwa **kweli.** Malkia huyu aliishi ndani ya inchi iliyokuwa mbali sana na Yerusalema, inchi ya Sheba, kwa kusini ya Saudi Arabia. Kwa wakati wa sasa inchi ya Sheba inaitwa Yemen. Ni karibu kilomètres elfu mbili toka Yerusalema. Lakini neno hili halikuzuiza malkia wa Sheba asiende kuonana na Solomono.

Ndani ya 1 Wafalme 10, Maandiko yanasema:

*1 Wakati malkia ya Sheba aliposikia habari za Solomono juu ya jina la Bwana, akakuja* ***kumjaribu kwa maulizo magumu****. 2 Akakuja Yerusalema na watumishi wengi sana, na ngamia waliobeba manukato, na zahabu nyingi sana na mawe madogo ya damani; na wakati*

> *alipofikia Solomono, alisemezana naye maneno yote yaliyokuwa moyoni mwake. 3 Na Solomono alimwelezea maulizo yake yote; wala halikuwa neno lililofichwa na mfalme, ambalo hakumwambia. 4 Na wakati malkia ya Sheba alipoona akili yote ya Solomono, na nyumba aliyojenga, 5 na chakula cha meza yake, na makao ya watumwa wake, na kazi ya watumishi wake, na mavazi yao, na wanyweshaji wake, na daraja yake ya kupandia hata nyumba ya Bwana, roho yake ilizimia.*
>
> *6 Naye alimwambia mfalme: Ilikuwa habari za kweli nilizosikia katika inchi yangu juu ya mambo yako, na ya akili yako. 7 Lakini sikusadiki habari hizi mpaka nilipokuja, na kuona kwa macho yangu; na* ***tazama, sikuambiwa nusu; akili yako na usitawi wako unazidi habari nilizosikia.*** *8 Wenye furaha watu wako, na wenye furaha watumishi wako hawa wanaosimama mbele yako siku zote, na kusikia akili yako. 9 Bwana, Mungu wako abarikiwe, aliyependezwa nawe, na kukuweka juu ya kiti cha ufalme cha Israeli; kwa sababu Bwana amependa Israeli milele, kwa sababu hii, amekufanya wewe kuwa mfalme, ufanye hukumu na haki."*

Inatupasa kuacha kusoma hapa kwa leo. Lakini huu si mwisho wa maneno ambayo Neno la Mungu linasema juu ya malkia ya Sheba. Zaidi ya miaka mia tisa nyuma ya wakati ule, Masiya alisema juu ya malkia ya Sheba na Mfalme Solomono: *"Malkia toka kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na kizazi hiki, naye atakihukumu; kwa sababu yeye alikuja toka miisho ya inchi kusikia akili ya Solomono; na* ***tazama, yeye aliye mkubwa kupita Solomono ni hapa.****"* (Matayo 12:42)

Ulisikia maneno Masiya aliyosema? Alisema ya kwamba **kwa njia ya kutafuta habari ya utukufu wa Solomono malkia ya Sheba atahukumu wote wanaokataa kutafuta utukufu wa Masiya.** Malkia ya Sheba aliweka roho kabisa kwa kuweza kuvumbua utukufu wa Solomono na kusikiliza masemo yake ya akili. Alifanya safari ndefu sana ya kilometres 4000 (kwenda na kurudi kwake), kujua kama maneno aliyosikia yalikuwa kweli! Habari hizi ni mafundisho makubwa kwa sisi. **Masiya**, aliyetoka mbinguni ana utukufu na akili na kujua na uwezo wingi kupita Solomono, lakini zaidi ya wanadamu **hawatambui** utukufu wake, na **hawataki kutafuta kujua** kama maneno haya ni kweli! Kwa sababu hii Masiya alisema: *"Malkia toka kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na kizazi hiki, naye atakihukumu; kwa sababu yeye alikuja toka miisho ya inchi kusikia akili ya Solomono; na tazama, yeye aliye mkubwa kupita Solomono ni hapa."* (Matayo 12:42)

Msomaji, **unatambua utukufu wa Masiya** aliyetumwa na Mungu? Au unafikili yeye ni kipimo kimoja na manabii tu? Unakumbuka maana ya neno hili *Masiya*? Ndiyo, ni *Yule aliyechaguliwa na Mungu*. Masiya ndiye aliyechaguliwa na Mungu kuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia. Hata hivi kufika leo zaidi ya watu hawafikili juu ya Masiya. Hawajui kama yeye ni nani kwa sababu hawakumtafuta kamwe ndani ya maandiko ya Manabii.

Mbele ya kumaliza somo hili, ni vizuri ufahamu ya kwamba Mfalme Solomono aliandika vitabu vitatu vingine vilivyo na mafundisho ya ndani ndani. Vitabu hivi ni *Mezali, Mhubiri,* na *Wimbo wa Solomono* navyo ni sehemu ya Maandiko Matakatifu. Kama baba yake Daudi, Solomono aliandika nyimbo vilevile zilizo ndani ya kitabu cha Zaburi. Kumaliza somo la leo, tunataka kusoma sura 72 ambayo Solomono aliandika ndani ya kitabu cha Zaburi. Ndani ya wimbo huu, **Solomono alitabiri ya kwamba Masiya atarudi duniani siku nyingine kuhukumu watu wote kwa haki.** Tusikilize maneno Mfalme Solomono aliyoandika juu ya Mfalme mkamilifu ambaye anampita ndani ya maneno yote.

Juu ya Masiya, Solomono aliandika ndani ya Zaburi 72:

> *2 Atahukumu watu wako kwa haki, na masikini zako kwa hukumu. 8 Atatawala toka bahari . . . hata miisho ya dunia. 9 Wao wanaokaa jangwani watainama mbele yake na adui zake wataramba mavumbi. 10 . . . wafalme wa Sheba na Seba [katika Arabia] watatoa zawadi. 11 Ndiyo,* ***wafalme wote wataanguka mbele yake,*** *mataifa yote watamtumikia. 17 Jina lake litadumu milele; jina lake litakuwa na wazao kwa wakati wote wa jua; watu wote watabarikiwa ndani yake; mataifa yote watamwita heri. 18 Heri ni Bwana Mungu, Mungu wa Israeli, anayetenda maneno ya ajabu sana; 19 na libarikiwe jina lake lenye utukufu kwa milele; dunia yote ijae na utukufu wake. Amina na Amina.*

Hivi Mfalme Solomono alitabiri ya kwamba siku moja watu wote wa dunia watanyenyekea Masiya, Mfalme wa wafalme na Mwamuzi wa dunia! Ndiyo, neno Mungu analotaka ni kwa sisi sote mmoja mmoja kumnyenyekea **sasa!** Basi wewe? Unanyenyekea Mungu kweli kweli? Unatambua utukufu na amri ya Masiya aliyetumwa na Mungu na atakayetumwa tena? Au unafikili juu yake kuwa kipimo kimoja na manabii? Kama ukiweka roho kutafuta Maandiko ya Manabii, utaona ya kwamba Masiya ni Mwokozi na Mwamuzi wa dunia; yule anayeshuhudiwa na manabii wote. Hili ndilo neno

Maandiko Matakatifu yanatangaza wakati yanaposema: *"Huyu manabii wote wanamshuhudia [Masiya] ya kwamba kwa jina lake kila mtu ambaye anamwamini atapewa usamehe wa zambi! . . .* ***Unaamini manabii?****"* (Matendo 10:43; 26:27)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, asante kwa kujifunza pamoja nasi. Mara ya nyuma, Mungu akitaka, tutasoma juu ya nabii wa Mungu, Elia, aliyeita moto kutoka mbinguni . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maneno Masiya aliyotangaza, akisema,

> ***"Malkia toka kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na kizazi hiki, naye atakihukumu; kwa sababu yeye alikuja toka miisho ya inchi kusikia akili ya Solomono; na tazama, yeye aliye mkubwa kupita Solomono ni hapa."*** (Matayo 12:42)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 53

# NABII ELIA

### 1 WAFALME 6-18

Salama kwako, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea pamoja ndani ya mfulizo *Njia ya Haki.*

Mara ya mbele, tulijifunza habari za Solomono, mwana wa nabii Daudi. Tuliona ya kwamba **Mungu alimpa hekima na ufahamu mkubwa sana**. Kwa wakati wa Mfalme Solomono, Yerusalema ulikuwa mji mzuri na wa mapambo kupita yote duniani. Lakini uzuri wa **Hekalu la Bwana Mungu** ambalo alijenga ulipita vitu vyote vingine. Solomono alijenga Hekalu kukomboa Hema ya Kusanyiko, ndiyo hema iliyosimamishwa na Musa na Waisraeli kwa ibada yao jangwani. Solomono alikuwa na watu wa kazi elfu mia mbili waliotumika kwa miaka saba kujenga pahali hapa pazuri pa kuabudu Bwana. Hata leo tunaweza kuona mawe makubwa ya msingi wa hekalu ambalo Solomono alijenga.

Wakati hekalu lilipokwisha makuhani walitoa sadaka ya **elfu za kondoo na ngombe kama mfano wa Mkombozi** atakayekuja na kumwanga damu yake ya damani kwa wenye zambi. Kwa njia hii waliweka kwa Mungu Hekalu ambalo walijenga kwa jina lake. Nyuma ya kutoa nyama wale na kuwateketeza juu ya mazabahu ya shaba hekaluni, makuhani walibeba sanduku ya agano (iliyokuwa ndani ya hema ya kusanyiko) na kuiweka ndani ya Patakatifu pa patakatifu ndani ya hekalu jipya. Wakati makuhani walipotoka Patakatifu pa patakatifu, mara moja utukufu wa Bwana ulijaza pahali pale. Kama utukufu wa Mungu ulivyojaza pahali patakatifu katika hema ya kuabudu Musa na Waisraeli waliyofanya jangwani, vivyo hivyo utukufu wa Mungu ulijaza Patakatifu pa patakatifu katika Hekalu ambalo Solomono alijenga katika Yerusalema.

Maandiko Matakatifu yanatupasha ya kwamba sehemu ya nyuma ya maisha ya Solomono haikuwa sawasawa na mwanzo yake. Sikiliza maneno yanayoandikwa ndani ya kitabu cha kwanza cha Wafalme, sura 11. Tunaona tena ya kwamba Neno takatifu la

Mungu halifichi zambi za manabii. Maandiko yanasema: *"Mfalme Solomono alipenda wanawake wageni wengi . . . Na ilikuwa wakati Solomono alipokuwa mzee, wanawake waligeuza moyo wake kufuata miungu mingine; na* ***moyo wake haukuwa mkamilifu kwa Bwana Mungu wake, kama moyo wa Daudi baba yake.****"* (1 Wafalme 11:1,4)

Halafu Solomono alijenga juu ya milima kwa upande wa mashariki wa Yerusalema pahali pa juu kwa wanawake wageni wake wote, waweze kuteketeza uvumba na kutoa sadaka kwa miungu yao. Wakati alipofanya hivi, Mungu alimkasirikia kwani Solomono alikuwa ameacha Neno la Mungu wa kweli aliye hai. Halafu Mungu alisema na Solomono,

> ***"Kwa sababu umefanya mambo haya,*** *nawe hukushika maagano yangu, na sheria zangu ambazo nilikuamuru,* ***hakika nitanyanganya ufalme usiwe wako****, nami nitampa mtumishi wako. Lakini sitaifanya katika siku zako, kwa ajili ya Daudi baba yako; lakini nitaunyanganya toka mkono wa mwana wako. Lakini sitaondoa ufalme wote; nitampa mwana wako kabila moja, kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu, na kwa ajili ya Yerusalema, ambao niliuchagua."* (1 Wafalme 11:11-13)

Maandiko yanatupasha ya kwamba nyuma ya mauti ya Solomono makabila ya Israeli waligombana na kupigana katikati yao. Makabila kumi na mawili yaliyotoka kwa wana wa Yakobo **yaligeuka mafungu mawili**, kama Mungu alivyosema na Solomono mbele. Hawakuwa taifa moja tena; waligeuka mataifa mawili, **Israeli na Yuda**. Makabila kumi ya Israeli kwa upande wa kaskazini waligeuka ufalme wa Israeli. Kabila la Yuda pamoja na kabila dogo la Benyamina waligeuka ufalme wa Yuda. Mfalme Daudi alikuwa mtu wa kabila la **Yuda**, na Mungu alikuwa ameahidi kuleta **Masiya** duniani kwa njia ya wazao wake.

Maandiko yanapasha ya kwamba mataifa haya mawili yalikuwa na wafalme wengi. Zaidi ya wafalme wa Israeli na Yuda walikuwa viongozi waovu; waliachana na Bwana na walifuata dini za mataifa ambayo yaliwazunguka. Katikati ya wafalme wote wa Israeli mmoja alikuwa mwovu kupita wao wote. Unajua kama alikuwa nani? Alikuwa **Mfalme Ahaba**. Ahaba alikuwa mfalme wa nane nyuma ya Solomono.

Juu ya Ahaba, Maandiko yanasema: *"Ahaba mwana wa Omuri alifanya yaliyo mabaya kwa macho ya Bwana kuliko wote ambao walimtangulia."* (1 Wafalme 16:30) Alioa **Yezebeli** vilevile, mwanamke

aliyekataa neno la Bwana. Zaidi ya ile Ahaba alijenga hekalu katika Israeli kwa jina la **Bali**, uliohesabiwa kama Mungu na mataifa kando kando. Hivi Ahaba alikasirisha Bwana sana kwa njia ya kuongoza Waisraeli kushika dini ya uwongo, dini bule, na manabii wake wa uwongo.

Lakini, kwa wakati ule kulikuwa na mtu mmoja katika Israeli aliyetembea pamoja na Mungu. Jina lake lilikuwa **Elia**. Siku moja, Mungu alituma Elia karibu na Mfalme Ahaba. *"Elia . . . akasema na Ahaba, "Kama Bwana, Mungu wa Israeli anavyoishi, na mbele yake ninasimama, hautakuwa umande wala mvua kunyesha miaka hii, ila kwa neno langu."* (1 Wafalme 17:1)

Hivi, kwa miaka mitatu na nusu mvua haikunyesha juu ya inchi ya Israeli. Kulikuwa na njaa kali katika inchi nzima. Ndani ya sura 18 Maandiko yanasema:

> *1 Na ilikuwa nyuma ya siku nyingi neno la Bwana lilikuja kwa Elia, katika mwaka wa tatu, kusema: Kwenda, ujionyeshe kwa Ahaba; nami nitanyesha mvua juu ya inchi. 2 Basi, Elia akakwenda ili ajionyeshe kwa Ahaba. . . 17 Wakati Ahaba alipoona Elia, Ahaba alimwambia: Ni wewe mwenye kutaabisha Israeli? 18 Naye alijibu: Si mimi mwenye kutaabisha Israeli, lakini ni wewe, na nyumba ya baba yako, kwa sababu umeacha amri za Bwana, nawe umefuata Bali. 19* ***Basi sasa, tuma na kunikusanyia Israeli wote katika mlima wa Karmeli,*** *na wale manabii wa Bali mia ine na makumi tano, na wale manabii wa Ashera mia ine, wenye kula chakula kwa meza ya Yezebeli.*
>
> *20 Basi, Ahaba akatuma kwa wana wa Israeli wote, akakusanya manabii pamoja hata mlima wa Karmeli. 21 Naye Elia alikaribia watu wote, akasema: Hata wakati gani mutasitasita katikati ya mawazo wawili?* ***Kama Bwana ni Mungu, mumfuate; lakini kama Bali ni Mungu, basi mumfuate yeye!*** *Nao watu hawakumjibu neno. 22 Kisha Elia aliwaambia watu: mimi nimebaki mimi peke yangu, nabii wa Bwana; lakini manabii wa Bali ni watu mia ine makumi tano. 23 Kwa sababu hii tupewe* ***ngombe wawili****, wao wajichagulie ngombe mmoja, wamkate vipande vipande, na kumweka juu ya kuni, lakini wasitie moto chini, nami nitatengeneza ngombe ya pili, na kumweka juu ya kuni wala sitatia moto chini. 24 Nanyi ombeni kwa jina la mungu wenu, nami nitaomba kwa jina la Bwana; na* ***Mungu yule anayejibu kwa moto, yeye ndiye Mungu.*** *Na watu wote walijibu, wakasema: Maneno haya ni mazuri.*
>
> *25 Naye Elia aliwaambia* ***manabii wa Bali****: Mujichague*

*ngombe mmoja, na kumtengeneza kwanza, kwa kuwa ninyi ni wengi; na mwitie jina la mungu wenu, lakini musitie moto chini. 26 Wakatwaa yule ngombe ambaye walipewa, wakamtengeneza, wakaitia jina la Bali tangu asubui hata azuhuri, wakisema: Ee Bali, utusikie. Lakini sauti haikuwa, wala mwenye kujibu. Nao walirukaruka juu ya mazabahu waliyofanya.*

*27 Na ilikuwa, wakati wa azuhuri, Elia aliwazihaki, akasema: Pazeni sauti zaidi; kwa maana yeye ni mungu; hakose amelala, lazima aamshwe. 28 Wakapaza sauti sana, wakajikata kwa visu na viwembe kama desturi yao, mpaka damu iliwatoka kwa nguvu. 29 Na ilikuwa wakati wa azuhuri ulipopita, walitabiri hata saa ya kutoa sadaka ya mangaribi, lakini sauti haikuwa wala mwenye kujibu, wala mwenye kuangalia.*

*30* ***Kisha Elia*** *aliwaambia watu wote: Munikaribie mimi; watu wote wakamkaribia. Akatengeneza mazabahu ya Bwana iliyobomolewa. 31 Elia akatwaa mawe kumi na mawili kama hesabu ya makabila ya wana wa Yakobo, kwake neno la Bwana lilimfikia, kusema: Jina lako litakuwa Israeli. 32 Naye alijenga mazabahu kwa mawe haya katika jina la Bwana; akachimba mfereji, kama wa vipimo viwili vya mbegu, ukizunguka mazabahu. 33 Kisha akatandika kuni, akakata yule ngombe vipande vipande, akamweka juu ya kuni. Naye alisema: Jazeni mapipa mane maji, na kuyamwanga juu ya sadaka ya kuteketezwa, na juu ya kuni.*

*34 Akasema: Fanyeni mara ya pili. Wakafanya mara ya pili. Akasema: Fanyeni mara ya tatu. Wakafanya mara ya tatu. 35 Na maji yalitelemuka pembeni ya mazabahu; akajaza mfereji maji vilevile.*

*36 Na ilikuwa wakati wa kutoa sadaka ya mangaribi, Elia nabii alikaribia, akasema: Ee Bwana, Mungu wa Abrahamu, wa Isaka, wa Israeli, ijulikane leo ya kuwa wewe ni Mungu wa Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako. 37 Unisikie, Ee Bwana, unisikie kusudi* ***watu hawa wapate kujua ya kuwa wewe, Bwana, ni Mungu, na ya kuwa wewe umegeuza mioyo yao wakurudie.***

*38 Pale pale moto wa Bwana ulishuka, ukateketeza sadaka ya kuteketezwa, na kuni, na mawe, na mavumbi, ukaramba maji yaliyokuwa ndani ya mfereji. 39 Na wakati watu wote walipoona, wakaanguka kifudifudi, wakasema:* ***Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu.***

*40 Na Elia aliwaambia: Kamateni manabii wa Bali, musiache*

> *hata mmoja kukimbia. Wakawakamata; na Elia aliwatelemusha hata kijito cha Kisoni, akawaua kule. Naye Elia alimwambia Ahaba: Panda, kula, kunywa; kwa sababu kuna sauti ya mvua tele. 42 Basi, Ahaba alipanda ili kula na kunywa. Elia akapanda hata juu ya Karmeli; akainama kifudifudi na kuweka uso wake kati ya magoti. . . 45 Na ilikuwa muda kidogo tu, mbingu zilikuwa nyeusi kwa mawingu na upepo, ikanyesha mvua kubwa sana.*

Habari hizi zinajaa utukufu na uwezo wa Mungu na hazihitaji kwa sisi kusema maneno mengine juu yao. Lakini, mbele ya kuagana nanyi, inatupasa kuwaza juu ya maneno nabii Elia aliyosema na watu wa Israeli. Mbele ya kusema na manabii mia ine na makumi tano wa uwongo wa Bali, Elia alisema na watu, ***"Hata wakati gani mutasitasita katikati ya mawazo mawili? Kama Bwana ni Mungu, mumfuate; lakini kama Bali ni Mungu, basi mumfuate yeye!"***

Waisraeli hawakujibu mara moja. Lakini wakati walipoona namna Bwana Mungu alivyojibu maombi ya Elia na kufanyiza moto kushukia mazabahu yake toka mbingu, makutano mazima wakaanguka kifudifudi, wakalalamika, ***"Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu."*** Hivi, ndani ya muda wa siku moja tu, nabii wa Mungu, Elia, alionyesha na kufunua ubaya wa manabii wa uwongo wa Bali mbele ya watu wote na kugeuza mioyo ya Waisraeli kurudia Mungu wao!

**Kwa nini Mungu alijibu maombi ya Elia?** Kwa sababu Elia alipenda Bwana Mungu na kuamini Neno lake. **Kwa nini Mungu aliona maombi ya manabii wa Bali bule?** Kwa sababu hawakuomba kwa Mungu mmoja wa kweli ambaye alijifunua kwa Abrahamu, Isaka, na taifa la Israeli. Manabii wa Bali waliona Neno la Mungu bule na walifuata desturi zao za dini na bidii lakini hawakutumikia Mungu aliye hai—kwa sababu hii bidii yao kwa maneno ya dini ilikuwa bila maana. Walikuwa kama watu kumi ndani ya mezali waliochimba shimo kwenda chini sana, na watu wengine kumi ambao waliijaza tena—kulikuwa na mavumbi mengi, lakini hakuna shimo! Vivyo hivyo manabii wa Bali waliweka roho sana juu ya dini yao, walifanya makelele mengi pamoja na maombi na sadaka zao, lakini yalikuwa yote bule—kwa sababu msingi wao haukuwa Neno la Mungu aliye hai. "Mavumbi mengi, lakini hakuna shimo!"

Hivi kwa siku ile kubwa sana, Elia aliagiza Waisraeli kuchagua, au:

> **Bwana Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo,**
> *au* **dini isiyokuwa na maana ya Bali;**
>
> **Kweli** *au* **uwongo;**

**Njia ya haki** *au* **njia ya uzalimu;**

**Neno aminifu la Mungu** *au* **maneno yasiyo maaminifu ya dini ya watu.**

Wewe ungejibu nini kwa ulizo la Elia: ***"Hata wakati gani mutasitasita katikati ya mawazo mawili?"*** Hata wakati gani mutasitasita katikati ya Neno la kweli la Mungu na desturi bule za watu? Maandiko yanasema: *"**Hakuna mtu anayeweza kutumikia bwana wawili;** kwa maana atachukia mmoja, na kupenda mwingine; au atashikamana na mmoja, na kuzarau mwingine. Hamuwezi kutumikia Mungu na mali."* (Matayo 6:24) Huwezi kuchanganya kutumikia Bwana Mungu na kutumikia dini bule ya watu. ***"Hata wakati gani mutasitasita katikati ya mawazo mawili?"***

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kusoma pamoja nasi. Mara ya nyuma tutaangalia habari za nabii mmoja aliyeshinda siku tatu ndani ya samaki mkubwa. Unajua jina la nabii huyu? Kutana nasi mara ya nyuma kwa kusikiliza habari zake za ajabu . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kufikili juu ya ulizo la Elia kwa Waisraeli:

> ***"Hata wakati gani mutasitasita katikati ya mawazo mawili? Kama Bwana ni Mungu, mumfuate!"*** (1 Wafalme 18:21).
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 54

# Nabii Yona

## Yona

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ameitayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele, tulijifunza habari za nabii wa Mungu, **Elia**. Elia alikuwa nabii mkubwa kwa sababu Roho ya Mungu alikuwa juu yake. Aliomba Mungu asiache mvua kunyesha na mvua haikunyesha katika inchi ya Israeli kwa miaka mitatu na nusu. Vilevile, Elia alishindana na manabii wa uwongo wa Bali na kuonyesha ubaya wa dini yao ya uwongo mbele ya Waisraeli wote. Hivi Mungu alitumika na nabii Elia kurudisha mioyo ya Waisraeli karibu na Bwana Mungu wao.

Halafu leo tunataka kuwaza juu ya habari za nabii mwingine aliyeishi nyuma ya Elia. Tutaona ya kwamba Mungu alichagua Mwisraeli, jina lake **Yona** (Yunus kwa Kiarabe) na kumwagiza **kwenda kuhubiri kwa watu wa inchi nyingine** waliokuwa adui za Waisraeli.

Tunasoma ndani ya kitabu cha Yona, ndani ya sura ya kwanza. Maandiko yanasema: (Yona 1) *1 Neno la Bwana lilikuja kwa Yona, mwana wa Amitai, likisema: 2 **Simama** uende kwa Ninawe, mji mkubwa, ulie juu yake, kwa maana maovu yao yamepanda mbele yangu."*

Ulisikia neno Bwana aliloagiza Yona? Mungu alimwagiza kwenda na kuonya watu wa mji wa Ninawe kutubu zambi zao—hata kama Ninawe ulikuwa mji mkubwa wa taifa la Asuria na Waasuria walikuwa watu waovu sana waliotaka kuharibu Waisraeli!

Kwa nini Bwana Mungu alitaka kutuma Yona kwa wageni wale waliozarau na kuchukia Waisraeli? Mungu alipenda adui za Waisraeli vilevile? Ndiyo! Mungu alikuwa karibu kuhukumu watu

wa Ninawe kwa sababu maovu yao yamepanda mbinguni. Lakini **Mungu hapendi kuharibu wenye zambi.** Mungu anataka kila mtu kutubu zambi zake, kuamini Neno la Mungu na kuokolewa. **Kwa sababu hii Bwana aliagiza Yona kwenda** kwa watu wa Ninawe na kuwaonya ili watubu zambi zao, wageuke kwa Mungu na kuponyeshwa.

Lakini Yona **hakutaka kwenda** na kuonya adui zake! Hakutaka kuwa nabii kwa mji wa Ninawe! Mungu alitaka watu wa Ninawe kutubu ili aweze kuwahurumia, lakini Yona alitaka Mungu kuwaazibu! Hivi Yona alikataa kwenda, akajaribu kukimbia Bwana Mungu. Basi aliweza kukimbia wapi mbali na Mungu?

Tuendelee na kuona kama Yona alifanya nini. Maandiko yanasema:

> (Yona 1) *3 **Yona akasimama kukimbia** hata Tarsisi toka uso wa Bwana; akashuka hata Yofa, akakuta merikebu ikikwenda Tarsisi, akalipa bei yake, akashuka ndani yake kwenda pamoja nao kwa Tarsisi toka uso wa Bwana.* [Tarsisi ni mbali sana na Ninawe.] *4 Lakini **Bwana akatuma pepo nyingi** baharini, na ilikuwa tufani kubwa baharini hata merikebu ilikuwa karibu na kuvunjika. 5 Nao wabaharia waliogopa, wakalia kila mtu kwa mungu wake; wakatupa baharini vyombo vilivyokuwa katika merikebu ipate kuwa nyepesi kwao. Lakini Yona alikuwa ameshuka mbavuni mwa merikebu; akalala na alikuwa na usingizi. 6 Basi kapiteni akakuja kwake, akamwambia: Una nini, Ee mtu unayelala usingizi? Amka, uombe Mungu wako, labda Mungu atatufikili hata tusipotee. 7 Wakasemezana kila mtu na mwenzake: Kujeni tupige kura, tujue kwa sababu ya nani ubaya huu ni juu yetu. Hivi wakapiga kura, kura ikaangukia Yona.*
>
> *8 Halafu wakamwambia: Utuambie, tunakuomba, kwa sababu ya nani ubaya huu ni juu yetu; kazi yako nini? Na unatoka wapi? inchi yako wapi? nawe ni mtu wa kabila gani? 9 Akawaambia: Mwebrania mimi, na ninaogopa Bwana, Mungu wa mbingu, aliyeumba bahari na inchi kavu. 10 Halafu watu wakaogopa sana, wakamwambia: Kwa sababu gani umefanya hili? Kwa maana watu wakajua ya kuwa amekimbia toka uso wa Bwana, kwa sababu aliwaambia.*
>
> *11 Kisha wakamwambia: Tutakufanyia nini, bahari iwe kimya kwetu? Kwa maana bahari ilizidi kuchafuka. 12 Akawaambia: Munitwae na kunitupa katika bahari; hivi bahari itakuwa kimya kwenu; kwa maana ninajua ya kwamba kwa sababu yangu tufani kubwa hii ni juu yenu. 13 Hata hivi watu wakavuta sana wapate*

> *kufika tena kwa pwani; lakini hawakuweza; kwa sababu bahari ikazidi kuchafuka juu yao.*
>
> *14 Kwa sababu hii wakalia kwa Bwana, wakisema: Tunakusihi, Ee Bwana, tunakusihi tusipotee kwa sababu ya uzima wa mtu huyu, wala usitie juu yetu damu safi; kwa maana wewe, Ee Bwana, umefanya sawasawa ilivyokupendeza. 15 Hivi wakatwaa Yona, wakamtupa katika bahari; bahari ikaacha kuchafuka kwake. 16 Ndipo watu wakaogopa Bwana sana. Wakatoa zabihu kwa Bwana, wakaapa viapo. 17* ***Bwana akatayarisha samaki mkubwa*** *kumeza Yona; na Yona alikuwa tumboni mwa samaki siku tatu, mchana na usiku.*

Tuache hapa. Kufika sasa, tunaona namna Mungu alivyofuata Yona, nabii ambaye alijaribu kumkimbia. Yona aliweza kukimbia, lakini hakuweza kuponyokia Mungu. Kwa nini Mungu aliwinda Yona? Mungu aliwinda Yona kwa sababu alimpenda na alitaka Yona kufanya mapenzi yake. Kwa sababu hii Mungu alituma samaki mkubwa sana kumeza Yona bila kumwua.

Taabu kabisa kwa Yona! Sasa alikuwa ndani ya tumbo la samaki mkubwa! Yona ataweza kufanya nini kujiokoa? Hakuna kitu! Hakuna neno ila kuitia Bwana Mungu. Mungu tu aliweza kumwokoa. Ndani ya sura 2, Maandiko yanapasha namna Yona alivyoomba kwa Bwana toka ndani ya samaki na kukiri zambi yake, zambi ya kukataa kutii Mungu. Kwa siku tatu Mungu alilinda Yona ndani ya samaki kufika wakati Yona alipofahamu ya kwamba kutii Mungu ni vizuri kupita kumkimbia. Kweli Yona alijifunza neno kubwa sana! Siku ya tatu alilia, ***"Wokovu unatoka kwa Bwana!"*** (Yona 2:9) Wakati Yona aliposema: *"Wokovu unatoka kwa Bwana,"* tunasoma katika Maandiko ya kwamba, *"Bwana alisema kwa samaki, akatapika Yona juu ya pwani."* (Yona 2:10)

Ndani ya sura 3, Maandiko yanaendelea kuanza na shairi 1:

> (Yona 3) *Na neno la Bwana lilikuja kwa Yona, mara ya pili, likisema: 2* ***Simama*** *uendele kwa Ninawe, mji mkubwa ule, uuhubiri habari ambayo ninakuambia. 3 Hivi* ***Yona akasimama, akakwenda kwa Ninawe****, sawasawa na neno la Bwana. Basi Ninawe ulikuwa mji mkubwa sana, wa safari ya siku tatu. 4 Yona akaanza kuingia mjini kwa safari ya siku moja, akalia, akasema: Bado siku makumi ine na Ninawe utaangamizwa.*
>
> *5* ***Watu wa Ninawe wakaamini Mungu;*** *wakatangaza kufunga chakula, wakavaa gunia, toka mkubwa hata mdogo sana katikati yao. 6 Habari zikafika kwa mfalme wa Ninawe, akasimama toka kiti*

> *chake cha ufalme, akaondosha mavazi yake juu yake, akavaa gunia, akakaa katika majivu. 7 Akafanya tangazo, akawaambia katika Ninawe kwa amri ya mfalme na wakubwa wake akisema: Wala mtu wala nyama, wala ngombe wala mbuzi wasionje kitu; wasile chakula wala wasinywe maji, 8 lakini watu wavae gunia, watu na nyama, na walie na nguvu kwa Mungu; ndiyo, wageuke kila mtu toka njia yake mbaya, na toka ukali ulio mkononi mwao. 9 Nani anayejua ya kama Mungu hatageuka na kujuta, na kuacha kasirani yake kali, tusipotee? 10* ***Mungu akaona matendo yao, ya kama wakageuka toka njia yao mbaya; Mungu akajuta mabaya ambayo aliyasema atawafanyia, wala hakuyafanya.***

Hivi tunaona ya kwamba **Mungu alihurumia** watu wa Ninawe, kwa sababu waliamini neno alilotuma kwao. Waninawe walitubu zambi zao na roho za kuvunjika, wakageuka kwa Bwana. **Lakini Yona hakufurahi** kwa sababu Mungu alirehemu watu wa Ninawe. Sikiliza maneno yanayoandikwa ndani ya sura ya 4, ndiyo sura ya mwisho ya kitabu cha Yona.

Maandiko yanasema ndani ya sura 4, kuanza na shairi 1,

> (Yona 4) *1* ***Lakini Yona aliona uchungu*** *sana; akakasirika. 2 Akaomba Bwana, akisema: Ninakuomba, Ee Bwana, si hili nililosema wakati nilipokuwa katika inchi yangu? Kwa sababu hii nilifanya mbio kukimbia hata Tarsisi; kwa sababu nilijua ya kuwa wewe ni Mungu wa neema, ukijaa na huruma, si mwepesi wa kukasirika, na wa rehema nyingi, ukijuta mabaya. 3 Kwa sababu hii sasa, Ee Bwana, ondosha kwangu, ninakusihi, maisha yangu, kwa maana ni vema kwangu kufa kuliko kuishi. 4 Bwana akasema: Unafanya vizuri kukasirika?*
>
> *5 Kisha Yona akatoka mjini, akakaa kwa upande wa mashariki wa mji, akajifanyia kibanda kule, akakaa chini yake kwa kivuli hata aone nini itakayotokea juu ya mji. 6 Bwana Mungu akatengeneza boga, akaiotesha juu ya Yona iwe kivuli kwa kichwa chake kwa kumponyesha toka huzuni yake. Basi Yona akafurahi sana kwa sababu ya boga. 7 Lakini Mungu akatengeneza mdudu wakati wa asubui kesho yake; akapiga boga, ikakauka. 8 Na ilikuwa wakati jua lilipotoka, Mungu akatengeneza pepo za mashariki nyingi; jua likapiga kichwa cha Yona hata akazima roho, akajiombea afe, akasema: Ni vema kwangu kufa kuliko kuishi. 9 Mungu akamwambia Yona: Unafanya vizuri kukasirika kwa sababu ya boga? Akasema: Ninafanya vizuri kukasirika hata kufa. 10 Bwana akasema: Umehurumia boga usiyotumikia wala*

> *usiyootesha; iliyoota usiku na iliyopotea usiku; 11 nami nisihurumie Ninawe, mji ule mkubwa; ndani yake ni watu wengi zaidi ya elfu mia na makumi mbili wasiotambua mkono wao wa kuume wala mkono wao wa kushoto; na ngombe wengi vilevile?* Huu ndio mwisho wa kitabu cha Yona.

Tunaweza kujifunza maneno mengi juu ya tabia ya mtu na tabia ya Mungu ndani ya habari za nabii Yona. Neno moja linaonekana wazi kabisa: **Mungu haonyeshi tofauti kwa mtu fulani.** Yona alikuwa na upendeleo kwa Waisraeli, lakini Mungu hakuonyesha upendeleo. **Moyo wa Mungu ulikuwa namna nyingine kabisa na ule wa Yona.**

**Moyo wa Yona** ulijaa upendeleo, lakini **moyo wa Mungu** unajaa mapendo na rehema kwa watu wote. Yona alipenda watu wake mwenyewe na kuchukia adui zake, lakini Mungu alipenda Waisraeli na watu wa Ninawe. Yona alitaka watu wa Ninawe **kuangamia** kwa sababu walikuwa adui wa Israeli, lakini Mungu alitaka **watubu** zambi zao, kupokea neno lake na kuokolewa. **Mungu hana tofauti**. Si neno kama wewe ni nani, kama wewe ni mtu wa namna gani, **Mungu anakupenda.** Hapendi zambi na uasi wako, lakini anakupenda wewe. **Mungu anapenda kila mtu ndani ya kila taifa** na anataka kila mtu kukiri zambi zake mbele yake, kusikia Kweli, kuifahamu, kuiamini, na kuokolewa.

Watu wengine wanafikili ya kwamba Mungu haweki roho juu ya kila mtu duniani, ya kwamba alichagua (siyo na sheria wala kanuni) watu wengine kuteketezwa katika ziwa la hadeze na wengine kufurahi katika paradiso. Hata kama ni kweli ya kwamba zaidi ya watu watakufa ndani ya zambi zao na kuhukumiwa kwa sababu ya gazabu ya haki ya Mungu, haifai kwetu kufikili ya kwamba Mungu haweki roho juu ya wale wanaoangamia kwa sababu ya ujinga. Maandiko Matakatifu yanatupasha ya kwamba Mungu ***"anataka watu wote waokolewe na kupata kujua sana yaliyo kweli."*** (1 Timoteo 2:4) Bwana *"hataki mtu mmoja kupotea, lakini wote* ***wafike kutubu****."* (2 Petro 3:9) Lakini wale wanaokataa kutubu watahukumiwa na Mungu kwa sababu ***"hawakupokea mapendo kwa kweli, wapate kuokolewa*** *. . . wahukumiwe wote wasioamini kweli, lakini walifurahi katika uzalimu."* (2 Watesalonika 2:10,12) Haya ndiyo maneno ambayo Maandiko ya Bwana Mungu yanatujulisha. **Mungu ni mwema na mwenye rehema** na ametayarisha njia kwa wokovu wa kila mtu. Lakini **Mungu ni mtakatifu na mwenye haki** vilevile na atahukumu kila mtu asiyepokea njia yake ya haki kupata wokovu.

Rafiki, usiache mtu kukudanganya. Mungu haonyeshi upendeleo, naye hafurahi kuangamiza wenye zambi. **Mungu anataka kila mtu duniani kujua kweli, kuiamini na kuokolewa!** Kwa sababu hii Mungu aliongoza manabii zamani kuandika Neno lake ili tuweze **kujua** njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha, kui**pokea** na ku**okolewa!** Mtu ye yote anayepokea njia ya wokovu ya Mungu atakwenda mbinguni. Mtu ye yote ambaye anaikataa au kutoitunza, ataharibiwa! Mungu hana upendeleo kwa watu. Kama ilivyoandikwa, Mungu *"anataka watu wote waokolewe! . . . Lakini ninyi musipotubu mutaangamia wote!"* (1 Timoteo 2:4; Luka 13:3)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma tutajifunza juu ya nabii mkubwa aliyetabiri maneno mengi sana juu ya Mkombozi atakayekuja duniani kuokoa wenye zambi. Nabii yule mkubwa ni Isaya, nabii wa Mungu aliyeishi miaka mia saba mbele ya kufika kwa Masiya duniani.

Mungu akubariki wakati unapokumbuka maneno mawili ambayo Mungu alijaribu kufundisha nabii wake asiyekuwa mwaminifu, ndiye Yona:

1) *"**Wokovu unatoka kwa Bwana!**"* (Yona 2:9)

2) ***"Mungu hana upendeleo kwa mtu!"*** (Matendo 10:34)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 55

# Nabii Isaya

### Isaya

Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele, tulijifunza habari za nabii Yona aliyejaribu kukimbia Bwana. Lakini, kujaribu kukimbia Mungu ni kama kujaribu kukimbia kivuli chako mwenyewe. Mungu alikaa pamoja na Yona saa zote, hata ndani ya samaki mkubwa!

Leo tunataka kusoma juu ya nabii aliyeishi nyuma ya wakati wa Yona. Jina lake linajulikana sana ndani ya Maandiko Matakatifu. Ni **nabii Isaya** aliyeishi miaka mia saba mbele ya wakati Masiya alipozaliwa. Isaya alikuwa kuhani aliyetumikia Mungu ndani ya hekalu ambalo Solomono alijenga katika Yerusalema. Kila siku ilipasa Isaya na makuhani wengine kutolea Mungu sadaka za nyama juu ya mazabahu. Sadaka hizi zilikuwa mfano wa Masiya atakayemwanga damu yake kwa zambi za dunia.

Sikiliza neno lililopata Isaya siku alipotoa sadaka ndani ya hekalu la Bwana. Ndani ya kitabu cha Isaya, sura 6, Isaya aliandika:

> (Isaya 6) *1 Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia,* ***niliona Bwana akikaa juu ya kiti cha ufalme, juu na kunanyuliwa;*** *na pindo za nguo zake zilijaza hekalu. 2 Maserafi walisimama juu yake: kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka. 3 Na mmoja akaitana na mwingine, wakisema:* ***Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana wa majeshi; dunia nzima imejaa utukufu wake.*** *4 Na misingi ya visingiti vya milango ilitetemeka kwa sababu ya sauti ya mwenye kulia, na nyumba ilijaa moshi. 5 Na nilisema:* ***Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu***

> ***mwenye midomo michafu, na ninakaa katikati ya watu wenye midomo michafu; kwa sababu macho yangu yameona Mfalme, Bwana wa majeshi.*** *6 Kisha mmoja wa maserafi akaruka kwangu, na alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, aliotwaa na makoleo; toka juu ya mazabahu; 7 akagusa kinywa changu nalo, akisema, Tazama, hili limegusa midomo yako; na uovu wako umeondolewa, na zambi yako imesamehewa. 8 Kisha nilisikia sauti ya Bwana akisema: Mimi nitatuma nani, na nani atakayekwenda kwa sisi? Nikasema: Mimi hapa; unitume mimi."*

Hivi Bwana Mungu alifunua utukufu wake kwa Isaya na kumwita kutangaza Neno lake kwa Waisraeli, ndio Wayuda, na kuliandika ndani ya kitabu kwa vizazi watakaozaliwa nyuma. Kitabu cha Isaya ni kirefu na mafundisho yake ni ndani ndani. Hatuna saa kuangalia maneno yote yaliyo ndani. Lakini tunaweza kujumlisha habari kubwa za Isaya hivi:

**1)** Isaya aliwaambia Wayuda **habari mbaya** juu ya zambi zao na azabu ambayo walistahili kupata.

**2)** Isaya aliwatangazia **Habari Njema** juu ya Masiya atakayekuja duniani kubeba azabu kwa zambi zao.

Tusome kwanza mashairi machache yanayoonyesha **habari mbaya** Mungu alizojulisha Isaya ili aweze kuzitangaza kwa Wayuda na kwa mtu ye yote aliyekuwa na masikio kwa kusikia. Katika sura ya kwanza, nabii Isaya aliandika:

> (Isaya 1) *2* ***Sikieni, Ee mbingu, na sikiliza, Ee dunia, kwa maana Bwana amesema:*** *Nimekulisha watoto na kuwalea, nao wamehuni kwangu. 3 Ngombe anajua bwana wake, na punda anajua pahali pa kulisha pa bwana wake; lakini Israeli hajui, watu wangu hawafikili. 4 Aa, taifa la zambi, watu waliokuwa wazito na uovu, kizazi cha wafanya mabaya, watoto wanaofanya kwa uharibifu: wameacha Bwana, wamezarau Mwenye Utakatifu wa Israeli, wamerudia nyuma.* ***13 Musilete tena zabihu za bule; uvumba unanichukiza; kuandama mwezi na sabato, kuita makusanyiko; sivumilii uovu na makutano ya dini. 14 Siku zenu za kuandama mwezi na karamu zenu za mwaka, roho yangu inazichukia; maneno haya yanakuwa kwangu mzigo; ninachoka kuyachukua. 15 Na wakati munaponyanyua mikono yenu, nitaficha macho yangu kwenu; hata wakati munapoombaomba sana, sitasikia."***

Hii ndiyo namna nabii Isaya alivyokemea Wayuda kwa sababu ya udanganyifu wao. Alijumlisha zambi yao hivi: ***"Bwana anasema: 'Watu hawa wananikaribia na vinywa vyao, na wananiheshimu na midomo yao, lakini mioyo yao ni mbali nami. Wananiabudu bule, wakifundisha yaliyo maagizo ya watu.'"*** (Matayo 15:8; Isaya 29:13)

Nyuma ya kukemea Wayuda kwa ukaidi na uovu wao, alianza kuwaambia **Habari Njema,** iliyo na uwezo kusafisha mioyo ya wote ambao wanaiamini. Ndani ya saa inayobaki, tusome mengine ya maneno ya ajabu Isaya aliyoandika juu ya Masiya atakayekuja duniani kuokoa wenye zambi. Aliandika:

> ***"Kujeni, na tufanye shauri pamoja, Bwana anasema, hata zambi zenu ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kabisa, kama theluji; hata ni nyekundu kama nyekundu ya damu zitakuwa kama manyoya ya kondoo."*** (Isaya 1:18)
>
> (Isaya 40) *1 Mufariji mufariji watu wangu, Mungu wenu anasema. . . 3 Sauti ya mtu anayelia katika jangwa,* ***Tengenezeni njia ya Bwana****, nyosheni mapito katika jangwa kwa Mungu wetu! 4 Kila bonde litanyanyuliwa, na kila mlima na kilima kitashushwa; njia zinazokunjama zitanyoshwa na pahali pa kuparuza patafanywa sawa. 5 Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, na wote wenye mwili watauona pamoja; kwa kuwa kinywa cha Bwana kimesema maneno haya. . . 9 Ee Sayuni, wewe unayehubiri habari njema, panda juu ya mlima mrefu; Ee Yerusalema, wewe unayehubiri habari njema, paza sauti kwa nguvu; uipaze, usiogope, uiambie miji ya Yuda,* ***Tazameni Mungu wenu. 10 Tazameni, Bwana Mungu atakuja kwa uwezo!***
>
> *"Bwana mwenyewe atawapa ninyi alama;* ***tazama, bikira atapata mimba naye atazaa mtoto mwanamume, na ataita jina lake Emanueli - maana yake Mungu pamoja nasi!"*** (Isaya 7:14; Matayo 1:23)

Mungu alikuwa akifunua **siri kubwa** kwa njia ya nabii Isaya! Mungu alikusudi kutuma **Roho yake** ndani ya tumbo la uzazi la bikira, ndiye mwanamke asiyelala na mwanamume kamwe! Hii ndiyo namna Masiya atakavyozaliwa duniani. Kama unavyojua, Masiya hakuwa na baba aliyekuwa mtu wa dunia. Mbele ya kuzaliwa kwake, alikuwa mbinguni, kwa sababu yeye ni **Neno** aliyekuwa pamoja na Mungu katika mwanzo. Isaya alitabiri ya kwamba Masiya atakuwa **Mungu ndani ya mwili wa mtu**. Kweli ya kushangaza kabisa! Mungu, aliye Roho, alikusudi kuweka Roho na Neno lake

mwenyewe ndani ya tumbo la uzazi la bikira, kisha kuzaliwa duniani kama mtoto mchanga! Hili ndilo neno Isaya alilotabiri akisema: *"Bikira atapata mimba naye atazaa mtoto mwanamume, na ataita jina lake Emanueli - maana yake* ***Mungu pamoja nasi****!"*

Ndani ya sura zinazofuata, Isaya aliandika maneno mengi juu ya Masiya. Alisema:

> *"Watu wale waliotembea katika giza wameona* ***nuru kubwa****; wale waliokaa katika inchi ya kivuli cha kufa, nuru imengaa juu yao. . . Maana kwa ajili yetu* ***mtoto amezaliwa,*** *tumepewa* ***mtoto mwanamume****; . . . Na jina lake litaitwa* ***Mwenye ajabu, mwenye shauri, Mungu Mwenye uwezo, Baba ya milele, Mkubwa wa salama.****"* (Isaya 9:2,6) *"Macho ya vipofu yatafunguliwa, na masikio ya viziwi yatafunguliwa. Ndipo kiwete atarukaruka kama ayala, na ulimi wa bubu utaimba."* (Isaya 35:5,6)

Ndani ya mashairi haya, Isaya alitabiri ya kwamba Masiya ataleta utakatifu na rehema ya Mungu kwa dunia. Alitabiri vilevile ya kwamba Masiya atafanya kazi nyingi za uwezo ambazo hakuna mtu alifanya mbele, hivi watu wote watajua ya kwamba huyu ndiye Masiya mtakatifu aliyekuja toka Mungu! Kwa sababu hii nabii Isaya aliandika ya kwamba Masiya ataitwa: *"****Mwenye ajabu, mwenye shauri, Mungu Mwenye uwezo, Baba ya milele, Mkubwa wa salama.****"* Ni wazi ya kwamba Isaya hakuwa sawasawa na watu kwa wakati wa sasa wanaosema Masiya alikuwa nabii tu kama manabii wote wengine. Nabii Isaya alitambua utukufu wa Mkombozi, aliyetoka kwa Mungu.

Mbele ya kumaliza somo hili, sharti tusome sura moja nyingine, **sura 53**. Sura hii ni **ya ajabu kupita maneno yote mengine ambayo nabii Isaya aliandika,** kwani ndani yake alitabiri namna Masiya atamwanga damu yake kama kondoo anayetolewa kama sadaka, kubeba azabu kwa zambi za dunia. Sikiliza vizuri Habari Njema ambazo Mungu alimpa nabii wake Isaya, miaka mia saba mbele ya wakati wa Masiya.

Maandiko Matakatifu yanasema:

> (Isaya 53) ***1 Ni nani aliyeamini habari zetu: na mkono wa Bwana amefunuliwa nani? 2 Maana atakuwa mbele yake kama chipuko, na kama shina katika inchi kavu; yeye hana sura wala uzuri, na wakati tunapomwona hana uzuri hata tumtamani. 3 Amezarauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa***

***huzuni, na mwenye kujua taabu: na kama mtu ambaye watu wanamfichia nyuso zao, alizarauliwa, na hatukumhesabu kuwa kitu. 4 Kweli amechukua taabu zetu, na amebeba huzuni zetu; lakini tulimwona akipigwa, akiteswa na Mungu, na kuhuzunishwa. 5 Lakini aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu, azabu ya salama yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. 6 Sisi sote kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mmoja kwa njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.***

***7 Alionewa, na aliteswa; lakini hakufungua kinywa chake; kama mwana-kondoo anayepelekwa kuchinjwa, na kama kondoo anavyonyamaza mbele yao wanaokata manyoya yake; hakufungua kinywa chake. 8 Aliondolewa kwa kuonewa na kuhukumiwa, na kwa kizazi chake, nani aliyewaza ya kuwa amekatiliwa mbali na inchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. 9 Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; hata yeye hakufanya jeuri, wala hila haikuonekana kinywani mwake. 10 Hata hivi ilipendeza Bwana kumchubua; amemhuzunisha. Wakati utakapotolea nafsi yake kuwa zabihu kwa zambi, ataona uzao wake, atazidisha siku zake, na mapenzi ya Bwana yatasitawi katika mkono wake. 11 Ataona ya taabu ya nafsi yake, naye atatulia; kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki; naye atachukua maovu yao. 12 Kwa sababu hii nitamgawia sehemu pamoja na wakubwa, naye atagawa nyara pamoja na wahodari, kwa sababu alimwanga nafsi yake hata kufa, akahesabiwa pamoja na wale wenye kukosa, na alichukua zambi za watu wengi, na kuombea wenye kukosa.***

Haya ndiyo maneno Isaya aliyoandika juu ya mateso ambayo Masiya atavumilia kulipa kwa zambi zetu. Ndiyo, ilipasa Mkombozi kuteswa na kumwanga damu yake kwa watu wote wenye zambi ili Mungu aweze kusamehe zambi zetu pamoja na kuwa mwenye haki. Kwa sababu hii Isaya aliandika: *"Lakini aliumizwa kwa makosa yetu,* ***alichubuka kwa maovu yetu*** *. . . Sisi sote kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mmoja kwa njia yake mwenyewe; na* ***Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote****."* (Isaya 53:5,6) Shairi hili la kuogofya linajumlisha habari za kitabu cha Isaya: **habari mbaya** na **Habari Njema**.

1) Kwanza, **habari mbaya** ni ya kwamba sisi sote ni wenye zambi na hatuna njia kujiokoa wenyewe! Kwa sababu hii Isaya aliandika ya kwamba ***"Sisi sote kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mmoja kwa njia yake mwenyewe!"***

2) Habari Njema ndizo: Mungu alitayarisha njia kuokoa wenye zambi. Ni kwa njia ya mauti na ufufuko wa Masiya. Kwa sababu hii Isaya aliandika: ***"Aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu, . . . na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."***

Rafiki, una**fahamu** ukubwa wa zambi yako mbele ya Mungu Mtakatifu? Unaamini ya kwamba Masiya aliyezaliwa na bikira alikuwa *"Mungu pamoja nasi"*? Unajua kwa sababu gani ilipasa Masiya kumwanga damu yake kama kondoo ya sadaka?

Waza sana juu ya masemo haya ya kuleta uzima ya nabii Isaya. Mungu anataka kukusaidia kufahamu maneno yote Isaya aliyoandika ndani ya sura 53.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kusoma pamoja nasi. Mungu akubariki wakati unapowaza sana juu ya habari hizi toka Bwana kwa wewe kwa njia ya nabii Isaya:

> ***"Kujeni na tufanye shauri pamoja, Bwana anasema, hata zambi zenu ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kabisa; kama ni nyekundu ya damu zitakuwa kama manyoya ya kondoo."*** (Isaya 1:18)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 56

# Nabii Yeremia

### Yeremia

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya somo la mbele, tulijifunza ya kwamba nabii **Isaya** aliandika maneno mengi juu ya Masiya atakayekuja. Miaka elfu saba mbele ya kuzaliwa kwa Masiya, Mungu aliweka ndani ya nia ya Isaya namna Mwokozi huyu wa wenye zambi atakavyokuja toka mbele ya Mungu, kuzaliwa na malkia, kuishi maisha matakatifu, na kufanya maajabu ambayo hakuna mtu aliweza kufanya. Lakini, Isaya alitabiri vilevile ya kwamba Masiya atamwanga damu yake, kama mwana-kondoo, kulipa kwa zambi za dunia. Na wakati sadaka yake itakapotimizwa, atashinda mauti na kufufuliwa toka kaburi, na kuleta uzima wa milele kwa wote ambao wanamwamini. Leo tunakusudi kusoma juu ya nabii mkubwa mwingine wa Mungu, **nabii Yeremia**.

Yeremia aliishi karibu miaka mia moja nyuma ya nabii Isaya. Kama tulivyoona mbele, watu wa Israeli hawakufungana tena pamoja kama taifa moja. Walikuwa mataifa mawili: Israeli na Yuda. Kwa wakati wa Yeremia, ufalme wa **Israeli**, uliokuwa kwa upande wa kaskazini, uliharibiwa. Mungu alitoa watu wa Israeli kwa mikono ya adui zao, kwa sababu hawakuamini habari zilizotangazwa na manabii na kutubu zambi zao. Hivi, wa mataifa ya Israeli **Yuda tu lilibaki**. Yuda lilikuwa taifa kwa upande wa kusini; mji wake mkubwa ulikuwa Yerusalema pahali hekalu lililojengwa na Solomono lilipokuwa. Kama tulivyojifunza mbele, Mungu aliahidi kuleta Masiya duniani kwa njia ya kabila la Yuda.

Yeremia alikuwa Myuda. Alizaliwa ndani ya mji mdogo karibu kilomètres tano toka Yerusalema. Baba ya Yeremia alitumikia

Mungu kwa kazi ya kuhani hekaluni. Kwa wakati ule zaidi ya Wayuda katika Yerusalema walifuata kwanza **dini karibu karibu** na kushikana na mazoeo ya wazazi wao, **lakini hawakutii Neno la Bwana Mungu**. Lakini Yeremia alikuwa mtu aliyependa Neno la Mungu sana na kulitii; alitazamia siku wakati Mungu atakapotuma Masiya duniani.

Sasa tusikie namna Mungu alivyoita Yeremia kuwa nabii. Ndani ya sura ya kwanza ya kitabu cha Yeremia aliandika:

> (Yeremia 1) *4 Neno la Bwana lilikuja kwangu, kusema: 5* ***Ilipokuwa sijakuumba bado katika tumbo nilikujua, na ilipokuwa hujatoka bado tumboni, nilikutakasa, nimekuweka kuwa nabii la mataifa.*** *6 Nami nikasema: Ee Bwana Mungu! tazama siwezi kusema; kwa sababu mimi ni mtoto. 7 Lakini Bwana akaniambia: Usiseme: Mimi ni mtoto, kwa maana utakwenda kwa kila mtu ambaye nitakutuma kwake, nawe utasema kila neno ambalo nitakuagiza. 8 Usiogope mbele yao, kwa sababu mimi ni pamoja nawe nikuokoe, anasema Bwana. 9 Basi Bwana akanyosha mkono wake, akanigusa kinywa changu; Bwana akaniambia: Tazama, nimetia maneno yangu katika kinywa chako. 10 Angalia, nimekuweka leo juu ya mataifa, na juu ya falme, ili kuondosha na kubomoa, na kuharibu na kuangamia, ili kujenga na kupanda."*

Hivi Mungu aliita Yeremia kuwa nabii wake. Mungu alimwagiza kwendea Wayuda wenzake na kuwajulisha ya kwamba Mungu atawahukumu kama wasipotubu zambi zao na kurudi karibu na Bwana na Neno lake takatifu. Kazi ya Yeremia ilikuwa nguvu kwa sababu **Wayuda hawakutaka mtu ye yote kuwaambia ya kwamba kazi zao za dini hazikupendeza Mungu.** Lakini Yeremia hakuwa mwenye kupendeza watu. Hivi, kwa miaka makumi mbili na ine, Yeremia alihubiri katika Yerusalema na ndani ya inchi ya Yuda, akisema: "Mungu anataka niwaonye ninyi ya kwamba kama musipotubu zambi zenu na kutii neno la Mungu—Mungu ataruhusu jeshi la taifa la Babeli kuja na kuingia Yerusalema. Wataharibu mji na hekalu vilevile! Na watapeleka watu wengi katikati yenu kama wafungwa kwa inchi iliyo mbali!" Hizi ndizo habari Yeremia alizotangaza kwa Wayuda waliokaa katika Yuda.

Tusome mashairi mengine toka maandiko ya Yeremia ndani yao alionya Wayuda wenzake. Ndani ya Yeremia, sura 7 tunasoma, kuanza na shairi 1:

> (Yeremia 7) *1 Neno la Bwana lililokuja kwa Yeremia, kutoka kwa Bwana, kusema: 2* ***Simama kwa mlango wa nyumba ya Bwana, ukatangaze hapa neno hili,*** *ukisema:*
>
> *Sikilizeni neno la Bwana, ninyi Yuda wote, munaoingia katika milango hii ili kuabudu Bwana. 3 Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: Tengenezeni njia zenu, na matendo yenu, nami nitawakalisha ninyi pahali hapa. 4 Musitumainie maneno ya uwongo, mukisema: Hekalu la Bwana, Hekalu la Bwana, Hekalu la Bwana ndiyo maneno haya. 5 Maana kama mukitengeneza kabisa njia zenu na matendo yenu; kama mukihukumu hukumu ya haki kati ya mtu na jirani yake; 6 kama musipoonea mgeni, wala yatima, wala mjane, wala kumwanga damu isiyo na kosa pahali hapa, wala kufuata miungu mingine kwa hasara yenu wenyewe, 7 ndipo nitakapowakalisha ninyi pahali hapa, katika inchi hii ambayo niliwapa baba zenu, tokea zamani hata milele. 8* ***Angalieni, munatumainia maneno ya uwongo, yasiyoweza kuwa faida kwenu.*** *9 Mutaiba, mutaua, mutazini, mutaapa uwongo . . . na kufuata miungu mingine ambayo hamujui; 10 kisha mutakuja na kusimama mbele yangu katika nyumba hii, inayoitwa kwa jina langu, na kusema: tumepona; ili mupate kufanya machukizo haya yote?"*

Hivi Yeremia alihamakia Wayuda **waliotenda sawasawa walijua Mungu** lakini walimkana ndani ya matendo yao. Ndani ya sura 17, Yeremia aliongeza maneno mengine:

> (Yeremia 17) 5 *Bwana anasema hivi: Amelaaniwa mtu yule anayeamini mtu, anayefanya mtu kuwa mkono wake, na moyoni mwake ameacha Bwana . . . 9* ***Moyo ni mdanganyifu kuliko vyote, una ugonjwa wa hatari;*** *nani anayeweza kuujua? 10 Mimi Bwana ninapeleleza moyo, ninajaribu viuno, hata kumpa kila mtu yanayopasa kwa njia yake, kwa matunda ya matendo yake."*

Hivi Yeremia alikemea watu wa Yuda na kuwajulisha: "Kama musipotubu makosa yenu na kurudi kwa Mungu, majeshi ya Babeli wataharibu mji wa Yerusalema na hekalu hili, nanyi mutageuka watumwa wao!"

Unafikili nini? Unafikili watu wa Yuda walitubu na kusikiliza neno Bwana alilosema nao kwa njia ya Yeremia? **Zaidi yao hawakuweka roho juu ya maonyo haya!** Hata makuhani hawakuamini masemo ya Yeremia. Ndiyo, wakati makuhani waliposikia maneno aliyosema, walimfunga na kumpiga fimbo na kufunga miguu yake na minyororo kwa siku ile. Ilishinda makuhani kuamini

ya kwamba Mungu ataruhusu adui zao, Wababeli, kuingia Yerusalema na kuharibu mji na hekalu ambalo Solomono alijenga. Walifikili neno hili haliwezi kutokea kamwe. Walikasirikia Yeremia kwa sababu alitabiri ya kwamba Yerusalema utaharibiwa na aliandika maneno ya Mungu ndani ya kitabu.

Si watu na makuhani tu waliokataa masemo ya nabii wa Mungu, ndiye Yeremia. Mfalme aliyakataa vilevile. Wakati mfalme aliposoma kitabu ambacho Yeremia aliandika, **alikata kitabu vipande vipande** na kisu na kuvitupa ndani ya moto kwa kiwanja hata kitabu kizima kiliteketea. Hili ndilo neno ambalo mfalme wa Yuda alifanya. Hakutubu zambi yake, na hakupokea neno la Bwana. Ndiyo, mfalme aliteketeza kitabu cha Yeremia, **lakini hakuweza kugeuza amri ya Mungu**. Na Mungu aliongoza Yeremia kuandika maneno yake yote tena ndani ya kitabu kingine.

Ukisoma kitabu cha Yeremia, utaona ya kwamba **mfalme na makuhani na watu wa Yuda walitesa Yeremia** sana na kumfunga tena na tena. Siku moja waliweka Yeremia ndani ya shimo lililokwenda chini sana na liliokuwa na matope kwa upande wa chini. Lakini Mungu alimponyesha kwa njia ya kutuma kwake mtu wa Afrique ambaye alimwondoa shimoni.

Neno kubwa ambalo inatupasa kuwaza juu yake ni ya kwamba, hata zaidi ya Wayuda **walikataa kusikiliza** nabii Yeremia, si kusema ya kwamba hawakusikiliza mtu mwingine! **Walisikiliza** watu ambao walijiita manabii—lakini walikuwa **manabii wa uwongo!** Maandiko yanatujulisha ya kwamba watu wengi ambao walijiita manabii wa Mungu walikuwa wadanganyi, kwa sababu **mahubiri yao hayakutoka kwa Mungu.** Hivi, wakati Yeremia alipokuwa akitabiri ya kwamba hukumu ya Mungu itakayoangukia Yerusalema, manabii wa uwongo walisema na watu wa Yuda wakisema, "Sivyo, sivyo! maangamizi ambayo Yeremia alitabiri juu yao hayatatokea! Babeli haiwezi kuharibu Yerusalema! Hakuna mtu anayeweza kuharibu hekalu la Mungu! Hakutakuwa na uharibifu! Mutakaa na salama tu! Salama peke yake—hakuna kitu kingine ila salama!"

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Lakini Yeremia alisema na Wayuda wote akisema, kuanza na sura 23 na shairi 16:

> *16 Bwana wa majeshi anasema hivi:* ***Musisikilize maneno ya manabii wakitoa unabii; wanafundisha maneno yasiyo na maana****; wanasema maono ya mioyo yao wenyewe; hayakutoka katika*
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

> *kinywa cha Bwana. 21* ***Sikutuma manabii hawa, lakini wali-kwenda mbio; sikusema nao, lakini walitabiri.*** *22 Lakini kama wangalisimama katika baraza yangu, ndiyo, wangalisikizisha watu wangu maneno yangu, na kuwageuza waache njia zao mbaya, na uovu wa matendo yao.*

Hivi Yeremia alionya Wayuda kukaa na ange kwa maneno ya wale waliohubiri maneno ya uwongo. Ni huzuni kwa sababu zaidi ya watu wa Yuda hawakuweka roho juu ya maonyo ya nabii wa Mungu, Yeremia. **Waliamini masemo ya manabii wa uwongo**. Hata hivi, mwishoni, **wakati saa ilipokuwa imepita**, mfalme, makuhani, watu, na manabii wa uwongo waliona nani alitangaza **neno la kweli la Mungu**! Walifahamu kwa sababu kila neno Yeremia alilosema mbele juu ya uharibifu wa Yerusalema lilitokea. Neno la Mungu ni kweli kila mara.

Sikiliza Maandiko, ndiyo Yeremia 52, kuanza na shairi 4:

> (Yeremiah 52) *4 Na ilikuwa katika mwaka wa tisa wa kumiliki kwa Zedekia [mfalme wa Yuda] . . .* ***Nebukadreza****, mfalme wa Babeli, akakuja, yeye na jeshi lake lote, juu ya Yerusalema, akapanga hema zake juu yake; nao wakajenga maboma kando yake pande zote. 5 Basi mji huu ulizungushwa . . . 6 Katika mwezi wa ine, siku ya tisa ya mwezi, njaa ilizidi sana ndani ya mji, hata hakuna chakula kwa watu wa inchi. 7* ***Ukuta wa mji ukabomolewa*** *. . . [Hivi askari wali-funga mfalme wa Yuda] . . . 9 Nao wakashika mfalme, wakamchukua kwa mfalme wa Babeli . . . naye akatoa hukumu juu yake. 10 Mfalme wa Babeli akaua wana wa Zedekia mbele ya macho yake . . . 11 Akatoboa macho ya Zedekia; tena mfalme akamfunga kwa minyororo, akamchukua kwa Babeli. . . 13 [Kisha Nebukadreza, mfalme wa Babeli na askari zake] wakateketeza nyumba ya Bwana, na nyumba ya mfalme; na nyumba zote za Yerusalema, hata kila nyumba kubwa aliteketeza kwa moto. 14 . . . akabomoa kuta zote za Yerusalema. 15 Kisha Nebuzaradani, mkubwa wa askari, akachukua wafungwa wa-nyonge wa watu nao watu waliobaki walioachwa katika mji, na wale walioasi na kukimbilia mfalme wa Babeli . . . 16 Lakini Nebuzaradani, mkubwa wa askari, akaacha watu walio masikini kabisa ili wawe walinzi wa mizabibu na wenye kulima. 27 . . .* ***Ndivyo walivyochukuliwa Yuda katika utumwa toka inchi yake.***

Hivi tunaona ya kwamba **Mungu alitimiza kila neno** alilotabiri kwa njia ya Yeremia, nabii wake. Sasa Wayuda walijua ya kwamba maneno ya Yeremia yalikuwa **maneno ya kweli.** Lakini kujua neno

hili hakuwasaidia, kwa sababu walikuwa wafungwa sasa mikononi mwa askari Wababeli!

Tumalize somo letu la leo na mawazo gani? Labda tulimalize na wazo hili: Siku ya hukumu, kila mzao wa Adamu atajua maneno gani yaliyokuwa kweli na maneno gani yaliyokuwa wongo. Lakini **Mungu anataka utambue *sasa* yaliyo kweli na yaliyo uwongo—kwa sababu siku ya hukumu kujua maneno haya uliyozarau maisha yako mazima duniani hakutakusaidia!** Siku ya hukumu saa ya kutubu itakuwa imepita, kwa sababu utakuwa umekufa katika zambi zako! Kwa sababu hii neno la Mungu linasema: *"Tazama **sasa** ni wakati wa kukubaliwa; tazama **sasa** ni siku ya wokovu."* (2 Wakorinto 6:2)

***"Wapenzi, musiamini kila roho, lakini jaribuni roho, kama zimetoka kwa Mungu; kwa sababu manabii wa uwongo wengi wametokea duniani!"*** (1 Yoane 4:1)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma tutaona nini ilipata Wayuda waliopelekwa kwa Babeli . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya ahadi hii toka Bwana, na kuandikwa na nabii Yeremia. Bwana Mungu anasema,

> ***"Nanyi mutanitafuta, na kuniona, wakati mutakaponitafuta kwa moyo wenu wote."*** (Yeremia 29:13)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 57

# Nabii Danieli

### Danieli 1,6

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Mara ya mbele, tulisoma ndani ya kitabu cha **Yeremia**. Nabii Yeremia aliishi karibu miaka mia sita mbele ya kuja kwa Masiya. Tuliona ya kwamba Yeremia alionya Wayuda wenzake, akiwaambia kama wasipotubu zambi zao na kurudi karibu na Mungu, jeshi la taifa la Babeli wataharibu mji wao mkubwa, Yerusalema na kuwafunga. Ni huzuni, kwani zaidi ya Wayuda walisikiliza **manabii wa uwongo** na walikataa kuweka roho juu ya tangazo la Yeremia. Hivi tulisoma ya kwamba jeshi la Babeli walikuja, wakaharibu Yerusalema na kupeleka Wayuda kwa inchi ya mbali, ndiyo Babeli. Maneno yote yalitokea namna Mungu alivyotabiri kwa njia ya Yeremia, nabii wake.

Lakini hata kama Yerusalema uliharibiwa, si kusema Mungu alikuwa ameacha kabisa Wayuda, watu wale ambao aliwachagua zamani. Mungu hakuweza kusahau **agano** alilofanya na Abrahamu, Isaka na Yakobo, wakati alipowaambia, *"Mataifa yote ya dunia watabarikiwa kwa njia yenu."* Mungu hakusahau **shauri lake** kutuma Mkombozi duniani kwa njia ya taifa la Wayuda waliokuwa wazao wa Abrahamu. Hivi Maandiko yanatupasha namna Mungu alivyolinda Wayuda katika Babeli kwa **miaka makumi saba** kufika wakati alipowarudisha kwa Yerusalema, kama alivyoahidi. Tutasoma juu ya maneno haya ndani ya somo la nyuma.

Leo tunataka kusoma juu ya kijana Myuda mmoja, aliyekuwa mmoja wa wafungwa waliopelekwa kwa Babeli. Kijana huyu ni **Danieli**—nabii wa Mungu. Maana ya jina hili Danieli ni ***Mungu ni mwamuzi wangu***. Jina hili linajumlisha ushuhuda wa Danieli. Danieli hakuogopa mtu. Aliogopa mmoja tu, ndiye Mungu Mwenyezi. Watu wote watalazimishwa kusimama mbele ya Mungu huyu siku nyingine. Danieli hakuweka roho juu ya mawazo ya watu juu yake. Maneno Mungu tu aliyofikili juu yake yalikuwa neno kubwa

kwa mafikili yake. Mungu alikuwa mwamuzi wa Danieli. Danieli aliamini neno nabii Solomono aliloandika miaka mingi mbele, ndiyo haya: *"**Kuogopa watu** kunaleta **mtego**; lakini yeye **anayetumainia Bwana** atakuwa na **salama.**"* (Mezali 29:25)

Mungu aliongoza Danieli kuandika kitabu chenye mafundisho ya ndani. **Katika kitabu cha Danieli** kuna mafunuo mengi ambayo mtu kwa akili yake ya umtu hakuweza kutabiri. Mungu tu anajua nini itatokea kwa wakati wa kuja. Lakini nabii Danieli aliandika **historia ya mataifa mengi** ya dunia—aliandika historia yao hata wakati mataifa haya yasipokuwa bado kwa wakati ule! Kwa mfano, Danieli aliandika namna falme za Persia, na Yunani na Roma zitakavyoanza na maneno wafalme wao watakayofanya. Aliandika mia za miaka mbele ya mwanzo wa zaidi ya falme hizi! Na vilevile, kama zaidi ya manabii wa Mungu, Danieli aliandika juu ya **kuja kwa kwanza na kuja kwa pili kwa Masiya.** Danieli alitabiri ya kwamba wakati Masiya atakapokuja mara ya kwanza *"atakatiliwa mbali"* (Danieli 9:26) — maana yake, atauawa kama zabihu kwa zambi, lakini wakati Masiya atakaporudi kwa dunia atahukumu dunia kwa haki. Sikia ono la nabii Danieli juu ya kuja kwa pili kwa Masiya:

> *"Nikaangalia hata viti vya ufalme viliwekwa, na mmoja aliye **mzee wa siku** akaketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nyole za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha ufalme kilikuwa ndimi za moto, na magurudumu yake moto unaowaka. Na mto wa moto ukatoka, ukapita mbele yake; elfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi walisimama mbele yake; hukumu ikawekwa, vitabu vikafunguliwa!"*
>
> *Nikaona katika maono ya usiku, na tazama, pamoja na mawingu ya mbingu alikuja mmoja aliye mfano wa **mwana wa watu**, akakaribia huyu mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wote, mataifa yote, na lugha zote wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, isiyopita kamwe, na ufalme wake ufalme usioweza kuangamizwa."*
>
> (Danieli 7:9,10,13,14)

Halafu, tukikosa saa kutafuta maneno ya ndani ndani yote ya Mungu ndani ya kitabu cha Danieli, tutatumia mwisho wa saa yetu leo kwa kuwaza juu ya **maisha ya Danieli mwenyewe.**

Ndani ya sura ya kwanza ya Danieli, tunaona ya kwamba Nebukadneza alichagua **vijana Wayuda** wengine waweze kufundishwa

kumtumikia katika serikali yake. Alichagua vijana walioonekana vizuri na waliokuwa na akili—wenye kuweza kujifunza maneno mbalimbali, hata herufi za nguvu za lugha ya Babeli. **Danieli** alikuwa katikati ya wale waliochaguliwa na mfalme.

Hivi Danieli alianza kujifunza ndani ya madarasa ya Babeli. Lakini mara moja siku ya kwanza Danieli alipata **mashaka**. Mfalme mkubwa wa Babeli alikuwa ameagiza kwa vijana ndani ya darasa yake kunywa mvinyo nzuri zaidi na kula vyakula vizuri kabisa. Lakini, mvinyo na vyakula hivi vilikuwa vimetolewa kwa sanamu. Danieli ataweza kushiriki ndani ya ibada ya sanamu? Sivyo, hata kidogo! Kwa nini? Kwa sababu Danieli aliogopa **Mungu.** Danieli alichagua kufa kupita kufanya kitu kisichopendeza Mungu, Bwana yake. Hivi tunasoma ndani ya Maandiko: *"Lakini **Danieli alikusudi moyoni mwake ya kuwa hatajichafua** kwa chakula cha mfalme, wala kwa mvinyo ambayo alikunywa; kwa hivi aliomba yule mkubwa wa matowashi ampe ruhusa asijichafue."* (Danieli 1:8)

Maandiko yanatupasha namna gani Mungu alimponyesha toka mashaka yake, akambariki na kumpa hekima na ufahamu: *"Katika kila **neno la hekima na ufahamu** ambalo aliwauliza mfalme, akaona ya kuwa [Danieli] **alishinda mara kumi** waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake wote."* (Danieli 1:20) Hivi kwa karibu miaka makumi saba, Danieli alitumikia wafalme wane, na Mungu alikuwa pamoja naye.

Ndani ya saa inayobaki leo, tunataka kuangalia **neno moja lililotokea katika maisha ya Danieli**—linaloonyesha ya kwamba Danieli aliogopa Mungu tu peke yake. Tutaona ya kwamba Danieli alikuwa namna nyingine na maliwali (watu wa serikali) waliotumikia mfalme. Ilikuwa desturi ya watu wale kutosema kweli na kupokea rushwa kwa sababu hawakuogopa Mungu hata kidogo. Lakini Danieli alikataa udanganyifu na uzalimu wote kwa sababu woga wa Mungu ulijaza moyo wake. Alichagua kutupwa ndani ya pango la simba zaidi ya kufanya neno lisilopendeza Mungu.

Danieli alikuwa mzee sasa na alikuwa akitumikia mfalme wa ine na uaminifu. Kwa wakati huu ufalme wa Babeli haukuitwa Babeli tena, lakini Persia, kwa sababu mataifa mawili, ndiyo Wamedi na Wapersi, walikuwa wameshinda ufalme wa Babeli na kuugawa kwa sehemu mbili, kama nabii Danieli alivyotabiri mbele.

Ndani ya Danieli sura 6, kuanza na shairi 1 tunasoma:

> *"Ilipendeza Dario kuweka juu ya ufalme maliwali mia moja makumi mbili, wawe juu ya ufalme wote; 2 na juu yao akaweka wakubwa*

*watatu, na Danieli alikuwa mmoja wao; ili maliwali hawa watoe hesabu kwao na ili mfalme asipate hasara. 3 Basi* ***Danieli huyu akapata heshima kuliko wakubwa na maliwali kwa sababu roho bora ilikuwa ndani yake****; mfalme akafikili kumweka juu ya ufalme wote.*

*4 Halafu wakubwa na maliwali walitafuta njia ya kushitaki Danieli kwa maneno ya ufalme; lakini hawakuweza kuona sababu wala kosa; kwa maana alikuwa mwaminifu, wala halikuonekana kosa wala kuanguka ndani yake. 5 Halafu watu hawa wakasema:* ***Hatutapata sababu ya kushitaki Danieli huyu****, tusipoipata katika mambo ya sheria ya Mungu wake.*

*6 Halafu wakubwa hawa na maliwali wakakusanyika pamoja mbele ya mfalme, wakamwambia hivi: Mfalme Dario, uishi milele. 7*
*Wakubwa wote wa ufalme na manaibu, na maliwali, na washauri na wasimamizi wamefanya shauri pamoja, ili kuweka amri ya kifalme, na kutoa amri ya nguvu, hata* ***mtu ye yote atakayeomba kitu kwa mungu ye yote au mtu ye yote kwa siku makumi tatu ila wewe, Ee mfalme, atupwe katika pango la simba.*** *8 Sasa, Ee mfalme, simamisha amri hii na tia mkono kwa maandiko haya hata yasibadilike, sawasawa na sheria ya Wamedi na Wapersi, isiyoweza kubadilika. 9*
*Kwa hivi mfalme Dario aliweka mkono chini ya maandiko na amri.*

*10* ***Wakati Danieli alipojua ya kuwa maandiko haya yamewekwa mkono, akaingia nyumbani mwake; (basi madirisha yake yalikuwa wazi chumbani mwake kwa upande wa Yerusalema;) akapiga magoti yake mara tatu kila siku, akaomba, akashukuru mbele ya Mungu wake kama mbele.*** *11*
*Halafu watu hawa walikusanyika, wakakuta Danieli akiomba na kusihi mbele ya Mungu wake. 12 Halafu wakakaribia, wakasema na mfalme juu ya amri ya mfalme: Wewe hukutia mkono juu ya amri ile, ya kwamba kila mtu atakayeomba kitu kwa mungu ye yote au mtu ye yote katika siku makumi tatu ila kwako mfalme, atatupwa katika pango la simba? Mfalme akajibu na kusema: Neno hili ni kweli, sawasawa na sheria ya Wamedi na Wapersi isiyogeuka. 13 Halafu wakajibu na kusema mbele ya mfalme, Danieli yule aliye wa wana wa uhamisho wa Yuda, hakuheshimu, Ee mfalme, wala amri uliyotia mkono, lakini anaomba mara tatu kila siku.*

*14 Halafu mfalme, wakati aliposikia maneno haya, akakasirika sana, akakaza moyo wake ili kuponyesha Danieli; akajitaabisha hata jua likashuka ili kumwokoa. 15 Halafu watu wale wakakusanyika*

*pamoja mbele ya mfalme, wakamwambia mfalme: Ujue, Ee mfalme, ya kuwa ni sheria ya Wamedi na Wapersi, lisibadilike amri wala sheria mfalme anayoweka. 16 Halafu mfalme akaagiza, wakaleta Danieli,* ***wakamtupa ndani ya pango la simba.*** *Basi mfalme akasema, akamwambia Danieli: Mungu wako, ambaye unamtumikia daima, anaweza kukuponyesha. 17 Jiwe likaletwa, likawekwa juu ya kinywa cha pango; mfalme akalitia muhuri kwa muhuri wake mwenyewe, na muhuri wa wakubwa wake; lisibadilike neno lo lote katika maneno ya Danieli. 18 Halafu mfalme akakwenda kwa nyumba yake, akashinda usiku ule akifunga chakula, wala vinanda havikuletwa mbele yake; usingizi wake ulimkimbia.*

*19 Halafu mfalme akaamka asubui mapema, akakwenda kwa haraka kwa pango la simba. 20 Na wakati alipokaribia pango, alilia kwa sauti ya huzuni kwa Danieli. Mfalme akasema na kumwambia Danieli: Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, Mungu wako ambaye unamtumikia daima, anaweza kukuponyesha na simba hawa? 21 Halafu Danieli akamwambia mfalme:* ***Ee mfalme, ishi milele. 22 Mungu wangu ametuma malaika yake na amefunga vinywa vya simba, nao hawakuniumiza: kwa sababu sikuonekana na kosa mbele yake; na mbele yako vilevile, Ee mfalme, sikufanya kosa****. 23 Halafu mfalme akafurahi sana, akaagiza watoe Danieli katika pango la simba. Hivi Danieli akatolewa katika pango, wala alama yo yote ya kuumia haikuonekana katika mwili wake, kwa sababu alitumainia Mungu wake.*

*24 Mfalme akaagiza, wakaleta watu wale walioshitaki Danieli, wakawatupa katika pango la simba, wao, watoto wao na wake wao;* ***simba waliwashinda****, wakavunja mifupa yao vipande vipande wakati wasipofika bado chini katika pango.*

*25 Halafu mfalme Dario aliandika kwa watu wote, na makabila yote na lugha zote wanaokaa katika dunia yote: Salama iongezwe kwenu. 26 Ninaweka amri, ya kuwa katika mamlaka yote ya ufalme wangu watu watetemeke na kuogopa mbele ya Mungu wa Danieli: maana yeye ni Mungu aliye hai, anayedumu milele, na ufalme wake ni ufalme usioharibika na mamlaka yake inadumu hata mwisho. 27* ***Anaponyesha na kuokoa, anatenda alama na maajabu mbinguni na duniani; aliyeponyesha Danieli na nguvu za simba****!"* Amina.

Ulisikia maneno mfalme aliyosema wakati alipoona namna Mungu alivyookoa Danieli toka simba? Alisema, *Ninaweka amri, ya kuwa katika mamlaka yote ya ufalme wangu watu watetemeke na* ***kuogopa***

***mbele ya Mungu wa Danieli****: maana yeye ni Mungu aliye hai, anayedumu milele!"*

Wewe unayesikiliza leo, unaogopa Mungu wa Danieli? Labda unauliza, **"Mungu wa Danieli ni nani?"** Mungu wa Danieli ni Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo. Mungu wa Danieli ni Mungu wa manabii Musa na Daudi. Mungu wa Danieli ni Mungu ambaye alitupa sisi Maandiko Matakatifu. Yeye ni Mungu aliyeahidi kuokoa wenye zambi toka uwezo ulio mkubwa kupita uwezo wa simba, ndio uwezo wa Shetani, na zambi, na hadeze! Mungu wa Danieli ni **Mungu**—Mungu wa pekee wa kweli!

**Unaogopa Mungu wa Danieli? Hatuulizi** kama ukiogopa rafiki zako na mawazo yao, au kama ukiogopa wazazi wako na desturi zao, au wachawi na maneno wanayotaka kwako! Neno ambalo tunakuuliza ndilo hili: Unaogopa **Mungu**? Unataka kupendeza Bwana Mungu na kutii Neno lake takatifu? Danieli aliogopa **Mungu,** na kwa sababu hii hakuogopa watu. Danieli alifurahi kushinda usiku mmoja katika pango la simba kupita kufanya neno lisilopendeza Bwana Mungu wake! Basi wewe? Unaogopa Mungu? Unamwogopa namna Danieli alivyomwogopa? Unachukia uzalimu kama Danieli? Unapenda Neno la Mungu kama Danieli? Au wewe ni sawasawa zaidi ya wanadamu wanaogeuza kweli, na wanaosukumwa na mapendo ya mali, na wasioweka roho juu ya Maandiko Matakatifu? **Unaogopa Mungu?**

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, tutafikili juu ya unabii wa ajabu wa Zekaria, mmoja wa manabii walioishi nyuma ya Danieli. . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya kweli hii kubwa:

> ***"Kuogopa watu kunaleta mtego: lakini yeye anayetumainia Bwana atakuwa na salama."*** (Mezali 29:25)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 58

# Nabii Zekaria

### Zekaria

Salama iwe kwako, rafiki. Asante kwa kufika na kujifunza somo lingine la mfulizo *Njia ya Haki.*

Kwa masomo mawili ya mbele, tulijifunza ya kwamba Yeremia, nabii wa Mungu, alionya Wayuda wenzake ya kwamba wakikataa kusikia Neno la Mungu na kutubu zambi zao, Mungu ataacha askari za Babeli kuja, kuharibu inchi yao na kuwapeleka kwa inchi ya mbali. Zaidi ya Wayuda hawakuweka roho juu ya maonyo ya Yeremia. Hivi jeshi la Babeli lilifika toka mashariki, wakaharibu Yerusalema, wakavunja helalu na kufunga Wayuda na kuwapeleka kwa Babeli, kama nabii Yeremia alivyotabiri. **Hivi Wayuda walisambazwa, kwa sababu walikataa kutii neno la manabii wa Mungu.**

Lakini kutoaminifu wa Wayuda kuliweza kuzuiza uaminifu wa Mungu? Sivyo, hata kidogo! Sikiliza maneno nabii Yeremia aliyosema na Wayuda waliokuwa wafungwa sasa katika inchi ya Babeli kwa sababu ya zambi zao. Alisema nao:

> (Yeremia 29) *4 Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli, anawaambia hivi watu waliochukuliwa wafungwa, ambao niliwafanya wachukuliwe toka Yerusalema mpaka Babeli: 10 . . . "Wakati Babeli utakapotimizwa miaka makumi saba, nitawaangalia ninyi, na kutimiliza neno langu kwenu, kwa kuwarudisha ninyi pahali hapa [Yerusalema]. 11* ***Maana ninajua mawazo ninayowaza juu yenu, anasema Bwana, ni mawazo ya salama, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho."***

Tangazo hili la Yeremia lilijulisha Wayuda ya kwamba hata wao walikuwa wamesahau Mungu, **Mungu hakuwasahau!** Nyuma ya miaka makumi saba, Mungu alikusudi kuwarudisha kwa inchi ya babu zao. Kwa sababu hii Yeremia aliwaambia Wayuda waliokuwa wafungwa katika Babeli: Kweli, **Mungu ni mwaminifu** {ndiye

mwenye kutimiza maagano}. Mungu hakusahau ya kwamba alikuwa ameahidi kubariki mataifa yote ya dunia kwa njia ya wazao wa Abrahamu, Isaka na Israeli. Mungu hakusahau ya kwamba alikusudi kuwekea Waisraeli neno lake ili waweze kulipitisha kwa wazao wote wa Adamu. Ndani ya masomo yetu tumeona ya kwamba Mungu alichagua manabii wake toka Wayuda, na kuwaongoza kutangaza Neno lake takatifu na kuliandika kwa vizazi watakaozaliwa nyuma. Tunajua namna Mungu alivyoweka Tora ndani ya nia ya Musa na nyimbo katika kitabu cha Zaburi ndani ya roho ya Daudi. Tuliona namna Mungu alivyoongoza Wayuda wengine kama Yosua, Samweli, Solomono, Isaya, Yeremia, na Danieli kuandika kitabu cha Mungu. Tuliona namna Maandiko yote ya manabii wa Mungu yanaonyesha njia ya ajabu ambayo Mungu alitayarisha kutuma Mwokozi wa dunia kwa njia ya taifa la Israeli.

Leo tutaona namna **Mungu alivyorudisha Wayuda** kwa inchi ya Yuda pahali Masiya atakapozaliwa, na kuendelea mbele na shauri lake kuleta Masiya duniani. Tutajifunza namna Wayuda walivyorudi kwa Yerusalema nyuma ya kuwa wafungwa kwa miaka makumi saba, kama nabii Yeremia alivyokuwa ametabiri.

Wakati tunapoanza kusoma leo, tukumbuke ya kwamba kwa wakati huu Babeli iliitwa Persia kwa sababu Wapersia walikuwa wameshinda Wababeli. Tukisoma ndani ya sura ya kwanza ya kitabu cha Ezra, Maandiko yanasema:

> (Ezra 1) *1 Katika mwaka wa kwanza wa Kiro mfalme wa Persia, **ili neno la Bwana kwa kinywa cha Yeremia lipate kutimizwa, Bwana akasukuma roho ya Kiro**, **mfalme wa Persia,** afanye tangazo katika ufalme wake wote, na kuliandika vilevile kusema: 2 Kiro, mfalme wa Persia, anasema hivi: Bwana Mungu wa mbingu amenipa falme zote za dunia; naye akaniagiza **nimjengee nyumba kwa Yerusalema** katika Yuda. 3 Basi nani katikati yenu aliye wa watu wake? Mungu wake awe pamoja naye; apande kwa Yerusalema ulio katika Yuda, kujenga nyumba ya Bwana, Mungu wa Israeli . . . 5 Halafu wakaondoka wakubwa wa baba za Yuda na Benyamina, na makuhani, na Walawi, hata wote ambao Mungu alisukuma katika roho waende kujenga nyumba ya Bwana iliyo katika Yerusalema. 6 Nao wote ambao waliwazunguka wakatia mikono yao nguvu kwa vyombo vya feza na zahabu, na vitu, na nyama, na vitu vya damani, zaidi ya yote yaliyotolewa kwa moyo. 7 Kiro mfalme vilevile akatoa vyombo vya nyumba ya Bwana ambavyo Nebukadneza alivileta toka Yerusalema, na kuviweka nyumbani mwa miungu yake.*

Mungu alitimiza neno aliloahidi miaka mingi mbele kwa kinywa cha nabii wake Yeremia? Kabisa! Tumeona mbele namna Mungu alivyoruhusu mfalme wa Babeli **kuharibu** Yerusalema, na kubomoa hekalu la Mungu—**namna Yeremia alivyotabiri.** Na sasa tunaona namna Kiro, mfalme wa Persia, alivyoagiza Wayuda wo wote waliotaka, kurudi kwa inchi yao na **kujenga tena** hekalu na mji wa Yerusalema—**namna nabii Yeremia alivyotabiri**. Kweli, Bwana ni Mfalme wa wafalme. Ni yeye anayetawala nyakati na majira. Maneno yote anayosema yatafanyikana! Nabii Solomono aliandika, *"Moyo wa mfalme ni mkononi mwa Bwana kama njia za maji; anaugeuza pahali po pote anapotaka."* (Mezali 21:1)

Halafu Maandiko yanapasha namna fungu la Wayuda walivyoondokea inchi ya Persia na kusafiri tena kwa inchi ya Yuda na mji wa Yerusalema. Myuda mmoja aliyeitwa **Zerubali** alikuwa kiongozi wao. Wakati walipofikia Yerusalema, walisumbushwa sana kwa sababu mji mzima uliharibiwa, na hekalu la Bwana ambalo Solomono alikuwa amejenga lilibomoka. Majivu na mabomoko ya mawe tu yalibaki.

Hivi Maandiko yanapasha ya kwamba Wayuda walikutana kwanza kwa pahali hekalu la Bwana lilipokuwa mbele. Wakajenga pale mazabahu kutoa sadaka na walitoa nyama wengine kama sadaka. Pamoja walishukuru na kusifu Bwana kwa sababu aliwalinda katika Babeli na Persia kwa miaka makumi saba na aliwarudisha tena kwa inchi yao. Mungu alikuwa pamoja na Wayuda wale, kuwasaidia na kuwapatisha nguvu—hivi nyuma ya taabu nyingi na miaka mingi ya kazi ya nguvu—waliweza kujenga tena **hekalu la Bwana, mji wa Yerusalema, na hata kuta ambazo ziliuzunguka.**

Labda unauliza: "Basi habari hizi za kurudi kwa Wayuda kwa Yerusalema zina maana gani kwa mimi?" Rafiki, kurudi kwa Wayuda kwa Yerusalema ni neno kubwa sana kwa sababu **Masiya** atazaliwa ndani ya inchi ile ya **Yuda**, kwa upande wa kusini. Ilikuwa lazima kwa Wayuda kurudi kwa inchi ya Yuda ili Mkombozi wa dunia—**Mkombozi wako**—aweze kuzaliwa pale!

Kwa wakati wa kurudi kwa Wayuda kwa Yerusalema, Mungu alisimamisha nabii jina lake **Zekaria** {*Zakaria* kwa lugha ya Waarabe}. Mungu alituma Zekaria kupatisha imani ya Wayuda nguvu ndani ya Mungu na ahadi zake. Zekaria aliwatangazia habari kubwa. Saa iliyowekwa na Mungu kutuma Masiya ilikuwa ikikaribia! Nyuma ya miaka 500 tu Mkombozi atakuja duniani.

Tuangalie mengine ya masemo Mungu aliyoweka ndani ya nia ya Zekaria. Maandiko yanasema ndani ya sura 1 ya kitabu cha Zekaria, kuanza na shairi la kwanza:

> (Zekaria 1) *1 Neno la Bwana lilikuja kwa Zekaria, mwana wa Berekia, mwana wa Ido, nabii, likisema: 2 Bwana amekasirikia sana baba zenu. 4* ***Musiwe kama baba zenu*** *waliolilia manabii wa mbele wakisema: Bwana wa majeshi anasema hivi: Rudieni sasa toka njia zenu mbaya na katika matendo yenu mabaya; lakini hawakusikia wala hawakunisikiliza, Bwana anasema. 5 Baba zenu, wao ni wapi? Na manabii, wanaishi milele? 6 Lakini maneno yangu na sheria zangu nilizoagiza watumishi wangu manabii; hazikupata baba zenu?"*

Ulisikiliza vizuri **onyo** la nabii Zekaria kwa Wayuda? Alisema nao, *"Bwana alikasirikia baba zenu sana! Musiwe kama baba zenu!"* Kwa sababu gani Mungu alikasirikia baba za Wayuda? Mungu aliwakasirikia kwa sababu **hawakuweka roho juu ya maneno ya manabii** ambao alituma katikati yao. Na kwa sababu hii walipelekwa kwa Babeli kama wafungwa. Babu zao walikuwa watu wa dini, lakini Mungu hakuwafurahia kwa sababu hawakuangalia masemo ya manabii. Wayuda wa wakati ule walikuwa kama watu wa wakati wa sasa wanaosema, "Ndiyo, sisi tunaamini manabii wote!" Lakini inaonekana wazi ya kwamba hawaweki roho juu ya **maneno manabii waliyoandika** ndani ya Maandiko Matakatifu. Wana **dini**, lakini hawajuani na Mungu mwenyewe. Zaidi ya babu za Wayuda walikuwa hivi. Hawakufurahia maneno ya manabii. Waliheshimu Mungu na midomo yao lakini hawakupokea Neno lake ndani ya **mioyo** yao. Kwa sababu hii Mungu alituma mtumishi wake Zekaria karibu na Wayuda, kuwaonya kusudi wasiige mfano mbaya wa babu zao waliosema, "Mungu, Mungu, Mungu!" na midomo yao, lakini walioona bule Neno ambalo Mungu alituma kwao kwa njia ya manabii wake.

Nyuma ya kuonya Wayuda, nabii Zekaria alianza kuwapasha habari za **Mkombozi** atakayekuja. Hatuna saa kusoma maneno yote nabii Zekaria aliyoandika juu ya Masiya, lakini tunaweza kusoma sehemu za unabii wake.

Ndani ya kitabu cha Zekaria, sura 9, nabii Zekaria alitabiri ya kwamba **Masiya ataingia Yerusalema akitembea juu ya punda**. Alisema, *"Furahi sana, Ee binti ya Sayuni; piga kelele, Ee binti ya Yerusalema; tazama, mfalme wako anakuja kwako; mwenye haki, na akiwa na wokovu, mwenye unyenyekevu na* ***anapanda kipunda****, hata mwana wa punda."* (Zekaria 9:9)

Ndani ya sura 11, Zekaria aliandika unabii wa kushangaza. Hatuna saa kueleza maneno yote ndani yake. Neno moja Zekaria alilotabiri ni ya kwamba **Masiya atauzwa kwa vipande makumi tatu vya feza.** Nabii Zekaria aliandika:

> *"Nikawaambia: Kama mukipendezwa, munipe mshahara wangu; sivyo, acheni. Basi walipima* ***vipande vya feza makumi tatu*** *kwa mshahara wangu . . . Nikachukua* ***vipande makumi tatu vya feza, nikatupia mfinyanzi ndani ya nyumba ya Bwana. . ."*** (Zekaria 11:12,13)

Ndani ya sura 12 Zekaria alitabiri ya kwamba Wayuda hawatauza Masiya lakini watamwua! Alisema: Bwana anasema,

> *"Na nitamwanga juu ya nyumba ya Daudi, na juu ya wenyeji wa Yerusalema, roho ya neema na ya maombi, nao* ***watamtazama ambaye walimchoma;*** *na watamwombolezea kama mtu anavyoombolezea mwana wake mzaliwa pekee, na wataona uchungu juu yake, kama mtu anavyoona uchungu kwa mwana wake mzaliwa wa pekee . . . Na mmoja atamwambia:* ***Vidonda hivi nini katika mikono yako? Naye atajibu: Vidonda vile nilivyotiwa katika nyumba ya rafiki zangu.****"* (Zekaria 12:10; 13:6)

Na masemo haya Zekaria alitabiri ya kwamba Masiya atakuwa na vidonda ndani ya mikono yake. Atapata vidonda hivi wapi? Wayuda wenzake watasukuma Waroma kumsulibisha. Halafu Waroma watafunga mikono na miguu yake kwa msalaba na nyuma watatoboa mbavu zake na mkuki. Maneno yote yalitokea namna Zekaria alivyotabiri. Maneno Zekaria aliyoandika **yalipatana kabisa** na maneno nabii Daudi aliyotabiri mia za miaka mbele ndani ya kitabu cha Zaburi, pahali alipoandika juu ya Masiya: *"Wametoboa mikono yangu na miguu yangu."* (Zaburi 22:16)

Rafiki, Mungu anataka tujue ya kwamba **mauti ya Masiya msalabani ni sehemu kubwa zaidi ya njia** aliyotayarisha zamani kuokoa wana wa Adamu toka azabu ya zambi zao. **Ilikuwa lazima kwa Masiya, mwenye haki, kuteswa na kufa kwa wazalimu! Hizi ndizo habari za manabii wote wa Mungu**. Unafahamu maneno haya vizuri? Unafahamu maneno Zekaria aliyotabiri juu ya Masiya karibu miaka mia tano mbele ya kuzaliwa kwake? Unaamini kweli kweli **habari** za manabii—ya kwamba Masiya atateswa na kufa na, akiwa wa kwanza atakayefufuliwa toka wafu, atatangaza usamehe kwa zambi na pahali katika Paradiso kwa wote wanaoamini jina lake?

**Unaamini manabii?** (Ona Matendo 26:18-27) Au wewe ni kama Wayuda, walioheshimu manabii wa Mungu na midomo yao, lakini hawakuamini habari walizotangaza?

Juu ya habari za manabii, Maandiko yanasema:

> ***"Musibeue unabii."*** (1 Watesaslonika 5:20) *"Basi tuna neno la unabii lililo imara zaidi, **na inawafaa ninyi kuliangalia,** kama taa inayongaa katika pahali pa giza hata mapambazuko, na nyota ya asubui itasimama mioyoni mwenu."* (2 Petro 1:19) ***"Unaamini manabii?"*** (Matendo 26:27)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Msomaji mwenzetu, asante kwa kusoma pamoja nasi. Mungu akitaka, ndani ya somo la nyuma tutasikia maneno toka nabii aliye-andika kitabu cha mwisho wa Maandiko Matakatifu mbele ya kuja kwa Masiya duniani . . .

Mungu akubariki wakati unapojaribu kujibu na roho ya kweli ulizo hili kubwa toka Neno la Mungu:

> ***"Unaamini manabii?"*** (Matendo 26:27)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 59

# Jumlisho la Unabii wa Manabii

### Malaki

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kuendelea tena na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Kwa siku nyingi tumejifunza ndani ya sehemu ya kwanza ya Maandiko Matakatifu. Sehemu ile inaitwa **Agano la Kwanza**. Inajulikana vilevile kama *Agano la Kale.* Sehemu hii ni Tora, Zaburi, na Maandiko mengine ya Manabii. Kama tulivyoona, Mungu alitumika na zaidi ya manabii makumi tatu katika muda wa miaka elfu moja mia tano kuandika kitabu cha Agano la Kwanza.

Somo la leo ni somo kubwa sana, kwa sababu tutatimiza safari yetu ndani ya sehemu ya kwanza ya Maandiko Matakatifu. Lakini, mbele ya kuangalia sura za mwisho za kitabu cha Agano la Kwanza, tunataka kusemezana kidogo juu ya maneno tuliyojifunza ndani ya kitabu hiki toka siku ya kwanza kufika sasa. **Tunaweza kujumlisha habari za manabii wote na mawazo makubwa haya matatu:**

**1**. Mungu ni **mtakatifu** na ni lazima kwake kuhukumu kila zambi.

**2**. Watoto wote wa Adamu wanazaliwa wenye **zambi** na itawapasa kusimama mbele ya hukumu ya Mungu.

**3**. Mungu alifanya shauri kutuma **Mkombozi** mtakatifu atakayevumilia azabu ya zambi kwa wana wa Adamu.

Manabii wote walihubiri kweli hizi tatu. Tutaje kweli hizi tatu tena:

1) **Mungu ni Mtakatifu**, na hawezi kuona zambi bule.

2) **Mtu ni mwovu**, amejaa zambi, na hana njia kujiokoa toka azabu ya zambi.

3) **Mungu ana shauri** kusafisha wenye zambi na kuwaokoa toka hukumu.

Umefahamu kweli hizi tatu? Kweli hizi tatu zimeshika roho yako? Unafahamu kipimo cha utakatifu wa Mungu?

Unafahamu ukubwa wa zambi zako machoni mwa Yule ambaye atalazimishwa kukuhukumu? Unajua ya kwamba Mungu ana shauri kukusafisha toka zambi zako?

Ndiyo, **Mungu ni mtakatifu** na **mtu ni mwovu**. Tumeona **kweli hizi mbili** tena na tena ndani ya masomo yetu katika Maandiko Matakatifu. Ni kwa sababu ya utukufu wake Mungu aliumba moto usiozimika kwa Shetani na kila mtu ambaye anamfuata. Kwa sababu ya utakatifu wake Mungu alifukuza Adamu na Hawa toka shamba la Paradiso siku walipokula matunda toka mti ambao Mungu alikataza. Kwa sababu ya utakatifu wake Mungu aliagiza wana wa Adamu kutoa nyama kuwa sadaka ya kuteketezwa kufunika zambi. Na kwa sababu ya utakatifu wake hakukubali sadaka ya Kaina. Kwa sababu Mungu ni mtakatifu aliharibu wenye zambi kwa wakati wa Noa na garika na alinyesha moto juu ya watu wa Sodomo na Gomora kwa wakati wa Abrahamu. Kwa sababu ya utakatifu wake Mungu ameweka siku atakapohukumu dunia na haki.

Sikia maneno manabii ya Mungu waliyoandika juu ya utakatifu wa Mungu na uovu wa mtu. Walisema: *"Wewe si tangu milele, Ee Bwana Mungu wangu, mtakatifu wangu? . . . Wewe uliye na macho safi zaidi hata usiweze kutazama mabaya, na usiyeweza kutazama ukaidi!"* (Habakuki 1:12,13) *"Sisi sote tumekuwa kama kitu kichafu, na haki zetu ni kama vitambaa vya kupasukapasuka vya taka!"* (Isaya 64:6) Basi Mungu akiwa mtakatifu hivi na mtu ikiwa mwovu hivi, nani anayeweza kuokolewa? Namna gani tunaweza kuokolewa toka moto wa milele wa hadeze? Namna gani wana wa Adamu wanaweza kushinda kwa milele mbele ya Mungu aliye safi na mtakatifu?

Jibu kwa ulizo hili ni **kweli ya tatu** ya mafundisho ya manabii. Nyuma ya kuhubiri ya kwamba Mungu ni **mtakatifu** na ya kwamba wana wa Adamu ni waovu, waliendelea kutangaza ya kwamba Mungu alikuwa na **shauri** kuokoa wana wa Adamu toka zambi zao.

Habari kubwa zaidi ya kitabu cha Agano la Kwanza (Agano la Kale) ni ya kwamba Mungu aliahidi kutuma duniani **Mkombozi mwenye haki atakayekufa kwa pahali pa wana waovu wa Adamu** kuwaokoa wote ambao wanamwamini. Hili lilikuwa shauri na ni shauri la Mungu kuokoa wenye zambi. Kwa njia ya damu iliyomwangika ya Mkombozi Mungu ataweza kusamehe zambi na kupatanisha wenye zambi naye, bila kuacha kuwa mwenye haki.

Kuendelesha shauri lake kutuma Mwokozi duniani, Mungu aliita **Abrahamu** kwa kufanya naye taifa jipya. Manabii wa Mungu na Masiya watatoka kwa taifa hili. Mungu alisema na Abrahamu: *"Nitakubariki. . . uwe baraka. . . na ndani yako* ***jamaa zote za inchi*** *watabarikiwa."* (Mwanzo 12:2,3) Hivi Abrahamu alizaa **Isaka** wakati alipokuwa mzee, na Isaka alizaa **Yakobo**. Yakobo alizaa **wana kumi na wawili**, waliokuwa baba za makabila ya **Israeli**. Hivi tunajifunza ya kwamba wakati Mungu alipoita Abrahamu, alikuwa akiendesha shauri lake kutuma Mwokozi duniani kwa sababu Masiya atazaliwa toka jamaa ya Abrahamu na taifa la Israeli.

Kisha tuliona ya kwamba wana wa Israeli walihama toka inchi ya Kana, wakapanga katika Misri pahali walipogeuka watumwa wa Wamisri. Lakini Mungu hakusahau wazao wa Abrahamu, Waisraeli. Aliita **Musa** kufungua Waisraeli na kuwaongoza kufika kwa inchi ambayo Mungu aliahidi mzazi wao Abrahamu miaka mingi mbele. Mungu alitumika vilevile na nabii Musa kutupa sisi kitabu kinachoitwa **Tora** na kilicho msingi wa maneno yote Mungu aliyofunua watu tangu wakati ule.

Nyuma ya wakati wa Musa, tuliona ya kwamba Mungu alituma manabii wengi kwa Israeli, lakini zaidi ya Waisraeli hawakuweka roho juu ya maneno ya manabii. Lakini kutoaminifu kwa Waisraeli hakukuzuiza uaminifu wa Mungu na njia aliyotayarisha kutuma Masiya duniani! Hivi tuliona namna Mungu alivyochagua **Daudi** kuwa mfalme wa Israeli na nabii atakayeandika nyingi za nyimbo nzuri sana ndani ya kitabu cha **Zaburi**. Nabii Daudi aliandika maneno mengi juu ya Masiya na namna wana wa Adamu watamtesa na hata kutoboa mikono na miguu yake. Lakini Daudi alitabiri vilevile ya kwamba wakati Masiya atakapokwisha kumwanga damu yake kama sadaka inayoondosha zambi, atashinda mauti na kufufuka toka kaburi!

Ndani ya safari yetu katika Maandiko Matakatifu, tuliona vilevile ya kwamba si Musa na Daudi tu walioandika juu ya Masiya. **Manabii wote wa Mungu walitangaza kuja kwa Masiya.** Kwa mfano, nabii **Isaya** alitangaza ya kwamba Masiya atazaliwa namna nyingine na watu waliozaliwa kufika siku ile. Alisema: *"Bikira atapata mimba naye atazaa mtoto mwanamume, na ataita jina lake Emanueli; maana yake Mungu pamoja nasi."* (Isaya 7:14; Matayo 1:23) Nabii aliandika neno hili mia za miaka mbele.

Kuna nabii mwingine aliyeishi kwa wakati wa Isaya. Jina lake lilikuwa **Mika**. Mungu alifunulia Mika jina la mji pahali Masiya

atakapozaliwa. Sikiliza vizuri maneno nabii aliyoandika. Ndani ya sura 5 ya kitabu cha Mika tunasoma: *"Lakini wewe, **Betelehemu**-Efurata, ulio mdogo katika elfu za Yuda, katika wewe atatokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; matokeo yake ni tangu zamani, tangu milele."* (Mika 5:2) Hivi Mika alitangaza ya kwamba Masiya atazaliwa ndani ya mji wa Betelehemu, pahali Mfalme Daudi alipozaliwa! Masomo matatu nyuma, kwa mwanzo wa Kitabu 3, tutajifunza ya kama Mungu alitimiza unabii huu, kwa sababu Masiya alizaliwa ndani ya mji wa Betelehemu, kama nabii wa Mungu, ndiye Mika, alivyotabiri mia za miaka mbele.

Kweli Mungu alitayarisha vizuri sana njia kwa kufika kwa Mwokozi! **Kuna mia za mashairi ndani ya Kitabu kitakatifu cha Mungu, ndani yao manabii walisema juu ya kuja kwa Masiya.** Labda unauliza: Kwa nini Mungu aliweka ndani ya nia za manabii mawazo haya yote juu ya Masiya **mbele** ya kuja kwake duniani? Kwa sababu ya neno kubwa moja: Mungu aliongoza manabii kuandika maneno mengi juu ya kuja kwa Masiya mbele ya kuja kwake, ili wakati alipofika na kutimiza maneno yote ambayo manabii waliandika juu yake, tuweze kujua kabisa, **bila shaka hata nusu**, ya kwamba yeye na yeye pekee ni Mwokozi aliyetumwa na Mungu. Mungu hataki kukudanganya! Anataka ujue kama Masiya, Mwokozi wa wenye zambi ni nani, ili uweze kumwamini na kumfuata na kuokolewa toka zambi zako. Hii ndiyo sababu moja ambayo ilimsukuma kutupa sisi Kitabu hiki cha ajabu ambacho tunaweza kutegemea kabisa kinachoitwa Agano la Kwanza—ili tuweze kutambua nini ni **kweli** na nini ni **uwongo.**

Halafu kwa kumaliza safari yetu ndani ya Agano la Kwanza, tunataka kusoma toka kitabu cha **Malaki**, kitabu cha mwisho cha Agano la kwanza. Maneno ya nabii Malaki ni maneno makubwa, kwa sababu ni maneno ya mwisho ambayo Mungu alituma kwa wana wa Adamu mbele ya kufika kwa Masiya duniani. Miaka mia ine tu ilibaki kufika kuzaliwa kwa Mkombozi.

Sikiliza maneno nabii Malaki aliyoandika ndani ya sura ya mwisho ya Agano la kwanza. Alisema,

> *"Tazameni, ninatuma mjumbe wangu, naye **atatayarisha njia mbele yangu**: na Bwana ambaye munamtafuta atakuja mbio hekaluni mwake; na mjumbe wa agano ambaye munampenda, tazameni, anakuja, Bwana wa majeshi anasema . . . Mimi ni Bwana, sigeuki . . . Lakini kwa ninyi munaoogopa jina langu, **jua la haki** litapanda, na kupona katika mabawa yake!"* (Malaki 3:1,6; 4:2)

Hivi nabii Malaki alitabiri ya kwamba Mungu alikusudi kutuma nabii mmoja mbele ya Masiya atakayetayarisha njia mbele yake. Unajua kama nabii huyu alikuwa nani? Ndani ya somo la nyuma, tuatona ya kwamba yule atakayetayarisha njia mbele ya Masiya alikuwa nabii **Yoane** {*Yahya*}.

Lakini, Malaki aliandika vilevile, ***"Mjumbe wa agano ambaye munampenda, tazameni, anakuja . . . mimi Bwana, sigeuki."*** (Malaki 3:1,6). Karibu miaka mia mbili mbele, nabii Yeremia alikuwa ametabiri:

> *"Angalia, siku zinakuja, anasema Bwana, nitakapofanya* ***agano jipya*** *na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa agano lile nililofanya na baba zao, katika siku nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika inchi ya Misri, lile agano langu ambalo walilivunja, hata mimi nikikuwa bwana wao, anasema Bwana. Lakini hili agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli, nyuma ya siku zile, anasema Bwana, nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika . . . nitasamehe uovu wao, wala zambi yao sitakumbuka tena."* (Yeremia 31:31-34)

Na maneno haya, Mungu alikuwa akitangaza ya kwamba Masiya ataleta agano jipya kama alivyoahidi zamani. Agano Jipya halitategemea watu wasioheshimu agano la Mungu; litategemea Mungu aliye mwaminifu na mwenye rehema hata kutuma duniani Masiya, Mjumbe wa Agano.

Kwa elfu za miaka Mungu aliamrisha sadaka za nyama ili aweze kusamehe zambi za wana wa Adamu. **Sadaka za nyama** zilikuwa sehemu kubwa ya **Agano la Kwanza** ambalo Mungu aliwapa wanadamu kwa njia ya **manabii wake.** Lakini **Masiya** ataletea dunia **Agano Jipya,** kwa sababu **atatimiza mfano wa sadaka zote za nyama** (sadaka hizi zilikuwa mfano wa Mkombozi atakayemwanga damu yake kwa zambi kwa wakati wa kuja), na kwa njia hii ataweka kando Agano la Kwanza.

Masiya hatakuja **kufuta** (ondoa kabisa) masemo ya manabii, lakini **kuyatimiza**. Kwa sababu hii Malaki anaita Masiya *"Jua la Haki."* Namna gani Masiya atakuwa sawasawa na jua? Manabii walifanana na mwezi au tawafa zinazoleta nuru ndogo katika dunia la giza. Lakini Masiya ni jua linalopanda, kwa sababu alikuja kufukuza giza la zambi zetu na kututembeza ndani ya **njia ya haki kwa milele**! Nani anayehitaji mwezi au tawafa wakati jua linapokwisha kupanda? Masiya ni **Jua la Haki**! Ndani ya somo la nyuma, ndilo somo la

kwanza la Kitabu 3, tutasikia ya kwamba Zakaria, baba ya nabii Yoane, alisema juu ya Masiya vivyo hivyo, akisema: "*Kwa sababu ya upole wa rehema zake Mungu wetu,* ***katika mwanga uliotoka juu kutufikia, kuwaangazia, wanaokaa katika giza, na katika uvuli wa mauti,*** *na kuwaongoza miguu yetu katika njia ya salama."* (Luka 1:78,79) Amina!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Hivi, rafiki, tumefika kwa mwisho wa safari yetu ndani ya vitabu vya Agano la kwanza. Ndani ya **Kitabu cha tatu,** Mungu akitaka, tutaanza sehemu nzuri kabisa inayofuata, ndiyo Agano Jipya — kitabu cha Habari Njema {*Injil*}. Ndani ya Habari Njema tutaona namna Masiya alivyotimiza maneno manabii waliyosema ndani ya Agano la kwanza . . .

Usikose kuendelea na **Kitabu cha Tatu** cha mfulizo huu ***Njia ya Haki*** na kujifunza mwisho wa habari hizi kubwa zaidi.

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya onyo hili:

> ***"Tuna neno la unabii lililo imara zaidi, na inawafaa ninyi kuliangalia, kama taa inayongaa katika pahali pa giza hata mapambazuko, na nyota ya asubui itasimama mioyoni mwenu."*** (2 Petro 1:19)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~